

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Sita – Tarehe 27 Aprili, 2016

(Bunge lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NDG. NENELWA M. WANKANGA - KATIBU MEZANI: Hati za kuwasilisha mezani.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI , OFISI YA RAIS, TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI NA UTAWALA BORA (MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI):

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

MHE. JASSON S. RWEIKIZA - MWENYEKITI WA KAMATI YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:

Taarifa ya Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa mwaka wa fedha 2015/2016 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Taarifa ya Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu utekelezaji wa majukumu yao Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa mwaka wa fedha 2015/2016 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio na Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA - MSEMaji MKUU WA KAMBI YA UPINZANI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Ofisi Rais (Utumishi na Utawala Bora) kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

NDG. NENELWA M. WANKANGA - KATIBU MEZANI: Maswali.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 51

Ajira kwa Wahitimu wa Vyu Vikiu

MHE. ESTHER M. MMASI aliuliza:-

Serikali kupitia taasisi za umma zimeweza kufanya tafiti nzuri kujua uhalisia wa suala la ajira kwa vijana waliohitimu vyuo vikuu:-

Je, ni kwa namna gani Serikali inaweza kutumia majibu ya tafiti hizo kupitia *convocation office* ndani ya taasisi ya umma katika kutatua changamoto za ajira katika nchi yetu?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU (MHE. ANTONY P. MAVUNDE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Michael Mmasi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara imekuwa ikifanya au kutumia tafiti zilizokwisha kufanywa na taasisi mbalimbali ili kushughulikia

changamoto za ajira, upangaji wa mipango na utatuzi wa changamoto za ajira kwa vijana wa vyuo vikuu na wengineo.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa na tafiti hizo zinasaidia Serikali kupanga na kutekeleza mikakati ifuatayo:-

(i) Programu ya Kukuza Ujuzi inayolenga kuwapatia wafanyakazi na vijana maarifa na stadi za kazi ili waweze kuajirika na kujijiri.

(ii) Mfuko wa wa Maendeleo ya Vijana unaolenga kuwapatia vijana mafunzo na mikopo nafuu ya kujijiri. Mfuko unawahamasisha wahitimu kuanzisha vikundi vya uzalishaji na makampuni ili wajiirika na kuajiri wengine.

(iii) Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambalo linadhamini wahitimu wachanga kupata mikopo nafuu katika Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB) kwa njia ya ushindani ili waweze kufanya shughuli za kujijiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuweka mazingira rafiki ya uwezeshaji kwa vijana na wahitimu wa vyuo vikuu ili kutatua changamoto za ajira katika nchi yetu kwa kushirikiana na wadau husika kama waajiri, taasisi za elimu, taasisi za kifedha na vijana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Esther Mmasi swali la nyongeza.

MHE. ESTHER M. MMASI: Mheshimiwa Naibu Spika, moja kati ya mipango ya Serikali ni pamoja na kuinua ujuzi wa vijana wahitimu kutoka vyuo vikuu kutoka asilimia 2 mpaka 12. Je, nini mpango wa Serikali katika kutekeleza mikakati hii hadi kufika mwaka 2019/2020?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, moja ya mikakati ya Serikali katika kuinua sekta ya ujasiriamali kwa vijana wa Kitanzania ni pamoja na kuwekeza kiasi cha shilingi bilioni 1.6 kupitia Mfuko wa Vijana, Baraza la Uwekezaji la Taifa.

Je, Serikali ina mkakati gani katika kuanzisha Baraza la Taifa la Vijana ili kuongeza ufanisi lakini pia kuongeza fursa nyingi na wanufaikaji wengi kupitia Mfuko huu wa Vijana?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la tatu, kupitia ...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Esther, maswali ni miwili tu. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU (MHE. ANTONY P. MAVUNDE): Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la kwanza aliulizia kuhusu mpango wa ukuzaji ujuzi, nataka tu nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tumekwishaanza mpango mkakati wa kukuza ujuzi ambao utahusisha wahitimu mbalimbali wa vyuo vikuu, lakini na wanafunzi ambao bado katika vyuo vikuu. Katika mpango wetu huu utahusisha pia mafunzo ya uanagenzi pamoja na *internship* na lengo lake ni kukuza ujuzi kwa wanafunzi na wahitimu wa vyuo vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika swali lake la pili ameulizia kuhusu Baraza la Vijana la Taifa na nataka nimpe tu taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari Serikali na Bunge hili lilipitisha Sheria Na.12 ya Uundwaji wa Baraza la Vijana la Taifa na tayari Kanuni zimekwishakamilika kwa ajili ya kuanza rasmi uundwaji wa Baraza hili ambalo litakuwa likiwakilisha matatizo mbalimbali ya vijana lakini pia litakuwa sehemu ya kisemeo cha vijana katika kuwasilisha matatizo mbalimbali ambayo yanawakabili.

Kwa hiyo, tunaamini kupitia Baraza hili, vijana watakuwa wamepata sauti na sisi kama Serikali tutakuwa sehemu ya kushirikiana nao katika kutatua kero na changamoto ambazo zinawakabili vijana.

Na. 52

Kushindwa kwa Utekelezaji wa Mradi wa Kupeleka Umeme Vijijini

MHE. SELEMANI J. ZEDI aliuliza:-

Je, Serikali kupitia REA inachukua hatua gani kwa Mkandarasi CHICCO ambaye ameshindwa kukamilisha utekelezaji wa Mradi wa Kupeleka Umeme Vijijini Awamu ya Pili (REA II) katika vijiji vya Mwangoye, Mbutu na Mambali?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkandarasi CHICCO kutoka China alishinda zabuni ya usambazaji wa umeme vijijini REA Awamu ya Pili katika Mkoa wa Tabora. Ni kweli kwamba mkandarasi huyu alianza kazi kwa kusuasua hali iliyosababisha Wakala wa Nishati Vijijini kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni

pamoja na kumwandikia barua ya kutoridhishwa na kazi na kuongeza usimamizi wa kufuatilia utendaji wake. Hatua nyingine iliyochukuliwa ni pamoja na kumtaka mkandarasi huyo kuongeza kampuni nyingine (*sub-contractor*) ili kuharakisha shughuli za ujenzi wa mradi huo. Utekelezaji wa kazi hiyo wa mkoa mzima unaendelea ambapo kazi imekamilika kwa asilimia 82 na mradi unatarajiwa kukamilika mwishoni wa mwezi Juni, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kupeleka umeme vijiji vya Mambali, Mbutu pamoja na Mwangoye inaendelea na imefikia utekelezaji kama ifuatavyo:-

(i) Kijiji cha Mambali kazi ya kupeleka umeme imekamilika kwa asilimia 100 na wateja wapatao 49 wameunganishiwa umeme.

(ii) Kijiji cha Mwangoye kazi ya kujenga njia ya umeme imekamilika. Taratibu za ufungaji wa transfoma zinaendelea na umeme unatarajiwa kuwashwa mara baada ya kukamilika kwa ufungaji wa transfoma hizo.

(iii) Kijiji cha Mbutu hakikuwepo kwenye mradi huu hata hivyo mkandarasi CHICCO alipewa kazi ya ziada na mradi unaendelea. Mkandarasi amemaliza kazi ya upembuzi yakinifu na sasa yupo katika hatua za mwisho za kukamilisha michoro ya kiuhandishi kabla ya kuanza utekelezaji wa mradi wa umeme katika kijiji hiki.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi swali la nyongeza.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Bukene, nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ziara ambayo aliifanya katika Jimbo hili hivi karibuni na vijiji vyote vilivyotajwa kwenye swali hili vya Mwangoye, Mambali na Mbutu, Mheshimiwa Naibu Waziri alivipitia na kutoa maelekezo maalum kwa TANESCO, REA na CHICCO...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zedi, naomba uulize swali tafadhali.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Naibu Spika, sasa swali langu ni kwamba kutokana na mwikio mkubwa wa wananchi katika kijiji cha Mwangoye, Mambali na Mbutu, jambo ambalo limefanya wananchi wengi kufanya *wiring* na kuwa tayari na fedha ya kulipia, lakini kuna upungufu mkubwa wa nguzo na vifaa vya kuunganishia.

Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kutumia *forum* hii kutoa agizo au kauli maalum kwa watendaji wa REA, TANESCO na CHICCO kuhakikisha kwamba wananchi wote wa Mwangoye, Mambali na Mbutu ambao wameshajiandaa kupata umeme wanapatiwa nguzo na vifaa vya kuunganishiwa ili waweze kupata huduma muhimu ya nishati?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, sina uhakika kama kulikuwa na swali, lilikuwa ni ombi la kutoa tamko lakini kama unaona kuna swali karibu ujibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu niongeze maelezo kwenye shukrani alizotoa na mimi namshukuru sana Mheshimiwa Zedi kwa pongezi na shukrani za kuunga mkono. Nampongeza sana pamoja na wananchi wa Bukene. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye swali lake, kimsingi siyo swali lakini anataka wananchi wake wapate uhakika. Ni kweli kabisa nguzo zinaendelea kwenda Bukene katika vijiji vyote vitatu na katika mwezi ujao wananchi wapatao 50 watapatiwa umeme kwa sababu nguzo wameshapelekewa.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea niwakumbushe tu kidogo, maswali yetu yawe mafupi kwa sababu kila swali lina muda wa dakika sita tu. Kwa hiyo, wote tuwe tunaangalia muda tunaotumia kuuliza maswali lakini pia muda Mawaziri tunaotumia kujibu. Tuendeleo na swali linalofuata.

Na. 53

Tatizo la GN. Na .28 ya Mwaka 2008

MHE. HAROON M. PIRMOHAMED aliuliza:-

Katika GN. Na. 28 ya mwaka 2008 inawataka wananchi wanaoishi katika vijiji 21 vilivyopo katika Jimbo la Mbarali, Wilaya ya Mbarali, Mkoani Mbeya wahame ili kupisha Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ingawa wananchi katika vijiji hivyo wameishi katika maeneo hayo tangu enzi za mababu zao:-

Je, ni lini Serikali itafuta GN. Na. 28 ya mwaka 2008 ili wananchi katika vijiji hivyo waweze kuishi bila kubughudhiwa pamoja na kuendelea na shughuli zao za kilimo na ufugaji?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Haroon Mulla Pirmohamed, Mbunge wa Mbarali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tangazo la Serikali Na. 28 la mwaka 2008 lilihusu kuhifadhiwa Bonde la Usangu kama sehemu ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha hatua ambayo ulihusisha kutunza vyanzo vya maji kwa ajili ya shughuli za kilimo na kibinadamu, uzalishaji wa umeme na matumizi ya kiikolojia kwa maslahi mapana ya kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanaoishi katika vijiji 21 vilivyopo katika Jimbo la Mbarali, Wilaya ya Mbarali, Mkoani Mbeya wamewasilisha malalamiko yao Serikalini wakipinga uhalali wa mpaka mpya uliotokana na Tangazo la Serikali nililolitaja na hivyo kuendelea kuwepo ndani ya mpaka. Aidha, baadhi ya wananchi waliotii sheria na kuondoka katika maeneo husika wamelalamikia viwango vya fidia vilivyolipwa katika kipindi cha mwaka 2006 hadi 2008 baada ya taratibu zote za kiserikali ikiwemo kufanya tathmini kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikifanya kila jitihada kutatua mgogoro huo katika ngazi mbalimbali ikiwemo vikao vya ushauri baina ya wadau wakiwemo wananchi katika eneo husika, uongozi wa Wilaya ya Mbarali na Mkoa wa Mbeya, Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliunda timu ya wataalam na kupitia upya mipaka iliyotangazwa ili kutoa ushauri wa kitaalam juu ya mipaka hiyo na kuwasilisha ripoti kwenye Kamati ya pamoja kati ya Mkoa wa Mbeya na Wizara ya Maliasili na Utalii na kuhakiki malipo ya fidia kwa wananchi waliohama kupisha eneo lililojumuishwa kwenye Hifadhi ya Taifa Ruaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhakiki huo ulikusudia kuondoa malalamiko ya mapunjo yaliyojitokeza kutoka kwa baadhi ya wananchi, kupitia na kuhakiki maeneo yote ya mpaka ardhini ili kujua maeneo gani yataathiriwa na mpaka mpya na kuona ni kwa namna gani mpaka utaweza kurekebishwa bila kuathiri lengo kuu la kuhifadhi sehemu ya eneo hilo la Bonde la Usangu. Mapedekezo yatakayotokana na kazi hii yatatumika kufanya maamuzi sahihi juu ya mipaka ya eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kusisitiza kuwa eneo la Bonde la Usangu, lililolitajwa kwenye GN. Na. 28 ya mwaka 2008 ni eneo linalolindwa

kisheria na umuhimu wake bado uko pale pale. Hivyo, badiliko lolote la mipaka ndani yake litahitajika kufanyika kwa kuzingatia taratibu za kisheria kupitia Bunge lako Tukufu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Haroon Pirmohamed swali la nyongeza.

MHE. HAROON M. PIRMOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, katika jibu lake la msingi Mheshimiwa Waziri amesema Serikali iliunda timu ya wataalam kupitia upya mipaka iliyotangazwa ili kutoa mapendekezo kuhusu mipaka hiyo ya GN. Na. 28. Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba zoezi hili litamalizika lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa mgombea Urais kupitia CCM katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka jana aliwaahidi wananchi wa Mbarali wanaoishi katika vijiji hivyo 21 kumaliza kero hiyo na kwa kuwa mgombea huyo sasa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Je, Mheshimiwa Waziri kuendelea kuchelea kutoa jibu hili haoni kama anapinga ahadi aliyotoa Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ni lini au ni baada ya muda gani zoezi hilo ambalo linakamilishwa na Kamati iliyoundwa litakamilika? Nimepitia taarifa ya awali ya Kamati hiyo ambayo tumesema inakamilisha kazi iliyopewa, napenda kukufahamisha kwamba kazi hiyo ndani ya kipindi cha mwezi mmoja itakuwa imekamilika ikiwa ni pamoja na kwenda kufanya ukaguzi wa maeneo yanayohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, pengine jambo muhimu si kuzungumzia zaidi kwamba kuna ukiukwaji au kuna utaratibu ambao unaonekana kupingana na ahadi aliyotoa Mheshimiwa Rais, jambo la msingi hapa ni kwamba kazi hii ni muhimu na suala la kushughulikia changamoto za wananchi pia ni ahadi ya Serikali hii ya Awamu ya Tano na katika kipindi hicho ambacho nimekisema suala hilo litakuwa limekamilika na kupatiwa uvumbuzi.

Na. 54

Ng'ombe Wanaoingia katika Hifadhi ya Kigosi - Ushetu

MHE. ELIAS J. KWANDIKWA aliuliza:-

(a) Je, katika kipindi cha mwaka 2010 - 2015, ni ng'ombe wangapi wametaifishwa na Serikali kwa kuingia katika Hifadhi ya Kigosi eneo linalopakana na Jimbo la Ushetu katika Kata za Ulowa, Ubagwe, Ulewe, Nyamkende na Idalia?

(b) Je, ni utaratibu gani unatumika kuua ng'ombe wanaoingia kwenye hifadhi; na ni ng'ombe wangapi waliuawa katika kipindi cha mwaka 2010 - 2015?

NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na utalii, kwa mara nyingine tena, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Elias John Kwandikwa, Mbunge wa Ushetu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 27(1), kila mtu ana wajibu wa kulinda maliasili ya Jamhuri ya Muungano. Aidha, Sheria ya Kuhifadhi na Kulinda Wanyamapori, Na. 5 ya mwaka 2009, vifungu vya 18(2) na 21(1) vinakataza mtu yeyote kuingiza mifugo, kuchunga au kulisha mifugo ndani ya Hifadhi za Taifa, Mapori ya Akiba na Mapori Tengefu. Chini ya kifungu cha 111(1) cha sheria hiyo, mtu aliyepatikana na hatia ya kuingiza mifugo ndani ya hifadhi atanyang'anywa mifugo hiyo kwa amri ya Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na changamoto kubwa ya wafugaji kuingiza mifugo wengi katika Pori la Kigosi wanaohatarisha ustawi wa hifadhi hiyo. Serikali Wilaya ya Ushetu na Mkoa wa Shinyanga wamekuwa wakitoa elimu kwa wananchi juu ya athari ya kupeleka mifugo ndani ya hifadhi kwa Mapori ya Akiba na msimamo wa sheria.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2010 - 2015 hakuna ng'ombe waliotaifishwa na Serikali katika Wilaya ya Ushetu.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imebaini kwamba watu wanaopeleka mifugo ndani ya mapori ya Kigosi/Moyowosi ni pamoja na wageni toka nchi ya jirani ambao wanaingia hifadhini na silaha za kivita. Katika

jitihada za kuwatoa wafugaji wa aina hii katika hifadhi, maafa yametokea hapa na pale. Askari kadhaa Wanyamapori wamepoteza maisha, mifugo kadhaa wameuawa katika mazingira ya aina hii; hata hivyo Serikali haina sera, sheria, kanuni au utaratibu wa kuua mifugo.

NAIBU SPIKA. Mheshimiwa Elias John Kwandikwa, swali la nyongeza.

MHE. ELIAS J. KWANDIKWA: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Napenda niulize maswali madogo mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa kuna ng'ombe 320 waliotaifishwa tarehe 08/2/2016 na kwa kuwa haeleweki hao ng'ombe wameuzwa kwa nani, kiasi cha pesa kilichopatikana na kiko wapi.

Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kufuatilia kwa kina ili na mimi niweze kujua hao ng'ombe wameuzwa kwa nani na hicho kiasi kilichopatikana kimepelekwa wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii alipokuwa kwenye ziara yake Bukombe tarehe 2 mwezi wa nne alipofuatana na Mheshimiwa Waziri wa Mifugo ili kuondoa changamoto hii ya suala la mifugo kuingia kwenye hifadhi alitoa agizo kwamba wafugaji watengewe maeneo kabla ya tarehe 15/06/2016. Je, utaratibu huo na zoezi hilo limefikia wapi? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Elias Kwandikwa kwa kufuatilia kwa ukaribu suala hili na kwa kweli anastahili kuchaguliwa kuwa Mbunge wa eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na swali lake la pili la utaratibu ule, tumepanga kukutana na Mheshimiwa Waziri wa Maliasili katika kipindi cha mwisho wa wiki hii kujadiliana utaratibu ambao tutaufuata kuhusu mambo haya ya ardhi. Tunategemea pia kumshirikisha Waziri wa Ardhi kwa sababu utengaji wa maeneo mengine ya malisho unaanzia kwenye Kamati za Vijiji za Matumizi Bora ya Ardhi ambapo jambo hilo halifanywi na Waziri wa Maliasili wala Waziri wa Kilimo. Kwa hiyo, kwenye utaratibu ule wa makundi ya mifugo ambayo yanatokana na vijiji yatatengwa maeneo ya vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusu swali la kwanza, nimekuwa nikifuatilia hata mimi baada ya kuwa nimeambiwa na tuliongea pia na Waziri wa Maliasili, ni kweli sheria inakataza mifugo kuingia kwenye hifadhi na sisi Wabunge tuendeleo kutoa elimu hiyo ya kuwaambia wananchi wasiingize mifugo kwenye hifadhi ama kwenye Mapori ya Akiba. Vilevile kumekuwepo na ukiukwaji wa sheria ya baadhi ya watumishi wa Serikali wasio waaminifu kutumia fursa hiyo kama sehemu ya wao kujipatia kipato. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata hizo taarifa kwamba baadhi ya mifugo ambayo imekuwa ikitafishwa imekuwa ile ambayo wamiliki wake hawakuweza kuwapa fedha wale watu. Kwa hiyo, kwa wale ambao wanamalizana nao, kwa maana ya kutoa fedha wanaachiwa wanaondoka na mifugo. Hilo ni jambo ambalo liko kinyume cha sheria na taasisi zetu za Kiserikali ziendeleo kufuatilia na iwachukulie hatua watu ambao wanapindisha sheria kwa manufaa yao binafsi kwa sababu wanaipaka matope Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wengine wamekuwa wakitaifisha mifugo kwa sababu tu wanaenda kuinunua wao wenyewe kwa bei ya kutupa. Hilo na lenyewe liko kinyume cha taratibu za kisheria. Sheria inatakiwa ifuatwe ili kuweza kuendesha nchi kwa utawala bora na wale wananchi wajione hawajaonewa bali wamekiuka sheria na sheria imechukua mkondo wake.

Kwa hiyo, sisi kama Wizara pamoja na Wizara ya Maliasili tutaendeleo kutoa elimu lakini na kusimamia sheria ili haki iweze kutendeka.

Na. 55

**Ahadi ya Kujenga kwa Lami Barabara
toka Mika - Kirongwe**

MHE. VEDASTUS M. MANYINYI (K.n.y MHE. LAMECK O. AIRO) aliuliza:-

Serikali chini ya uongozi wa Rais Mstaafu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete ilitangaza Jimbo la Rorya kuwa Wilaya mpya na sasa ina miaka saba tangu kutangazwa na hitaji kubwa la kwanza ni kutekeleza ahadi ya Rais Mstaafu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na kurudiwa tena kuahidiwa na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano za kujenga kwa lami barabara ya kutoka Mika - Utegi - Shirati - Kirongwe yenye urefu wa kilometa 58, kwa kuzingatia umuhimu wake kwamba ni kiungo kati ya Tanzania na Kenya kupitia Rorya, itainua pato la Halmashauri kupitia ushuru wa mpakani na tarafa tatu kati ya nne kupata urahisi kuingia nchi jirani ya Kenya kwa ukaribu zaidi kuliko kutumia barabara ya kwenda Sirari:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara hii ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya Wilaya ya Rorya?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lameck Okambo Airo, Mbunge wa Rorya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mika – Utegi – Shirati – Ruariport/Kirongwe, yenye urefu wa kilometa 58 ni muhimu kwa Wilaya ya Rorya kiuchumi na kijamii, kwani inaunganisha Wilaya ya Rorya na Wilaya nyingine za Mkoa wa Mara pamoja na nchi jirani ya Kenya. Kwa kuzingatia umuhimu wa barabara hii, Serikali ilianza kujenga kwa awamu kwa kiwango cha lami barabara kutoka Mika – Ruariport au Kirongwe tangu mwaka wa fedha wa 2009 - 2010. Hadi sasa kipande cha barabara chenye urefu wa kilometa 7.5 kwenye barabara hii kimekamiliwa kujengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, sehemu iliyobaki itaendelea kujengwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Vedastus Manyinyi swali la nyongeza.

MHE. VEDASTUS M. MANYINYI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, namshukuru Naibu Waziri na mimi nakubaliana naye alivyosema kwamba barabara ile ina umuhimu mkubwa hasa ukilinganisha kwamba kuna uzalishaji wa samaki katika eneo hilo, lakini vilevile ni eneo ambalo linapita nchi yetu ya jirani.

Sasa ukiangalia toka 2009 hadi leo, zaidi ya miaka mitano ni kilometa 7.5 peke yake ndiyo barabara iliyowekewa lami, napenda kufahamu Serikali itakuwa tayari kwa mwaka huu kutenga fedha kwa ajili ya hicho kipande cha barabara ili kiweze kujengwa zaidi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, naomba ikumbukwe kwamba mbali na ujenzi wa barabara katika maeneo mbalimbali ambayo yako katika mpango lakini kutokana na umuhimu Mheshimiwa Rais mwaka jana tuliweza kumpa maombi maalum hasa kwa pale Musoma Mjini, tulimpa ombi la barabara ya kutoka Bweri - Makoko ambapo kipande kile zipo sekondari zisizopungua 14, je, Serikali sasa itakuwa tayari kutimiza ahadi hiyo kuanzia mwaka huu wa fedha?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, maswali yake yote mawili yanaongelea kutenga fedha kwa mwaka huu wa 2016/2017 kwa ajili ya kuendelea kujenga ile barabara ya Mika – Utegi – Shirati - Kirongwe pamoja na hii barabara aliyoiongelea ya Bweri - Makoko. Naomba kumuahidi kwamba hivi sasa tunavyoongea, wataalam wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, sekta ya ujenzi, wapo katika hatua ya mwisho ya kuangalia katika haka kasungura kadogo tulikokapata ni wapi tutenge kiasi gani. Kwa hiyo, naomba asubiri Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano itakapokuja itatoa majibu sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine moja ningependa kusesitiza, mahitaji ya ujenzi wa barabara ni makumbwa sana sehemu mbalimbali za nchi na *priority* (kipaumbele) kwa mwaka ujao wa fedha ni kukamilisha miradi ya muda mrefu ili kuondokana na gharama za makandarasi wanazotudai kutokana na kuchelewa kukamilisha miradi. Hivyo, tutahakikisha kwamba barabara zile ambazo zimeanza muda mrefu lazima kwanza zikamilike kabla hatujaingia katika eneo jipya.

Na. 56

Ukosefu wa Miundombinu ya Barabara Mlimba

MHE. SUSAN L. KIWANGA aliuliza:-

Licha ya Jimbo la Mlimba kuwa na uzalishaji wa mazao ya kilimo, linakumbwa na ukosefu mkubwa wa miundombinu ya barabara zinazopitika na madaraja, jambo linalosababisha wakulima kushindwa kusafirisha mazao yao kwenda kwenye masoko na hivyo kuendelea kuwa maskini licha ya kuwa na utajiri wa mazao ya kilimo:-

(a) Je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara ya Ifakara - Mlimba, Mlimba - Madeke na Mlimba - Uchindile?

(b) Je, ni lini Serikali itajenga madaraja ya kudumu katika Mito ya Mtunji, Chiwachiwa, Mngeta na Londo kwa kuwa yaliyopo sasa ni ya miti?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga, Mbunge wa Mlimba, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Ifakara - Mlimba - Madeke yenye urefu wa kilometa 231.53 inahudumiwa na Wakala wa Barabara (TANROADS) na barabara ya Mlimba - Uchindile inahudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero. Serikali imeanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Ifakara - Mlimba kwa kuanza na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa sehemu ya barabara ya kutoka Ifakara – Kihansi yenye urefu wa kilometa 126 kwa lengo la kuunganisha kipande cha barabara ya lami chenye urefu wa kilometa 24 kati ya Kihansi – Mlimba. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina inaendelea na inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa ujenzi wa madaraja ya kudumu katika Mito ya Mtunji, Chiwachiwa na Londo utatekelezwa na Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Aidha, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara (TANROADS), inaendelea na maandalizi ya ujenzi wa daraja la Mngeta. Hadi sasa ukaguzi wa eneo la kujenga daraja umefanyika na taratibu za ununuzi ili kumpata mkandarasi wa kujenga daraja hilo ziko katika hatua za mwisho.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga swali la nyongeza.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nauliza kwa kifupi ili na wengine wapate nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, amesema upembuzi yakinifu unakamilishwa Juni, 2016 lakini kwa uhakika niliokuwa nao kwa sababu ni miaka sita niko Bungeni na hili swali nimekuwa nikiuliuliza na wamekuwa wakisema liko kwenye upembuzi yakinifu. Kama upembuzi yakinifu unachukua miaka sita, je, lini sasa mkandarasi atapatikana na ujenzi wa barabara hii utaanza lini? Maana ni muda mrefu mno nimezungumzia barabara hii na watu wanateseka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, wananchi wa Mlimba wanasikia maana nimewaambia, kwa kuwa Jimbo la Mlimba linaunganika na Mkoa wa Njombe, lakini amezungumzia barabara ya kwenda mpaka Mlimba hukuzungumzia barabara ya kutoka Mlimba - Madeke Njombe. Ni nini mpango

wa Serikali wa kujenga barabara hiyo ili wananchi wa Mlimba waunganike na wa Mkoa wa Njombe ili waweze kupata fursa za kimaisha na za kiuchumi?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza la Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga anahoji dhamira ya Serikali na mimi naomba kumthibitishia kwamba Serikali hii ya Awamu ya Tano ina dhamira ya dhati na itatekeleza ahadi zake zote zilizoko katika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2015 -2020. Tumepewa dhamana ya kusimamia ahadi zote ikiwa ni pamoja na kuzikamilisha shughuli zote ambazo zilikuwa zimeanza kutoka Serikali ya Awamu ya Nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili linahusu kuunganisha Mlimba pamoja na Mkoa wa Njombe kupitia Madeke. Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga kwamba hoja yake tutaishughulikia. Barabara hii pia imeombwa na watu wa Njombe upande ule mwingine na ipo katika mpango wa TANROADS Mkoa wa Njombe na tutahakikisha wanashirikiana na TANROADS Morogoro ili barabara hii tuikamilishe yote kwa pamoja. *(Makofi)*

Na. 57

Ex- Arusha Coffee Estate

MHE. CECILIA D. PARESSO (K.n.y. MHE. JOSHUA S. NASSARI) aliuliza:-

Shamba Na.112 (*Ex-Arusha Coffee Estate*) lililopo Nduruma Wilaya ya Meru lililokuwa likimilikiwa na *Tanzania Flowers Ltd.* lenye ukubwa wa ekari 721 lilishawahi kufutwa mwaka 2000 na hati ya utwaaji ardhi (*Deed of Acquisition*) ikasajiliwa 12/6/2001 na aliyekuwa Waziri wa Ardhi wa wakati huo, Mheshimiwa Gideon Cheyo lakini hadi leo wawekezaji hao bado wanazidi kuiza ardhi hiyo ambayo ilifutwa kwa ajili ya kuwagawia wananchi wenye shida ya ardhi:-

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya jambo hilo hasa ikizingatiwa kuwa Serikali ilishawahi kuwaambia wananchi wa maeneo hayo kuwa shamba hilo halimilikiwi na wawekezaji tena?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari, Mbunge wa Arumeru, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, shamba Na.112 lilikuwa na ukubwa wa ekari 721 na lilikuwa eneo la Nduruma, Wilaya ya Arumeru Mkoa wa Arusha. Tarehe 14/11/1990 shamba hili lilimilikiwa kwa *Tanzania Flowers Ltd.* ya Arusha na mnamo tarehe 8/8/1991 na tarehe 2/10/1991 kampuni hiyo ililigawa shamba hilo katika sehemu saba na kuwauzia watu sita tofauti baada ya kufuata taratibu zote za kisheria na sehemu moja yenye ekari 80 iliendelea kumilikiwa na *Tanzania Flowers Ltd.* Kampuni zilizouziwa zilipewa hati kutokana na hatimiliki mama yenye Na.7320 hili lilifanyika kwa kuzingatia kufungu cha Sheria Na. 83 na 88 cha Sheria ya Usajili wa Ardhi. Mgawanyo wa shamba hilo ulikuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 6/12/2011, Serikali iliamua kulitwaa eneo linalomilikiwa na *Tanzania Flowers Limited* lenye Hati Na. 7320 ambalo kwa wakati huo lilikuwa na ukubwa wa ekari 80. Utwaaji huu ulisajiliwa kwa Waraka Na.14316. Hivyo basi, ekari 80 zilitwaliwa kwa ajili ya matumizi ya wananchi, na ardhi hiyo ilisharudishwa kwa Halmashauri Halmashauri ya Arumeru ndiyo wanahusika katika ugawaji wa shamba hilo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Paresso swali la nyongeza.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa Wilaya ya Arumeru Mashariki kwa kiasi kikubwa ardhi yake inamilikiwa na wawekezaji na ni ukweli mara nyingi kumetokea migogoro kutokana na wananchi kuwa na mahitaji makubwa ya ardhi, na kwa kuwa mpaka sasa mnasema ni ekari 80 tu imerudi katika Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru, je, Serikali haioni sasa uko umuhimu wa kupitia mashamba hayo na kufanya tathmini upya ili wananchi hawa ambao wanahitaji ardhi waweze kupata ardhi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Mkoa mzima wa Arusha maeneo mengi pia ardhi yao imemilikiwa na wawekezaji ikiwemo Wilaya ya Karatu ninayotoka na kumekuwa na mgogoro mkubwa sana wa wananchi kuhitaji ardhi kwa sababu ardhi nyingi imemilikiwa na wawekezaji mfano Shamba la Tembo Tembo liloko Karatu. Je, Serikali sasa iko tayari kufika Wilaya

ya Karatu na kufanya tathmini ya kuwatambua wawekezaji ili wananchi waweze kupata ardhi yao? (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza ametaka kujua Serikali ina mpango gani katika kuyatambua mashamba yote haya na kufanya tathmini ili yaweze kugawiwa kwa wananchi. Naomba niseme kwamba mpaka sasa Waziri alishapeleka barua katika Mikoa yote ikiwataka kwanza wao wayatambue kwa sababu wanayafahamu, lakini mpaka sasa Wizara yangu imeshabaini mashamba 22 katika Mkoa wa Arusha ambayo tayari yameshabatiliswa kwa minajili ya kuja kuwagawia wananchi wenye shida ya maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili anazungumzia habari ya mgogoro na uhitaji wa ardhi katika eneo la Karatu. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mimi mwenyewe nilifika Karatu na migogoro hiyo niliambiwa na wakati huo nilikuwa nashughulikia masuala ya Mabaraza ya Ardhi. Hata hivyo, kwa sababu Wizara imeweka mpango mzuri kwa ajili ya kuweza kuyafikia maeneo yote kwa wakati, tunajaribu kukusanya migogoro yote na ndiyo maana tuliomba tuweze kuipata na tuko tayari kurudi tena Karatu kwa ajili ya kutatua mgogoro huo ambao anazungumzia. Kabla ya Bajeti ya Wizara kuisha, Wabunge wote watakuwa wamegawiwa vitabu na wataweza kubaini migogoro ambayo tumeiainisha ambayo tunatarajia kuanza kuitembelea baada ya Bunge hili kumalizika. Kwa sababu migogoro ya ardhi ni suala mtambuka na Wizara zingine zitahusika. Kwa hiyo, kila Mbunge ataona katika Mkoa au Wilaya yake ni migogoro ipi ambayo Wizara imeiainisha kwa ajili ya kuipatia ufumbuzi.

NAIBU SPIKA: Tuendeleo, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Musa Rashid Ntimizi aulize swali lake.

MHE. MUSA R. NTIMIZI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, na kabla ya kuomba kujibiwa swali langu namba 58 naomba marekebisho kidogo kwenye jibu la Wizara (a) mstari wa tatu, Makao Makuu ya Wilaya imeandikwa Isikizye, naomba isomeke Isikizya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya marekebisho hayo kwa niaba ya wananchi wa Igalula naomba swali namba 58 lipate majibu.

Na. 58

Kituo cha Polisi – Kata ya Loya

MHE. MUSA R. NTIMIZI aliuliza:-

Wananchi wa Kata ya Loya katika Halmashauri ya Tabora (Uyui) wameitikia wito wa Serikali wa ulinzi kwa kujenga kituo kikubwa cha polisi katika kata yao:-

(a) Je, ni lini kituo hicho kitafunguliwa hasa ikizingatiwa kuwa Loya ni zaidi ya kilometa 120 kutoka Makao Mkuu ya Wilaya Isikizya ambako ndiko kwenye kituo cha polisi?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaongezea bajeti ya mafuta ili kuwarahisishia watendaji kazi maana maeneo ya Jimbo ni kubwa na yote yanahitaji huduma za kipolisi?

WAZIRI MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Musa Rashid Ntimizi, Mbunge wa Igalula, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza kuwashukuru wananchi na wadau wote walihusika katika kuchangia ujenzi wa Kituo cha Polisi Kata ya Loya katika Halmashauri ya Tabora (Uyui). Pamoja na mwitikio huo bado kituo hiki hakijakamilika sehemu ya kuhifadha silaha, huduma ya choo na makazi ya askari. Pindi vitu hivi vitakapokamilika kituo hiki kitafunguliwa na askari watapelekwa. Hivyo basi, namuomba Mheshimiwa Mbunge kuendelea na jitihada za kuwahamasisha wananchi wa Kata ya Loya ili kukamilisha ujenzi huo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mpango wa kuongeza bajeti ya mafuta katika maeneo mbalimbali kulingana na upatikanaji wa fedha ili kukidhi mahitaji ya doria, misako na operesheni mbalimbali katika kutoa huduma ya ulinzi na usalama kwa wananchi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ntimizi swali la nyongeza.

MHE. MUSA R. NTIMIZI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Wananchi wa Jimbo la Igalula hususani Kata ya Loya na Halmashauri yetu imefanya kazi kubwa sana kujenga kituo hicho cha polisi na nguvu kwa sasa imetuishia na kazi kubwa imefanyika. Serikali kupitia Wizara haioni umuhimu wa kusaidia nguvu hizi za wananchi katika kumaliza kituo hiki cha polisi na kiweze kuanza kufanya kazi? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kata ya Igalula na Kata ya Kigwa kuna vituo vya polisi ambavyo vingeweza kutoa huduma katika Kata ya Loya kipindi hiki hatuna kituo kituo cha polisi katika Kata ya Loya. Tatizo letu kubwa lililopo pale katika vituo hivi viwili vya polisi havina usafiri. Je, Wizara haioni umuhimu wa kuvipa usafiri vituo hivi vya polisi ili viweze kuendelea kutoa huduma katika maeneo ambayo hayana vituo vya polisi? (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali bado inaendelea na juhudi zake za kuhakikisha kwamba inajenga vituo mbalimbali katika nchi yetu. Kwa hiyo basi, pamoja na juhudi zilizofanywa na wananchi, nimwombe Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na Serikali na kuona kwa namna gani tunaweza tukakamilisha kituo hiki. Nina uhakika kabisa wananchi kwa juhudi walizozifanya bado kuna nafasi ya kuendelea kushirikiana na Serikali ili kukamilisha ujenzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili amezungumzia tatizo la usafiri. Ni kweli vituo vingi havina usafiri lakini Serikali katika bajeti yake ya mwaka huu inajipanga kuhakikisha kwamba inanunua magari mengi ili kuweza kuvipatia vituo mbalimbali usafiri na tutaangalia kituo kimojawapo kati ya alivyovisema tutaweza kukipatia usafiri. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwijage.

MHE. SVELINA S. MWIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa kituo cha Chalinze ni kituo ambacho kiko kwenye barabara kuu ya kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma na kituo hicho hakina *computer* hata *photocopy* hakuna.

Kwa hiyo, ukipata tatizo wanaenda kutoa *photocopy* nje kwenye *stationery*. Ni lini Serikali itaona umuhimu wa kuwawekea *photocopy machine* ya kuwa wanatumia kuliko kusambaza nje siri za kituo hicho? (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tu Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo hilo alinipigia simu, tuliongea naye na hayo anayosema Mheshimiwa Mbunge tuliyazungumza. Kwa hiyo, asiwe na wasiwasi ajue kwamba na Mbunge wa Jimbo hilo ameshanieleza tatizo hilo na tutalitatu. (Makofi/Kicheko)

Na. 59

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM aliuliza:-

Moja ya majukumu ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa mujibu wa Ibara ya 130(c) ya Katiba ya nchi ni kufanya uchunguzi juu ya mambo yanayohusu uvunjaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora:-

Je, ni kwa kiasi gani Tume imefanikiwa kutekeleza jukumu hilo kwa kipindi cha mwaka 2010 - 2016?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora katika majukumu yake kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2010 - 2016 ilipokea na kuyachunguza jumla ya malalamiko 13,709. Kati ya malalamiko hayo, malalamiko 6,169 yalihitimishwa na malalamiko 7,540 yanaendelea kuchunguzwa. Mchanganuo wa malalamiko ni kama ifuatavyo:-

(i) Migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wawekezaji, wakulima na wafugaji, wananchi wa maeneo ya hifadhi;

(ii) Matumizi mabaya ya madaraka kwa watendaji;

(iii) Ukatili dhidi ya wanawake na watoto;

(iv) Ucheleweshwaji wa haki kwa mahabusu na wafungwa; na

(v) Matumizi ya nguvu kwa vyombo vya dola.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na taarifa hiyo, katika kipindi cha mwaka 2010 - 2016 Tume ilifanya tafiti kuhusu haki za watoto, ukatili dhidi ya watu wenye ulemavu wa ngozi, kutoa elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu na misingi ya utawala bora, kutembelea magereza na kufanya uchunguzi wa matukio ya uvunjwaji wa haki za binadamu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Masoud swali la nyongeza.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, nina maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, uvunjwaji huu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora inaathiri sana usalama wa raia na mali zao. Katika majibu ya Mheshimiwa Waziri amekiri na amesema kwamba mambo yaliyochunguzwa ni matumizi mabaya ya madaraka ya watendaji na matumizi ya nguvu ya vyombo vya dola.

Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri kile kinachoitwa Uchaguzi wa Marejeo kule Zanzibar na kubadilika kuwa Uchafuzi wa Makusudio, ni kwa kiasi gani Serikali ilifanya uchunguzi ikagundua udhalilishaji huu wa watu kupigwa bila hatia na kule Tumbatu nyumba zao kuchomwa moto? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, katika majibu ya Mheshimiwa Waziri amesema kwamba wametembelea magereza na kufanya uchunguzi wa kina. Naomba Mheshimiwa Waziri aniambie katika kutembelea magereza, wamefanya uchunguzi kiasi gani, wakafuatilia kiasi gani na wakagundua jambo gani pale ambapo Mashehe waliotoka Zanzibar waliopelekwa Tanzania Bara, waliofanyiwa vitendo vibaya, viovu, vichafu, vya kikatili na vya kishenzi walipolawitiwa. Tarehe 28 mimi nilikwenda kwenye Gereza la Segerea na wakasema kwamba hali yao ni mbaya na kinyesi chao hakizuiwi wanavuja mavi. *(Makofi)*

Je, tuambie Serikali hii, katika misingi ya uvunjaji wa haki za binadamu...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Masoud hilo ni swali la tatu sasa.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Hilo ni la pili.

NAIBU SPIKA: La pili umeshauliza...

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Sijauliza swali la pili.

NAIBU SPIKA: Kwa namna gani, kwa namna gani mara tatu, sasa hayo ni maswali mengi *already*. Kama unafuta hilo la pili basi uliza sasa hili lile la katikati ulifute. *(Makofi)*

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Mheshimiwa Waziri wakati unajibu umesema kwamba mlikwenda kwenye magereza na kufanya uchunguzi, ni kiasi gani mmegundua malalamiko yaliyoko kwenye magereza na hasa pale ambapo kuna malalamiko ya muda mrefu ya Mashehe waliotoka Zanzibar ambapo walilawitiwa, vitendo vichafu, viovu...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Masoud, tafadhali uliza swali, umeanza na je, malizia. Uliza swali tafadhali, hayo maelezo tumeshayasikia.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Waziri, ni kwa kiasi gani malalamiko haya ya vitendo hivi viovu, vichafu, vibaya, vya kishenzi na vya kinyama walivyofanyiwa Mashehe wetu mtavifuatilia kwa kina? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kazi yake kubwa ni kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi. Mheshimiwa Mbunge anaposema kumetokea udhalilishaji wa haki za binadamu za kupindukia, napenda kujua kama hayo masuala malalamiko yalipelekwa kwenye Tume kwa sababu nachozungumzia hapa ni Tume ya Haki za Binadamu na jinsi ninavyojibu ni malalamiko ambayo yametolewa na wananchi. Kama nilivyosema kati ya mwaka 2010 mpaka mwezi huu ninapongea Tume imepokea na kushughulikia zaidi ya 13,709. Sasa kama hiyo ni mojawapo taarifa ya Tume nitaletewa na nitakuja kuiweka hapa Mezani kama Katiba inavyonitaka chini ya Ibara ya 131 (3). *(Makofi)*

Na. 60

Kuzifanyia Marekebisho Sheria zenye Mapungufu

MHE. FATMA H. TOUFIQ aliuliza:-

Baadhi ya sheria ikiwemo Sheria ya Mirathi ya Kimila, Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 pamoja na Sheria ya Hali za Watu zimekuwa na mapungufu makubwa na hivyo kuhitaji kutazamwa upya ili kufanyiwa marekebisho:-

Je, Serikali ina nia gani ya dhati ya kuwasadia wanawake na watoto wa kike kwa kuzifanyia marekebisho sheria hizo kandamizi na za kibaguzi hasa

ikizingatiwa kuwa nchi yetu imeridhia mikataba mbalimbali ya Kimataifa na ya kikanda juu ya masuala ya kuondoa ukatili na unyanyasaji dhidi ya wanawake na watoto?

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina nia ya dhati kabisa ya kizifanyia marekebisho Sheria ya Ndoa na zile zinazosimamia mirathi na urithi. Katika kutekeleza nia hiyo, mwaka 2008 Wizara iliandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri wenye mapendekezo ya kufanya marekebisho katika Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 na mapendekezo ya kutunga Sheria mpya ya Mirathi na Urithi. Baraza la Mawaziri ililiagiza Wizara ya Katiba na Sheria kuandaa Waraka Maalumu wa Serikali (*White Paper*) kwa ajili ya kukusanya maoni ya wananchi wengi iwezekanavyo kuhusu sheria hizo mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia agizo hilo, Wizara iliandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri wa utekelezaji wa maamuzi ya Baraza la Mawaziri kuhusu kukusanya maoni ya wananchi juu ya marekebisho ya Sheria ya Ndoa na kutungwa kwa Sheria mpya ya Mirathi na Urithi. Waraka huo ulifikishwa katika Baraza la Mawaziri mwezi Machi, 2010. Pamoja na kubainisha hoja ambazo wananchi wangetakiwa kuzitolea maoni, Waraka huo pia uliainisha utaratibu wa kukusanya maoni ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Disemba, 2010 kabla ya Waraka huo haujadiliwa na Baraza la Mawaziri, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa wakati huo, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete aliridhia kuanza kwa mchakato wa Mabadiliko ya Katiba na aliahidi kuunda Tume itakayokuwa na majukumu ya kukusanya maoni ya wananchi juu ya Mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza azma ya Rais, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilitunga Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Sura ya 83 ambayo ilisainiwa na Rais tarehe 29 Novemba, 2011. Sheria hii ndiyo iliyounda Tume ya Mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuundwa kwa Tume ya Mabadiliko ya Katiba mchakato wa kuandaa Waraka Maalumu wa Serikali (*White Paper*) kwa ajili ya kukusanya maoni ya wananchi kuhusu marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 na mapendekezo ya kutungwa Sheria mpya ya Mirathi

na Urithi ulisitishwa kwa muda. Serikali ilikuwa na matarajio kuwa wakati Tume ya Mabadiliko ya Katiba inakusanya maoni ya wananchi kuhusu mabadiliko ya Katiba huenda wananchi vilevile wangetoa maoni yanayohusu Sheria ya Ndoa na Sheria ya Mirathi na Urithi.

Baada ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba kukamilisha kazi yake imebainika kwamba maoni ya wananchi hayakujielekeza kwenye maudhui ya Sheria ya Ndoa na Sheria ya Mirathi na Urithi kama ilivyotarajiwa. Hivyo basi, Wizara ya Katiba na Sheria imeamua kuendeleza juhudi zake za awali kwa kukamilisha taratibu kuhusu kupata maoni ya wananchi juu ya marekebisho ya Sheria ya Ndoa na kutungwa kwa Sheria mpya ya Mirathi na Urithi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Toufiq swali la nyongeza.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa Serikali haijaanza kupokea maoni, je, imepangaje kushirikisha wanawake wengi zaidi katika kutoa maoni yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, Wizara itaanza lini maandalizi ya kuchukua maoni hayo? Ahsante! (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pamoja na Tume ya Kurekebisha Sheria imepanga kulifanya zoezi hili kama tulivyoelekezwa mwanzoni kwa kina na kwa kuwafikia wananchi wengi kadri iwezekanavyo na ndiyo sababu ya Baraza la Mawaziri kusema tusileta mabadiliko hapa bila kutumia utaratibu wa *white paper* ambao una lengo la kuwafikia wananchi wengi iwezekanavyo.

Kwa hiyo, tutahakikisha wanawake wengi iwezekanavyo tunawafikia na natoa wito kwa wananchi wote na wanawake wote Tanzania pale watakaposikia mchakato umeanza naomba wajitokeza kutoa maoni kuhusu sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuhusu maandalizi yanaanza lini, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Fatma Toufiq kwamba maandalizi yalishaanza na sasa hivi tunapitia nyaraka zote za mwanzo ziendane na hali halisi ya leo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Janet Mbene.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika sana kuwa masuala mengi yanayohusiana na mambo ya wanawake yanatafutiwa kila sababu yasifanyike yakakamilika. Tunataka kupata majibu ni lini sasa hizi sheria zitapitiwa na zilete majibu yanayotakiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake ni zaidi ya asilimia 51 ya nchi hii lakini mambo yao yanapigwa danadana kila siku. Tunataka hili jambo likamilishwe sasa, lilikuwa lisingoje Katiba kwa sababu ni la miaka mingi kabla hata ya Katiba. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilikuwa na dhamira njema kutumia mtindo wa *white paper* badala tu ya kupokea mapendekezo kutoka Wizara ya Katiba na Sheria ili wananchi wengi iwezekanavyo waweze kushiriki kwenye zoezi hili. Kama nilivyoeleza kwenye majibu yangu ya awali ni kwamba kipindi hicho ambacho tulitakiwa sisi tutumie utaratibu wa *white paper* ndiyo kipindi ambacho kulikuja pia mchakato wa Katiba Mpya ambao ulitutaka sasa tuwafikie wananchi wengi na ni gharama ambayo tusingeweza kuibeba kwa pamoja, huku tunafanya usahili kuhusu masuala ya Katiba Mpya na huku tunaendelea na masuala ya *white paper* kuhusu huo mchakato wa kubadilisha sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Janet Mbene, Serikali imefanya makubwa mno kuleta mabadiliko ya hali ya wanawake Tanzania. Mwaka 1999, naomba nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge, Serikali ilifanya maamuzi makubwa kwa sheria zake mbili za ardhi, Sheria Na.4 na 5 kuhakikisha kwamba mwanamke hadhaliliki tena katika kumiliki na kutumia ardhi. Sasa hivi mwanamke ana haki sawa kabisa na mwanaume.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile katika Mkutano huu tunaleta Muswada wa Sheria utakaohakikisha watoto wetu wote wanaosoma shule za msingi na sekondari wasiweze kukatisha masomo yao kutokana na masuala haya ya ndoa za mapema. Muswada huo utakuwa ni *miscellaneous amendment*, ambao utaleta mabadiliko kwenye Sheria ya Elimu ambapo watoto wote wa shule za msingi na sekondari hawataruhusiwa kuolewa, hawataruhusiwa kuoa ili wafaidi fursa iliyojitokeza chini ya Serikali ya Awamu ya Tano ya elimu bure kwa wote na wote ni mashahidi hapa jinsi ambavyo

wananchi na watoto wengi wameitikia fursa hii ya elimu bure na tunataka na watoto wa kike nao wafaidike *as much as possible*. Ahsante sana. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo...

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika, Mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Naomba ukae Mheshimiwa, nikiwa nimesimama huwezi kusimama. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo machache hapa. Tangazo la kwanza ni la Kikao cha Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mwenyekiti wa Kamati hii anaomba Wajumbe wakutane saa saba mchana, Jengo la Utawala, chumba namba 227.

Tangazo lingine ni kikao cha Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Makamu Mwenyekiti anaomba mkutane saa saba mchana, Jengo la Utawala, chumba namba 229.

Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni wengi sana huko kwenye *gallery*, lakini sijaletewa hapa tangazo la wageni, kwa hiyo, tutaendelea.

Waheshimiwa Wabunge, kuna mambo matatu. La kwanza ni kuhusu Mwongozo ulioombwa na Mheshimiwa Bashe kuhusu usahihi wa Wabunge wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kulipwa posho na mishahara wakati hawashiriki na kutimiza wajibu wao wa kuchangia kwenye mjadala wa Bunge la Bajeti.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Yule timu Lowassa. (Kicheko)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sugu, tafadhali!

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mwongozo.

Katika Kikao cha Tano, Mkutano wa Tatu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mnamo tarehe 25 Aprili, 2016, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, alisimama akitumia Kanuni ya 68(7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 kuomba Mwongozo wa Naibu Spika kuwa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeamua kutokushiriki mjadala lakini Wabunge wa Kambi hiyo wanasaini na kulipwa mishahara. Hivyo, aliomba mwongozo endapo ni haki na ni sahihi kwa Wabunge hao kupokea posho wakati hawashiriki na kutimiza wajibu wao wa kikatiba na kisheria.

Katika kujenga hoja yake Mheshimiwa Bashe alitumia Ibara ya 63(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ambayo inasomeka kama ifuatavyo; "Kwa madhumuni ya utekelezaji wa madaraka yake Bunge laweza:-

(b) Kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa kila mwaka wa Bajeti."

Aidha, Mheshimiwa Bashe alitumia Ibara ya 73 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1977 kufafanua kuhusu malipo ya mshahara, posho na malipo mengine kwa Wabunge. Ibara hiyo inasomeka kama ifuatavyo; "Wabunge wote wa aina zote watahika madaraka yao kwa mujibu wa Katiba hii, na watalipwa mshahara, posho na malipo mengine kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge."

Jambo linalohitaji kujibiwa katika hoja ya Mheshimiwa Bashe ni, je, ni haki na ni sahihi Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kupokea posho wakati hawashiriki na kutimiza wajibu wao wa kikatiba na kisheria?

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 73 imeainisha masharti ya kazi ya Mbunge. Masharti ya kazi ya Mbunge yameeleza kwamba Mbunge ana stahili kulipwa mshahara kwa kila mwezi. Aidha, masharti hayo yametoa ufafanuzi kuwa, Mbunge anapohudhuria vikao vya Bunge na Kamati zake atalipwa posho ya vikao kwa kiwango kitakachowekwa na Serikali kwa kuzingatia Sheria ya Fedha za Umma na Kanuni zake na Masharti ya Kanuni za Bunge kuhusu vikao. (Makofi)

Malipo ya mshahara kwa Mbunge ni suala la kikatiba na kisheria. Malipo hayo hulipwa kwa Mbunge kutokana na kazi yake ya Ubunge kama ilivyotajwa katika Ibara ya 73 ya Katiba. Malipo ya posho kwa Mbunge yameanzishwa kwa mujibu wa Katiba na pia yamewekwa katika Sheria ya Uendeshaji wa Bunge, Sura Na.115, chini ya kifungu cha 19. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, utaratibu unaotakiwa kuzingatiwa umefafanuliwa kwenye Waraka wa Rais wenye Masharti ya Kazi ya Mbunge yalioanza kutumika tarehe 25 Oktoba, 2010 na marekebisho yake ya tarehe 11 Juni, 2012 ambayo kwa pamoja yanaeleza kwamba Mbunge anapohudhuria vikao vya Bunge na Kamati zake atalipwa posho ya vikao kwa kiwango kitakachowekwa kwa kuzingatia Sheria ya Fedha, Kanuni zake na Masharti ya Kanuni za Mbunge kuhusu vikao.

Kwa maelezo hayo, malipo ya posho kwa Wabunge yanatokana na mahudhuria yao Bungeni na siyo kuchangia kama ambavyo wengi wetu tungenda itokee. *(Makofi)*

WABUNGE FULANI: Huyoooo.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane.

Kimsingi kuhudhuria Bungeni pekee si njia inayopendeza kwa kuwa Mbunge anapofika Bungeni anatarajiwa atekeleze majukumu yake ya Kikatiba kama yalivyoainishwa katika Ibara ya 63. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tabia hii haikubaliki na haistahili kuendelea. Badala ya Mbunge kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Katiba anahudhuria Bungeni ili tu alipwe posho. *(Makofi)*

Aidha, katika Mkutano huu Bunge lina jukumu zito la kujadili utekelezaji wa kila Wizara na Wabunge wote wanao wajibu wa kuchangia makadirio ya matumizi ya Serikali. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Tumewaachia Bunge lenu.

MBUNGE FULANI: Tokeni, Wabunge hewa.

NAIBU SPIKA: Kanuni ya 99 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, michango ya Wabunge ni muhimu kwa kuwa kupitia michango yao Wabunge wanatoa usimamizi mzuri wa shughuli za Serikali ambazo ni muhimu sana katika kuwaletea wananchi maendeleo.

Waheshimiwa Wabunge, nichukue fursa hii kuwataka Wabunge wote kuwa wazalendo kwa nchi yetu na kushiriki kikamilifu katika kuchangia bajeti iliyopo mbele yetu jambo ambalo ninaamini ndicho tulichotumwa na wananchi. Tabia ya kuhudhuria Bungeni kwa ajili ya kulipwa posho bila ya kuitolea jasho inabidi iachwe. *(Makofi)*

Vilevile ipo haja ya siku zijazo kurekebisha sheria tulizonazo ili kukabiliana na hali ya namna hii ili kuweka... *(Makofi)*

WABUNGE FULANI: Unakibeba chama chako.

(Hapa baadhi ya Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbilinyi tafadhali, mara ya pili.

Nadhani ipo haja ya siku zijazo kurekebisha sheria tulizonazo ili kukabiliana na hali ya namna hii ili kuweka utaratibu mahsusi utakaoweza kila Mbunge kulipwa posho baada ya kutekeleza majukumu yake ipasavyo na siyo kuandika kuhudhuria katika mkutano na vikao pekee. Huo ndiyo Mwongozo wangu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilisema yako mambo matatu, hilo ni la kwanza.

Jambo lingine nililotaka kutoa maelezo kidogo ni jambo ambalo tunalikuta katika Kanuni ya 64 ambayo inahusu mambo yasiyoruhusiwa Bungeni. Kanuni ya 64(1)(g) kinasema; "Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge:-

(g) hatatumia lugha ya kuudhi na inayodhalilisha watu wengine."

Waheshimiwa Wabunge, nimelazika kutoa maelezo haya kwa sababu ya lugha iliyotumika dhidi ya Mashehe ambao mpaka sasa hivi wako chini ya vyombo vya sheria. *(Makofi)*

Inawezekana kabisa lengo la Mbunge aliyekuwa akiuliza swali la nyongeza ilikuwa ni kwa ajili ya kuwatetea Mashehe hawa lakini mambo ambayo wao wamefanyiwa kama wanadamu na kama wamefanyiwa ni udhalilishaji kuyasema kwa namna yalivyosemwa na kwa lugha iliyotumika. *(Makofi)*

WABUNGE FULANI: Aaaaah.

NAIBU SPIKA: Sababu ni kwamba mambo ambayo anafanyiwa binadamu kama ambavyo mwingine ugonjwa wake asingependa kuutaja hata yule ambaye ametendewa jambo la kudhalilisha asingependa watu wengine walijue ili aweze kuendelea kuheshimika katika jamii. *(Makofi)*

(Hapa baadhi ya Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema jambo hilo, lingine ambalo nimeletewa taarifa ni lile lililoko katika Kanuni ya 66 kuhusu staha ndani ya Bunge. Zimekuwepo nyakati mbalimbali Waheshimiwa Wabunge tumekuwa hatuifuati Kanuni hii, nawakumbusha pia ninyi mkaisome na mimi

nitaisoma kwa haraka, kinasema; "(1) Wakati wa Vikao vya Bunge, Spika anapokuwa anaingia au kutoka katika Ukumbi wa Bunge, Wabunge na wageni wote waliopo katika ukumbi huo watasimama kwa utulivu mahali pao na kubaki kimya hadi Spika atakapokuwa ameketi katika Kiti chake au atakapokuwa ametoka kwenye ukumbi wa Bunge.

(2) Wakati Bunge linaingia kwenye Kamati ya Bunge Zima au katika Kamati ya Matumizi, Wabunge na wageni wote waliopo kwenye Ukumbi wa Bunge watasimama kwa utulivu mahali pao na kubaki kimya ili kutoa heshima kwa mchakato wa Bunge kuingia katika Kamati ya Bunge Zima au kwenye Kamati ya Matumizi na baadaye Bunge kurejea.

(3) Mbunge aliyepo Bungeni wakati wa mjadala atatakiwa; (a) Kuingia au kutoka kwenye ukumbi wa Bunge kwa staha na atainamisha kichwa kuelekea kwa Spika au kufanya mkunjo wa magoti kwa heshima, kila mara Mbunge huyo atakapokuwa akienda au kutoka mahali pake;

(b) Kutulia na kukaa kwa heshima mahali pake na hatatangatanga kwenye ukumbi wa Mikutano bila sababu;

(c) Kutopita kati ya Kiti cha Spika na Mbunge anayesema;

(d) Kutosoma kitabu chochote, gazeti au barua, isipokuwa kama vitu hivyo vinahusu shughuli za mjadala unaoendelea wakati huo; na

(e) Kuzima simu ya mkononi na kwa namna yoyote kutokutumia simu."

Waheshimiwa Wabunge, nimeagizwa niwakubushe Kanuni hiyo ya 66 na kwa kuwa nakala wote tunazo tuendeleo kuisoma ili tulinde staha ya Bunge. Katibu.

WABUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

NDG. NENELWA M. WANKANGA – KATIBU MEZANI: Hoja za Serikali kwamba, Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu...

WABUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Katibu naomba ukae. Mheshimiwa Mwalimu pale nyuma.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba mwongozo kwa Kanuni ya 68(7) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 44(4). Kwanza Kanuni ya 44 peke yake naomba niisome, inasema; "(1) Maswali ya nyongeza yanaweza kuulizwa na Mbunge yeyote kwa madhumuni ya kupata ufafanuzi zaidi juu ya jambo lolote lililotajwa katika jibu lililotolewa.

(4) Isipokuwa kama Spika ataelekeza vinginevyo, Wabunge watakaouliza maswali ya nyongeza hawatazidi watatu kwa swali moja la msingi na Mbunge hataruhusiwa kusoma swali lake." (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge limeshuhudia leo maswali yakipita bila maswali ya nyongeza. Utaratibu huu ukiendelea, unawanyima Wabunge haki ya kuuliza masuala yanayohusiana na Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako, kuendelea kutotoa ruhusa kwa Wabunge kuuliza maswali ya nyongeza, Serikali inakwepa kuulizwa maswali? Naomba Mwongozo wako. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ally Saleh.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nataka nipitie Kanuni ya 46 kupitia Kanuni ya 68(7) inayohusu Waziri kutojibu swali ambalo limeulizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la Mashehe limeulizwa hapa na sifikiri kama Waziri anayehusika amelijibu swali hilo vya kutosha. Kwa kuwa swali hili limekuwa likija mara nyingi na kama unavyoona ni swali ambalo liko hadharani sana na hawa Mashehe wako katika magereza kwa miaka mitatu mpaka leo kesi yao haijaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako labda utusaidie kupitia Waziri wa Mambo ya Ndani atuelezee hatua iliyofikiwa kuhusiana na kesi ya Mashehe hawa na Bunge liarifiwe kwa sababu ni *public case*, ni miaka mitatu hawajafikishwa Mahakamani mpaka leo na Waziri aliyeulizwa alishindwa kujibu swali hilo. Naomba Mwongozo wa Spika. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Esther Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nilikuwa naomba Mwongozo wako kufuatia majibu ya Mwongozo ambayo umeyatoa

na ni mazuri sana. Wakati tukisubiria hiyo sheria kutungwa, ni kwa nini sasa tusiweke utaratibu Wabunge ambao tunahudhuria humu ndani tuhakikishe tunaitendea haki nchi yetu kwa kuchangia maana kuna Wabunge zaidi ya asilimia 80 wanaingia ndani wanaishia kuzunguka kwenye viti tu na kuondoka hawachangii chochote. Sasa wakati tukisubiria hiyo sheria, naomba kabisa walau tuwe tunatumia *Hansard* kuwalipa Wabunge ambao wanakuwa wameongea humu Bungeni. Ahsante sana. (Makofi/Kicheko)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lema.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mwongozo wangu unahusu hii Kanuni ya 139, Wageni Bungeni, hususan Kanuni ya 2(b), inasema; Wageni wanapaswa wawe wamevaa mavazi ya heshima."

Mheshimiwa Naibu Spika, dada zetu ambao huwa mara nyingi wanakuja Bungeni wakiwa wamevaa *mini skirt* huwa wanarudishiwa getini kwa *embarrassment* lakini humu ndani kwenye *Speaker Gallery* kuna dada mmoja nafikiri ni Msingapore ama Mchina, *I don't know clearly*, lakini amevaa *proper mini skirt* na amepita getini. (Makofi)

Sasa mimi nataka niulize, je, Wazungu wanaruhusiwa, Wachina wanaruhusiwa lakini watu wengine hawaruhusiwi? Kanuni ya 139 inasema, wageni wanapaswa wawe wamevaa mavazi ya heshima, je, Wazungu mnawaogopa? (Makofi/Kicheko)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa Mwongozo na Wabunge wanne hapa. Nianze na Mwongozo ulioombwa mara ya mwisho na Mheshimiwa Lema kuhusu Kanuni ya 139(2)(b).

Waheshimiwa Wabunge, hapa kwenye hii Kanuni haijataja kwamba ni urefu ama ufupi wa nguo, isipokuwa Kanuni imesema wanapaswa wawe wamevaa mavazi ya heshima. Mpimaji wa vazi la heshima ni yule anayemruhusu huyu mgeni kuingia na kutoka. (Makofi)

WABUNGE FULANI: Aaaaaah. (Kicheko)

NAIBU SPIKA: Kwa hiyo, ikiwa yeye amepima akaona hilo ni vazi la heshima kwa huyo mgeni aliyeruhusiwa kuingia, huo ndiyo Mwongozo wangu, yeye ndiye anayepima. (Makofi)

WABUNGE FULANI: Wanawaogopa.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Mwongozo mwingine ulioombwa ni wa kulipa Wabunge kwa kutumia *Hansard* ili wale ambao wanakuwa hawajachangia wasilipwe.

Waheshimiwa Wabunge, katika Mwongozo nilioutoa nimesema hivi, tutatafuta namna ya kubadili sheria na pengine tuziangalie upya Kanuni zetu ili Wabunge waweze kuwajibika. Wakati wa mchakato huo, Wabunge mtapata fursa ya kutoa mawazo yenu, kwa hiyo, mawazo ya Mheshimiwa Esther yataweza kuchukuliwa wakati huo. Huo ndiyo Mwongozo wangu kwenye jambo hilo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mwongozo mwingine umeombwa kupitia Kanuni ya 46 kuhusu ukamilifu wa majibu yanayotolewa. Kwa hili, nitaangalia majibu ya Mheshimiwa Waziri kwenye *Hansard* na swali lililokuwa limeulizwa halafu mwongozo wake utatolewa wakati huo.

Waheshimiwa Wabunge, mwongozo wa kwanza ulikuwa umeombwa kuhusu Kanuni ya 44(4) inayosema; "Isipokuwa kama Spika ataelekeza vinginevyo, Wabunge watakaouliza maswali ya nyongeza hawatazidi watatu kwa swali moja la msingi na Mbunge hataruhusiwa kusoma swali lake."

Waheshimiwa Wabunge, unaposoma Kanuni ya 44, unapaswa usome na Kanuni ya 43, nitaisoma, Kanuni ya 43(1) inasema hivi; "Muda wa Maswali Bungeni utakuwa dakika tisini, isipokuwa katika Mkutano wa Bunge la Bajeti, ambapo muda utakuwa dakika sitini."

Waheshimiwa Wabunge, maana yake ni kwamba tunapoanza maswali saa 03.00 asubuhi tunatakiwa kumaliza maswali saa 04.00 asubuhi. Pia anayepanga idadi ya maswali ni Spika na ipo kwenye Kanuni hiyohiyo ya 43(2) inasema; "Spika anaweza kuweka kiwango cha juu cha maswali yatakayowekwa katika Orodha ya Shughuli ambayo anaona yanaweza kujibiwa katika muda uliowekwa."

Waheshimiwa Wabunge, muda uliowekwa ni saa moja, maswali yako kumi, kila swali dakika sita. Pale ambapo mwenye swali lake akiuliza maswali marefu maana yake dakika sita zake anakuwa kazimaliza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mimi niwaombe tutumie tu ule utaratibu wa kawaida. Kama kuna tatizo Jimboni kwako, peleka swali ili Wizara ijibu kikamilifu swali la kwako wewe, hili swali la nyongeza hutegemea Spika amepanga maswali mangapi kwa siku hiyo na muda tumeutaja wenyewe kwenye Kanuni

ni saa moja. Kwa hiyo, siwezi kuzidisha muda wala kupunguza kazi ambayo Mheshimiwa Spika ameipanga kwenye *Order Paper*. (Makofi)

Baada ya kuyasema hayo naomba tuendelee, Katibu.

NDG. NENELWA M. WANKANGA: Hoja za Serikali kwamba Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Majadiliano yanaendelea.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, samahani kabla hatujaendelea, sasa nimeletewa orodha ya wageni, naomba niwasome kwenu.

Wageni walioko Jukwaa la Spika ni Ndugu Peter Ilomo, Katibu Mkuu Ikulu; Engineer Mussa Iyombe, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais (TAMISEMI); Dkt. Laurean Ndumbaro, Katibu Mkuu Utumishi na Utawala Bora; Kuna Bi. Suzan Mlawi, Naibu Katibu Mkuu Utumishi na Utawala Bora; Dkt. Deodatus Mtasiwa, Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI (Afya); Ndugu Bernard M. Makali, Naibu Katibu Mkuu - TAMISEMI (Elimu); Ndugu Gerson Mdemu, Karani wa Baraza la Mawaziri na Ndugu Valentino Mlowola, Mkurugenzi Mkuu TAKUKURU. (Makofi)

Viongozi hawa wameambatana pia na viongozi wa taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Utawala Bora na TAMISEMI. (Makofi)

Mgeni wetu mwingine ni Jaji Francis Mutungi, Msajili wa Vyama vya Siasa Nchini. (Makofi)

Wageni waliopo jukwaa la wageni, kundi la kwanza ni wageni tisa wa Mheshimiwa Ummu Mwalimu, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kutoka Mtandao wa Mashirika ya Wazee wakiongozwa na Ndugu Sebastian Bulege ambaye ndiye Mwenyekiti wa Mtandao huo, karibuni sana. (Makofi)

Wageni 20 wa Mheshimiwa Antony Mavunde, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Walemavu kutoka Tanzania Youth Vision Association ya Dar es Salaam, karibuni sana. (Makofi)

Wageni sita wa Mheshimiwa Profesa Norman Sigalla King kutoka Chama cha Wasafirishaji Tanzania wakiongozwa na Ndugu Zakaria Hans Poppe, huyu ni Rais wa Chama cha Wasafirishaji Tanzania. (Makofi)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka kutoka Jimbo la Muleba Kusini wakiongozwa na Ndugu Kagem Tibaijuka. (Makofi)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Saumu Heri Sakala, Munge wa Viti Maalum, wakiongozwa na Ndugu Ally Shehekombo. (Makofi)

Wageni wengine ni wageni watano wa Mheshimiwa Doto Biteko kutoka Jimboni kwake Bukombe wakiongozwa na Ndugu Paul Bendera. (Makofi)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Ahmed Shabiby ambao ni Ndugu Ebenezer Msuya na Ndugu Amosi Oyombo. (Makofi)

Wageni ambao wapo kwa ajili ya mafunzo Bungeni, kuna wageni tisa wa Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum ambao ni wanafunzi kutoka UDOM. (Makofi)

Wageni wengine ni wanafunzi 30 na walimu wao kutoka Chuo cha Madini Dodoma. (Makofi)

Wengine ni wanafunzi 32 kutoka Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Dar es Salaam. (Makofi)

Wageni wengine ni wageni 20 wa Mheshimiwa Zainab Katimba, Mbunge wa Viti Maalum. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza kwa wageni, Katibu.

Naambiwa kuna orodha ya wageni wengine wanatoka Singapore, mmoja ni Koh Poh Koon, *Minister of State - Trade and Industry* toka Singapore. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, mniwie radhi, naomba nisome kwa kiingereza kwa ajili ya kuokoa muda maana hawa wageni wameandikwa vyeo vyao kwa Kiingereza. Mheshimiwa Tan Puay Hiang, *Singapore's High Commissioner to Tanzania*; Teo Siong Seng, *Chairman, Singapore Business Federation and Managing Director, Pacific International Lines*; Wan Chee Foong, *Head Group Business Development & Group Commercial Development, PSA*; Vigneswaran Sellakannu, *Assistant Vice President - Group Business Development (Africa)*; Rahul Ghosh, *Divisonal Director, IE Singapore*; Pung Wan Qing, *Senior Assistant Director, Ministry of Trade and Industry*; Bridget Shoo, *Assistant Director, Ministry of Trade and Industry*; Koh Jit Wei, *Assistant Director, Ministry of Trade and*

Industry; and Vinod Ashvin Ravi, Country Officer, Ministry of Foreign Affairs. (Makofi)

Wageni wengine ni *Engineer Joseph Malongo, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. (Makofi)*

Mgeni mwingine ni Balozi Mbelwa Kairuki, Mkurugenzi Idara ya Asia na Australasia, Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa. Huyu ni shemeji yetu. *(Makofi/Kicheko)*

Mwingine ni Ally Suleiman Ali, Afisa Mambo ya Nje, Idara ya Asia na Australasia, Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Katibu.

NDG. NENELWA M. WANKANGA: Hoja za Serikali kwamba Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Majadiliano yanaendelea.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017 – Ofisi ya Waziri Mkuu

(Majadiliano yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tulimaliza kuchangia siku ya Jumatatu kwa hiyo muda huu tutamkaribisha mtoa hoja ili aweze kuhitimisha hoja yake. Lakini nimeletewa taarifa hapa kwamba kabla Waziri Mkuu hajaja kuhitimisha hoja yake, atakuja Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu ili aanze kujibu baadhi ya hoja zenu Waheshimiwa Wabunge halafu baadaye atafuatiwa na Waziri Mkuu. Mheshimiwa Jenista. *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia Waheshimiwa Wabunge wote uzima na afya njema kiasi cha kutuwezesha kukutana tena leo katika ukumbi huu kwa majukumu yetu ya Kibunge lakini kwa manufaa ya Watanzania wote ambao tunawawakilisha ndani ya Bunge hili kwa ujumla wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Meza na Kiti chako ili kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge zinazohusiana na Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu toka nilipoteuliwa na Mheshimiwa Rais wetu kwa wadhifa huu wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia mambo ya Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kunipa dhamana hii kubwa. Naamini kabisa kwamba sote tunafahamu uzito wa majukumu ya kuwatumikia wananchi na umma mzima wa Watanzania. Naahidi kwamba nitajitahidi kutenda kazi zangu zote kwa moyo wote ili kuleta maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kwa dhati kabisa nimshukuru sana Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushirikiano mkubwa na miongozo mbalimbali anayonipa katika kutekeleza majukumu yangu ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu katika kipindi hiki kifupi cha Serikali ya Awamu ya Tano. Toka nimeingia madarakani nimeona kwa kweli Mheshimiwa Waziri Mkuu amesheheni umakini mkubwa wa uongozi na uongozi usioyumba katika kusimamia, kufuatilia masuala ya msingi yanayohusu maslahi ya umma. Ni mchapakazi na ni muadilifu katika uongozi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kwa dhati niwashukuru sana Manaibu Waziri wawili, Mheshimiwa Mavunde na Mheshimiwa Dkt. Possi kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Nimeamini hawa Naibu Mawaziri wawili kwa kweli ni vijana ambao ni ma-caterpillar wenye uwezo mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru pia Makatibu Wakuu wote, Wakurugenzi na viongozi wa taasisi mbalimbali ambazo ziko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi kubwa na ushirikiano ambao wamekuwa wakinipa katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati pia niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Peramiho kwa kunichagua lakini kwa kuendelea kuniunga mkono katika utekelezaji wangu wa majukumu haya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hii ambayo inanifanya leo kuja kuhitimisha hoja hii mbele yako isingeweza kufikia mahali hapa kama si Wajumbe wa Kamati mbili za Kudumu za Bunge ambao walifanya kazi ya umakini katika kupitia mapendekezo ya bajeti yetu na kuifanya bajeti hii iweze kuja hapa mbele yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, Ndugu yangu Mheshimiwa Mchengerwa na Naibu wake dada yangu Mheshimiwa Giga na Wajumbe wote wa Kamati ya Katiba na Sheria kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia wakati wa kuchambua bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya UKIMWI wakiongozwa na Mheshimiwa Mwenyekiti Hasna Mwilima na Makamu wake Mheshimiwa Kanyasu na Wajumbe wote kwa kazi kubwa waliyoifanya na ushirikiano mkubwa waliotupatia katika kuhakikisha kwamba tunafanikiwa katika kazi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe mwenyewe umejidhihirisha kwamba umekuwa kiongozi mahiri wa kuliongoza Bunge letu pamoja na Wenyeviti wa Bunge na Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Bunge. Kwa niaba ya Ofisi ya Waziri Mkuu, napenda niwapongeze, niwashukuru na niwatakie kila la kheri katika kutekeleza majukumu haya mazito wakiwemo Makatibu wanaotuhudumu katika Kamati mbalimbali za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(2) ya Kanuni za kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 inayohusu kujadili utekelezaji wa bajeti za Wizara, naomba sasa kwa heshima na taadhima uniruhusu nitoe ufafanuzi katika maeneo mbalimbali ambayo Waheshimiwa Wabunge waliyachangia na kutaka kupata ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachukua maeneo machache na maeneo mengine Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuja mbele hapa leo wakati wa kuhitimisha hoja hii basi atayatolea ufafanuzi wa kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapokwenda kutoa ufafanuzi wa maeneo haya, nawashukuru sana Wabunge wote waliochangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na hasa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi ambao walishiriki kikamilifu na kwa ufanisi katika kuchangia mapendekezo ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zake kwa mwaka wa huu wa fedha wa 2016/2017. Niwahakikishie tulikuwa wasikivu na tumeyachukua maoni na ushauri wenu na kama yote hayatajibiwa ipasavyo hapa basi Ofisi yangu itafanya utaratibu wa kuyajibu kwa maandishi na Waheshimiwa Wabunge mtaweza kuyapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kujibu hoja hizi pia kwa niaba ya Ofisi ya Waziri Mkuu, nitoe pole sana kwa maeneo mbalimbali katika nchi yetu ya Tanzania waliokumbwa na maafa ya mafuriko. Tumekuwa tukishuhudia

katika Bunge letu na sehemu nyingine, maeneo mbalimbali katika nchi yetu ya Tanzania yamekumbwa na mafuriko makubwa na Watanzania wengi wamejikuta wakihangaika na hii yote ni kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa na mvua zilivyonyesha kwa wingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaendelea kushirikiana na Kamati zetu za Maafa, lakini tuendeleo kuwaagiza viongozi wote katika maeneo mbalimbali wahakikishe wanaendelea kuchukua tahadhari na hasa kuwahamisha wananchi katika maeneo hatarishi ili kuweza kuepusha majanga ya maafa katika kipindi hiki ambacho utabiri unaonyesha tutakuwa na mvua nyingi sana zinazoweza kupelekea kupatikana kwa maafa mengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujibu hoja hizi, nianze na hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati zote mbili, nikianza na hoja zilizotolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria alituagiza Serikali kufanya uchambuzi wa kina wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kubaini tuhuma zilizotolewa katika miradi ya NSSF na kuchukua hatua za kisheria za kuwawajibisha watu wote waliohusika katika kadhia hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakubaliana na ushauri huo wa Kamati, ripoti ya hesabu za Serikali imeshatolewa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndani ya Bunge. Kwa hiyo, kwa kufuata taratibu zile zile za kikanuni lakini taratibu za Serikali za kufuatilia ripoti hiyo, Serikali inachidi kwamba italifanyia kazi suala hilo kwa namna yoyote ile itakayowezekana ili kuendana na agizo la Kamati kama lilivyowekwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali kupitia SSRA kwa kushirikiana na Benki Kuu kwa mujibu wa kifungu cha 39 kikisomwa pamoja na kifungu cha 40 na 48 cha Sheria Na.8 ya mwaka 2008, Sheria ya SSRA itaendelea kufanya ukaguzi maalum kwa maana ya *special inspection* kwenye vitega uchumi vyote ndani ya Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Sheria Na. 8 ya mwaka 2010 ilianza kutumika mwezi Septemba 2010. Sheria hiyo iliyomuunda Mdhibiti Mkuu wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ililetwa kwa maana halisi ya kuondoa migongano ya kisheria katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, lakini vilevile ilitaka kuweka sera jumuishi za uwekezaji ndani ya mifuko hiyo na ilitaka pia kusimamia suala zima la kuongeza wigo na ufinyu wa hifadhi ya jamii katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nafasi ya pekee, naomba nimpongeze sana Mkurugenzi Mkuu wa SSRA dada Irene kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya katika kusimamia sekta yetu ya hifadhi ya jamii nchini. Na sisi kama Serikali tutaendelea kumpa ushirikiano na niwaombe Waheshimiwa Wabunge mnaweza kumtembelea na kupata ushauri mara zote bado anaendelea kusimamia sekta hii vizuri na kwa uadilifu wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, agizo lingine lilikuwa ni SSRA iendeleo kusimamia na kuchukua hatua kali kwa waajiri ambao hushindwa kuwasilisha michango ya wanachama wakiwemo waajiri wa sekta binafsi na taasisi za Serikali. Kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha Sheria Na. 8 ya mwaka 2008, SSRA ina wajibu wa kutekeleza na kulinda maslahi ya wanachama wote katika mifuko yetu.

Hata hivyo, SSRA imekuwa ikijikuta wakati mwingine ikipata shida katika kusimamia suala zima la kuwalazimisha waajiri kuhakikisha kwamba wanapeleka michango yao kwa wakati katika mifuko hii ya hifadhi ya jamii. Hivyo basi, SSRA kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu tumeandaa rasimu ya mabadiliko ya Sheria Na. 8 ya mwaka 2008 kwa lengo la kuipa nguvu SSRA ipate meno ya kuhakikisha kwamba waajiri wote wanakusanya michango na kuifikisha kwenye Mfuko ya Hifadhi ya Jamii kwa wakati na kuondoa usumbufu kwa wanachama wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati iliagiza Serikali ichukue hatua za dharti na za makusudi kuboresha mitambo na mazingira ya Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ili kuiwezesha idara hiyo kufanya shughuli zake kwa ufanisi na kibiashara. Tunayo mipango ya muda mrefu na muda mfupi katika kuhakikisha kwamba tunaboresha Idara hiyo ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Kwa sasa tumeamua kabisa kuyatambua mazingira hayo magumu ya Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na tumeamua kwa haraka kuanza kuchukua hatua za dharura za kukarabati mitambo yote ambayo ilikuwa imenunuliwa na bado inaweza kufanya kazi nzuri ya kuweza kurahisisha kazi katika kiwanda hiki. Tumejipanga kwa mpango wa muda wa kati na muda mrefu ili kuhakikisha tunaendelea kuboresha mazingira na majengo ya kiwanda hicho. Vilevile kwa kushirikiana na taasisi za Serikali ikiwemo Benki ya TIB na taasisi nyingine tumeamua kufanya kazi kwa pamoja ili kuboresha kiwanda hicho. Pia tuna mpango wa kujenga kiwanda kingine katika Makao Makuu ya nchi hapa Dodoma ambacho kitakuwa cha kisasa na kinaweza kukidhi mahitaji ya Taifa na tayari Serikali imepata ekari tano za kuweza kujenga kiwanda hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliagizwa pia kwamba Serikali ijitahidi kadiri inavyoweze kuboresha huduma za maafa ili kuiwezesha Serikali kutoa misaada ya haraka pindi maafa yanapotokea katika nchi yetu ya Tanzania mahali popote. Serikali imeanza kuchukua hatua za dhati kabisa kuhakikisha tunaboresha huduma za Idara ya Maafa katika nchi yetu ya Tanzania. Hii ni pamoja na kupitishwa kwa Sheria ya Usimamizi wa Maafa Na. 7 ya mwaka 2015.

Pamoja na kazi hizi tunazozifanya, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mkurugenzi anayesimamia Idara ya Maafa nchini kwa kazi kubwa anayoifanya kuhakikisha kwamba kwa *resources* hizo ndogo tulizonazo lakini shughuli hii imeendelea kufanyika kwa ufanisi na Waheshimiwa Wabunge wengi walisema na kumpongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo sheria hiyo inaweka maagizo mbalimbali ya kisheria yanayotakiwa kufuatwa ikiwemo kuanzishwa kwa Kamati za Maafa katika ngazi ya Kata, Wilaya, Mikoa. Kamati hizo zinaweza kutoa mchango mkubwa wa awali katika kusimamia suala zima la maafa pale yanapotokea na kutambua pia viashiria hatashiri ili kuchukua hatua kama vile kuwahamisha watu katika maeneo yanayoonekana ni hatarishi na hasa wakati wa masika kama inavyotokea sasa.

Waheshimiwa Wabunge, niwaombe sana tuendeleo kushirikiana na viongozi wenzetu na hasa wale viongozi wa Kamati za Maafa katika maeneo yetu ili kusaidiana kuhakikisha kwamba ama tunatoa taarifa mapema majanga haya yanapotokea ama tunachukua nafasi ya kushauri kuchukua tahadhari katika maeneo mbalimbali ili kupunguza maafa katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Kamati na Waheshimiwa Wabunge wengine waliomba Serikali iongeze fungu kwa ajili ya Idara hii ya Maafa. Serikali imeendelea kuweka fedha kwa Idara hii ya Maafa kwa kuzingatia ukomo wa bajeti. Vilevile tumeendelea kufanya kazi kwa kushirikiana na Wizara na taasisi nyingine ili kuhakikisha vifaa vya misaada ya maafa katika nchi nzima vinapatikana. Serikali imeweka maghala mbalimbali kwa ajili ya huduma hii katika mikoa mbalimbali nchini kwa kuzingatia kanda. Serikali pia imejiandaa na inaendelea kufanya tathmini ya majanga yaliyokwisha kutokea, imeendelea kuwafundisha wataalam mbalimbali mbinu na namna bora za kukabiliana na maafa na majanga mengine nchini ili majukumu haya yaweze kusimamiwa vema na Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tuliagizwa pia na baadhi ya Wabunge waliochangia na vilevile Kamati ya Katiba na Sheria ya kwamba Serikali ichukue hatua za makusudi kukamilisha haraka ujenzi wa jengo la makazi ya

Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa Dodoma. Naomba kulihakikisha Bunge lako Tukufu kwamba awamu ya kwanza ya ujenzi wa makazi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, yanayojumuisha nyumba na makazi ya Waziri Mkuu, ofisi binafsi na nyumba ya wageni imekwishakamilika na kukabidhiwa Serikalini tarehe 19 Februari 2016. Awamu ya pili ambayo itajumuisha ujenzi wa uzio, barabara, mandhari, nyumba za walinzi, wasaidizi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu na uwekaji wa samani ikiwemo ujenzi wa barabara. Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 2.5 kwa mwaka huu wa fedha kwa ajili ya kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ulitolewa wito na Wabunge kadhaa ndani ya Bunge lako ya kwamba Serikali iboreshe huduma za malipo kwa wastaafu wakati wa kustaafu na kusiwe na mapungufu na kadhaa nyingine kwa wastaafu wanapomaliza muda wao wa kazi. Hadi kufikia Juni 2015, idadi ya wastaafu wote kwa kila mfuko wa pensheni katika nchi yetu ya Tanzania wale ambao walikuwa wamekwishalipwa kupitia Hazina ilikuwa ni wastaafu 89,532. Aidha, utaratibu wa kuhakiki wastaafu kwa mifuko yote hufanyika kila mwaka kwa lengo la kubaini mahali walipo na kama tayari mafao yao ya kustaafu wamekwishayapata. Serikali inaadhi kuendelea kusimamia zoezi la malipo ya pensheni kwa wastaafu kwa utaratibu unaotakikana mara kwa mara ili kupunguza kadhaa ya hii kubwa wanayoipata wastaafu wetu katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, agizo lingine lilikuwa Serikali iweke utaratibu wa pensheni ya wazee wote hata wale ambao hawakuwa wakifanya kazi katika sekta rasmi. Agizo hili Serikali imelipokea na agizo hili limewekwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi katika mwaka wa 2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, rasimu ya andiko la Mpango wa Pensheni kwa Wazee wote na Watu Wenye Ulemavu imekwisha kukamilika. Hatua inayofuata kwa sasa ni ushirikishwaji wa wadau na taasisi zinazohusika na utekelezaji wa mpango huu ili mara tutakapokuwa tumekubaliana na wadau wote tuanze sasa kujipanga ndani ya Serikali na kulipa pensheni hii kwa wazee wetu kama ilivyoainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi pia walishauri elimu ya hifadhi ya jamii itolewe ili watu wengi zaidi wajiunge na mifuko hiyo. Naomba niwahakikishe Waheshimiwa Wabunge kwamba wigo wa hifadhi ya jamii katika nchi yetu ya Tanzania umeendelea kupanuka ingawa siyo kwa speed kubwa. Mpaka sasa takribani asilimia 8.8 ya nguvu kazi ya Taifa imeshajunga katika Hifadhi ya Jamii ingawa asilimia hiyo bado ni ndogo. Kwa hiyo, kwa mujibu wa Sheria Na. 8 ya mwaka 2008 ya SSRA kazi kubwa nyingine ambayo imekuwa sasa ikifanywa na SSRA ni kuhakikisha inachukua jukumu hilo

la kuanza kutekeleza mpango mkakati wa kuongeza wigo wa hifadhi ya jamii nchini yaaani *Social Security Extention Strategy*. Hii ni pamoja na kuweka mkakati wa mawasiliano yaani *Social Security Communication Strategy* kwa makundi mbalimbali kupitia vyombo mbalimbali vya habari ili kufikia lengo hilo. Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba Watanzania wengi na hasa vijana waliopo katika sekta isiyo rasmi wanaingia katika mfumo huu wa pensheni ili kuweza kuwaandalia maisha yao ya baadaye kwa namna moja au nyingine.

Serikali iliwezesha Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi kiuchumi kushughulikia masuala ya wafanyabiashara wadogowadogo wakiwemo bodaboda, akina mama lishe na wajasiriamali. Sheria ya Baraza la Uwezeshaji Wananchi kiuchumi ilitungwa mwaka 2004 na Sera ya Baraza hilo ilitolewa mwaka 2004. Kwa sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshazindua mpango mkakati wa utekelezaji wa kazi za Baraza hili lakini vilevile ameshazindua uanzaji wa utekelezaji wa shughuli hizi za Baraza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hivi Baraza limeshaanza kutengeneza programu kupitia NSSF na Baraza lenyewe na kutoa mikopo yenye riba nafuu kwa waendesha bodaboda katika SACCOS 16 za bodaboda katika Mikoa ya Dae es Salaam, Arusha, Mbeya, Dodoma, Kigoma, Tanga, Rukwa, Mara na Geita lakini kazi hii itaendelea katika mikoa mingine. Naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mkurugenzi anayesimamia sekta hii Dada Beng'i Issa kwa kazi nzuri anayoifanya na jinsi alivyojipanga kuhakikisha anatusaidia kujibu tatizo la ajira kwa vijana kupitia mpango huu wa uwezeshaji wananchi kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kukuarifu kwamba kwa sasa Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Tanzania, limeanza pia kutoa mafunzo maalum kabisa kwa vijana wetu wanaojiunga na Jeshi la Kujenga Taifa. Tunafahamu vijana wetu wengi pia wanajiunga na Jeshi la Kujenga Taifa na wanapomaliza mafunzo yao wengi wamekuwa wakikosa kuajiriwa. Baraza limeshaanza kuwafundisha viongozi katika makambi mbalimbali ya Majeshi yetu ya Kujenga Taifai ili wanapowafundisha vijana wetu katika mafunzo ya kijeshi wawafundishe jinsi ya kuunda vikundi na kupatiwa mikopo ili waweze kujajiri wao wenyewe. Nichukue nafasi hii kuwashukuru sana viongozi wote wa Jeshi la Kujenga Taifa nchini kwa ushirikiano mkubwa na jinsi walivyopokea wito huu wa kuwasaidia vijana wetu Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza pia linasimamia mpango wa akiba na mikopo kupitia VICOBA na SACCOSS. Niendeleo kuwaomba vijana wengi wajijunge kwenye mipango hiyo ya akiba na mikopo lakini na VICOBA ili tuanze

kuwaweka katika mifumo ya kukopesheka na kuwasaidia kujijiri na kuwaajiri wenzao pale wanapoanza kufanikiwa katika mipango tuliyojiwekea. (Makofi)

Mchango mwingine ulihusu miradi ya MIVARAF katika nchi yetu ya Tanzania. Mchango huu uliletwa na Mheshimiwa Edwin Ngonyani na Wabunge wengine. Naomba niwathibitishie kwamba mradi wa MIVARAF utafika katika maeneo yote ambayo yamekwishapangwa. Naomba niahidi mbele ya Bunge lako Tukufu tutawashirikisha Wabunge wote wanaohusika na mradi huu ili wajue miradi inayofanyika katika maeneo yao na watupe ushirikiano wa kuifuatilia na kuitizama inavyoendelea. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni hoja iliyotolewa na Kamati ya Mapambano dhidi ya UKIMWI, ikiomba Serikali kutenga fedha ya kutosha kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI na Dawa za Kulevya. Agizo hilo limezingatiwa na kama mlivyoona Serikali imeanza sasa kuweka fedha kwenye Mfuko Maalum wa kisheria katika mapambano dhidi ya UKIMWI. Takribani Watanzania 670,000 kwa sasa wanaishi kwa kutumia dawa lakini waliopimwa na kugundulika wanaishi na Virusi vya UKIMWI, ni takribani Watanzania 1,500,000. Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kuhakikisha kwamba tunafanya kazi ya kutosha katika eneo hilo. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge kwa kuwa pia ni Wajumbe wa Kamati za UKIMWI katika Halmashauri zetu basi tushirikiane kuangalia fedha zinazotengwa katika eneo hilo zinatumika ipasavyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyotolewa ni kuhusu tatizo la dawa za kulevya nchini, lilitolewa pia na Kamati hiyo hiyo ya UKIMWI. Kamati ilitutaka tuhakikishe kwamba tunafanya kila linalowezekana kuhakikisha tunapambana na tatizo hili la dawa za kulevya nchini. Naomba niwathibitishie sheria tuliyoitunga mwaka 2015 imeanza kuchukua mkondo wake na tayari adhabu kali zimeanza kutolewa kwa wale wote ambao wamekuwa wakijihusisha na biashara ya dawa za kulevya katika nchi yetu ya Tanzania. Sheria imetoa adhabu kali sana kwa makosa ya kujihusisha na matumizi ya biashara hiyo ambayo ni kifungo cha maisha. Sheria hiyo pia imetoa adhabu kali kwa wale wote wanaowahusisha watoto katika suala zima la matumizi ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni kuhakikishia Serikali inahamishia Makao Makuu Dodoma na hasa kwa kutunga sheria. Naomba niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge kwamba sheria ya kuhamishia Makao Makuu ya nchi Dodoma imeshaandaliwa na imeshaanza kupita katika vikao vya kisheria vya kiutaratibu ili hatimaye tuilete katika Bunge lako Tukufu iweze kujadiliwa na kupitishwa. Tutashirikiana na Wabunge kuhakikisha kwamba zile

kero ambazo zimekuwa zikitokea Dodoma kwa namna moja ama nyingine zinazohusu sheria basi zitarekebishwa kwa haraka. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Manaibu Waziri wangu wakijibu maswali, walizungumzia mambo mengi yanayohusu wafanyakazi, lakini vilevile yanayohusu walemavu, naomba niwathibitishie tumejipanga vizuri kukabiliana na changamoto zote za wafanyakazi katika nchi yetu ya Tanzania, kuboresha maisha yao, kuangalia sheria zile ambazo zimekuwa zikitumika kuwakandamiza katika maeneo ya kazi, tutazisimamia ili kuhakikisha sheria za kazi zinatekelezwa. Tumejipanga kuhakikisha kwamba suala zima la walemavu tunalipa kipaumbele katika Ofisi ya Waziri Mkuu, tutalisimamia na kutoa ushirikiano na hivyo kuhakikisha dhamira njema ya Serikali katika kuwajali na kuwahudumia walemavu katika nchi yetu ya Tanzania inafikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijamaliza kutoa majibu haya ya awali na kumpisha Mheshimiwa Waziri Mkuu aweze kumaliza majibu mengine yaliyobakia, nitumie nafasi hii kuwatakiwa wafanyakazi wote maandalizi mema ya sherehe za Mei Mosi ambazo zitafanyika Kitaifa katika Mkoa wa Dodoma. Sisi kama Serikali tunawahakikishia kwamba tupo pamoja nao, tutashirikiana nao na tutaendelea kufanya kazi nao kwa kuzingatia sheria na taratibu ili kuongeza tija na kukuza uchumi wa nchi yetu kama vile tunavyofahamu wafanyakazi ni nguzo muhimu katika kuleta maendeleo ya Watanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba kwa heshima na taadhima nichukue nafasi hii tena kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nikirudia kuanza na Wabunge Wajumbe wa Kamati zote mbili lakini na Wabunge wote waliochangia hapa ndani ya Ukumbi wa Bunge. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Tanzania.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunipa afya njema hadi leo ninapohitimisha majadiliano ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka huu wa fedha 2016/2017. Ninakushukuru sana wewe mwenyewe Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Mheshimiwa Spika ambaye kwa sasa hayupo Mezani na Wenyeviti wote wa

Bunge kwa kusimamia kwa umakini mkubwa majadiliano ya hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia niwashuhukuru Waheshimiwa Mawaziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Possi, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mavunde, Mbunge wa Dodoma Mjini, Makatibu Wakuu wote watatu, Wakurugenzi na Wakuu wa taasisi zote za Ofisi ya Waziri Mkuu. Nitumie nafasi hii pia kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kunipa ushirikiano mkubwa wakati wote katika utumishi lakini pia katika kuandaa shughuli hii ambayo leo tunaihitimisha hapa mbele. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka pia niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kwa ujumla wenu, kwa namna ya pekee kwa michango yenu ya kina ambayo imefanikisha kwa kiasi kikubwa kuboresha mipango na kazi ambazo zimekusudiwa kutekelezwa na Serikali katika mwaka huu wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kutoa majibu, maelezo mbalimbali ya wachangiaji, nitumie nafasi hii kupitia Bunge lako Tukufu kutoa pole kwa wananchi wetu waliokumbwa na maafa makubwa kule Mkoani Morogoro, Wilaya ya Kilosa lakini pia Wilaya za Rombo na Moshi Vijijini Mkoani Kilimanjaro. Taarifa si nzuri sana kwa sababu Wilayani Rombo tumeweza kupoteza kwa vifo Watanzania wenzetu wanne, Moshi Vijijini Watanzania watatu lakini pia kuna uharibufu mkubwa wa nyumba, mali, ikiwemo mashamba na vyakula. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kuwapa pole wote na wale ambao wametangulia mbele za haki tumwombe Mwenyezi Mungu aweke roho zao mahali pema peponi. Serikali itafanya jitihada za kuokoa wale ambao bado wamekwama na janga hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii pia kuwapa taarifa Watanzania kwamba Taasisi yetu ya Hali ya Hewa imeendelea kutupa tahadhari kubwa kwamba kipindi kilichobaki kufikia mwanzo mwa Mei, mvua zitaendelea kunyesha kwa kasi kubwa.

Kwa hiyo basi, wale wote ambao wako maeneo hatarishi waanze kuondoka katika maeneo hayo waende maeneo salama ili kuepusha majanga yanayoweza kujitokeza tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwa nimetoa salamu za shukrani pamoja na pole kwa waliopata maafa, sasa nijikite katika mjadala huu ambao ulichangiwa na jumla ya Wabunge 93; Waheshimiwa Wabunge waliochangia

kwa maneno ni 80 na waliochangia kwa maandishi 13. Wote hawa wameweza kutoa mchango wao kwa kina kupitia bajeti yetu ambayo leo hii niko hapa kwa ajili ya kuhitimisha. Napenda niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa hoja zao nzuri. Hata hivyo, kutokana na muda, naomba nisiwataje kwa majina lakini naomba majina yao yaingizwe katika *Hansard*.

Serikali imejibu hoja hizo kupitia Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri lakini hoja zilizosalia zitajibiwa kwa maandishi. Aidha, na mimi nitatumia nafasi hii kutoa ufafanuzi wa hoja chache huku nikijua kwamba kwenye hotuba yangu nilizungumzia sekta mbalimbali za Wizara za Kisekta lakini pia nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba sekta zote ambazo zimechangiwa zitajibiwa vizuri na Wizara husika, mimi nitajikita kwenye maeneo ya kiseru kupitia sekta hizo zote ambazo zimeweza kuzungumziwa.

Aidha, napenda nitumie nafasi hii ya awali kuwashukuru tena Wabunge wote kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa pamoja na Makamu wa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan, kwa utendaji wao na kasi nzuri waliyonayo katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawashukuru wote wale ambao wameonesha nia ya dhati ya kuunga mkono jitihada hizi za viongozi wetu wakuu katika kutekeleza kauli mbiu ya hapa kazi tu. Ni dhahiri kwamba wananchi wengi wamemuunga mkono Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makamu wa Rais. Hivyo, ni wajibu wetu sisi kama viongozi na wawakilishi wao kuonyesha njia bora ya kutekeleza kauli mbiu hiyo na utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mimi naamini kabisa kuwa mijadala yote iliyowasilishwa hapa itatusaidia sana kuwa makini zaidi katika kukidhi matarajio ya wananchi wetu katika Serikali ya Awamu ya Tano. Pongezi mlizozitoa Waheshimiwa Wabunge, zimetutia moyo sana na kutupa nguvu zaidi kama Serikali katika kuimarisha utendaji wetu katika kipindi hiki ambacho Serikali inatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa hoja ambazo zilitolewa kwa mujibu wa Kanuni ya 99(13) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba sasa nichukue nafasi hii kujibu na kufafanua baadhi ya maeneo ya hoja za Waheshimiwa Wabunge kama zilivyojitokeza. Katika ufafanuzi huu Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Mawaziri walijikita kujibu hoja

zilizochangiwa na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, sikusudii kurudia ila nataka tu niweke nyongeza ya majibu ya Mwanasheria Mkuu juu ya kipengele cha *instrument*. Eneo hili lina mchakato mrefu, pamoja na uwezo na mamlaka aliyonayo Mheshimiwa Rais ni kwamba Mheshimiwa Rais anaendelea kuiunda Serikali yake, alianza na Mawaziri na Makatibu Wakuu ambao ndiyo watendaji wa Serikali wameteuliwa mwanzoni mwa Januari.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia lazima kuwe na utaratibu wa kila Wizara baada ya kuwa Mheshimiwa Rais ameziunganisha Wizara mbalimbali ili sasa kupata uwezo mzuri wa kuweza kutengeneza hiyo *instrument* ambayo taratibu zake zimeendelea. *Instrument* hiyo baada ya kuwa imekamiliika na hawa watendaji lazima itangazwe na Gazeti la Serikali. Taratibu zote zikiwa zimeshakamilika ni lazima sasa itangazwe kwenye Gazeti la Serikali lakini utangazaji wa Gazeti la Serikali hauwi kama ilivyo kwenye magazeti yetu ya kawaida ambayo yanatangazwa kila siku, ni baada ya kuwa tumeshapata hoja za kutosha zilizo kwenye Gazeti la Serikali ndiyo unaweza kulitangaza ili wananchi waweze kuona.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwape faraja kwamba *instrument* za Wizara zote zimeshakamilika na zimesainiwa tarehe 20/04/2016 sasa tunasubiri kutangaza, wakati wowote Mheshimiwa Rais atakapoamua kutangaza zitakuwa zimetoka. Kwa hiyo, Mawaziri walioko kazini sasa wanafanya kazi kwa mujibu wa maelekezo ya Mheshimiwa Rais lakini pia na Ilani ya Chama kinachotawala ambacho kimeunda Serikali hii. Kwa hiyo, nataka niwape faraja kwamba *instrument* ipo na imeshasainiwa na watendaji wetu wanafanya kazi kwa mujibu wa *instrument* hiyo. (Makofi)

Naomba sasa nianze na maeneo ya jumla yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge na kama muda ukiruhusu nitaelezea machache pia ya kisékta kama ambavyo nimeeleza. Nianze na hoja ambayo imezungumzwa sana ya kuitaka Serikali iilipe MSD deni la shilingi bilioni 1.13 ili iweze kuendesha shughuli za kusambaza dawa, vifaa tiba na vitendanishi nchini. Nataka nieleze kwamba taarifa iliyotolewa ya MSD kwamba Serikali inadaiwa na jumla ya shilingi bilioni 134 na siyo ile shilingi bilioni 1.34 kama ilivyokuwa imechangiwa. Hata hivyo, nataka nilipe taarifa Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imeshaanza kushughulikia deni hilo kwa kumwelekeza Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhakiki deni hilo. Mpaka sasa CAG ameshahakiki madeni jumla ya shilingi bilioni 67 na kazi ya uhakiki inaendelea na malipo yatakuwa yanatoka kadri ambavyo CAG atakavyokuwa anaweza kuhakiki ili tuone madai haya na uhalisia wake. Ndiyo mkakati tulionao katika kuhakikisha deni hili la MSD linamalizika. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ilikuwa ni ununuzi wa dawa za kufubaza makali ya virusi vya UKIMWI lililochangiwa na Wabunge kadhaa pamoja na Kamati ya Bunge ya masuala ya UKIMWI. Kama nilivyoeeleza katika hotuba yangu Serikali inao mpango wa kuendelea kununua dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI kwa kutumia vyanzo vya ndani na kufanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi chache Barani Afrika zinazoweza kuwanunulia wananchi dawa hizo kwa kutumia fedha zake za ndani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufanikisha mpango huo, Serikali imeanzisha Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI ikiwa ni mojawapo ya mikakati ya kupunguza utegemezi wa wahisani katika ununuzi wa dawa za ARV na mfuko huo unachangiwa sana na Serikali na sekta binafsi. Hivyo naziomba sekta binafsi pamoja na wadau mbalimbali kujitokeza kuchangia mfuko huo. Aidha, Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 imeshatenga fedha zaidi ya shilingi bilioni 10 kwa ajili ya dawa za ARV.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni suala la vibali vya kuagiza mchele kutoka nje. Limezungumzwa sana na Waheshimiwa Wabunge, napenda pia kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa hali ya uzalishaji wa mazao ya nafaka hapa nchini imeendelea kuwa nzuri kila msimu. Takwimu za uzalishaji mpunga zinaonesha uwepo ongezeko katika kipindi cha miaka sita iliyopita na takwimu zinaonesha kwamba kiasi cha uzalishaji wa mpunga kimeongezeka kwa tani 1,669,825 kutoka mwaka 2009/2010 hadi kufikia tani 1,936,000 kwa mwaka 2014/2015 sawa na ongezeko la asilimia 14.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ambayo tunaifanya sasa Serikali ni kuhakikisha kwamba kupitia Wizara ya Kilimo tunaweka mkakati wa uzalishaji wa nafaka zaidi ili tuweze kuzalisha kwa kiwango kikubwa. Ninayo matumani pia kwamba kwa sasa tunayo hifadhi ya kutosha ya chakula kwenye maghala yetu na mkakati huo unaendelea ili tuweze kuwa na akiba ya kutosha kwenye maeneo yetu. Kutokana na mwelekeo mzuri huu wa uzalishaji wa mchele hapa nchini, Serikali imesitisha kutoa vibali vya uagizaji wa mchele kutoka nje kwa lengo la kuleta unafuu lakini pia uthamani wa mchele ulioko ndani na kuimarisha masoko yaliyoko ndani kwa zao hili la mchele. Kwa hiyo, niwahakikishie Watanzania kwamba hatutakuwa na vibali vya kuagiza mchele kutoka nje.

Hata hivyo, napenda pia kuagiza vyombo vya dola kuendelea kuimarisha ulinzi wa mipaka yetu yote hasa katika mwambao wa Bahari ya Hindi ili kuzuia uingizwaji holela wa mchele wa magendo kutoka nje ya nchi kwa

lengo la kulinda wafanyabiashara na mchele ambao tunao ndani uweze kuingia kwenye masoko tunayoyakusudia. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hili, naomba kuzungumzia suala la upungufu wa sukari nchini. Ni kweli kwamba uzalishaji wa sukari nchini upo chini ya kiwango cha mahitaji. Mahitaji ya sukari nchini ni tani 420,000 na kiwango cha uzalishaji nchini ni tani 320,000 na kweli tuna upungufu wa tani 100,000 na sasa hivi tumeanza kuona upungufu wa sukari.

Nataka niwaambie sukari iliyokuwepo kwenye maghala yetu na viwanda vyetu imepungua lakini tumeshaiagiza na baada ya muda mfupi kutoka sasa sukari itakuwa imeingia nchini. Sukari ambayo tumeiagiza ni ile tu iliyopungua kwa lengo la kuzuia kuingiza sukari nyingi ikadhoofisha viwanda vyetu tulivyonavyo nchini huku tukiwa tumeshaweka malengo ya uzalishaji wa ndani ya nchi ili kuweza kufikia mahitaji ya Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda kuwaeleza wananchi kwamba sukari itaingia baada ya muda mfupi. Nawasihi wafanyabiashara wote wenye sukari, wenye maduka, waitoe sukari waliyonayo kwa sababu takwimu tuliyonayo sasa hivi nchini tuna tani zisizopungua 37,000 ambazo tunaamini zinaendelea kuuzwa na hii itakapoingia itaweza kukamilisha na kuzuia upungufu wa sukari tulionao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kauli hii, natoa agizo kwa Maafisa Biashara kwenye Halmashauri za Wilaya, wafanye ufuatiliaji kwenye maduka yetu kuona kwamba sukari haifichwi kwa lengo la kuuza kwa bei ya juu ili sukari iuzwe kwa bei elekezi ambayo imetolewa na Serikali ili wananchi waweze kupata sukari wakati wote wanaohitaji. Kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba Watanzania na wafanyabiashara wote, sukari hii ambayo tunajua tunayo nchini itatolewa nje ili wananchi waweze kununua kwenye maduka yetu tena kwa bei ileile elekezi kwa sababu upungufu huo unaotamkwa hauko kwa kiwango hicho lakini hata hivyo ule upungufu ambao tunao tayari taratibu za uagizaji wa sukari umeshakamilika na wakati wowote itaingia kwenye soko. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu ni ile hoja ya mfumo wa stakabadhi za ghala, ambao umechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi na Serikali. Mfumo huu ulianzishwa kwa zao la korosho kwanza, kwa nia ya kuwawezesha wakulima kuuza mazao yao kwa utaratibu wa ushindani baada ya kuyakusanya katika maghala ya Vyama vya Ushirika vilivyo kwenye maeneo yao. Hii ilikuwa inalenga kuwawezesha wakulima kupata kipato zaidi ikilinganishwa na mifumo mingi iliyokuwepo huko nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, nakiri kwamba mfumo huu umeleta changamoto nyingi na malalamiko mengi. Nataka niwahakikishie Watanzania na wakulima wa zao la korosho nchini, kwamba mfumo huu ni mzuri, lakini changamoto zake ni zile ambazo zimesababishwa na Watendaji wetu, nami nikiri kwamba tunao usimamizi mbovu wa Vyama vya Ushirika (AMCOS), lakini ia usimamizi mbovu wa Vyama vyetu Vikuu pamoja na Bodi yenyewe. Vilevile uwepo wa makato holela ya hovyoy, pia kunakuwa na riba za juu za mabenki yetu ambapo yote haya kwa pamoja yanapelekea mkulima kuwa na pato dogo ambalo pia wakulima wamekuwa wakilalamika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa Serikali ambao sasa tunafanya mapitio ya mazao yetu yote makuu nchini ya kuondoa matatizo yaliyojikita kwenye maeneo haya ikiwemo kuyaondoa makato ya hovyoy hovyoy yaliyopo kwenye mazao haya. Kwa mfumo huu wa Stakabadhi Ghalani ambao umeanza kwenye zao la Korosho, tumebaini pamoja na upungufu niliousema ya usimamizi mbovu, lakini tuna makato tisa ambayo mkulima huwa anakatwa na yote haya yanamsababisha mkulima kupata pato dogo na hatimaye wakulima kulalamika. Mpaka sasa tumeshafanya vikao vya pamoja, Wizara pamoja na Bodi, tumekubaliana na Serikali imeondoa makato sita kati ya tisa ili kuweza kumfanya mkulima aweze kupata tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, makato tuliyoyaondoa ni gharama ya usafirishaji ya zao la mkulima kutoka nyumbani kwake mpaka kwenye maghala na kazi hiyo tumewaachia Vyama vya AMCOS vyenye na viko Vyama vya AMCOS vimenunua magari yao, watanunua matrekta yao, watasafirisha wenyewe kwa gharama zao wenyewe badala ya kuwakata kutoka chama kikuu cha ushirika kwa thamani ya shilingi 50. Tumesema kuanzia sasa, minada yote itafanywa kwenye maeneo ya wakulima ili wakulima wenyewe washuhudie minada yao. Badala ya kuipeleka minada eneo la mbali, linamfanya mkulima anashindwa kujua mnada uliofanywa ni wa kiasi gani na una uhalali wa kiasi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna hii itaweza kumdhihirishia mkulima kuona wanunuzi na kusikia kila mnunuzi ananunua kwa kiasi gani na watafanya maamuzi ya kuwaachia korosho au lah ili waweze kupata tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kato la pili ni ushuru wa maghala unaotozwa kule ambapo korosho zinatunzwa. Tumeondoa ushuru huu kwa sababu kila Chama cha Ushirika kimejenga ghala lake. Wakulima walishachangia ujenzi wa ghala lao na korosho zao zitatunzwa kwenye ghala lao na mnada utakaofanywa kwenye eneo lao, hautamlazimisha mkulima kukatwa shilingi

50/= ya kulipa kwenye maghala. Kwa hiyo, makato hayo tumeyaondoa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, makato mengine ni ya mkulima kulipa Chama Kikuu. Mkulima hana mahusiano na Chama Kikuu zaidi ya kwamba chenyewe ndiyo kinaratibu. Chama Kikuu kimeundwa na AMCOS na kwa hiyo, Chama Kikuu kitatoza mchango kwa AMCOS na kwa hiyo, Chama Kikuu hakiwezi kumtoza mkulima. Tumefuta mchango huo na badala yake fedha ile itarudi kwa mkulima ili iweze kuongeza tija yake. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na malipo yanalipwa Sekretarieti ya Mkoa, asilimia moja. Fedha hizi ni nyingi kwenda Mkoani, watu wa Mkoa watafanya kazi zao kwa mujibu wa ajira yao ya kufuatilia mwenendo wa zao la Korosho na wala hakuna sababu ya mkulima kuichangia Ofisi ya Mkoa shilingi moja, hiyo ilikuwa ni kupunguza mapato ya mkulima. Tumeiondoa na sasa hivi mapato haya hayatakuwepo tena. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulikuwa na makato ya unyaufu wa zao la korosho. Sheria ya Unyaufu inatekelezwa tu pale ambapo korosho itakaa zaidi ya miezi sita na siyo mwezi mmoja. Kwa hiyo, zao hili lilikuwa linakatwa asilimia 0.5 ya unyaufu ambayo tunasema sasa tumeiondoa na fedha hiyo itarudi kwa mkulima mwenyewe, tukiamini kutoka siku mkulima anapeleka ghalani mpaka siku ya mnada haiwezi kuchukua muda wa miezi sita. Kwa hiyo, makato hayo tumeyaondoa na mkulima atapata hela yake. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kato lingine ambalo tunaanza kuliangalia sasa ni riba ya benki ambapo AMCOS huwa zinakopa benki. Mfumo wa Stakabadhi Ghalani haulazimishi AMCOS kwenda kukopa benki. Unapokwenda kukopa benki inashawishi viongozi wa AMCOS kugawana kwanza na hawalipi na badala yake malipo hayo hulipwa na mkulima. Kwa hiyo, tunaanza kuangalia uwezekano wa AMCOS kukopa benki au mkulima apeleke mazao, asubiri siku ya mnada ili aweze kuuza apate fedha yake yote, badala ya utaratibu wa sasa wa kulipa kidogo kidogo. Wanalipa malipo ya kwanza, malipo ya pili, hiyo haitakuwepo tena kama AMCOS itapeleka mazao hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mkakati huu unaacha malipo yafuatayo tu; mchango wa Halmashauri wa mazao wa 3% mpaka 5%; Mfuko wa Wakfu ambao tumeupa kazi ya kununua magunia na mbolea na kuhakikisha kwamba mkulima anapata pembejeo; na mkulima kuichangia AMCOS yake iliyopo kwenye eneo lake na siyo Chama Kikuu. Kwa hiyo, makato hayo ndiyo pekee ambayo mkulima sasa atakuwa anachangia na kwahiyo,

tumeondoa zaidi ya shilingi 360 ambazo alikuwa anakatwa mkulima bila sababu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea na zoezi hili la kufanya mapitio ya kila zao maarufu ikiwemo la pamba, kahawa, chai pamoja na tumbaku ili kuhakikisha kwamba wakulima wa mazao haya, wanapata unafuu. Na mimi nitalisimamia mwenyewe kwa kupita kwenye maeneo hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya Benki ya Maendeleo ya Kilimo. Pamoja na kuipongeza benki hiyo kwa kutoa huduma kwa wananchi na Mikoa, lakini pia kulikuwa na changamoto ambazo Waheshimiwa Wabunge walizionyesha kwamba Benki ya Kilimo ina mtaji mdogo ikilinganishwa na mahitaji na kwahiyo, Serikali iliombwa iweke utaratibu mzuri kwa ajili ya kuhakikisha kwamba benki hii inapata unafuu wa kuweza kuhudumia wakulima nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika hotuba yangu, Serikali ilizindua Benki ya Maendeleo ya Kilimo ili kuwawezesha wakulima kupata mikopo yenye riba nafuu kwa ajili ya kuendeleza na kukuza shughuli za kilimo nchini. Kitaalam kilimo ni pamoja na shughuli za kilimo cha mazao, uvuvi, mifugo na maliasili, hivyo naamini kuwa hata wavuvi na wafugaji waliopo katika Jiji la Dar es Salaam, wanastahili kutumia huduma za mikopo kutoka benki hii.

Kwa mara nyingine tena niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa ujumla kuwa Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha wadau wengine wa maendeleo ili kuongezea benki hii mtaji wake; lakini bado Serikali pia imeongeza benki nyingine inaitwa *TIB Maendeleo* na *TIB Ushirika (TID Development na TIB Corporate)*. Zote hizi nazo tumezongeza kwenye mifumo ya mikopo kwa ajili ya kilimo. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wenzangu na wakulima wote nchini, tunayo fursa kubwa sasa kukopa kwenye Benki ya Kilimo, lakini pia na *TID Development* na *TIB Corporate* ili kuweza kuongeza mtaji wa shughuli za kilimo.

Kulikuwa na suala la hifadhi ya jamii nalo pia ni jambo ambalo Waheshimiwa Wabunge wengi walichangia. Kwenye eneo hili Wabunge waliomba Sera ya Uwekezaji wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii pamoja na kupunguza idadi ya mifuko hiyo iweze kuangaliwa tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetoa miongozo ya uwekezaji iliyotolewa na Mamlaka ya Usimamizi ya Udhhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (*SSRA*) na Benki Kuu ya Tanzania. Aidha, kaguzi za mara kwa mara zinafanyika kuhusu uwekezaji wa mifuko hii ya jamii. Sambamba na hatua hizo, Serikali

imekwishatoa maelekezo kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuona namna itakavyoshiriki katika sekta ya viwanda ili kuchangia katika uchumi wa viwanda, kuongeza fursa za ajira na hatimaye kujipatia wanachama wengi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kupunguza idadi ya mifuko ya hifadhi ya jamii, ushauri uliotolewa umepokewa na ni mzuri na tayari Serikali inakamilisha utafiti wa kina kuhusu hali ya mifuko na namna ya kupunguza idadi ya mifuko iliyopo. Kwa sasa hatua inayoendelea ni kupokea maoni ya wadau ili kuwezesha mabadiliko husika kufanyika kwa wakati muafaka. Napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba mawazo yenu tutaendelea kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ilikuwa ni mchakato wa kura za maoni na Katiba Iliyopendekezwa. Iitakiwa Serikali itoe tamko kuhusu maandalizi ya utekelezaji wa mchakato wa kura za maoni katika Katiba Iliyopendekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Kura ya Maoni ya mwaka 2013 mchakato wa kura za maoni kuhusu Katiba Iliyopendekezwa unasimamiwa na Tume ya Uchaguzi (NEC) kwa Tanzania Bara na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) kwa upande wa Tanzania Zanzibar. Zoezi hilo lilipangwa kufanyika tarehe 30 Aprili, 2015 lakini likaahirishwa kwa sababu zifuatazo:-

Moja, kutokamilika kwa zoezi la kuandikisha wapigakura wakati muda wa kura ya maoni ukiwa umekaribia.

Pili, mchakato wa kura ya maoni ya Katiba Inayopendekezwa ni sawasawa na mchakato wa uchaguzi, kwahiyo, Tume zisingeweza kuendesha kura ya maoni pamoja na Uchaguzi Mkuu kwa pamoja. Hivyo njia pekee ilikuwa ni kuahirisha kura ya maoni ili ikuendesha uchaguzi wa mwaka 2015 kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia haya, kwa kuwa Tume hizi mbili ndizo zilizoahirisha mchakato huo kwa sababu zilizoenezwa na pia ndizo zenye dhamana ya kuendesha zoezi hilo, napenda kutoa taarifa kwenye Bunge lako Tukufu kuwa taarifa na ratiba mpya ya kura za maoni zitatolewa na Tume hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya ratiba ya uchaguzi iliyotakiwa Serikali iweke utaratibu mpya wa ratiba ya upigaji kura ili kuwezesha chaguzi zote za Rais, Wabunge, Madiwani na Serikali za Mitaa zifanyike kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nieleze tu kwamba uendeshaji wa usimamizi wa Uchaguzi Mkuu ambapo Rais, Wabunge na Madiwani ndio unawahusu na uchaguzi wa Serikali za Mitaa unasimamiwa na kuratibiwa na kuendeshwa kwa sheria na mamlaka mbili tofauti kama ifuatavyo:-

Moja, uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani unasimamiwa na sheria mbili ambazo ni Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa Sura ya 292 na uchaguzi huo husimamiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unasimamiwa na sheria mbili ambazo ni Sheria ya Mitaa, Mamlaka ya Wilaya Sura Namba 287 na Sheria ya Serikali za Mitaa, Mamlaka za Miji Sura Namba 288. Uchaguzi huu usimamiwe na Wizara yenye dhamana na masuala ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo huo uliwekwa ili kutowachanganya wananchi katika upigaji kura, kwani kwa kufanya chaguzi hizo zote kuwa pamoja, zingeweza kusababisha karatasi za kura kuwa na picha rundo au nyingi kiasi kwamba mpigakura angeshindwa kuweza kutambua kwa haraka. Pamoja na maelezo haya, Serikali imepokea mapendekezo na nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba tutaendelea kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulikuwa na suala la uhakiki wa majina ya wapigakura ya kwamba Serikali iongeze muda wa uhakiki wa majina kabla ya kupiga kura ili kuwawezesha wananchi wengi waweze kupiga kura.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Tume ya Taifa ya Uchaguzi imekamilisha zoezi la tathmini baada ya uchaguzi (*post-election evaluation*) na inakamilisha uchambuzi wa tathmini hiyo na matokeo ya tathmini hiyo yatawezesha kuboresha maeneo mbalimbali likiwemo suala la uwekaji wazi daftari la kudumu la wapiga kura.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na utafiti wa wananchi ambao hawakupiga kura nalo pia lilijitokeza na Waheshimiwa Wabunge walichangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Sheria za Uchaguzi; kujiandikisha na kupiga kura ni haki na hiyari ya mwananchi. Hata hivyo Tume ya Taifa ya Uchaguzi imefanya tathmini za uchaguzi, pamoja na mambo mengine na kubaini sababu za baadhi ya maeneo wananchi kujitokeza wachache kupiga kura. Uchambuzi wa taarifa hiyo utakapokamilika, Tume itabainisha sababu ya baadhi ya wananchi kutokujitokeza kupiga kura pamoja na mapendekezo ya hatua za kuchukua ili wananchi wengi waweze kujitokeza kwenye chaguzi zijazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na mchango wa Waheshimiwa Wabunge juu ya vigezo vya kugawanya Majimbo ya Uchaguzi. Eneo hili ni kwamba vigezo vinavyotumika kugawa majimbo kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ni pamoja na wastani wa idadi ya watu, hali ya kiuchumi, ukubwa wa eneo la jimbo husika, mipaka ya kiutawala, hali ya kijiografia, upatikanaji wa mawasiliano, mpangilio wa maeneo ya makazi ya watu yaliyopo, lakini mazingira ya muungano wenyewe, uwezo wa ukumbi wa Bunge na idadi ya Viti Maalum vya Wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2015 Tume ilipokea maombi 77 ya kuanzishwa au kagawa majimbo ambapo Halmashauri 37 ziliwasilisha maombi ya kugawa majimbo ya uchaguzi na maombi 40 yalitoka katika Majimbo yakiomba kugawanywa. Kati ya maombi yaliyowasilishwa, maombi 35 yalikitidhi vigezo na yalistahili kugawanywa.

Hata hivyo, kutokana na ongezeko la Halmashauri mpya ambazo kisheria ni majimbo ya uchaguzi, ongezeko la idadi ya Wabunge wanawake na Viti Maalum na uwezo wa ukumbi wa Bunge, Tume iliamua kutumia vigezo vitatu ili kupata idadi ya majimbo yanayoweza kugawanywa. Vigezo hivyo ni hivi hapa wastani wa idadi ya watu, mipaka ya kiutawala na uwezo wa ukumbi wetu wa Bunge kwa kutumia vigezo hivyo vitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ilianzisha Majimbo 25 kwa mchanganuo ufuatao; majimbo 19 yalitokana na ongezeko la Halmashauri mpya na majimbo sita yalitokana na kigezo cha wastani wa idadi ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikia pia maombi ya kugawa majimbo katika Wilaya ya Chemba na Sumbawanga, natarajia kwamba kwa kuzingatia vigezo vilivyotajwa hapo juu, Tume itaangalia uwezekano wa kugawa majimbo hayo iwapo yanakidhi vigezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kwa sasa hatutaweza kutamka maeneo mapya ya utawala, hii ikiwemo na maombi ya Wilaya, Halmashauri hata Mikoa. Hii ni kutokana na mamlaka zile mpya ambazo tumezipa maeneo mapya bado hatujakamilisha kuzijenga na kuzipa uwezo wa uendeshaji wa shughuli za Serikali kwenye maeneo mapya. Baada ya kuridhika kwamba tumeshakamilisha hayo, tutawapa taarifa na jambo hili tutaendelea kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na jambo la miradi ya REA kutaka miradi ya usambazaji umeme vijijini ikamilishwe na leo nimefurahi nimefikia Naibu Waziri hapa akitoa ufafanuzi. Kwa ufafanuzi ule, niwahakikishie tu

kwamba vile vijiji vyote ambavyo vilishaingia kwenye Mpango wa REA, kazi hizo zinaendelea, lakini Awamu ya Tatu Itakapoanza vijiji vyote vilivyobaki tunatarajia vitaingia kwenye mpango ili tuweze kuhakikisha kwamba tunakamilisha. Malengo yetu vijiji vyetu nchini vipate umeme na wananchi wetu wote wapate umeme wa kutosha kwenye maeneo yao. Uwezo huo tunao na tunawaahidi kwamba Serikali itakamilisha jambo hili kwenye maeneo yetu kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala la uwezeshaji wananchi vijijini ambapo pia ilitakiwa Serikali iweke utaratibu wa vigezo vitakavyozingatiwa kwa wananchi kabla ya kutoa Shilingi milioni 50 zile ambazo zinaenda vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo hili, niseme tu kwamba mradi unalenga kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kutenga shilingi milioni 50 kwa kila kijiji kama Mfuko wa uwezeshaji kwa ajili ya kukopesha vikundi vya wajasiriamali kupitia Ushirika wa Kuweka na Kukopa katika vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017 zimetengwa shilingi bilioni 59 kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi huo. Ili kuwapatia mikopo wakopaji, masharti yafuatayo yatatumika katika kutekeleza mpango huu. *(Makofi)*

Moja, ni kikundi cha kifedha kiwe kimesajiliwa na Halmashauri na Tume ya Ushirika; pili, kikundi kiwe na Katiba, uongozi uliochaguliwa kidemokrasia na kupata mafunzo ya mikopo; tatu, kikundi kiwe chini ya asasi ya kiraia inayotambulika na yenye uzoefu wa shughuli za mikopo; nne kikundi kionyeshe uzoefu wa kukopeshana kwa muda wa mwaka mmoja tangu kuanzishwa kwa historia ya urejeshaji wa mikopo hiyo kwa asilimia kuanzia 95.

Pia dhamana ya Serikali itakuwa kwenye kiasi cha msingi cha mkopo na siyo kwenye kiasi ambacho kimechanganywa na riba. Sita, kikundi kitaweka amana akiba ya fedha benki katika akaunti maalum; asilimia 10 ya mkopo ndani ya kikundi, hautazidisha riba zaidi ya asilimia 11, lakini mkopo wa SACCOS itafuata Kanuni ya Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2013. Kwa hiyo, ni vyema sasa Waheshimiwa Wabunge tukaendelea kuhamasisha kwenye maeneo yetu ili vikundi mbalimbali vianze kusajiliwa na viweze kuingia kwenye utaratibu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ilikuwa ni suala la CDA kutokuwa na Sheria ya Makau Makuu, hili limejibiwa vizuri na Waziri, Mheshimiwa Jenista Mhagama kwamba sheria imekamili, bado taratibu zinaendelea ili kuweza kuifanya CDA sasa kuwa kwenye sheria iliyo kamili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo lilichangiwa ni suala la uchakavu wa meli ya *MV Serengeti* ya Ziwa Victoria; Waheshimiwa Wabunge hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais. Nataka niwahakikishie, hata nilipokuwa Mkoani Kagera niliwahakikishia wananchi kwenye mkutano wa hadhara kwamba ahadi hii ya kupata meli mpya itatekelezwa, itakayoweza kufanya safati zake kwenye Ziwa Victoria. Kwa hiyo, wananchi waendeleo kuwa na subira katika kipindi hiki ambacho tunaendela kuomba bajeti hapa. Na mimi nawaomba Waheshimiwa Wabunge tupitishie hii bajeti ili tuendeleo kufanya kazi za Serikali ikiwemo na ahadi ambazo Mheshimiwa Rais ameahidi katika maeneo mbalimbali nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo lilikuwa limehitaji mchango lakini na majibu, ni uwepo wa Makau Makuu wa Wilaya ya Nyang'hwale, ambapo sasa kumetokea na mkanganyiko kule. Nataka niwahakikishie Wana-Nyang'hwale wote kwamba bado Serikali inatambua kuwa Makao Makuu ya Wilaya ni Karumwa, ambayo ilipendekezwa na ninyi wenyewe na sisi wajibu wetu sasa ni kuanda *certificate* au cheti kwa ajili ya kuthibitisha uwepo wa Makao Makuu hayo.

Kwa hiyo, sasa nawasihi wananchi kupitia pia Mheshimiwa Mbunge ambaye ataonana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili kupata hicho cheti muweze kuendelea na shughuli za maendeleo kwenye Wilaya yenu ya Nyang'hwale ikiwa chini ya Makao Makuu pale Karumwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ambazo zilikuwa mezani kwangu siyo nyingi na hivyo naomba nihitimishe hoja hizi kwa hayo yafuatayo kwamba, kama nilivyosema hapo awali kwamba muda hautoshi kujibu hoja zote zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, hata hivyo nirudie kusema kuwa Serikali yetu inayoongozwa na chama cha Mapinduzi, imejipanga vizuri sana katika kila sekta hasa za kiuchumi na kijamii, kuhakikisha kwamba wananchi wake wanajiletea maendeleo yao na Serikali hii itasimamia maendeleo hayo na maeneo ambayo yamekosa fursa, tutahakikisha kwamba tunapeleka fursa hizo ili wananchi waweze kwenda sambamba na hizo fursa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona juhudi kubwa za Mheshimiwa Rais katika kuhakikisha tunakuwa na mapato ya kutosha kutuwezesha kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi na hususan katika sekta ya kilimo, miundombinu, elimu, afya, nishati na madini. Wito wangu bado unabaki pale pale kwa watendaji wa Serikali walioko kwenye maeneo haya kutoa huduma kwa wananchi ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanatarajia Serikali hii kuwa itawapokea, itawasikiliza na kuwahudumia na jukumu hili Serikali imewapa watumishi wa Serikali ili waweze kutenda hayo kwa wananchi, wananchi waone kabisa wapo kwenye nchi yao na kwamba inawajali na inaweza kuwaletea mafanikio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kupitia maombi yangu ya leo kwenu Waheshimiwa Wabunge ya fedha za maendeleo ambazo tunatarajia tuzipeleke kwenye maeneo yetu, tulikuwa na tatizo la upitishaji wa mikataba ya thamani ya mikataba yenyewe kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitumie nafasi hii sasa kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa kwa sasa Serikali imefanya mapitio na hasa kupitia Gazeti la Serikali Toleo Namba 121 la tarehe 24/4/2016 imepandisha kiwango cha thamani za mikataba inayopaswa kupitiwa au kuhakikiwa kwanza na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kutoka shilingi milioni 50 ya awali hadi shilingi bilioni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya mikataba hii ya shilingi milioni 50 imekuwa ikileta matatizo makubwa kwenye Halmashauri. Mradi mdogo wa shilingi milioni 50, mkataba uende kwa Mwanasheria Mkuu. Tumegundua kuna mrundikano mkubwa wa mikataba hii pale kwa Mwanasheria Mkuu. Sasa Serikali imefanya marekebisho, mikataba ya kwenye Halmashauri itakayotakiwa kwenda kwa Mwanasheria Mkuu ni kuanzia shilingi bilioni moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo basi, mikataba yote yenye thamani ya chini ya shilingi bilioni moja itahakikiwa na mamlaka yenyewe ya Halmashauri au taasisi husika kwa ajili ya manunuzi. Hatua hii itaharakisha kasi ya manunuzi na hivyo kasi ya maendeleo pia katika Halmashauri inaweza kufikiwa kwa haraka. Hata hivyo, Mamlaka za Ununuzi hazizuiliwi kuomba ushauri kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mikataba ya kiwango cha chini ya shilingi bilioni moja kwa ajili ya kujiridhisha tu kwamba walichofanya ndicho chenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watakaokuwa wanahakiki mikataba hiyo katika Mamlaka za Ununuzi (*procure re-entities*) watapaswa kuzingatia Sheria ya Ununuzi na sheria nyinginezo zinazohusu mikataba hiyo na maadili ya Wanasheria lazima yazingatiwe katika utumishi wa umma ili kulinda maadili sahihi ya namna ya upitishaji wa mikataba hii. Kinyume cha hapo, kama maadili hayataweza kutekelezwa, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na wale watendaji wetu kwenye Halmashauri zote, pale ambapo mikataba hiyo itapitiwa na pia itaweza kupindishwa kwa mujibu wa taratibu hizi za Serikali

zinavyotaka hatua kali itachukuliwa na hatutasita kuchukua hatua kwa wale wote ambao hawawezi kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mwisho, narudia tena kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, kwamba tumeshirikiana katika siku hizi zote hapa tukiwa tunachangia hoja mbalimbali kutoa maoni ya utendaji bora wa mwaka wa fedha ujao kwa Ofisi ya Waziri Mkuu na mimi pamoja na Mawaziri wangu, Makatibu Wakuu wangu, Wakurugenzi na Wakuu wa Taasisi pamoja na watumishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Kwa kuwa pia niliomba na nilieleza pia utendaji wa Serikali kwenye Wizara nyingine zote, nataka niwahakikishie, bajeti hizi zinazoletwa kwenu ambazo naamini mtaziridhia kuzipitisha ili tuanze kazi tarehe 1 Julai, tutasimamia maadili, tutasimamia uaminifu, tutasimamia uwezo mzuri wa kitaalamu katika utendaji wa kazi za kila siku ili Watanzania waweze kupata tija ndani ya nchi yao. Na ninyi kama Wabunge mtatusaidia sana kuona mwenendo wa utendaji wa Serikali kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu kwamba tutaendelea kushirikiana kwa pamoja, tutafanya hivyo bila kujali vyama vyetu, tutafanya hivyo kwa kujali maslahi ya Watanzania wote na tuendeleo kushirikiana kwa pamoja, na mimi kama Msimamizi Mkuu wa Shughuli za Serikali nitashirikiana nanyi kuhakikisha kwamba miradi yetu inafikiwa kwa kiwango kinachostahili. *(Makofi)*

Sasa basi nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa ujumla, tushirikiane kuivusha nchi yetu katika hatua tuliyonayo kiuchumi, tunahitaji kusonga mbele, kwani wananchi wetu wanahitaji maendeleo, na sisi ndio wenye jukumu la kuwaongoza wananchi wetu kufikia malengo tuliyoyatarajia. Naomba sana, nitakapokuja kuwaomba fedha mridhie ili tuanze kazi ile mnayotarajia tuifanye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ndio ilikuwa kauli yangu ya msingi ya mwisho kwa Wabunge wenzangu ili tuweze kuungana kwa pamoja na sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nitawahoji baada ya hatua itakayofuata.

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 15 – Tume ya Usuluhishi na Uamuzi

Kif. 1001 - Admin. & HR Mgt..... Sh. 2,435,301,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Tuendeleo.

Fungu 25 – Waziri Mkuu

Kif. 1001 - Admin. & HR Mgt..... Sh. 4,034,253,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zitto!

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, mshahara wa Waziri Mkuu kifungu hicho, Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema hapa kwamba zimetengwa jumla ya shilingi bilioni 59 kwa ajili ya kila kijiji kupatiwa fedha shilingi milioni 50 lakini katika vote yake hii namba 25 hakuna kabisa kifungu hicho. Kwa hiyo, naomba kupata maelezo ya Waziri Mkuu, fedha hizo zimetengwa wapi? Kwa sababu hazipo kwenye Ofisi yake Waziri Mkuu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mjumbe, nadhani hoja yako uilete tukifika Fungu 37 kwa sababu hiki tunachojadili hapa hakiwezi kuwa na hiyo hoja. Kwa hiyo, uitunze tutakapofika Fungu 37 utaileta.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Fungu 27 – Msajili wa Vyama vya Siasa

Kif. 1001 - Admin. and HR Mgt.....Sh.18,793,991,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu

Kif. 1001 - Admin. and HR Mgt..... Sh. 3,326,329,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zitto, unaweza kuleta hoja yako.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Programu ya 10, Subvote 1001 mshahara wa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu ametamka mbele ya Bunge hapa kwamba, zimetengwa jumla ya shilingi bilioni 59 kwa ajili ya Mfuko wa *Village Empowerment*, kupeleka shilingi milioni 50 kila Kijiji; na katika hotuba yake wameeleza kwamba fedha hizi zitaratibiwa na *National Economic Empowerment Council*, lakini katika mafungu yote ya Ofisi ya Waziri Mkuu hakuna eneo lolote linaloonyesha fedha hizo.

Kwa hiyo, naomba maelezo ya Waziri Mkuu, fedha hizi ziko wapi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Swali la Mheshimiwa Mbunge ni hoja ya msingi, lakini kwa kuzingatia majukumu ya Kikatiba ya Ofisi ya Waziri Mkuu ya Uratibu na kwa mujibu wa Sheria ya Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 na Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004, jukumu la Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi katika fedha hii ni kuratibu mfumo utakaowekwa kwa ajili ya matumizi hayo. Fedha hii imetengwa kupitia vote ambayo itasimamiwa na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutakapofika kwenye hotuba ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, fedha hiyo tutakuta imetengwa. Hata hivyo, katika uratibu wa fedha hiyo, namna ya kuzifanyia kazi, kuzisimamia, baada ya Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kuweka utaratibu huo, tunashirikiana pia na TAMISEMI kuhakikisha kwamba utaratibu ule sasa utafuatwa lakini fedha imetengwa katika fungu hilo. *(Makofi)*

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Fungu la TAMISEMI, hakuna hiyo fedha. Naomba Serikali ifungue mafungu ya TAMISEMI, fedha hiyo haipo. Kwa hiyo, haipo Ofisi ya Waziri Mkuu wala haipo TAMISEMI. Fedha hiyo iko wapi? Haipo hiyo fedha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri TAMISEMI hatujaifikia, lakini naona unataka kutoa maelezo.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na wewe.

Mheshimiwa Mbunge asubiri tu, tutakapofika TAMISEMI atakapoona haipo, basi ana uwezo wa kutuuliza vizuri zaidi, lakini nirejee kusema na kulisita kwamba Baraza linaandaa miundombinu TAMISEMI, fedha hiyo imetengwa kupitia Baraza.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, vitabu hivi vya bajeti...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zitto, samahani, naomba ukae. Samahani, naomba ukae.

Nadhani jibu lake lililotoka, kitabu cha TAMISEMI kwa sasa hivi hatukonacho hapa. Tutaweza kuunganisha hizo hoja zote kwa pamoja; tukikiona cha TAMISEMI, huku hatujakuta, hiyo tume- record kwamba haipo. Tutakapofika TAMISEMI tusipokikuta, tutachukua kuanzia hapo.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zitto umeshauliza mara mbili tayari.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Ninakusaidia wewe, kila kitu kipo humu. Kila kitu kipo kwenye kitabu hiki.

MWENYEKITI: Ni sawa lakini TAMISEMI italetwa pia.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Haipo kwenye TAMISEMI!

MWENYEKITI: Ndiyo nasema, TAMISEMI haiko mbele yetu sasa hivi. TAMISEMI haiko mbele yetu sasa hivi! TAMISEMI italetwa, iko chini ya Ofisi ya Rais.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, taratibu za uendeshaji wa Kamati ya Matumizi Serikali inafanya kazi kama moja, haifanyi Serikali kwamba Waziri wa Kazi peke yake, Waziri wa nini peke yake, ninachokueleza ni kwamba kwenye vote zote; ya TAMISEMI na Ofisi ya Waziri Mkuu, fedha hiyo shilingi bilioni 59 haipo.

Kwa hiyo, naomba kwa sababu Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo inayosimamia suala hili la *village empowerment*, itueleze fedha hiyo iko wapi?

Waziri wa TAMISEMI yuko hapa, aeleze kama ipo kwenye kifungu chake. Kwenye vitabu humu hakuna! Angalieni vitabu, watendaji wako waangalie vitabu, haipo! *(Makofi)*

MWENYEKITI: Sawa, naomba ukae Mheshimiwa. Mheshimiwa Jenista, kabla hujasimama samahani.

Waheshimiwa wabunge, ni hivi, tukisema kwamba, kitabu kilichopo mbele yetu tuangalie na vingine vyote, Wajumbe wengine kwanza watakuwa hawajasoma, lakini pia...

(Hapa Mheshimiwa Kabwe Z. R. Zitto alisimama)

MWENYEKITI: Ngoja, ngoja Mheshimiwa Zitto umeshamaliza hoja. Kabla Mheshimiwa Waziri hajasimama, tuwekane tu sawa. Hiki tulichonacho mbele yetu, wakati utakuja tutaanza tena mafungu moja baada ya lingine tutakapoifikia TAMISEMI. Kwa hiyo, wakati huo kama kitu kimesemwa TAMISEMI sasa hivi kitabu ni hiki hiki, tutakapoifikia TAMISEMI tutaangalia hapo.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu Waheshimiwa Wabunge wanielewe. Ofisi ya Waziri Mkuu ukisema sasa tufate hii hotuba ya Waziri Mkuu halafu sasa kila fungu la Kisera alilolizungumzia tuulize kwamba, sasa kwenye kitabu chake kwenye vitabu hivi vya Ofisi ya Waziri Mkuu fungu hilo liko wapi haitakuwa ni sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafungu haya ya Waziri Mkuu yanaeleza kazi ambazo zitafanywa ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Itakapofika mafungu ya kisékta kwa hiyo, kila jambo limetengwa katika sekta litaonekana hata kama fedha hiyo haitakuwa imetengwa TAMISEMI inaweza kuwa imetengwa kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi tunacholiambia Bunge hili, fedha hiyo imetengwa na Baraza la Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi limeanza hayo maandalizi na kabla ya bajeti hii haijaisha fedha hiyo itaonekana na wananchi watapewa fedha hiyo mwaka huu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wajumbe, nimeletewa orodha na Wajumbe kutoka Kamati ya Chama cha CCM, sijapata orodha nyingine. Wajumbe hao

wako wanne; tutaanza na Mheshimiwa Neema William Mgaya ambaye anataka maelezo hapa. Mheshimiwa Neema Mgaya.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, lakini suala langu naona liko sawa, sihitaji tena kuuliza. (Makofi)

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako, kwenye Kamati ya Matumizi vyama vinatengeneza orodha? Toka lini imeanza na kwa kanuni gani?

MWENYEKITI: Kuna mshahara wa Waziri hapa Mheshimiwa Zitto.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mmeanza lini?

MWENYEKITI: Kuna mshahara wa Waziri, naomba ukae, samahani.

Waheshimiwa Wajumbe, hiki kifungu tunachokijadili kinasema *Admistration and HR Management*, kuna *salaries* ziko hapa zimetajwa na Kanuni zinataka kifungu cha kuhusu mshahara kinapofika Wajumbe waweze kusema hivyo. Utatafutiwa Mheshimiwa Zitto uwe na utulivu kidogo, tafadhali usijibizane, kikao kitakuwa hakiendi.

Waheshimiwa Wajumbe, kwa hiyo, nimeletewa orodha hapa. Kanuni nitawasomea nitakapoiangalia, lakini ipo hiyo Kanuni kwa hiyo, nitawasomea. (Makofi)

Mheshimiwa Japhet Hasunga!

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mshahara wa Waziri, nipo kwenye Programu 10, *Subvote* 1001. Katika mchango wangu wa maandishi, nilichangia kuhusu waajiri mbalimbali wa sekta binafsi ambao wamekuwa hawazingatii Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ya mwaka 2004; na hivyo nilitaka kujua kwamba Serikali inakusudia kuchukua hatua gani kwa waajiri wengi ambao wamekuwa hawazingatii hiyo sheria na hivyo kusababisha wafanyakazi wengi kufanya kazi bila barua za ajira wala mikataba ya ajira? Naomba nipate maelezo. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ni kweli Mheshimiwa Mbunge amesema sheria hiyo inatoa maagizo kwa waajiri wote wazingatie zile *labour standards* kwa mujibu wa Sheria za Kazi tulizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumekuwa tukipata shida wakati mwingine, *procedures* za kufuatwa katika kuhakikisha waajiri wanafanya *compliance* na Sheria za Kazi zimekuwa na mlolongo mrefu. Ili kuhakikisha sasa waajiri wote wanafuata sheria hizo za kazi, Wizara yetu chini ya uongozi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu tumeamua hapa katika sheria ambazo zitaletwa mbele ya Bunge lako Tukufu kuja kurekebisha tumeona ni lazima tulete sheria hiyo ili tutoe meno kwa wale Wakaguzi wetu, Maafisa Kazi ili wanapokwenda kukagua angalau wawe na uwezo pia wa kuwapiga *fine* wale Waajiri ambao wanakiuka Sheria za Kazi nchini na hiyo itatusaidia kuwafanya wengi waweze kufanya *compliance* na sheria tulizonazo.

Wakati huo huo, taratibu za kufuatwa kwenye sheria nyingine na adhabu nyingine zitakuwa zinaendelea kuchukuliwa kwa mujibu wa sheria. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Maida Abdallah.

MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Niko kwenye Mshahara wa Waziri Programu 10. Napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba katika mkakati wa Serikali sasa hivi ni kufufua viwanda au ni uendelezaji wa viwanda.

Nilitaka kumwuliza kwamba katika mkakati huo, bajeti ya mwaka huu 2016/2017 Serikali imejipanga vipi au imetenga fedha kiasi gani katika uendelezaji na ufufuaji wa viwanda? Kwa sababu viwanda vinahitaji gharama kubwa, fedha nyingi, lakini pia kuwa na uhakika wa ajira ya wananchi nchini. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti kwa ajili ya maendeleo ya viwanda na sekta ya viwanda nchini, itakuja kutolewa taarifa yake vizuri atakapofika mbele ya Bunge lako Mheshimiwa Waziri anayehusika na sekta ya viwanda katika nchi yetu ya Tanzania.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Janet Mbene!

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Niko kwenye Programu 10, fungu la 1001. Langu ni suala la mfumo wa mpango mzima wa maendeleo. Ninachelea kusema kuwa sioni mahali ambako tumezingatia masuala ya wanawake na jinsia kiasi kwamba tunajikuta kuwa hatuna hakika katika mipango yote ya maendeleo wanawake watafaidika kwa kiasi gani, wanaume kwa kiasi gani, vijana na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tuna Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ambayo iliainisha kabisa kwamba katika kila mpango wa maendeleo, ni lazima Wizara zote, Idara zote, Taasisi zote zizingatie ushiriki wa wanawake katika kila hatua ya maendeleo na kwa hali hiyo, kuweka mipango mahususi itakayozingatia maendeleo ya wanawake katika kila eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tumejikita katika BRN ambayo itaharakisha maendeleo ya nchi hii, tumejikita katika maendeleo ya viwanda, sasa wanawake ambao ni asilimia zaidi ya 51 nchi hii; wanawake ambao ni wazalishaji karibu 80% vijijini, wanaozalisha asilimia 60 ya chakula cha nchi nzima, wao wako wapi katika mpango huu ili kuhakikisha kuwa wametengewa Bajeti, mafunzo, nyenzo, pembejeo na vitu vyote ambavyo vinahitajika katika kukuwakuza kimaendeleo? Kwasababu wao ni wachangiaji wakubwa sana wa maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara au Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo inayotoa mwongozo kwa Wizara nyingine zote. Kama Ofisi ya Waziri Mkuu haijaainisha hiyo kwa uwazi kabisa, nachelea kusema, hata Wizara nyingine zitakuwa hazijaweka hii; na hii ina maana kuwa hata Bajeti itakayokuwa imewekwa, haitazingatia mchango mahususi wa wanawake. Naomba hilo lizingatiwe na tuambiwe hapa ni kiasi gani Bajeti hii italenga wanawake. Ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Janet Mbene kwa kuwa mpiganaji imara kabisa wa kuhakikisha usawa wa kijinsia unazingatiwa katika shughuli zote za maendeleo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali tunatambua mchango wa wanawake katika maendeleo ya nchi yetu ya Tanzania; na hivyo basi, tumekuwa tukitafsiri sera zile zote ambazo zinawagusa wanawake kwa namna moja ama nyingine; na maagizo ya Serikali yameshakutolewa kwamba kila

Wizara, kila Idara, kila Taasisi ya umma ihakikishe kunakuwa na *focal person* ambaye ataendesha Dawati la Jinsia katika eneo lake na hivyo atatafsiri kila mpango wa kibajeti katika eneo lake la kazi kuhakikisha kwamba wanawake wanapewa kipaumbele. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano halisi wa jambo hili unajitokeza pia katika suala zima la *own source* ambazo zimekuwa zikipatikana kwenye *local government*, 5% imekuwa ikitengwa kwa vijana na 5% imekuwa ikitengwa kwa wanawake. Kwa hiyo, tunaomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa madawati hayo ya jinsia, kazi hiyo imekuwa ikifanyika na tutaomba tu Waheshimiwa Wabunge tuendeleo kushirikiana na sisi kama Serikali tutaendelea kusimamia hilo ili kuwapa haki wanawake wa Tanzania kwa sababu wana mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi yetu. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Janet Mbene!

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu, lakini hayo ndiyo majibu ambayo yamekuwepo kwa miaka yote. Sasa tupo katika *mode* ya kuruka. Sasa hivi tupo katika *mode* ya maendeleo ya kasi na tunafanya kazi tofauti na mazoea yetu. Naomba ioneshwe wazi, asilimia ngapi itakwenda kwa wanawake? Ajira ngapi zitakuwa *created* kwa wanawake? Wanawake wangapi watapata mafunzo, hata kama ni kwa *percentage*? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kusema kuna Madawati, hakuna Dawati hata moja linalofanya kazi kenye Wizara zetu. Mimi nilikuwa Naibu Waziri, najua. Hakuna Madawati hayo! Tusizungumzie nadharia, sasa hivi tuko kwenye utekelezaji na utendaji wa maendeleo na hii nchi lazima iendeleo; na iendeleo kwa kushirikisha wananchi wake wote pamoja na wanawake. Zaidi ya asilimia 51 hamwezi kuwapuuzia jamani, lazima sasa mwabebe nao washiriki katika maendeleo. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tu Mheshimiwa Janet Mbene anataka kuendelea tu kutusisitiza kama Serikali kwamba ni lazima tuhakikishe tunalisimamia eneo hilo vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uwepo wa Madawati. Madawati hayo yapo na yamekuwa yakifanya kazi na wako wanawake wamekwenda na wamekutana na hayo Madawati na wamehudumiwa. Mfano mwingine, sasa

hivi tuna Dawati zuri sana liko kwenye Jeshi la Polisi Tanzania. Limekuwa likifanya kazi nzuri, likisimamia unyanyasaji wa wanawake katika maeneo mbalimbali nchini. Kwa hiyo, hiyo ni mifano ya Madawati ambayo tumekuwa nayo na yakiendelea kufanya kazi za kusimamia masuala ya akina mama. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunapitisha Mpango wa Maendeleo wa mwaka mmoja na wa muda mrefu, masuala ya usawa wa kijinsia yamejitokeza na Waheshimiwa Wabunge mkirejea kwenye zile *documents* za Mpango mtaona ni kwa kiasi gani Serikali iliyazingatia hayo masuala ya usawa wa kijinsia katika Mpango wetu wa Maendeleo.

Hata hivyo, Serikali inaendelea kuchukua ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na kubwa kwetu tutaendelea kuhimizana kusaidia kusimamia na kuhakikisha Madawati hayo yanafanya kazi ili Bajeti za nchi yetu ziwahudumie wanawake kama inavyotakikana. (Makofi)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wajumbe, kulitokea hoja hapa ya Kikanuni kwamba ni kanuni ipi inataka vyama ndiyo vilete orodha. Kanuni ya 101(3) na ya (4) nitazisoma. Kanuni ya (3): "Mbunge atakayeamua kutumia kifungu chenye mshahara wa Waziri ataruhusiwa tu iwapo ataomba ufafanuzi wa suala mahususi la sera na hatazungumzia zaidi ya jambo moja."

Kanuni ya (4); "Kwa kuzingatia masharti ya fasiri ya (3), Kamati za Vyama zitawasilisha kwa Spika majina ya Wabunge watakaomba kupata ufafanuzi wa suala mahususi la sera na Spika atatoa nafasi kwa Wabunge kwa kuzingatia uwiano." Kwa hiyo, Kanuni ya 101, kifungu cha (3) na cha (4) kinavitaka Vyama vilete orodha, isipokuwa kwa chama sasa kama ACT na chama NCCR-Mageuzi wao wako mmoja mmoja, wanaweza kujileta majina yao wao wenyewe. Waheshimiwa Wajumbe. (Makofi/Vigelelele)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 - Finance and Accounts	Sh. 1,030,002,000/=
Kif. 1003 - Policy and Planning.....	Sh. 4,355,225,000/=
Kif. 1004 - Internal Audit Unit.....	Sh. 327,753,000/=
Kif. 1005 - Govn't Commun. Unit.....	Sh. 259,898,000/=
Kif. 1006 - Procurement Mgt Unit.....	Sh. 385,405,000/=
Kif. 1007 - Legal Service Unit	Sh. 191,350,000/=
Kif. 1008 - Mgt Inform. Syst. Unit.....	Sh. 219,602,000/=
Kif. 2001 - Civil Affairs & Contingencies.....	Sh. 4,269,428,000/=
Kif. 2002 - National Festivals.....	Sh. 708,496,000/=

Kif. 3001 - Parliamentary & Political Affairs.....	Sh. 645,649,000/=
Kif. 4001 - Investment & Private Sector Development.....	Sh. 3,452,787,000/=
Kif. 5001 - Coordination of Govn't Business.....	Sh. 828,214,000/=
Kif. 7001 - Government Printer.....	Sh. 3,857,590,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Fungu 61-Tume ya Taifa ya Uchaguzi

Kif. 1001 - Admin. & HR Management.....	Sh. 1,481,494,000/=
Kif. 1002 - Planning, Monitoring and Evaluation Division.....	Sh. 148,500,000/=
Kif. 1003 - Finance and Accounts Unit.....	Sh. 209,480,000/=
Kif. 1004 - Internal Audit Unit.....	Sh. 180,984,000/=
Kif. 1005 - Legal Service Unit.....	Sh. 131,824,000/=
Kif. 1006 - Procurement Mgt & Logistics Unit.....	Sh. 178,647,400/=
Kif. 2001 - Election Mgt Division.....	Sh. 202,964,000/=
Kif. 2002 - Permanent National Voters Registration System Division....	Sh. 381,652,000/=
Kif. 2003 - Voters Education and Public Information Division.....	Sh. 230,268,600/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Fungu 65 - Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu)

Kif. 1001 - Administration & HR Mgt.....	Sh. 2,795,925,200/=
Kif. 1002 - Finance and Accounts.....	Sh. 257,728,000/=
Kif. 1003 - Policy and Planning.....	Sh. 182,031,800/=
Kif. 1004 - Internal Audit Unit.....	Sh. 108,844,000/=
Kif. 1005 - Procurement Mgt Unit.....	Sh. 57,880,000/=
Kif. 1006 - Govt. Comm. Unit.....	Sh. 87,940,000/=
Kif. 1007 - Information and Comm. Techn. Unit.....	Sh. 10,000,000/=
Kif. 1008 - Legal Service Unit.....	Sh. 10,000,000/=

Kif. 2001 - Labour.....	Sh. 5,284,210,000/=
Kif. 2002 - Employment Division.....	Sh. 1,900,050,000/=
Kif. 2003 - Registrar of Trade Unions.....	Sh. 82,240,000/=
Kif. 2004 - Arusha Regional Labour Office.....	Sh. 2,955,000/=
Kif. 2005 - Dodoma Regional Labour Office.....	Sh. 2,955,000/=
Kif. 2006 - Geita Regional Labour Office	Sh. 0
Kif. 2007 - Iringa Regional Labour Office.....	Sh. 2,955,000/=
Kif. 2008 - Kagera Regional Labour Office.....	Sh. 2,955,000/=
Kif. 2009 - Kigoma Regional Labour Office.....	Sh. 2,955,000/=
Kif. 2010 - Kilimanjaro Regional Labour Office.....	Sh. 2,955,000/=
Kif. 2011 - Lindi Regional Labour Office.....	Sh. 2,945,000/=
Kif. 2012 - Manyara Regional Labour Office.....	Sh. 0
Kif. 2013 - Mara Regional Labour Office.....	Sh. 2,955,000/=
Kif. 2014 - Mbeya Regional Labour Office.....	Sh. 2,955,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba tuwe tunajibu
kukubaliana na hivi vifungu.

Kif. 2015 - Morogoro Regional Labour Office.....	Sh. 2,955,000/=
Kif. 2016 - Mtwara Regional Labour Office.....	Sh. 2,955,000/=
Kif. 2017 - Mwanza Regional Labour Office... ..	Sh. 2,955,000/=
Kif. 2018 - Njombe Regional Labour Office....	Sh. 2,955,000/=
Kif. 2019 - Pwani Regional Labour Office.....	Sh. 2,955,000/=
Kif. 2020 - Rukwa Regional Labour Office.....	Sh. 2,955,000/=
Kif. 2021 - Katavi Regional Labour Office.....	Sh. 0
Kif. 2022 - Ruvuma Regional Labour Office... ..	Sh. 2,955,000/=
Kif. 2023 - Shinyanga Regional Labour Office.....	Sh. 2,955,000/=
Kif. 2024 - Simiyu Regional Labour Office.....	Sh. 0
Kif. 2025 - Singida Regional Labour Office... ..	Sh. 2,955,000/=
Kif. 2026 - Tabora Regional Labour Office.....	Sh. 2,955,000/=
Kif. 2027 - Tanga Regional Labour Office.....	Sh. 2,955,000/=
Kif. 2028 - Temeke Regional Labour Office....	Sh. 2,955,000/=
Kif. 2029 - Kinondoni Regional Labour Office.....	Sh. 2,955,000/=
Kif. 2030 - Ilala regional Labour Office.....	Sh. 2,955,000/=
Kif. 2031 - Social Security Division.....	Sh. 78,132,000/=

Kif. 2032 - Youth Development..... Sh. 438,260,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Fungu 91- Tume ya Kudhibiti Dawa za Kulevya

Kif. 2001 - Administration & HR Mgt..... Sh. 2,340,236,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Fungu 92 - Tume ya Kudhibiti UKIMWI

Kif.1001 - Administration & HR Mgt..... Sh. 143,773,000/=

Kif.1002 - Finance Admn & Resource

Mobilisation.....Sh. 3,471,342,000/=

Kif.1003 - Monitoring, Evaluation,

Research & Mis..... Sh. 146,328,000/=

Kif.1004 - Advocacy, Information,

Education and Com..... Sh. 100,320,000/=

Kif.1005 - District and Community

Response..... Sh. 736,308,000/=

Kif.1006 - Procurement & Mgt Unit..... Sh. 54,972,000/=

Kif.1007 - Legal Unit.....Sh. 39,480,000/=

Kif.1008 - Mgt Information System..... Sh. 78,030,000/=

Kif.1009 - Internal Audit Unit..... Sh. 101,676,000/=

Kif.1010 - Social Programs..... Sh. 53,028,000/=

Kif.1011 - Government Comm.....Sh. 36,420,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

MATUMIZI YA MAENDELEO

Fungu 37- Ofisi ya Waziri Mkuu

Kif. 1001 - Administration &HR Mgt..... Sh. 4,500,000,000/=

Kif. 1003 - Policy and Planning..... Sh. 3,027,000,000/=

Kif. 2001 - Civil Affairs &ContingenciesSh. 2,471,970,000/=

Kif. 4001 - Investment and Private

Sector DevelopmentSh. 30,498,699,000/=

Kif. 5001 - Coordination of
Government Business.....Sh. 99,819,951,000/=

Kif. 7001 - Government PrinterSh. 150,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Fungu 61 – Tume ya Taifa ya Uchaguzi

Kif. 1002 - Planning, Monitoring and EvaluationSh. 0

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Fungu 65 - Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu)

Kif. 1003 - Policy and PlanningSh. 1,489,531,184/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 - Employment DivisionSh. 15,000,000,000/=

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Sasa mbona mna haraka sana!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Peter Serukamba!

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda angalau twende taratibu, maana tunakwenda haraka sana. Nilitaka kuuliza hapa kwenye suala la mambo ya pensheni, sasa sijui naweza nikauliza hapa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Peter Serukamba, pensheni kwenye maendeleo au? Kwa sababu tulishapita kile kitabu kingine. Hiki tuko cha maendeleo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kif. 2032 - Youth DevelopmentSh. 1,000,000,000/=

MBUNGE FULANI: Rudia!

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wajumbe, kuna hebu ngoja asome tena Katibu huo ukurasa halafu tuangalie kwenye vitabu vyetu kama upo.

MBUNGE FULANI: Ni 2032!

NDG. NENELWA M. WANKANGA - KATIBU MEZANI: Ukurasa 141 Fungu 65, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi Ajira Vijana na Watu wenye Ulemavu. Cha kwanza ni 1003 shilingi 1,489,531,184/=.

MWENYEKITI: Hicho tumeshakiafiki.

NDG. NENELWA M. WANKANGA – KATIBU MEZANI: Kinachofuata ni 2002 shilingi 15,000,000,000/=

MWENYEKITI: Kimeshaafikiwa!

NDG. NENELWA M. WANKANGA – KATIBU MEZANI: Kinachofuata ni 2032 shilingi 1,000,000,000/=.

MWENYEKITI: Sawa.

MHE. KANGI A. N. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kangi Lugola, unaongelea kifungu kipi?

MHE. KANGI A. LUGOLA: Niko hapo kwenye *Subvote 2032 Youth Development*, kwenye ile Kasma 4945, kwenye ile shilingi bilioni moja ya *Youth Development Fund*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na matatizo kwenye fedha ambazo zinatengwa kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na kama mtakumbuka, Bungeni hapa tuliwahi kupitisha kwamba ziwe zinatengwa shilingi bilioni tatu; na hasa ukizingatia kwamba kwenye Halmashauri kule ambako nako wanatakiwa wachangie 5% kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kumekuwa na shida kubwa sana, fedha hazitengwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kujua hii shilingi bilioni moja, kama kweli tuna dhamira ya dhati ya kuhakikisha kwamba vijana ambao tunakazania ajira wanaweza kupata fedha kwenye mfuko huu kwa shilingi bilioni moja. Nataka nipate ufafanuzi kama ile shilingi bilioni tatu tuliyosema kwa nini haitengwi, ni bilioni moja?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, kasma hii imetengewa shilingi bilioni moja na Serikali ukiangalia imeanza kutenga kwenye kifungu hicho baada ya kukihamisha kutoka kwenye ile iliyokuwa Wizara inashughulikia maendeleo ya vijana; ile ya kule nyuma. Tumetenga kwa mwaka huu Shilingi bilioni moja. Serikali itakuwa inaendelea kuongeza fedha kila pale ambapo fursa itakuwa inapatikana ya kuongeza fedha kwenye kifungu hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, fedha ambazo zimekuwa zikitumika kuwakopesha vijana wetu, nyingine pia zimekuwa zikipatikana kutoka katika mafungu mbalimbali. Kwa mfano, tumesema hapa tuna ule Mfuko wa Wanawake na Vijana kupitia Halmashauri za Wilaya; na wenyewe kama tutaosimamia ile 5% ya vijana na 5% ya wanawake itengwe, fedha ni nyingi sana ukiangalia kwenye zile *own source* za Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Vilevile wakati tunatoa hesabu zetu, mmeona kabisa na Baraza la Uwezesaji Wananchi Kiuchumi na lenyewe lina programu kama *program* ya *Young Graduates* katika kuhakikisha kwamba mikopo hiyo inatolewa. Kwa hiyo, nawaomba tu Waheshimiwa Wabunge, wanapooona kwamba vijana wao wako tayari, watafute namna ya kuwasiliana na sisi halafu tunaweza tukawa tunabadilishana uzoefu wa kuona vijana waende wapi ili wawezeshwe kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, katika tengeo lililopita kwenye miaka ya nyuma, Halmashauri ziliagizwa zianzisha SACCOS za vijana ili waweze kupata hii mikopo, lakini taarifa tulizonazo kwenye Ofisi zetu, Halmashauri nyingi hazikuanzisha hizo SACCOS na wala hazikwenda kuchukua hiyo mikopo kwa ajili ya kuwaendeleza vijana.

Kwahiyo, naomba nitumie nafasi hii pia tuwaombe sana wale wanaosimamia maendeleo ya vijana kwenye Halmashauri zetu wawe wanatekeleza maagizo kusudi hela zinapokuwa zimepatikana ziweze kuwa zinawafikia vijana wetu kwa wakati na kuwasaidia katika shughuli zao za maendeleo.

MWENYEKITI: Kifungu kinaafikiwa?

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kabla Katibu hajaendelea, tukumbushane tu; tujitahidi, Katibu anapokuwa anasoma, kama ni hicho kifungu ambacho una jambo, usimame kwa haraka kwa sababu tukishahoji haiwezekani tena kufungua mjadala. Katibu!

Fungu 91 - Anti Drug Commission

Kif. 5497 - *Implementation of HIV/AIDS Against IDU's* Sh. 0

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Fungu 92 – Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI

Kif. 1001 - *Administration and HR Mgt* Sh. 664,697,500/=

Kif. 1002 - *Finance, Admin. &*

*Resource Mobilization.....*Sh. 3,051,625,000/=

Kif. 1003 - *Monitoring, evaluation,*

Research and Mis Sh. 309,156,831/=

Kif. 1004 - *Advocacy, Information*

*Education &Comm.....*Sh. 774,547,950/=

Kif. 1005 - *District & Comm. Response.....*Sh. 378,763,000/=

Kif. 1006 - *Procurement Mgt Unit.....*Sh. 0

Kif. 1007 - *Legal Unit*Sh. 0

Kif. 1008 - *Management Information Systems* Sh. 0

Kif. 1009 - *Internal Audit Unit*Sh. 0

Kif. 1010 - *Special Programs*Sh. 57,033,132/=

Kif. 1011 – *Government Communication Unit.....* Sh. 0

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

(Bunge lilirudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa hoja, taarifa. *(Makofi)*

T A A R I F A

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU): Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi zake. Naomba sasa taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge lako Tukufu. Naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu
kwa mwaka 2016/2017 yalipitishwa na Bunge)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, makadirio ya Ofisi ya Waziri Mkuu yamepitishwa na Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nichukue fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu na fimu yake yote kwa kuleta bajeti ambayo imekubalika na Waheshimiwa Wabunge, lakini pia nitoe wito sasa kwa watendaji walio chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuweza kuitekeleza bajeti hii ambayo imepitishwa na Bunge siku ya leo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kutoa pongezi hizo, nasitisha Bunge mpaka saa 10.00 jioni. *(Makofi)*

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo!

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mwongozo huwezi kuomba mimi nikiwa nimesimama.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Naibu Spika, nilisimama, labda hujaniona.

NAIBU SPIKA: Mimi nimesimama, wewe pia huwezi kusimama ili uombe Mwongozo. Ndiyo Kanuni zinavyosema.

Waheshimiwa Wabunge, nimesitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni.

(Saa 6.33 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 10.00 jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Anderw J. Chenge) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa tuketi. Katibu!

NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI: Hoja za Serikali, Hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Utumishi na Utawala Bora kwamba Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2016/2017

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuiona siku ya leo tukiwa na afya njema na kipekee kabisa napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais, John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuiteua niongoze Ofisi yake kwa upande wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa namna ya pekee nimshukuru Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, pamoja na Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na maelekezo wanayotupatia katika kutekeleza majukumu yetu ya kutoa huduma bora kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nashukuru na kuipongeza Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa yaani LAAC kwa kutusimamia na kupitia hesabu za Serikali za Mitaa kwa umakini na kwa ukaribu na Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Mbunge; Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na viongozi wote kwa nyadhifa mbalimbali walizozipata kutokana Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa tena kuiongoza Zanzibar. Nawapongeza pia Wabunge wote wa Bunge la Kumi na Moja kwa kushinda uchaguzi na kuwawakilisha wananchi

katika chombo hiki muhimu cha kutunga sheria za nchi na kusimamia Serikali. Nawapongeza pia wote waliopata nafasi ya kuteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali, katika Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo, ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge na Tawala za Serikali za Mitaa, naomba kutoa kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likae, lipokee na lijadili na kupitisha Mpango wa Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mikoa na Halmashauri, yatasomeka kama yalivyoelezwa katika kitabu cha hotuba yangu ukurasa wa tatu hadi wa sita.

Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa, ziliidhinihiwa shilingi trilion 5.4 kwa ajili ya mishahara, matumizi mengineyo na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 395.588 ni kwa ajili ya Ofisi ya Rais TAMISEMI, shilingi bilioni 255.88 na shilingi 4,766,700,533,000/= ni kwa ajili ya mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilikadiria kukusanya shilingi 13,503,000/= hadi mwezi Machi, 2015 Ofisi imekusanya shilingi 1,650,000/= sawa na asilimia 12 ya makadirio. Maduhuli yanatokana na uuzaji wa nyaraka za zabuni. Maduhuli yamekuwa kidogo kutokana na kutokupatikana kwa fedha za maendeleo, hivyo ni zabuni chache tu ziliweza kuuzwa. Kwa upande wa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI zilikadiriwa kukusanya mapato ya shilingi bilioni 7.5 hadi mwezi Machi, 2016 lakini ni shilingi bilioni 5.092 ndizo zilizokusanywa sawa na asilimia 67 ya makadirio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Mikoa ilikadiria kukusanya shilingi milioni 225.7 kama maduhuli lakini hadi mwezi Disemba, 2015 kiasi cha shilingi bilioni 225.05 zilikusanywa sawa na asilimia 99.7. Maduhuli ya Mikoa yanatokana na mishahara isiyolipwa, tozo la pango kwenye nyumba za Serikali na mauzo ya nyaraka za zabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Mamlaka ya Serikali za Mitaa zilikadiria kukusanya shilingi bilioni 521.8, kama mapato ya ndani. Hadi mwezi Februari, 2016 jumla ya shilingi bilioni 231.6 zilikuwa zimekusanywa sawa na asilimia 44 na kwa upande wa mamlaka ya Serikali za

Mitaa makusanyo yanatokana na kodi na ushuru mbalimbali zinazotozwa katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa utekelezaji wa majukumu ya Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa, unazingatia misingi ya utawala bora, tarehe 23 Disemba, 2015 nilitoa Waraka Namba 13 ambao uliwaelekeza Wakuu wa Mikoa, kuacha kufanya kazi kwa mazoea na badala yake kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu ili kuboresha utoaji wa huduma bora kwa Umma.

Aidha, Waraka huo umetoa maelekezo kuhusu kuhimiza kuendelea na zoezi la kufanya usafi katika maeneo yao pamoja na usimamizi wa zoezi la kutoa elimu msingi bila malipo. Maelekezo yote niliyotoa yanaendelea kutekelezwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Watumishi wa Umma, wanaofanya kazi katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa, hatua mbalimbali zimechukuliwa kuhakikisha kuwa kunakuwepo na uwajibikaji thabiti. Hatua hizo ni pamoja na kuboresha misingi ya mifumo ya uwajibikaji na kuchukua hatua stahiki na kwa wakati kwa Watumishi wanaobainika kukiuka sheria, kanuni na taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2014/2015 watumishi 78 wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa wamechukuliwa hatua mbalimbali za kinidhamu na kijinai. Kati ya watumishi hao wamo Wakuregenzi, Wakuu wa Idara na watumishi wa kawaida. Aidha, katika mwaka wa fedha 2015/2016 watumishi waliochukuliwa hatua mbalimbali za kinidhamu na wengine kufikishwa Mahakamani ni 90. Hatua zilizo chukuliwa pamoja na watumishi husika zinapatikana katika hotuba yangu ukurasa wa kumi aya ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 12 Februari, 2015 muundo mpya wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ulipitishwa ili kukidhi mabadiliko mbalimbali ya majukumu hususan katika eneo la usimamizi wa rasilimali fedha ambapo Idara ya Ukaguzi na Ufuatiliaji wa Fedha ilianzishwa.

Lengo la kuanzishwa kwa Idara hii ni kuimarisha usimamizi katika Sekretarieti na Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kufanya ukaguzi katika mifumo uendeshaji, usimamizi na ufatiliaji wa masuala ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Machi, 2016 kaguzi maalum zilifanyika katika Manispaa za Ilemela, Kigoma, Ilala na Halmashauri ya Wilaya ya Nzega, Magu na Uyui. Vilevile ukaguzi wa kawaida ulifanyika katika Serikali

za Mikoa ya Tabora na Halmashauri ya Igunga na Uvinza. Kaguzi hizi zimebaini upungufu katika kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za matumizi ya fedha, manunuzi na kutokuzingatiwa kwa kanuni za miongozo ya kisekta; na wote waliohusika na upungufu huo wamechukuliwa hatua za kinidhamu na mamlaka zao za nidhamu. Aidha, ushauri uliotolewa katika Halmashauri hizo ili kurekebisha upungufu uliosababishwa na kaguzi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ufuatiliaji umefanyika katika Halmashauri za Mkoa wa Dodoma na kubaini kwamba kuna idadi ndogo ya wanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii na usimamizi hafifu kwa matumizi ya mfuko huo. Ushauri pia wa jinsi ya kuboresha uendeshaji na usimamizi wa Mfuko wa Afya ya Jamii, umetolewa kwa lengo la kuongeza idadi ya wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha azma ya Serikali, Awamu ya Tano kupitia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 Ibara ya 148 (d) na (f), Ofisi ya Rais, TAMISEMI, itaendelea kufanya ukaguzi wa ufanisi kawaida, maalum na ufuatiliaji wa kina katika Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa ili kuboresha utendaji kazi na hivyo kupata dhamani ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuhakiki na kulipa madeni ya watumishi wakiwemo walimu na wasiokuwa walimu kadri itakavyojitokeza. Hadi mwezi Oktoba, 2015 jumla ya shilingi bilioni 20,125 zimelipwa kwa watumishi wa umma. Serikali itaendelea kulipa madeni ya watumishi baada ya kuyahakiki na Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinaelekezwa kuwa waangalifu ili kuzuia uzalishaji wa madeni mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia mwaka wa fedha 2014/2015 hadi Machi, 2016 maeneo ya utawala mbalimbali yameanzishwa ikiwa ni pamoja na Mkoa mmoja wa Songwe na Wilaya sita ambazo ni Songwe, Kigamboni, Ubungo, Malinyi, Tanganyika na Kibiti. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi Morogoro na Chalinze - Pwani na Ifigi - Singida na Halmashauri za Miji ya Ifakara, Bunda, Mbulu, Kondoa, Newala na Mbinga pia zilianzishwa katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 30 Machi, 2016 Tanzania Bara ina Mikoa 26, Wilaya 139, Halmashauri 181, Tarafa 562, Kata 3,963, Mitaa 4,037, Vijiji 12,545 na Vitongoji 64,677. Lengo la kuanzisha maeneo hayo ya utawala ni kusogeza huduma karibu na wananchi na kuongeza kasi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa Halmashauri zinakuwa na uwezo wa kifedha ambao utaziwezesha kutimiza majukumu yao ipasavyo, hatua mbalimbali zimechukuliwa ili kuboresha makusanyo ya mapato ya ndani.

Hatua hizo ni pamoja na kufunga na kutumia mifumo ya kielekitroniki ya ukusanyaji na usimamizi wa mapato. Mifumo hiyo imeunganishwa na mifumo ya malipo kama vile Mabenki, M-Pesa, TIGO Pesa, Airtel Money ili kurahisisha ulipaji wa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeendelea kuratibu na kutoa utaaalam wa kiufundi katika miundombinu ya mfumo na TEHAMA katika ngazi ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mikoa, Halmashauri na kuwajengea uwezo Watumishi. Hadi Februari, 2016 Mamlaka ya Serikali za Mitaa 133 zimekuwa zikiendelea kutumia mfumo wa Epicor Toleo la 9.05 bila matatizo. Malipo yote kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa yanafanyika kwa utaratibu wa akaunti tisa kama ilivyoelekeza. Kwa kutumia mifumo hiyo, Halmashauri zimeweza kutekeleza majukumu kwa kufuata taratibu na miongozo iliyotolewa na Wizara ya Fedha. Aidha, taarifa za mapato na matumizi ya kila mwezi zinapatikana kutoka kwenye mifumo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mifumo ya ukusanyaji mapato, hadi mwezi Machi, 2016 Halmashauri 138 sawa na asilimia 74 zimekamilisha ufungaji na zimeanza kutumia mifumo ya kielekitroniki ya ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na Halmashauri nyingine 48 sawa na asilimia 26 zipo katika hatua mbalimbali. Matumizi ya mifumo hiyo imepunguza mianya ya ufujaji na upotevu wa mapato.

Hata hivyo, katika kuhakikisha mifumo mbalimbali ya kielektroniki inafanya kazi ipasavyo, Ofisi yangu kupitia Programu ya Maboresho ya Fedha za Umma Awamu ya Pili, imezijengea uwezo Halmashauri kwa kuziwezesha kufunga na kutumia mifumo ya mapato ijulikanayo kama *Local Government Revenue Collection Information System* na *I-Tax*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya mifumo ya kielektroniki imeonesha faida na mafanikio makubwa katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri. Kwa mfano, mapato ya ndani ya Halmashauri ya Jiji la Arusha yaliongezeka kutoka shilingi bilioni tano kwa mwaka wa fedha 2012/2013 hadi shilingi bilioni 10 kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Mapato ya Halmashauri ya Mtwara Mikindani yaliongezeka kutoka shilingi milioni 600 kwa mwaka 2013/2014 hadi shilingi bilioni 2.6 kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sanjari na matumizi ya kielekitroniki, katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri, Serikali pia zimefanyia marekebisho Sheria za Fedha za Serikali za Mitaa sura namba 290 na Sheria ya Kodi ya majengo. Hii yote inafanyika ili kuongeza wigo wa mapato ya Halmashauri, kwa kurejesha ushuru wa nyumba za kulala wageni na kuzipa

mamlaka Halmashauri za Wilaya kutoza na kukusanya kodi za majengo hayo. Kwa upande wa uthamini, sheria imeruhusu kufanya *mass valuation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mafanikio hayo, napenda kuchukua nafasi hii, kuagiza kuwa ifikapo tarehe 1 Julai, 2016 Halmashauri zote nchini ziwe zimefunga na kutumia mifumo ya kielektroniki katika kukusanya mapato yake ya ndani. Aidha, naziagiza Halmashauri kwamba mara baada ya mikataba ya sasa kwisha, ukusanyaji wa mapato kwa njia ya mawakala usitishwe na badala yake makusanyo yafanywe na Maofisa wa Halmashauri kwa kutumia mifumo ya kielektroniki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa maendeleo ya miji, pamoja na kwamba chimbuko la miji ni vijiji, kwa kipindi kirefu msisitizo wa kisera wa uendelezaji wa ardhi ulielekezwa zaidi mijini. Ongezeko la idadi ya watu, mara tatu katika sensa ya mwaka 1967, watu milioni 12.3 na mwaka 2012 watu milioni 44.9 limefanya vijiji viongezeka. Katika kipindi hicho, idadi ya wakazi mijini imeongezeka mara tano kutoka asilimia 5.7 hadi kufikia asilimia 29.1. Kuna sababu mbalimbali zilizofanya watu wengi kuhamia mijini, zikiwemo za kijamii na kiuchumi. Hii imesababisha kuwepo kwa migogoro mingi inayohusiana na uendelezaji wa ardhi na utoaji wa huduma mbalimbali mijini. Idadi ya Majiji, Manispaa, Miji na Wilaya nimeainisha katika kitabu cha hotuba yangu ukurasa wa 17 aya ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa vijiji, katika mwaka wa fedha 2014/2015, vijiji 1,550 sawa na asilimia 12.4 na vijiji 12,545 vilivyopo nchini vilikuwa vimeandaliwa mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya matumizi bora ya ardhi. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, vijiji 53 viliandaliwa mpango wa matumizi ya ardhi, lengo ni kufanya vijiji kuwa ni sehemu bora ya kuishi na kuondoa dhana kuwa maisha bora yako mijini tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza Sera ya Maendeleo Vijijini, sanjari na uendelezaji wa miji, Ofisi Rais, TAMISEMI, imeandaa rasimu ya sera, maendeleo ya Miji, ambapo iko katika kwenye hatua za mwisho. Sera hii itakuwa kiunganishi katika kuendeleza sawia maendeleo ya vijijini na mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ilitoa maelekezo kwa mamlaka ya Serikali za Mitaa kuandaa na kutekeleza mipango ya jumla, (*General Planning Schemes*) ya uendelezaji wa Miji kwa kupima na kumilikisha viwanja vya makazi, biashara, viwanja vya maeneo ya Umma, pamoja na kuandaa mipango shirikishi ya matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa Miji 26 ipo katika hatua mbalimbali, manispaa 15, miji midogo sita na majiji yote matano kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ukurasa wa 18 aya ya tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kurahisisha kazi ya kuwa na kumbukumbu sahihi za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeanza kutumia mfumo wa taarifa za kijiografia (*Geographical Information System*) katika kuandaa mipango ya jumla ya uendelezaji wa miji, mipango shirikishi ya matumizi bora ya ardhi. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 uthamini wa majengo 38,000 umefanyika nchini katika mradi wa *Tanzania Strategic Cities Project* unaotekelezwa kwenye miji minane ya kimkakati. Halmashauri nyingine zipo kwenye hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya TAMISEMI imeunda Baraza la Uthamini (*Rating Valuation Tribunal*) ambalo jukumu lake ni kusikiliza malalamiko ya uthamini wa majengo ili kuhakikisha kwamba taratibu za kutoza kodi za majengo kwa viwango vya uthamini zinazingatiwa. Hadi sasa malalamiko 107 yamepokelewa na kusikilizwa katika majengo 38,000 yaliyothaminiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano pamoja na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, imeandaa Mwongozo wa Anuani za Makazi utakaotumika kwenye utekelezaji wa Mpango wa Anuani za Makazi (*Post Code*) kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa utakaoanza kutekelezwa kuanzia mwaka wa fedha 2016/2017. Utekelezaji wa mpango huu utawezesha wananchi wote nchini kuwa na anuani halisi za makazi, biashara na kumbukumbu zao katika ulipaji wa kodi na vifo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zinazofanywa na Mfuko wa Barabara ni kuratibu, kuandaa mipango, ufuatiliaji, kutoa miongozo, msaada wa kiufundi na kutafuta vyanzo vya fedha kwa ajili ya kazi za matengenezo ya barabara na madaraja. Mamlaka ya Serikali za Mitaa zina mtandao wa barabara wenye urefu wa kilometa 108,946. Kwa sasa barabara zilizo katika hali nzuri ya kuridhisha ni kilometa 61,798 sawa na 57%. Barabara za lami ni kilometa 1,325 sawa na 1.2% na barabara za changarawe ni kilometa 22,089 sawa na 20.3%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mikakati iliyopo ni kuziimarisha barabara za Mamlaka za Serikali za Mitaa ili barabara ziwe katika hali nzuri na ya kuridhisha na zibaki katika hali hiyo nzuri. Vilevile kuendelea kuinua hali ya barabara za mijini kuwa za lami kupitia fedha za Mfuko wa Barabara, Benki ya Dunia, Shirika la Maendeleo la Kimataifa Uingereza (*DFID*), Jumuiya ya Ulaya (*EU*) na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (*USAID*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Serikali ilitenga shilingi bilioni 257.75 kwa ajili ya shughuli za matengenezo ya barabara. Hadi mwezi Machi mwaka 2016 jumla ya shilingi bilioni 137.6 zimepokelewa na kutumika kwa ajili ya kufanya matengenezo ya kawaida, matengenezo ya muda maalum na matengenezo ya maeneo korofi kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, TAMISEMI inatekeleza mradi wa kuboresha barabara katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Barabara zenye urefu wa kilometa 88 zinafanywa matengenezo kwa kiwango cha lami kwa gharama ya Shilingi bilioni 85.696; utekelezaji umekwishanza na upo katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza programu ya kuondoa vikwazo vya upatikanaji wa mawasiliano (*Bottleneck Removal*) katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Uingereza. Gharama za mradi wa mpango huo ni shilingi bilioni 25.978. Utekelezaji wa mradi huu uko katika hatua mbalimbali na kiasi cha shilingi bilioni 22.13 kimeshalipwa hadi Machi, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Serikali kwa kushirikiana na *USAID* imetekeleza mradi wa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha changarawe ambapo kilometa 178.4 zimetengenezwa kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa za Wilaya za Kongwa, Morogoro, Kiteto na Kilombero. Hadi Machi, 2016 Mamlaka za Serikali za Mitaa zilipokea kiasi cha shilingi bilioni 8.74, lengo la mradi ni kurahisisha usafirishaji wa mazao ya kutoka mashambani kupeleka kwenye masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inasimamia na kuratibu uandikishaji wa wanafunzi katika elimu msingi na kidato cha tano, kuajiri walimu, kutoa elimu kwa watu wazima na vijana nje ya mfumo rasmi wa shule na kuongeza miundombinu ya shule na kutoa mafunzo kwa watendaji katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na mafanikio makubwa katika Mpango wa Maendeleo ya elimu ya msingi Awamu ya Kwanza, *MMEM I* na *MMEM II*, ambao kwa sasa utekelezaji wake uko katika Awamu ya Tatu. Ili kuhakikisha kuwa elimu ya awali inatiliwa mkazo jumla ya shule 14,946 zina madarasa ya elimu ya awali kati ya shule 16,014 za msingi sawa na 93.33%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya awali imeongezeka kufikia wanafunzi 971,717, kati ya hao wavulana 480,053 na wasichana 491,663. Mwaka 2016 tumeongeza sasa kutoka wanafunzi 877,000; kati ya hao wavulana ni 436,778 na wasichana 440,711 mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeendelea na jukumu la kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa elimu ya msingi Awamu ya Tatu. Mpango huu umejikita katika kuinua stadi za masomo, uandikaji na kuhesabu yaani KKK kwa wanafunzi wa darasa la kwanza na la pili. Aidha, Waratibu Elimu Kata 784 wamepatiwa pikipiki kwa lengo la kuhamasisha na kufuatilia elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanikiwa kuongeza nyumba za walimu kutoka nyumba 41,835 mwaka 2010 hadi nyumba 58,448 mwezi Februari, 2016. Aidha, idadi ya matundu ya vyoo yameongezeka kutoka matundu ya vyoo 149,566 mwaka 2010 hadi matundu ya vyoo 206,000 mwaka 2016 sawa na ongezeko la 38%. Bado kuna upungufu wa matundu kama inavyoonekana kwenye majedwali ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile uwiano wa vitabu umeendelea kuimarika kutoka uwiano wa kitabu kimoja kwa watoto saba mwaka 2007 hadi uwiano wa kitabu kimoja kwa watoto watatu mwaka 2015. Lengo ni kuhakikisha uwiano wa kitabu kimoja kwa mwanafunzi mmoja ifikapo mwaka 2017. Juhudi hizi zinatokana na ushirikiano baina ya Halmashauri, wazazi na wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi waliotarajiwa kuandikishwa darasa la kwanza mwaka 2016 ni 1,433,840. Hadi kufikia mwezi Machi, mwaka 2016 jumla ya wanafunzi walioandikishwa ni 1,896,584. Idadi ya uandikishaji wa wanafunzi katika darasa la kwanza imeongezeka kutokana na Serikali kutekeleza Mpango wa Elimu Msingi Bila Malipo au inavyojulikana kama elimu bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi 775,273 wamesajiliwa kufanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi mwaka 2015, sawa na 75.24%. Kati ya wanafunzi waliosajiliwa wanafunzi 763,606 sawa na 98.5% ya wanafunzi waliosajiliwa walifanya mtihani wakiwemo wavulana 354,000 na wasichana 408,000. Takwimu zinaonesha kwa jumla kuwa, wanafunzi 266,000 sawa na 25.9% hawakuhitimu darasa la daba. Takwimu hizi zinatunesha kuwa hali ya mdondoko (*dropout*) ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, Watendaji wa Serikali na wadau wote wa elimu na

wazazi, tushirikiane ili kupunguza mdondoko wa wanafunzi katika ngazi ya elimu ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo mwezi Mei, 2016 Serikali inatarajia kutoa ajira za walimu wapatao 40,000 ikijumuisha wa Cheti, Stashahada na Shahada ili kukabiliana na upungufu wa walimu uliopo katika shule za msingi na sekondari nchini. Zaidi ya shilingi bilioni 17 zinahitajika kwa ajili ya kulipa posho pamoja na nauli za walimu wapya watakojiriwa na kupelekwa katika vituo vya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, TAMISEMI inaendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Elimu ya Sekondari Awamu ya Pili na kuimarisha elimu ya sekondari ili kuinua ubora wa elimu. Mpango huu unahusisha ujenzi wa miundombinu ya shule 264 za awamu ya kwanza ambao umekamilika kwa 64%. Serikali inaendelea kukamilisha ujenzi na uboreshaji wa shule 264 za awamu ya kwanza na kuendelea na uboreshaji wa miundombinu katika shule nyingine 528.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu 3,828 wa shule za sekondari wamepatiwa mafunzo na kuwajengea uwezo wa kufundisha na kujifunza. Hadi mwezi Juni, 2016 jumla ya walimu 8,828 wa Sekondari watakuwa wamepata mafunzo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za kidato cha tano zimeongezeka kutoka shule 179 mwaka 2010 hadi shule 279 mwaka 2016 ikiwa ni sawa na ongezeko la 55.87%. Ofisi ya Rais, TAMISEMI inatoa agizo kwa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuongeza nafasi kwa 25% kwa ajili ya wanafunzi waliofanya mitihani ya kidato cha nne mwaka 2015 na kuhakikisha kuwa Tarafa ambazo hazina madarasa ya Kidato cha V na VI zinakuwanayo. Ni imani yangu kuwa wanafunzi 89,929 waliofaulu mtihani wa kidato cha nne mwaka 2015 wa madaraja ya kwanza na ya tatu watapata nafasi ya kujiunga katika kidato cha tano kwa mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2015 Serikali ilipata msaada wa vitabu vya hisabati na sayansi 2,500,000 kutoka Shirika la Kimataifa la USAID na vilisambazwa katika shule za sekondari katika Halmashauri zote nchini. Aidha, katika kuimarisha masomo ya sayansi, maabara 10,389 zilipangwa kujengwa. Hadi kufikia mwezi Disemba, 2015 maabara 6,254 zimekamilika ambayo ni sawa na 60.2%, maabara 2,940 zipo katika hatua mbalimbali. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba chini ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MES II) nyumba 183 zenye uwezo wa kuishi walimu sita kila moja (*multipurpose houses*) zimejengwa katika Halmashauri 105.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ilishiriki katika mashindano ya 14 ya Shirikisho la Michezo ya Shule za Sekondari kwa nchi za Afrika Mashariki (FEASSSA) yaliyofanyika tarehe 16 hadi tarehe 24 mwezi wa nane mwaka 2015 katika Mji wa Huye, nchini Rwanda na washiriki walikuwa 322. Kati ya hao wanafunzi walikuwa 269 na waamuzi walikuwa 53. Aidha, mashindano ya michezo ya UMISSETA na UMITASHUMTA nayo yalifanyika jijini Mwanza katika viwanja vya Chuo cha Ualimu Butimba, kuanzia tarehe 8 Juni hadi 3 Julai mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie huduma ya afya, ustawi wa jamii na lishe. Ofisi ya Rais, TAMISEMI inatarajia kutekeleza utoaji wa huduma ya afya, ustawi wa jamii na lishe kwenye ngazi za Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kusimamia rasilimali watu, upatikanaji wa rasilimali fedha, dawa, vifaa tiba, kuimarisha uongozi na uendeshaji wa shughuli za afya ya msingi. Muundo huu mpya umewezesha utekelezaji wa sera, mikakati na miongozo inayotolewa na Wizara za Kisekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za afya katika Mikoa zimeendelea kuboreshwa kwa kufuata maelekezo ya Wizara za Kisekta. Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeendelea kuimarisha timu za afya za Mikoa zenye majukumu ya kusimamia na kuratibu shughuli za afya za Mikoa. Katika ngazi hii pia, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Afya imeendelea na juhudi za kuzijengea uwezo Timu za Afya za Mikoa, kutimiza programu mbalimbali ukiwemo Mradi wa *Regional Referral Hospital Management Program* unaotekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Japan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za afya za Halmashauri zinasimamiwa na timu za afya za Wilaya. Timu hizi zinasimamia Hospitali za Wilaya, vituo vya afya na zahanati. Majukumu ya Timu hizi ni kuhakikisha kuwa huduma bora za afya zinatolewa katika maeneo hayo ikiwa ni pamoja na elimu ya afya, upatikanaji wa dawa, vipimo, chanjo na huduma za mama na mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vya kutolea huduma za afya; hospitali, vituo vya afya na zahanati. Hadi sasa tunazo Halmashauri 181 kati ya hizo Halmashauri zenye Hospitali za Wilaya za Serikali ni 84 na Halmashauri 97 hazina Hospitali za Wilaya za Serikali. Halmashauri zisizo na Hospitali za Serikali hutumia Hospitali za Mashirika ya Umma au Taasisi za Kidini kama Hospitali Teule. Kata zenye vituo vya afya vya Serikali ni Kata 484 na Kata 3,506 hazina vituo vya afya. Vilevile vijiji 4,502 havina Zahanati za Serikali na vijiji 8,043 havina Zahanati za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni azma ya Serikali kuona kuwa kila Halmashauri inakuwa na kituo cha afya; kila Kata na inakuwa na hospitali, lakini pia, kila Kata inakuwa na kituo cha afyana kila kijiji kinakuwa na zahanati. Huduma za afya nchini kwa ngazi za hospitali, kituo cha afya na zahanati hutolewa na wadau mbalimbali wakiwemo mashirika ya dini, makampuni ya watu binafsi na watu binafsi. Hivyo, Serikali itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kuhakikisha kwamba, utoaji wa huduma huu unaendelea kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa majengo mbalimbali na kukarabati majengo na vituo vya kutolea huduma ya afya. Katika mwaka wa fedha 2014/2015 hospitali, vituo vya afya na zahanati zilicarabatiwa na kujengwa katika sehemu za majengo kwa kutumia karibu Shilingi bilioni 263.3. Katika mwaka wa fedha 2015/2016 hadi mwezi Februari, 2016 hospitali, vituo vya afya na zahanati zilicarabatiwa au nyingine kujengwa, sehemu ya majengo kwa kutumia shilingi bilioni 18.68.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeweka mkakati wa kuhakikisha kuwa hali ya upatikanaji wa dawa na vifaa tiba inazingatia mahitaji halisi katika vituo vya kutolea huduma za afya. Mkakati huo unahusisha ushiriki wa wananchi katika kusimamia suala la dawa na vifaa tiba kupitia Kamati za Afya za vituo, kushirikisha sekta binafsi na asasi za kiraia kwa uwazi na uwajibikaji na Halmashauri zinatumia utaratibu wa kuagiza dawa moja kwa moja kutoka Bohari ya Dawa kwa kutumia njia ya mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali mbalimbali za Mikoa zimefungua maduka ya dawa na bohari za dawa (MSD) kwa lengo la kuboresha huduma hizi. Maduka haya yamefunguliwa katika hospitali za Dar es Salaam (Hospitali ya Muhimbili), Mkoa wa Arusha (Mount Meru), Mkoa wa Mwanza (Sekou Toure) na Mkoa wa Mbeya (Hospitali ya Rufaa Mbeya) na Mikoa mingine iko katika hatua mbalimbali za kuanzisha maduka hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na tatizo la lishe duni, Serikali kwa kushirikiana na wananchi na wadau mbalimbali imeanza kuhuisha mikakati ya lishe ya miaka mitano kuanzia Julai, 2016 hadi Juni, 2021. Mkakati huo unahusisha masuala yafuatayo; uundaji wa Kamati za Lishe katika ngazi za Mikoa na Halmashauri, kufanya mapitio ya Sera ya Chakula na Lishe ya mwaka 2015, kutenga na kuajiri wataalam kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huduma ya ustawi wa jamii. Katika mwaka wa fedha 2015/2016 jumla ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu 369,401 wametambuliwa. Kati ya hao kati ya hao, watoto 99,061 wamepatiwa huduma mbalimbali zenye thamani ya shilingi bilioni 1.5. Serikali imejipanga

kuhakikisha kuwa watoto wote walio katika mazingira magumu wanapatiwa haki zao za msingi kama elimu na afya, malazi na chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeingia mkataba wa miaka mitano mpaka mwaka wa fedha 2019/2020 na Mashirika ya Kimataifa ya Maendeleo yakiwemo Switzerland, UNFPA, UNICEF, Ireland, Benki ya Dunia na Denmark wa kuendelea kushirikiana katika utoaji wa huduma za afya ya msingi nchini. Katika mwaka wa fedha 2015/2016 jumla ya shilingi bilioni 68.8 zilitengwa ambapo mikoa ilitengewa bilioni 3.7 na Halmashauri shilingi bilioni 65.118. Hadi kufika Februari, 2016 jumla ya shilingi bilioni 34 zilikuwa zimetolewa, sawa na 50%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za Mfuko wa Dunia wa kuthibiti Kifua Kikuu, UKIMWI na Malaria. Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeendelea kuratibu shughuli za *Global Fund* ikiwa na lengo la kuthibiti magonjwa matatu ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria. Katika mwaka wa fedha 2015/2016 jumla ya shilingi bilioni 1.9 zilipelekwa kwenye Mikoa kwa ajili ya kuzijengea uwezo mamlaka za Serikali za Mitaa katika kutekeleza shughuli ya udhibiti na magonjwa hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, TAMISEMI inaratibu shughuli za kuthibiti UKIMWI kwenye Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mkoa na Halmashauri. Kazi zilizofanyika ni pamoja na kutoa fedha kwa ajili ya chakula kwa wanaoishi na VVU na UKIMWI pamoja na kuanzisha miradi inayoweza kuwasaidia.

Aidha, Ofisi ya Rais, TAMISEMI itaendelea kuzijengea uwezo Kamati za UKIMWI za kata na vijiji ili kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa agizo la Mheshimiwa Rais, linatekelezwa kwa uendelevu, ukaguzi na uhamasishaji wa usafi katika majiji, manispaa na halmashauri za miji katika Mikoa 26 umefanyika. Pamoja na ukaguzi uliofanyika, Mikoa yote ilielekezwa kuendelea na shughuli ya kupendezesha mazingira ya miji kwa kuanza na maeneo ya wazi kando ya barabara na kwenye ofisi za umma na makazi ya watu. Natoa wito kwa wananchi wote kuhakikisha maeneo yao yanakuwa safi kwa wakati wote. Tabia ya usafi ikijengeka katika jamii, magonjwa ya kipindupindu na ya kuharisha yataondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mlipuko wa kipindupindu ulitokea mwezi Agosti, 2015. Hadi tarehe 12 Aprili, 2016 kulikuwa na jumla ya watu 20,751 waliyopata kipindupindu, kati ya hao 20,366 wametibiwa na kuruhusiwa na watu 31 walikuwa bado wanaendelea na matibabu na watu 327 waamepoteza maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikoa yenye wagonjwa wapya wa kipindupindu na idadi ya wagonjwa katika mabano ni Morogoro (12), Kilimanjaro (9); Pwani (4); Mara (4); Manyara (1); Arusha (1) na Tanga (2). Mikoa ya Njombe na Ruvuma haijatoa taarifa ya kuwepo kwa ugonjwa wa kipindupindu. Rai yangu kwa wananchi wote ni kwamba kinga ya kipindupindu ni kuhakikisha usafi wa mazingira unadumishwa. Tuweke ajenda ya usafi kuwa ni jambo la lazima kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 jumla ya kaya 189,000 zilijiunga na CHF ambapo zilipatikana jumla ya shilingi bilioni tisa. Kiasi cha fedha hicho ni Tele kwa Tele zilizotolewa kwa kaya zilizojiunga na Mfuko wa Bima ya Afya. Aidha, nawaagiza watumishi wote wa afya wahakikishe dawa na vifaa vinapatikana kwa wakati wote ili kuhakikisha kwamba wanatoa huduma ipasavyo kutokana na fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Uendelezaji wa Miji ya Kimkakati umetekelezwa kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia ambapo kiasi cha dola milioni 163 zilitolewa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za uimarishaji miundombinu. Maeneo ambako kumefanyika miradi hiyo ni miji yote mikubwa ikiwemo Dar es Salaam, Arusha, Tanga, Mwanza, Mbeya, Dodoma, Mtwara Mikindani, Kigoma Ujiji pamoja na Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu - Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu mwaka wa fedha 2010/2011 hadi 2015/2016 uboreshaji wa miundombinu ya huduma za mjini umegharimu dola za Kimarekani milioni 150.6. Kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa kiwango cha lami za barabara ambazo nimezitaja katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, programu ya kuimarisha Mamlaka za Miji 18; lengo la programu hii ni kuboresha utoaji wa huduma za msingi katika maeneo ya miji husika. Maeneo ya kuboreshwa ni pamoja na Mipango Miji, ukusanywaji wa mapato na huduma hasa kodi za majengo na usimamizi wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2014/2015 jumla ya shilingi bilioni 58.5 zilihidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za programu. Fedha hizi zilipokelewa na zimetumika. Taarifa halisi inaonekana katika ukurasa wa 41 hadi 42 wa hotuba yangu.

Katika mwaka wa fedha 2015/2016 kiasi cha shilingi bilioni 77.1 zilihidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Uendelezaji Jiji la Dar es Salaam yaani *Dar es Saaam Metropolitan Development Project*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na utekelezaji unaoridhisha wa Mradi wa Uendelezaji Mji wa Kimkakati, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Benki ya Dunia na *NORDIC* wameingia katika mkataba wa uanzishwaji wa Mradi wa uendelezaji wa Mji wa Dar es Salaam utakaogharimu dola za kimarekani milioni 330. Fedha hizo zitatolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Benki ya Dunia na *NORDIC* kama ilivyofafanuliwa katika hotuba yangu kwenye kitabu changu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 kazi zilizopangwa kufanyika ni kuimarisha miundombinu ya barabara za mrisho yaani *feeder roads* za Mjini zenye urefu wa kilometa 65 zinazounganisha Halmashauri za Jiji pamoja na barabara kuu ya usafiri wa mabasi yaendayo kasi Dar es Salaam yaani *DART*. Maelezo zaidi yapo kwenye kitabu changu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi bilioni 17.2 zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ambapo ziliombwa kwa ajili ya kuboresha mfumo wa usimamizi wa maendeleo ya miji katika Jiji la Dar es Salaam ili kuwezesha kuboresha utoaji wa huduma za msingi katika jamii.

Mnamo mwezi Machi, 2016 kiasi cha dola za Kimarekani 10,400,000 na shilingi za Tanzania bilioni 20.8 zimepokelewa na utekelezaji umeanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo, awamu ya kwanza ilifika ukomo mwaka wa fedha 2013/2014...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, omba fedha, taarifa yako yote itaingia kwenye Kumbukumbu za Bunge. Omba fedha sasa.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha kwa kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka wa fedha 2016/2017.

Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Taasisi zilizoko chini yake Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinaomba idhini ya jumla ya shilingi bilioni ... eeh! *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, mwacheni Mheshimiwa mtoa hoja, anaelewa anachowasilisha.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi 6,230,559,414,000/= kwa ajili ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mikoa na Halmashauri kwa mchanganuo kama ilivyooneshwa kwenye jedwali la kwenye kitabu changu cha hotuba. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba hii yapo majedwali ambayo yanafafanua kwa kina makadirio ya matumizi ya fedha za Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Taasisi zake. Hotuba hii pia inapatika kwenye tovuti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambayo ni www.tamisemi.go.tz. Naomba kutoa hoja.

HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, MHESHIMIWA GEORGE BONIFACE SIMBACHAWENE (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

Utangulizi

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuiona siku ya leo tukiwa na afya njema. Kipekee kabisa napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniadini na kunitiua niongoze Ofisi yake kwa upande wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Vile vile, kwa namna ya pekee, namshukuru Mheshimiwa Jasson Constantine Rweikiza (Mb) Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa pamoja na wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na maelekezo wanayotupatia katika kutekeleza majukumu yetu ya kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, Makamu wa Rais Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Kassim (Mb), Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mb), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa Dkt. Tulia Akson Mwansasu (Mb), Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano na viongozi wote kwa nyadhifa mbalimbali walizozipata kutokana na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Aidha, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa tena kuiongoza Zanzibar. Nawapongeza pia Wabunge wote wa Bunge la kumi na moja kwa kushinda uchaguzi na

kuwawakilisha wananchi katika chombo hiki muhimu cha kutunga sheria za nchi na kuisimamia Serikali. Nawapongeza pia, wote waliopata nafasi za kuteuliwa kushika nyadhifa walizonazo katika Serikali ya Awamu ya tano.

Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likae, lipokee, lijadili na kupitisha Mpango wa Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha wa 2016/17.

Majukumu ya OR-TAMISEMI, MIKOA na Mamlaka za Serikali Za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inatekeleza majukumu yafuatayo:-

- i. Kuratibu utekelezaji wa dhana ya Upelekaji wa Madaraka kwa Umma (D by D);
- ii. Kuratibu na kusimamia Tawala za Mikoa ili ziweze kuziwezesha Halmashauri katika kutekeleza wajibu wake;
- iii. Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Vijijini na Mkakati wake;
- iv. Kusimamia Wakala wa Usafiri wa Haraka katika Jiji la Dar es Salaam;
- v. Kuratibu usimamizi na uendeshaji wa Elimu ya Msingi na Sekondari katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- vi. Kuratibu na kusimamia uendeshaji wa Afya ya Msingi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- vii. Kusimamia utekelezaji wa miradi na programu zilizo chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; na
- viii. Kusimamia utendaji kazi wa Taasisi zilizo chini ya OR TAMISEMI ambazo ni, Chuo cha Serikali za Mitaa(Hombolo), Shirika la Elimu Kibaha, Tume ya Utumishi wa Walimu, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, na Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa (LAPF).

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mikoa majukumu yao ni pamoja na:-

- i. Kusimamia na kuratibu shughuli zote za maendeleo katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- ii. Kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa ili zitekeleze majukumu yake kwa ufanisi;
- iii. Kuhakikisha kwamba kunakuwepo amani na utulivu katika Mikoa;

- iv. Kufuatilia utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali inayotekelezwa na Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika maeneo yake;
- v. Kuratibu usimamizi na uendeshaji wa Elimu ya Msingi na Sekondari katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- vi. Kusimamia uendeshaji wa Afya ya Msingi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; na
- vii. Kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia misingi ya Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, utendaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa unaongozwa na majukumu ya msingi yafuatayo:-

- i. Kuhakikisha kuwa kunakuwepo na amani na utulivu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- ii. Kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia misingi ya Utawala Bora;
- iii. Kuhakikisha kuwa Serikali za Mitaa zinatoa huduma za kuridhisha, kuaminika, kwa wakati muafaka na zenye ubora kwa wananchi kulingana na Sera na Mikakati ya kisekta;
- iv. Kuhakikisha kuwa zinasimamia vema utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo pamoja na kusimamia matumizi ya fedha zinazopelekwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa lengo la kupata thamani ya fedha;
- v. Kuwaunganisha wadau wote wa maendeleo walioko katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kutumia vema rasilimali watu na fedha kwa manufaa ya jamii iliyopo katika Mamlaka hizo; na
- vi. Kuhakikisha kwamba makundi maalum na masuala mtambuka yanazingatiwa katika utoaji wa huduma mbalimbali, ikiwemo utunzaji wa mazingira, kudhibiti magonjwa ya mlipuko, UKIMWI na kuzuia na kupambana na rushwa.

Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha 2015/16

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/16, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ziliidhinishiwa **shilingi 5,417,149,119,969.00** kwa ajili ya mishahara, matumizi mengineyo na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizi, **shilingi 395,588,786,000.00** ni kwa ajili ya OR –TAMISEMI, Mikoa **Shilingi 254,859,800,969.00** na **shilingi 4,766,700,533,000.00** ni kwa ajili ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Maduhuli na Mapato ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/16, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ilikadiria kukusanya **Shilingi 13,503,000.00**. Hadi mwezi Machi, 2015 Ofisi imekusanya **shilingi 1,650,000.00** sawa na **asilimia 12** ya makadirio. Maduhuli hayo yanatokana na uuzaji wa nyaraka za zabuni. Maduhuli hayo yamekuwa kidogo kutokana na kutopatikana kwa fedha za maendeleo, hivyo ni zabuni chache zimeuzwa. Kwa upande wa Taasisi zilizo chini ya OR – TAMISEMI, zilikadiriwa kukusanya mapato ya **shilingi 7,583,319,100.00**. Hadi mwezi Machi, 2016 **shilingi 5,092,545,190.00** zimekusanywa sawa na **asilimia 67** ya makadirio.

Maduhuli ya Mikoa

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/16, Mikoa ilikadiria kukusanya **shilingi 225,793,743** kama maduhuli. Hadi mwezi Desemba 2015, kiasi cha **shilingi 225,050,999** zilikusanywa sawa na **asilimia 99.7**. Maduhuli ya Mikoa yanatokana na mishahara isiyolipwa, tozo la pango kwenye nyumba za Serikali na mauzo ya nyaraka za zabuni.

Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/16, Mamlaka za Serikali za Mitaa zilikadiria kukusanya **shilingi 521,879,000,000.00** kama mapato. Hadi mwezi Februari, 2016 jumla ya **shilingi 231,651,527,779.00** zilikuwa zimekusanywa sawa na **asilimia 44**. Kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, makusanyo yanatokana na kodi na ushuru mbalimbali unaotozwa na Mamlaka hizo kutokana na vyanzo vya mapato vilivyokubaliwa. Ofisi yangu imeendelea kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa kukusanya mapato, kwa kuboresha usimamizi na mifumo ya ukusanyaji mapato kwa kutumia TEHAMA na kubuni vyanzo vingine vya mapato pamoja na kuziba mianya ya ufujaji na uvujaji wa mapato.

Utawala bora na uwajibikaji

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa utekelezaji wa majukumu ya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa unazingatia misingi ya utawala bora, tarehe 23 Desemba, 2015 nilitoa Waraka namba 13 ambao unawaelekeza Wakuu wa Mikoa kuacha kufanya kazi kwa mazoea na badala yake kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu ili kuboresha utoaji wa huduma bora kwa Umma. Aidha, Waraka huo umetoa maelekezo kuhusu kuhimiza kuendelea na zoezi la kufanya usafi katika maeneo yao, pamoja na

usimamizi wa zoezi la kutoa elimumsingi bila malipo. Maelekezo yote niliyotoa yanaendelea kutekelezwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa watumishi wa Umma wanaofanya kazi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, hatua mbalimbali zimechukuliwa kuhakikisha kuwa kunakuwepo na uwajibikaji thabiti. Hatua hizo ni pamoja na kuboresha misingi na mifumo ya uwajibikaji na kuchukua hatua stahiki na kwa wakati kwa watumishi wote waliobainika kukiuka Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/15, watumishi **78** wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wamechukuliwa hatua mbalimbali za kinidhamu na kijinai. Kati ya Watumishi hao, Wakurugenzi wa Halmashauri watano (5) wamevuliwa madaraka na kupangiwa kazi nyingine na Wakurugenzi watatu (3) wamefunguliwa kesi mahakamani na kesi zao bado zinaendelea. Watumishi wengine ni Wakuu wa Idara na watumishi wa kawaida wa Halmashauri ambao wapo waliofukuzwa kazi, kuachishwa kazi na wengine kushtakiwa Mahakamani. Katika mwaka wa fedha 2015/16, hadi kufikia mwezi Machi, 2016 watumishi **90** wamechukuliwa hatua mbalimbali za kinidhamu na wengine kufikishwa Mahakamani. Kati ya watumishi hao, Wakurugenzi watatu (3) wamevuliwa madaraka na kupangiwa kazi nyingine, wakurugenzi watano (5) wamefikishwa Mahakamani, Wakurugenzi kumi (10) wamesimamishwa kazi na kupewa mashtaka ya nidhamu. Aidha, watumishi wengine wamechukuliwa hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufukuzwa kazi au kushushwa vyeo. Lengo la hatua hizi ni kuleta tija na kuweka nidhamu kazini na matumizi bora ya rasilimali na madaraka katika utumishi wa Umma.

Mabadiliko ya Muundo wa OR - TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, tarehe 12 Februari, 2015, muundo mpya wa Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ulipitishwa ili kukidhi mabadiliko mbalimbali ya majukumu hususan katika eneo la usimamizi wa rasilimali fedha ambapo Idara ya Ukaguzi na Ufuatiliaji wa Fedha (*Inspectorate and Finance Tracking Division*) ilianzishwa. Lengo la kuanzisha Idara hii ni kuimarisha usimamizi katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kufanya ukaguzi katika mifumo, uendeshaji, usimamizi na ufuatiliaji wa masuala ya fedha.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2016 kaguzi maalum zilifanyika katika Manispaa ya Ilemela, Kigoma, Ilala, Halmashauri ya Wilaya ya Nzega, Magu na Uyui. Vile vile, ukaguzi wa kawaida ulifanyika katika Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora, Halmashauri za Igunga na Uvinza. Kaguzi hizi zimebaini

mapungufu katika kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za matumizi ya fedha, manunuzi na kutozingatiwa kwa kanuni na miongozo ya kisekta. Wote waliohusika na mapungufu hayo wamechukuliwa hatua za kinidhamu na mamlaka zao za nidhamu. Aidha, ushauri umetolewa katika Halmashauri hizo ili kurekebisha mapungufu yaliyobainishwa kutokana na kaguzi hizo. Vile vile, ufuatiliaji umefanyika katika Halmashauri za Mkoa wa Dodoma na kubaini kwamba, kuna idadi ndogo ya wanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) na usimamizi hafifu wa matumizi ya Mfuko huo. Ushauri wa jinsi ya kuboresha uendeshaji na usimamizi wa Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) umetolewa kwa lengo la kuongeza idadi ya wanachama na matumizi bora ya fedha zinazokusanywa.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha azma ya Serikali ya Awamu ya Tano kupitia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 Ibara ya 148 (d) na (f), OR-TAMISEMI itaendelea kufanya ukaguzi wa ufanisi, kawaida, maalumu na ufuatiliaji wa kina katika Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa ili kuboresha utendaji kazi na hivyo kupata thamani ya fedha (*value for money*).

Madeni ya Watumishi

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuhakiki na kulipa madeni ya watumishi wakiwemo walimu na wasiokuwa walimu kadri yanavyojitokeza. Hadi mwezi Oktoba, 2015 jumla ya **shilingi 20,125,578,770.05** zimelipwa kwa watumishi wa Umma. Serikali itaendelea kulipa madeni ya watumishi baada ya kuyahakiki. Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa inaelekezwa kuwa waangalifu ili kuzuia kuzalisha madeni mapya.

Uanzishwaji wa Maeneo Mapya ya Utawala

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka wa fedha 2014/15 hadi mwezi Machi 2016, maeneo ya utawala mbalimbali yameanzishwa ikiwa ni pamoja na mkoa mmoja (1) wa Songwe na Wilaya sita (6) ambazo ni Songwe (Songwe), Kigamboni (Dar es Salaam), Ubungo (Dar es Salaam), Malinyi (Morogoro), Tanganyika (Katavi) na Kibiti (Pwani). Aidha, Halmashauri za Wilaya za Malinyi (Morogoro), Chalinze (Pwani) na Ifigi (Singida) na Halmashauri za Miji ya Ifakara (Morogoro), Bunda (Mara), Mbulu (Manyara), Kondoa (Dodoma), Newala (Mtwara) na Mbinga (Ruvuma) pia zilianzishwa katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 30 Machi 2016, Tanzania Bara ina Mikoa 26, Wilaya 139, Halmashauri 181, Tarafa 562, Kata 3,963, Mitaa 4,037, Vijiji 12,545 na Vitongoji 64,677. Lengo la kuanzisha maeneo haya ya utawala ni kusogeza huduma karibu na wananchi na kuongeza kasi ya maendeleo.

Kuimarisha Ukusanyaji wa Mapato ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa halmashauri zinakuwa na uwezo wa kifedha ambao utaziwezesha kutekeleza majukumu yao ipasavyo, hatua mbalimbali zimechukuliwa ili kuboresha makusanyo ya mapato ya ndani. Hatua hizo ni pamoja na kufunga na kutumia mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji na usimamizi wa mapato. Mifumo hiyo imeunganishwa na mifumo ya malipo kama vile mabenki, M-pesa, Tigo Pesa na 'Airtel Money' ili kurahisisha ulipaji wa kodi.

Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Machi 2016, Halmashauri **138** sawa na asilimia **74** zimekamilisha ufungaji na zimeanza kutumia mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato na Halmashauri nyingine 48 sawa na asilimia 26 zipo katika hatua mbalimbali za ufungaji wa mifumo hii. Matumizi ya mifumo hii imepunguza mianya ya ufujaji na uvujaji wa mapato kwa kuwezesha usajili na utunzaji wa taarifa za walipa kodi, aina za kodi, kiasi kilicholipwa na kinachodaiwa na kuwezesha malipo kulipwa moja kwa moja benki. Katika kuhakikisha mifumo mbalimbali ya kielektroniki inafanya kazi ipasavyo, Ofisi yangu kupitia Programu ya Maboresho ya Fedha za Umma Awamu ya IV (**PFRMP 1V**), imezijengeta uwezo halmashauri kwa kuziwezesha kufunga na kutumia mifumo ya mapato ijulikanayo kama *Local Government Revenue Collection Information Management System (LGRCIS)* na *I-tax*.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya mifumo ya kielektroniki imeonesha faida na mafanikio makubwa katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ya halmashauri. Kwa mfano, mapato ya ndani ya halmashauri ya jiji la Arusha yaliongezeka kutoka **shilingi bilioni 5.0** mwaka wa fedha 2012/13 hadi **bilioni 10.5** mwaka wa fedha 2015/16 na mapato ya halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani yaliongezeka kutoka **shilingi milioni 600** mwaka wa fedha 2013/13 hadi **shilingi bilioni 2.6** mwaka wa fedha 2015/16. Hii inaonyesha wazi kwamba mifumo hii ina uwezo mkubwa wa kuzuia uvujaji na ufujaji wa mapato ya halmashauri.

Mheshimiwa Spika, sanjari na matumizi ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ya halmashauri, Serikali pia imezifanyia marekebisho Sheria za Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290 na Sheria ya Kodi ya Majengo (*The Urban Authorities (Rating) Cap 289*) ili kuongeza wigo wa mapato ya halmashauri kwa kurejesha ushuru wa nyumba za kulala wageni na kuzipa mamlaka halmashauri za wilaya kutoza na kukusanya kodi ya majengo haya. Kwa upande wa uthamini, sheria hiyo imeruhusu kuanzishwa kwa njia ya Uthamini wa Mkupuo

(Mass Valuation). Lengo la utaratibu huu ni kurahisisha zoezi la uthamini na kupunguza gharama.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mafanikio haya, napenda kuchukua nafasi hii kuagiza kuwa ifikapo tarehe 01 Julai, 2016, halmashauri zote nchini ziwe zimefunga na kutumia mifumo ya kielektroniki katika kukusanya mapato yake ya ndani. Aidha, naziagiza halmashauri kwamba, mara baada ya mikataba ya sasa kwisha, ukusanyaji wa mapato kwa njia ya mawakala usitishwe na badala yake makusanyo yafanywe na maafisa wa halmashauri kwa kutumia mifumo ya kielektroniki.

Usimamizi wa Maendeleo ya Miji

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais - TAMISEMI inasimamia maendeleo mijini na vijijini. Lengo ni kuhakikisha kuwa ardhi iliyoko mijini na vijijini inaandaliwa mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa kufuata Sheria na Miongozo iliyopo. Uzoefu unaonesha kwamba miji inatoa mchango mkubwa kwenye ukuaji wa pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba chimbuko la miji ni vijiji, kwa kipindi kirefu, msisitizo wa ki-sera wa uendelezaji wa ardhi ulielekezwa zaidi mijini. Ongezeko la idadi ya watu mara tatu kati ya Sensa ya mwaka 1967 (watu milioni 12.3) na 2012 (watu milioni 44.9) limefanya vijiji viongezeka. Katika kipindi hicho idadi ya wakazi mijini imeongezeka mara tano kutoka asilimia 5.7 hadi kufikia 29.1. Kuna sababu mbalimbali zinazofanya watu wengi kuhamia mijini zikiwemo za kijamii na kiuchumi. Hii imesababisha kuwepo kwa migogoro mingi inayohusiana na uendelezaji wa ardhi na utoaji wa huduma mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa vijiji, katika mwaka wa fedha 2014/15, vijiji 1,550 sawa na asilimia 12.4 ya vijiji 12,545 vilivyopo nchini vilikuwa vimeandaliwa mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya matumizi ya ardhi. Katika mwaka wa fedha 2015/16, vijiji 53 viliandaliwa mpango wa matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna majiji matano (5), manispaa ishirini na moja (21), miji ishirini na mbili (22) na miji midogo themanini na saba (87) inayotambulika kisheria. Katika mwaka wa fedha 2015/16, OR - TAMISEMI imetambua miji mia sita (600) inayochipukia kwenye maeneo mbalimbali nchini ambayo inahitaji kutambuliwa, kupangwa na kuendeshwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Sera ya Maendeleo Vijijini sanjari na uendelezaji wa miji, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeandaa Rasimu ya Sera ya

Maendeleo ya Miji ambayo iko kwenye hatua za mwisho kupata idhini ya mamlaka husika ili iweze kuanza kutekelezwa. Sera hii itakuwa kiunganishi katika kuleta maendeleo sawia vijijini na mijini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2015/16, OR-TAMISEMI ilitoa maelekezo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa, kuandaa na kutekeleza mipango ya jumla ya uendelezaji miji, kwa kupima na kumilikisha viwanja vya makazi, biashara, viwanda na maeneo ya umma, pamoja na kuandaa mipango shirikishi ya matumizi bora ya ardhi ya Vijiji.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa miji inaendelezwa kwa mpangilio, miji ishirini na sita (26) ipo katika hatua mbalimbali za kuandaa mipango ya jumla ya uendelezaji (General Planning Schemes - GPS). Miji hiyo, ni manispaa kumi na tano (15) za Dodoma, Kigoma - Ujiji, Mtwara - Mikindani, Moshi, Morogoro, Iringa, Sumbawanga, Songea, Lindi, Singida, Tabora, Mpanda, Shinyanga, Musoma na Bukoba na halmashauri sita (6) za miji ya Kibaha, Korogwe, Njombe, Babati, Bariadi na Geita. Aidha, majiji matano (5) ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya na Tanga nayo yanaandaa mipango hiyo.

Mheshimiwa Spika, ili kurahisisha kazi na kuwa na kumbukumbu sahihi za Mamlaka za Serikali za Mitaa, OR-TAMISEMI imeanza kutumia mfumo wa taarifa za kijiografia (Geographical Information System - GIS) katika kuandaa mipango ya jumla ya uendelezaji wa miji, mipango shirikishi ya matumizi ya ardhi ya vijiji na uhakiki wa mipaka ya vijiji, wilaya na mikoa. Mfumo huu umerahisisha uandaaji shirikishi wa mipango endelevu ya matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/16, uthamini wa majengo 38,000 umefanyika chini ya mradi wa Tanzania Strategic Cities Project (TSCP) unaotekelezwa kwenye miji minane (8) ya kimkakati na halmashauri nyingine zipo kwenye hatua mbambali za kufanya uthamini wa majengo ndani ya maeneo yao ya utawala.

Mheshimiwa Spika, OR-TAMISEMI imeunda Baraza la Uthamini (Rating Valuation Tribunal) ambalo jukumu lake ni kusikiliza malalamiko ya uthamini wa majengo ili kukamilisha taratibu za kuanza kutoza kodi ya majengo kwa viwango vya uthamini. Hadi sasa, malalamiko 107 yamepokelewa na kusikilizwa katika majengo 38,000 yaliyoathaminiwa.

Mwogozo wa Anuani za Makazi

Mheshimiwa Spika, OR - TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano pamoja na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeandaa mwongozo wa anuani za makazi utakaotumika kwenye utekelezaji wa mpango wa anuani za makazi na postikodi kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa utakaoanza kutekelezwa kuanzia mwaka wa fedha 2016/17. Utekelezaji wa mpango huo utawezesha wananchi wote nchini kuwa na anuani halisi ya makazi, biashara, kumbukumbu za vizazi na vifo na ulipaji kodi. Aidha, anwani hizi zitarahisisha huduma za zimamoto, magari ya wagonjwa, usambazaji wa huduma muhimu (umeme na maji), ulipaji kodi na uzuiaji wa matendo ya uhalifu.

Mfuko wa Barabara

Mheshimiwa Spika, kazi zinazofanywa na mfuko huo ni kuratibu, kuandaa mipango, ufuatiliaji, kutoa miongozo, msaada wa kiufundi na kutafuta vyanzo vya fedha kwa ajili ya kazi za matengenezo ya barabara na madaraja. Mamlaka za Serikali za Mitaa zina mtandao wa barabara wenye urefu wa km. 108,946. Hali ya barabara za Mamlaka za Serikali za Mitaa, imeendelea kuwa bora. Kwa sasa barabara zilizo katika hali nzuri na ya kuridhisha ni km 61,798 sawa na asilimia 57, barabara za lami ni km 1,325 sawa na asilimia 1.2 na barabara za changarawe ni km 22, 089 sawa na asilimia 20.3.

Mheshimiwa Spika, mikakati iliyopo ni kuziimarisha barabara za Mamlaka za Serikali za Mitaa ili barabara zilizo katika hali nzuri na ya kuridhisha zibaki kuwa katika hali nzuri. Vilevile kuendelea kuinua hadhi ya barabara za mijini kuwa za lami kupitia fedha za Mfuko wa Barabara, Benki ya Dunia, Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza (DFID), Jumuiya ya Ulaya (EU) na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/16, Serikali ilitenga **shilingi bilioni 257.75** kwa ajili ya shughuli za matengenezo ya barabara. Hadi mwezi Machi 2016, jumla ya **shilingi bilioni 137.643** zimepokelewa na kutumika kwa ajili ya kufanya matengenezo ya kawaida (routine Mainatanance), matengenezo ya muda maalum (periodic maintenance) na matengenezo ya maeneo korofi (spot improvement) kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, OR-TAMISEMI inatekeleza mradi wa kuboresha barabara katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nne (4) za Iringa, Mufindi, Songea na Mbinga kwa fedha kutoka Jumuiya ya Ulaya. Barabara zenye urefu wa km. 88 zinafanyiwa matengenezo kwa kiwango cha lami kwa gharama ya shilingi **bilioni 85.696**. Utekelezaji umekwishanza na upo katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza programu ya kuondoa vikwazo vya upitikaji wa barabara (roads bottleneck removal) katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza (DFID). Gharama za mradi kwa mpango huo ni **shilingi bilioni 25.978**. Utekelezaji wa mradi huu uko katika hatua mbalimbali na kiasi cha **shilingi bilioni 22.139** kimeshalipwa hadi Machi 2016.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/16, Serikali kwa kushirikiana na USAID imetekeleza mradi wa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha changarawe ambapo **km. 178.4** zimetengenezwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa nne (4) za Kongwa, Morogoro, Kiteto na Kilombero. Hadi Machi 2016, Mamlaka za Serikali za Mitaa zilipokea kiasi cha **shilingi bilioni 8.74**. Lengo la mradi ni kurahisisha usafirishaji wa mazao kutoka mashambani kupelekwa kwenye masoko.

Matumizi ya Mifumo ya TEHAMA

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/16, OR - TAMISEMI imeendelea kuratibu na kutoa utaalum wa kiufundi kwenye miundombinu na mifumo ya TEHAMA ngazi ya OR – TAMISEMI, Mikoa na Halmashauri kwa kuwajengea uwezo watumishi wa ki-TEHAMA; kufunga vifaa vya mawasiliano kwa njia ya luninga na uimarishwaji wa kituo cha TEHAMA (data center); kusimamia mifumo ya udhibiti na matumizi ya fedha (Epicor), kufunga Mfumo wa Makusanyo wa Kodi na Tozo, (Local Government Revenue Collection Information System – “LGRCIS”), na kuwezesha ngazi mbalimbali kutumia takwimu katika kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Spika, hadi Februari 2016, Mamlaka za Serikali za Mitaa 133 zimekuwa zikiendelea kutumia mfumo wa Epicor Toleo la 9.05 bila matatizo. Malipo yote kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa yanafanyika kwa utaratibu wa akaunti 9 kama ilivyoelekezwa. Kwa kutumia mifumo hiyo, halmashauri zimeweza kutekeleza bajeti kwa kufuata taratibu na miongozo iliyotelewa na Wizara ya Fedha. Aidha, taarifa za mapato na matumizi za kila mwezi zinapatika kutoka kwenye mfumo.

Usimamizi wa Elimu

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inasimamia na kuratibu uandikishaji wa wanafunzi katika elimumsingi na kidato cha tano, kuajiri walimu, kutoa elimu kwa watu wazima na vijana nje ya mfumo rasmi wa shule, kuongeza miundombinu ya shule na kutoa mafunzo kwa watendaji katika ngazi mbalimbali.

Elimu ya Awali na Msingi

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na mafanikio makubwa kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi Awamu ya I (MMEM I) na ya II ambao kwa sasa utekelezaji wake uko katika Awamu ya III. Ili kuhakikisha kuwa elimu ya awali inatiliwa mkazo, jumla ya shule 14,946 zina madarasa ya Elimu ya Awali kati ya shule 16,014 za msingi sawa na asilimia 93.33 ya shule shule zote za msingi zilizopo. Hali ya uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya awali imeongezeka kufikia wanafunzi 971,717 (Wavulana 480,053 na Wasichana 491,663) mwaka 2016 kutoka wanafunzi 877,489 (Wavulana 436, 778 na Wasichana 440, 711) mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Elimu ya Msingi, OR-TAMISEMI imeendelea na jukumu la kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi Awamu ya Tatu (MMEM III) kwa lengo la kuimarisha elimu ya msingi nchini ambao umejikita katika kuinua Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu kwa wanafunzi wa darasa la kwanza na la pili. Hadi mwezi Juni, 2016, jumla ya walimu 15,000 wanatarajiwa kupata mafunzo ya kuwajengea uwezo katika ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, katika kusaidia kuimarisha ufuatiliaji na usimamizi wa Elimu katika ngazi za Kata, Waratibu Elimu Kata wapatao 784 waliwezesha kwa kupatiwa pikipiki. Lengo ni kuhakikisha kwamba, wanafunzi wa darasa la kwanza na la pili nchini wanajua Kusoma, Kuandika na Kuhesabu kabla ya kuingia darasa la tatu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanikiwa kuongeza nyumba za walimu kutoka 41,835 mwaka 2010 hadi nyumba 58,448 mwezi Februari 2016. Aidha, idadi ya matundu ya vyoo imeongezeka kutoka 149,566 mwaka 2010 hadi 206, 658 mwezi Februari 2016 sawa na ongezeko la asilimia 38.18. Bado kuna upungufu wa matundu ya vyoo 464, 676 ikiwa ni (matundu ya vyoo 380, 373 shule za Msingi na 84, 303 Sekondari). Vilevile, uwiano wa vitabu umeendelea kuimarika kutoka uwiano wa 1:7 mwaka 2007 hadi uwiano wa 1:3 mwaka 2015. Lengo ni kufikia uwiano wa 1:1 ifikapo mwaka 2017. Juhudi hizi zinatokana na ushirikiano baina ya halmashauri, wazazi/walezi na Wadau mbalimbali wa Maendeleo na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Wanafunzi waliotarajiwa kuandikishwa darasa la kwanza mwaka 2016 ni 1,433,840. Hadi kufikia mwezi Machi 2016, jumla ya wanafunzi walioandikishwa ni 1,896,584 (wavulana 960, 877 na wasichana 935,707). Idadi ya uandikishaji wa wanafunzi katika darasa la kwanza imeongezeka kutokana na Serikali kutekeleza mpango wa Elimu Bila Malipo.

Mheshimiwa Spika, Wanafunzi 775,273 wakiwemo wavulana 361,307 na wasichana 413,966 walisajiliwa kufanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi mwaka 2015, sawa na asilimia 75.24. Kati ya wanafunzi waliosajiliwa, wanafunzi 763,606 sawa na asilimia 98.50 ya wanafunzi waliosajiliwa walifanya mitihani wakiwemo wavulana 354,706 na wasichana 408,900. Takwimu zinaonesha kuwa jumla ya wanafunzi 266,900 sawa na asilimia 25.90 hawakuhitimu darasa la saba. Takwimu hizi zinatuaonesha kuwa hali ya mdondoko (*dropout*) ni kubwa. Naomba kutumia fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, watendaji wa Serikali na wadau wote wa Elimu na wazazi tushirikiane ili kupunguza mdondoko wa wanafunzi katika ngazi ya elimu ya msingi.

Mheshimiwa Spika, kati ya wanafunzi waliofanya mtihani wa darasa la saba mwaka 2015 jumla ya wanafunzi 518,034 sawa na asilimia 67.84 walifaulu mitihani yao wakiwemo wavulana 253,904 na wasichana 264,130. Wanafunzi 518,034 sawa na asilimia 100 wakiwemo wavulana 253,904 na wasichana 264,130 walichaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2016. Natoa wito kwa walimu kufanya kazi kwa bidii ili kuhakikisha wanafunzi wanafanya vizuri zaidi katika masomo. Aidha, nawasihi wazazi na walezi kushirikiana na walimu kuhakikisha kuwa watoto wote waliochaguliwa kuingia kidato cha kwanza wanaripoti shuleni.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwezi Mei 2016, Serikali inatarajia kutoa ajira za walimu wapatao 40,000 ikijumuisha wa cheti, Stashahada na Shahada ili kukabiliana na upungufu wa walimu uliopo katika shule za Msingi na Sekondari nchini. Zaidi ya **shilingi bilioni 17** zitahitajika kwa ajili ya kulipa posho pamoja na nauli za walimu wapya watakoajiriwa na kupelekwa katika halmashauri zote nchini.

Elimu ya Sekondari

Mheshimiwa Spika, OR - TAMISEMI inaendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari awamu ya pili (MMES II) ili kuimarisha Elimu ya Sekondari. Lengo la mpango huu ni kuinua ubora wa elimu. Aidha, utekelezaji wa mpango huu unahusisha ujenzi wa miundombinu ya shule 264 za awamu ya kwanza ambao umekamilika kwa asilimia 64. Serikali inaendelea kukamilisha ujenzi na uboreshaji wa shule 264 za awamu ya kwanza na kuendelea na uboreshaji wa miundombinu katika shule nyingine 528.

Mheshimiwa Spika, walimu 3,828 wa shule za Sekondari wamepatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo katika ufundishaji na ujifunzaji. Hadi kufikia mwezi Juni, 2016 jumla ya Walimu 8,828 wa Sekondari watakuwa wamepata mafunzo hayo. Wadau wengine wanaoshirikiana na Serikali kuwajengea uwezo

Walimu wa shule na Waratibu Elimu Kata nchini ni pamoja na Agakhan Foundation (Walimu 2,366) na EQUIP-T (Walimu 12,253).

Mheshimiwa Spika, shule za kidato cha tano (5) zimeongezeka kutoka shule 179 mwaka 2010 hadi shule 279 mwaka 2016, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 55.87. OR - TAMISEMI ilitoa agizo kwa mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuongeza nafasi kwa asilimia 25 kwa ajili ya wanafunzi waliofanya mtihani wa kidato cha nne mwaka 2015 na kuhakikisha kuwa Tarafa ambazo hazina madarasa ya kidato cha 5 na 6 zinakuwa nayo. Ni imani yangu kuwa, wanafunzi 89,929 waliofaulu mtihani wa kidato cha Nne mwaka 2015 wa madaraja ya I – III watapata nafasi ya kujiunga na kidato cha tano (5) mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2015, Serikali ilipata msaada wa vitabu vya Hisabati, na Sayansi 2,500,000 kutoka Shirika la Kimataifa la USAID na vilisambazwa katika shule za sekondari katika halmashauri zote nchini. Aidha, katika kuimarisha masomo ya sayansi, maabara 10,389 zilipangwa kujengwa. Hadi kufikia mwezi Desemba, 2015 maabara 6,254 zimekamilika ambazo ni sawa na asilimia 60.2 na maabara 2,940 zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Natumia fursa hii kuwaagiza Wakuu wa Mikoa na Wilaya ambao hawajakamilisha ujenzi wa maabara hizo kuongeza nguvu katika kusimamia na kukamilisha ujenzi wa maabara hizo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba, chini ya Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari MMES II, nyumba 183 zenye uwezo wa kuishi walimu sita kila moja (multi-unit houses) zinaendelea kujengwa katika Halmashauri mia moja na tano (105).

Michezo Mashuleni

Mheshimiwa Spika, Tanzania ilishiriki katika mashindano ya 14 ya Shirikisho la Michezo ya Shule za Sekondari kwa Nchi za Afrika Mashariki (FEASSA) yaliyofanyika kuanzia tarehe 16 hadi 24/08/2015 katika mji wa Huye nchini Rwanda. Washiriki walikuwa 322, kati yao wanafunzi walikuwa 269, viongozi, walimu na waamuzi walikuwa 53. Aidha, mashindano ya michezo ya UMISSETA na UMITASHUMTA nayo yalifanyika jijini Mwanza kwenye viwanja vya Chuo cha Ualimu Butimba kuanzia tarehe 8/06/2015 hadi 3/07/2015 kwa kuwajumuisha wanafunzi 1,753 wa sekondari na 2,456 wa shule za msingi Tanzania.

Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais TAMISEMI inaratibu utekelezaji wa utoaji wa huduma za afya, ustawi wa jamii na lishe kwenye ngazi ya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kusimamia rasilimali watu, upatikanaji wa rasilimali fedha, dawa, vifaa tiba, kuimarisha uongozi na uendeshaji wa shughuli za afya ya msingi. Muundo huu mpya umewezesha utekelezaji wa sera, mikakati na miongozo inayotolewa na Wizara ya Kisekta.

Timu za Usimamizi za Mikoa

Mheshimiwa Spika, Huduma za Afya katika Mikoa imeendelea kuboreshwa kwa kufuata maelekezo ya Wizara ya Kisekta. OR-TAMISEMI imeendelea kuimarisha Timu za Afya za Mikoa zenye jukumu la kusimamia na kuratibu shughuli za Afya za Mikoa. Katika ngazi hii pia, OR-TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Afya imeendelea na juhudi za kuzijengea uwezo timu za Afya za Mikoa kupitia programu mbalimbali ukiwemo mradi wa "*Regional Referral Hospital Management Programme*" (RRHMP) unaotekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Japan.

Timu za Usimamizi za Halmashauri

Mheshimiwa Spika, huduma za afya za halmashauri zinasimamiwa na timu za Afya za Wilaya. Timu hizi zinasimamia Hospitali za Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati. Majukumu ya timu hizi ni kuhakikisha kuwa huduma bora za afya zinatolewa katika maeneo yao ikiwa ni pamoja na elimu ya afya, upatikanaji wa dawa, vipimo, chanjo na huduma za mama na mtoto.

Vituo vya kutolea huduma za Afya (Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati)

Mheshimiwa Spika, hadi sasa tunazo Halmashauri **181**, kati ya hizo halmashauri zenye Hospitali za Wilaya za Serikali ni **84**, na Halmashauri **97** hazina Hospitali za Wilaya za Serikali. Halmashauri zisizo na Hospitali za Serikali hutumia Hospitali za Mashirika ya Umma au Taasisi za dini kama Hospitali Teule. Kata zenye Vituo vya Afya vya Serikali ni Kata **484** na Kata **3,506** hazina Vituo vya Afya. Vile vile, Vijiji **4,502** vina Zahanati za Serikali na Vijiji **8,043** havina Zahanati za Serikali. Ni azma ya Serikali kuona kuwa kila halmashauri inakuwa na Hospitali, kila Kata inakuwa na kituo cha afya na kila kijiji kinakuwa na zahanati. Huduma za afya nchini kwa ngazi ya Hospitali, kituo cha afya na zahanati hutolewa na wadau mbalimbali wakiwemo mashirika ya Dini, makampuni na watu binafsi. Hivyo, Serikali itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuhakikisha

kuwa huduma za afya zinawafikia wananchi wote kwa viwango na ubora unaotakiwa.

Ujenzi na ukarabati wa Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa majengo mapya na ukarabati wa majengo yaliyochakaa katika vituo vya kutolea huduma za afya. Katika mwaka wa fedha **2014/15**, hospitali, vituo vya afya na zahanati zilikarabatiwa na nyingine kujenga sehemu ya majengo kwa kutumia **shilingi 263,346,623,044.10**.

Katika mwaka wa fedha **2015/2016** hadi mwezi Februari 2016 Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati zilikarabatiwa/kujenga sehemu ya majengo kwa kutumia **shilingi 18,684,860,267.01**. Ukarabati na ujenzi uliofanyika umechangia katika kuboresha utoaji wa huduma za afya.

Upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka mkakati wa kuhakikisha kuwa hali ya upatikanaji wa dawa na vifaa tiba inazingatia mahitaji halisi katika vituo vya kutolea huduma za afya. Mkakati huo unahusisha ushiriki wa wananchi katika kusimamia suala la dawa na vifaa tiba kupitia Kamati za Afya za vituo, kushirikisha Sekta Binafsi na Asasi za Kiraia kwa uwazi na uwajibikaji na halmashauri zinatumia utaratibu wa kuagiza dawa moja kwa moja kutoka Bohari ya Dawa kwa kutumia njia ya mtandao.

Mheshimiwa Spika, Hospitali mbalimbali za Mikoa zimefungua maduka ya dawa ya Bohari ya Dawa (MSD) kwa lengo la kuboresha huduma. Maduka yamefunguliwa katika Mikoa ya Dar es Salaam (Hospitali ya Muhimbili), Mkoa wa Arusha (Mount Meru), Mkoa wa Mwanza (Sekou toure) na Mkoa wa Mbeya (Hospitali ya Rufaa Mbeya). Mikoa mingine iko katika hatua mbalimbali za kuanzisha maduka hayo ya dawa.

Huduma za Lishe

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na tatizo la lishe duni nchini, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeanza kuhuisha mkakati wa Lishe wa miaka mitano kuanzia Julai 2016 hadi Juni 2021. Mkakati huo unahusisha masuala yafuatayo:- uundwaji wa kamati za lishe katika ngazi za Mikoa na Halmashauri, kufanya mapitio ya Sera ya Chakula na Lishe ya mwaka 2014, kutenga na kuajiri wataalamu wa Lishe katika ngazi ya Mikoa na Halmashauri, kutoa elimu na kuhamasisha kuhusu afya na lishe bora na kutoa tiba kwa

watoto wenye utapiamlo mkali, unaenda sambamba na kuhuisha mkakati wa lishe.

Huduma za Ustawi wa Jamii

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa fedha 2015/16 (hadi kufikia Februari 2016) jumla ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu 369,401 wametambuliwa. Kati ya hao, watoto 99,061 wamepatiwa huduma mbalimbali zenye thamani ya **shilingi 1,507,375,750**. Serikali imejipanga kuhakikisha kuwa watoto wote walio katika mazingira magumu wanapatiwa haki zao za msingi kama elimu, afya, chakula na malazi. Aidha, jumla ya watoto 6,574 wamekumbwa na unyanyasaji na ukatili. Kati ya hao, watoto 2,108 mashauri yao yamefikishwa polisi na watoto 985 mashauri yao yamefikishwa mahakamani. Vile vile, jumla ya mashauri 1,080 yamepata suluhisho. OR-TAMISEMI itaendelea kuimarisha usimamizi wa huduma kwa wazee, watoto, watu wenye ulemavu na familia katika ngazi za Mikoa na halmashauri kulingana na sera, sheria, na Miongozo iliyopo.

Shughuli za Mfuko wa Pamoja wa Afya

Mheshimiwa Spika, Serikali imeingia mkataba wa miaka mitano (kuanzia mwaka wa fedha 2015/16, mpaka mwaka wa fedha 2019/20) na mashirika ya Kimataifa ya maendeleo ikiwamo, Switzerland, UNFPA, UNICEF, Ireland, Benki ya Dunia na Denmark, wa kuendelea kushirikiana katika utoaji wa huduma za afya za Msingi Nchini. Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya **shilingi 68,875,456,000** zilitengwa, ambapo Mikoa ilitengewa **shilingi 3,757,007,000** na Halmashauri **shilingi 65,118,449,000**. Hadi kufikia februari 2016, jumla ya **shilingi 34,437,728,000** zilikuwa zimetolewa sawa na asilimia 50. Fedha hizi zimetumika kuboresha miundombinu, upatikanaji wa dawa na vitendea kazi.

Shughuli za Mfuko wa Dunia wa kudhibiti Kifua Kikuu, UKIMWI na Malaria (Global Fund)

Mheshimiwa Spika, OR-TAMISEMI imeendelea kuratibu shughuli za 'Global Fund' ikiwa na lengo la kudhibiti magonjwa matatu ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria. Katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya **shilingi bilioni 1.9** zimepelekwa kwenye Mikoa kwa ajili ya kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa katika utekekezaji wa shughuli za uthibiti wa magonjwa hayo.

Shughuli za UKIMWI kwa Sekta zote

Mheshimiwa Spika, OR-TAMISEMI inaratibu shughuli za kudhibiti UKIMWI kwenye OR-TAMISEMI, Mikoa na Halmashauri. Kazi zilizofanyika ni pamoja na; kutoa fedha kwa ajili ya chakula kwa watu wanaoishi na VVU na UKIMWI pamoja kuanzisha miradi ya uzalishaji mali, kutoa misaada kwa watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu kama sare za shule, vifaa vya shule, chakula na kuanzishiwa miradi inayosimamiwa na walezi wao. Uhamasishaji na utaoaji wa elimu ya kujikinga na maambukizi ya VVU kwenye kata, shule za msingi na sekondari na vikundi vya vijana unaendelea. Aidha, OR-TAMISEMI inaendelea kuzijengea uwezo kamati za UKIMWI za Kata na Vijiji ili kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Shughuli za usimamzi wa usafi

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa agizo la Mheshimiwa Rais linatekelezwa kwa uendelevu, ukaguzi na uhamasishaji wa usafi katika Majiji, Manispaa na Halmashauri za Miji katika Mikoa 26 umefanyika. Pamoja na ukaguzi uliofanyika, mikoa yote ilielekezwa kuendelea na shughuli za kupendezesha mazingira ya miji kwa kuanza na maeneo ya wazi, kando ya barabara na kwenye ofisi za umma. Natoa wito kwa wananchi wote kuhakikisha maeneo yao yanakuwa safi kwa wakati wote. Tabia ya usafi ikijengeka katika Jamii, magonjwa ya kipindupindu na kuharisha yataondoka.

Hali ya mlipuko wa Kipindupindu

Mheshimiwa Spika, mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu ulitokea mwezi Agosti 2015. Hadi tarehe 12 Aprili 2016, kulikuwa na jumla ya watu **20,751** waliopata kipindupindu. Kati ya hao, watu **20,366** wametibiwa na kuruhusiwa, watu **31** walikuwa bado wanaendelea na matibabu na watu **327** wamepoteza maisha. Mikoa yenye wagonjwa wapya wa kipindupindu na idadi ya wagonjwa katika mabano ni Morogoro (12), Kilimanjaro (9), Pwani (4), Mara (4), Manyara (1), Arusha (1) na Tanga (2). Mikoa ya Njombe na Ruvuma haijatoa taarifa ya kuwepo kwa ugonjwa wa kipindupindu. Ni aibu kwa Taifa letu kuendelea kuwa na wagonjwa wa kipindupindu. Rai yangu kwa wananchi wote ni kwamba, kinga ya kipindupindu ni kuhakikisha usafi wa mazingira unadumishwa. Tuweke ajenda ya usafi kuwa ni jambo la lazima kwa kila mtanzania.

Mfuko wa Afya ya Jamii (Community Health Fund –CHF)

Kwa mwaka wa fedha 2014/15, jumla ya kaya **1,089,086** zilijiunga na CHF na kuchangia jumla ya **shilingi 9,654,299,000**. Kiasi cha fedha za tele kwa tele

zilizotolewa ni **shilingi 1,091,288,820**. Kwa mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya kaya zilizojiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii ni **1,361,695** na kuchangia jumla ya **shilingi 13,348,919,000**. Kiasi cha fedha za tele kwa tele zilizotolewa ni **shilingi 2,445,102,770**. Nitoe wito kwa viongozi katika ngazi za Mikoa na Halmashauri kuwahamasisha wananchi kujiunga na mfuko huu ili kulinda afya zao na kupata matibabu kwa mwaka mzima bila gharama za nyongeza. Aidha, nawaagiza watumishi wa afya wahakikishe dawa na vifaa vinapatikana kwa wakati wote ili wananchi waweze kupata huduma ipasavyo. Kwa upande wake Serikali itahakikisha fedha za kununua dawa na vifaa tiba zinapelekwa kwa Mamlaka husika kwa wakati.

Mradi wa Uendelezaji Miji ya Kimkakati (Tanzania Strategic Cities Project - TSCP)

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Uendelezaji Miji ya Kimkakati (Tanzania Strategic Cities Project - TSCP) umetokelezwa kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia ambapo jumla ya Dola za Kimarekani **milioni 163** zilitolewa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za uimarishaji miundombinu. Pia, Serikali ilipata Ruzuku ya Dola za Kimarekani **milioni 12.7** toka Serikali ya Denmark (RDE) kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mradi katika jiji la Arusha, Tanga, Mwanza/Ilemela, Mbeya na katika manispaa za Dodoma, Mtwara Mikindani na Kigoma Ujiji pamoja na Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma (CDA).

Mheshimiwa Spika, lengo la mradi huo ni kuboresha huduma za msingi za miji na ufikiwaji wake kwa kufanya yafuatayo; (i) Uboreshaji wa miundombinu, (ii) ununuzi wa vitendea kazi (magari, na vifaa vya ujenzi na matengenezo) (iii) kuboresha ukusanyaji wa mapato ya ndani na usimamizi wake.

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka wa fedha 2010/11 hadi 2015/16, uboreshaji wa miundombinu na huduma za mijini umegharimu Dola za Kimarekani **milioni 150.6**. Kazi zilizofanyika ni pamoja na; ujenzi kwa kiwango cha lami barabara zenye urefu wa km 141, ujenzi wa maeneo maalum matano (5) ya kutupia taka ngumu (landfills); Kujenga vituo vitatu (3) vya mabasi madogo (daladala); vituo vinne (4) vya mabasi makubwa; na vituo viwili (2) vya kuegesha magari ya mizigo. Aidha, karakana ya magari ya Manispaa ya Dodoma imekarabatiwa na mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa km 17.3 imejengwa. Vile vile, vifaa na mitambo ya usafi na ukusanyaji wa taka ngumu vimenunuliwa. Waathirika katika maeneo ambayo miradi ilitekelezwa wamelipwa fidia, vitendea kazi kama magari, kompyuta, na vifaa vya kukusanyia taarifa za mifumo ya kijiografia (GIS) na TEHAMA vimenunuliwa, na mafunzo ya usimamizi wa miradi kwa watumishi yametolewa.

Programu ya Kuimarisha Mamlaka za Miji 18 (Urban Local Government Strengthening Programme – ULGSP)

Mheshimiwa Spika, lengo la Programu hii ni kuboresha utoaji wa huduma za msingi katika maeneo ya miji husika. Maeneo yaliyoboreshwa ni pamoja na; mipango miji; ukusanyaji wa mapato ya ndani hasa kodi ya majengo; usimamizi wa fedha na manunuzi; miundombinu ya miji na utunzaji wake; mifumo ya uwajibikaji na usimamizi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa 18.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/15, jumla ya **shilingi 58,548,463,830.26** ziliidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za programu. Fedha hizi zilipokelewa mwishoni mwa mwaka wa fedha 2014/15, hivyo, utekelezaji wake umefanyika kuanzia Julai 2015. Utekelezaji ni kama ifuatavyo: Barabara za lami katika Halmashauri Manispaa ya Moshi (km 5.35) na Halmashauri ya Mji wa Kibaha (km 1.2) zimekamilika; Ujenzi wa machinjio sita (6) za kisasa unaendelea katika miji ya Lindi, Geita, Shinyanga, Morogoro, Singida, na Songea; Ujenzi wa masoko sita (6) unaendelea katika miji ya Korogwe, Mpanda, Geita, Musoma, Tabora na Sumbawanga; Ujenzi wa vituo vitano (5) vya mabasi unaendelea katika miji ya Korogwe, Mpanda, Njombe, Kibaha na Singida; na ukarabati wa vituo viwili (2) vya mabasi katika miji ya Iringa na Sumbawanga unaendelea. Vilevile, ununuzi wa vifaa hamsini (50) vya kuhifadha taka ngumu na magari saba (7) ya kusombea taka umefanyika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/16, kiasi cha **shilingi 77,196,235,361.6** ziliidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu, kujenga uwezo wa watumishi katika usimamizi na ununuzi wa vitendea kazi katika Miji 18 hapa nchini. Fedha hizi zimepokelewa Aprili 2016 hivyo utekelezaji wake unaendelea.

Mradi wa Uendelezaji Jiji la Dar es Salaam (Dar es Salaam Metropolitan Development Project – DMDP)

Mheshimiwa Spika, kutokana na utekelezaji unaoridhisha wa mradi wa uendelezaji Miji ya Kimkakati (TSCP), Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Benki ya Dunia na NORDIC wameingia mkataba wa uanzishaji wa mradi wa Uendelezaji Jiji la Dar es Salaam (DMDP) utakaogharimu Dola za Kimarekani **milioni 330.3** ambazo zitatolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Benki ya Dunia na NORDIC. Kiasi cha Dola za Kimarekani **milioni 5.00** zitazolewa na NORDIC kwa ajili ya kukabiliana na changamoto za Mabadiliko ya Tabia Nchi na Dola za Kimarekani **milioni 300** zitatolewa na Benki ya Dunia. Serikali itachangia kiasi cha Dola za Kimarekani **milioni 25.3** kwa ajili ya kulipa fidia kwa Wananchi watakaoathirika na mradi

huu. Mradi utazihusisha halmashauri nne (4) za:- Manispaa za Ilala, Kinondoni na Temeke na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, kazi zilizopangwa kufanyika ni: kuimarisha miundombinu ya barabara za mlisho (feeder roads) zenye urefu wa **km 65.7** zitakazounganisha halmashauri za jiji pamoja na barabara kuu ya usafiri wa mabasi yaendayo haraka (DART); kujenga barabara za mitaa zenye urefu wa **km 145** zitazounganisha maeneo yaliyopangwa kiholela na barabara kuu katika kata **14** za jijini Dar es salaam, kudhibiti mafuriko kwa kujenga mifereji mikubwa ya kutiririsha maji ya mvua yenye urefu wa **kilometa 31.8** na mingine midogo katika maeneo yanayoathiriwa na mafuriko ya mara kwa mara katika mabonde ya jiji la Dar es Salaam; kuimarisha mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani; kuimarisha mfumo wa ukarabati na matengenezo ya miundombinu; kusaidia uandaaji wa mipango ya pamoja ya usafirishaji na matumizi ya ardhi katika ukanda wa mabasi yaendayo haraka (Intergrated Transport and Land Use Planning along BRT Corridor) na, kuboresha mfumo wa mipango miji katika manispaa za jiji la Dar es Salaam (Urban Planning Systems).

Mheshimiwa Spika, shilingi **17,296,000,000.00** zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka 2015/16, ambazo ziliombwa kwa ajili ya kuboresha mfumo wa usimamizi wa Maendeleo ya miji katika jiji la Dar es Salaam ili kuliwezesha kuboresha utoaji wa huduma za msingi za jamii. Mnamo mwezi Machi 2016, kiasi cha **dola za Kimarekani 10,400,000.00** sawa na **shilingi bilioni 20.8** zimepokelewa na utekelezaji wa shughuli zilizopangwa umeanza.

Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP)

Mheshimiwa Spika, Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP) Awamu ya I ilifikia ukomo wake mwaka wa fedha 2012/13 na kuongezewa muda hadi mwaka 2015/16 ili kukamilisha miradi mbalimbali iliyokuwa inaendelea. Katika mwaka wa fedha 2015/16, baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeendelea kutekeleza na kukamilisha miradi hiyo ya maendeleo ya kilimo ambayo ilikuwa haijakamilika. Shughuli zilizokuwa zinaendelea kutekelezwa ni pamoja na ujenzi wa skimu za umwagiliaji, malambo 3 ya kunyweshea mifugo, ununuzi wa mashine 3 za kukamulia mafuta ya mbegu, ununuzi wa mashine 9 za kukoboa na kusaga nafaka, usambazaji wa pembejeo kama mbegu bora za mazao, mbolea na madawa ya kuoshea mifugo, ununuzi na usambazaji wa kuku bora, ujenzi wa maghala, ujenzi wa masoko ya mazao, kukarabati machinjio, kutoa chanjo kwa mifugo, kutoa mafunzo ya kilimo na ufugaji bora kwa wakulima na wafugaji, kuanzisha mashamba darasa, kutoa mafunzo kazini kwa maafisa ugani, ununuzi wa kompyuta na pikipiki, kufanya shughuli za

usimamizi, tathmini na ufuatiliaji wa shughuli zilizotekelezwa, ujenzi wa majosho mawili, ukarabati wa vituo vitatu (3) vya rasilimali za kilimo vya kata (Ward Agricultural Resource Centres- WARCs) na ujenzi wa km 61 za barabara za vijijini/mashambani. Aidha, katika kipindi hicho idadi ya maafisa ugani, imeongezeka kutoka wataalam 3,326 mwaka wa fedha 2006/07 na kufikia wataalam 13,532 kwa mwaka wa fedha 2015/16. Kati ya hao, 8,756 ni wataalam wa kilimo, 4,283 wataalamu wa mifugo na 493 ni wataalamu wa sekta ya uvuvi.

Sekta ya Ngozi

Mheshimiwa Spika; sekta ya ngozi ina mchango mkubwa katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa kuwa ina uwezo mkubwa wa kuingiza fedha za kigeni. Kutokana na umuhimu huo, Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa sekta ya ngozi, ilibuni na kuandaa mkakati wa kufufua na kuendeleza sekta ya ngozi nchini mwaka 2007. Utekelezaji wa mkakati huu unagharamiwa na Serikali kupitia mfuko wa maendeleo ya mifugo (*Livestock Development Fund-LDF*). Halmashauri 55 zilianza utekelezaji kulingana na uwezo wa Mfuko huo. Hivi sasa halmashauri zinazotekeleza mkakati huo zimeongezeka hadi sabini na tano (75).

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa sekta ya ngozi, inaendelea kuwahamasisha na kuwaelimisha wananchi kuongeza thamani na ubora wa ngozi tangu zinapozalishwa, kutunzwa, kusafirishwa na kuuzwa ndani na nje ya nchi. Jumla ya wafugaji **3,525**, wachinjaji na wachunaji **2,541**, wawambaji ngozi na wachambuzi wa madaraja **1,018**, wafanyabiashara **400**, maafisa ugani **2,325**, madiwani na viongozi wengine wa Serikali **2,549**, walihamasishwa na kupewa mafunzo juu ya umuhimu wa zao la ngozi, utunzaji na uhifadhi wa ngozi kutoka hatua ya mwanzo ya uchinjaji na uchunaji hadi uhifadhi. Aidha, ujenzi na ukarabati wa miundombinu kama vile meza **29** za kuchunia ngozi, fremu **127** za kukaushia ngozi zilizengwa na machinjio **53** yamekarabatiwa hadi kufikia Desemba, 2015.

Mheshimiwa Spika, OR-TAMISEMI itaendelea kushirikiana na wadau kuhamasisha na kuhimiza sekta binafsi ndani na nje ya nchi kuongeza kasi ya kufufua na kujenga viwanda vya kusindika ngozi hapa nchini na viwanda vya kutengeneza bidhaa za ngozi ili hatimaye kuongeza thamani ya ngozi ili kupata mapato zaidi badala ya kuuza ngozi ghafi. Aidha, nazielekeza halmashauri kutumia sheria ndogo kudhibiti utoroshaji wa ngozi kupitia mipaka isiyo rasmi kati ya nchi yetu na majirani zetu.

Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RWSSP)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya **shilingi 130,780,984,062** zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Maji Vijijini. Hadi Desemba, 2015 jumla ya **shilingi 78,344,103,752** ambazo ni sawa na **asilimia 60** zilikuwa zimepelekwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Sekretarieti za Mikoa zilipangiwa kiasi cha **shilingi 1,500,000,000**. Hadi kufikia Machi 2016, kiasi cha **shilingi 791,300, 000** sawa na **asilimia 52** zilikuwa zimepelekwa mikoani.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/16, Mamlaka za Serikali za Mitaa zilipanga kujenga vituo vya kuchotea maji 6,063 ambavyo vinatarajiwa kutumiwa na watu 1,515,721. Hadi kufikia mwezi Machi 2016, vituo 1,306 vimejengwa sawa na **asilimia 21.5**. Aidha, ujenzi katika maeneo mbalimbali unaendelea.

Programu ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu (PFM)

Mheshimiwa Spika, Programu ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu ilianza mwaka 2006/07 chini ya ufadhili wa Serikali ya Finland. Lengo la Programu lilikuwa ni kuwashirikisha wananchi katika usimamizi na uhifadhi wa maliasili, ikiwemo misitu. Usimamizi unaenda sambamba na kuwawezesha wananchi kufanya shughuli mbadala za kujiongezea kipato ambazo ni rafiki na mazingira. Programu hii ilitekelezwa katika Mikoa ya Lindi, Morogoro, Tanga, Kigoma, Ruvuma, Rukwa na Kagera.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Usimamizi Shirikishi wa misitu ilifikia ukomo mwezi Februari, 2016. Kupitia programu hii, vijiji 195 vimewezeshwa kutambua, kutenga na kuhifadhi rasilimali zilizomo katika misitu ya jamii **226** yenye jumla ya hekta 293,795 kwenye halmashauri za Kalambo, Handeni, Kilindi, Ruangwa na Nachingwea.

Mheshimiwa Spika, sehemu kubwa ya misitu katika halmashauri haijahifadhiwa kisheria na hivyo, kukosa haki ya vijiji kumiliki na kusimamia. Serikali imezielekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga fedha katika bajeti ya mwaka 2016/17 kushughulikia suala hilo.

TAASISI ZILIZO CHINI YA OFISI YA RAIS TAMISEMI

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nitoe taarifa ya utekelezaji wa taasisi zilizo chini ya OR-TAMISEMI.

Shirika la Elimu Kibaha

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2015/16, Shirika lilitarajia kuhudumia wagonjwa 200,000 katika Hospitali Teule ya Rufaa ya Mkoa wa Pwani - Tumbi, kutoa elimu ya utabibu kwa wanachuo 230 katika Chuo cha Maafisa Tabibu Kibaha, kutoa elimu ya Msingi na Sekondari kwa wanafunzi 2,740, kuboresha miundombinu na upatikanaji wa vitendea kazi kwa wafanyakazi 896, kutekeleza miradi ya maendeleo kama vile ukarabati wa majengo, ujenzi wa maabara, kuchimba visima na kuendeleza upanuzi wa jengo la hospitali ya Tumbi.

Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Machi 2016, Shirika lilitokeleza yafuatayo: kutoa huduma ya kinga na tiba kwa wagonjwa 102,826 pamoja na huduma kwa wahanga wa ajali za barabarani, kutoa elimu ya utabibu kwa wanachuo 154 katika chuo cha Maafisa Tabibu Kibaha. Aidha, Shirika lilipata kibali cha kuanzisha kozi ya uuguzi, na chuo kimechukua wanafunzi 54 wa stahhada ya uuguzi. Chuo kilichukua wanafunzi 50 wa cheti cha Afya ya Jamii. Jina la chuo limebadilishwa na kuwa Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Kibaha (Kibaha College of Health and Allied Science); kutoa huduma ya elimu kwa wanafunzi 2,713 (1,712 Sekondari na 1,001 Shule ya Msingi); kutoa huduma za maktaba kwa wananchi 29,351 Wanajamii 453 walipatiwa elimu ya ufundi stadi katika fani ya kilimo, mifugo, useremala, uashi, ushonaji, usimamizi wa hoteli, umeme, ufundi wa magari, ufundi bomba na udereva kupitia Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha. Wanajamii 492 kutoka kata za Mkuza, Sofu na Picha ya Ndege walipatiwa mafunzo ya ufugaji kuku, kilimo cha mbogamboga na ujasiriamali. Aidha ng'ombe 147 waliendelea kuhudumiwa na lita 53,690 za maziwa zilizalishwa na kuuzwa kwa wanajamii.

Chuo Cha Serikali Za Mitaa Hombolo

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Serikali za Mitaa kilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Bunge Na. 26 ya Mwaka 1994, Sura ya 396 na toleo lililorejewa mwaka 2002. Madhumuni ya kuanzishwa kwa chuo hiki ni kuisaidia Serikali katika kutatua changamoto zinazozikabili Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia programu za mafunzo, tafiti na ushauri elekezi. Mwaka 2009, chuo hiki kiliteuliwa na Serikali kuwa Taasisi Kiongozi ya Mafunzo (Lead Training Institute) katika kuratibu na kusimamia ubora wa mafunzo yatolewayo kwa watumishi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/16, chuo kimeweza kutoa mafunzo na ushauri elekezi kwenye maeneo mbalimbali ya uendeshaji ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini na kukiingizia chuo jumla ya **Shilingi 658,057,000.00**. Aidha, katika kipindi hicho, chuo kilidahili wanafunzi wapya **1,865** kwenye kozi mbalimbali nane (8) zinazotolewa kwa sasa. Kati ya

wanafunzi hao, **1,137** ni wanawake na **728** ni wanaume na kufanya chuo kuwa na jumla ya wanafunzi **3,097** ambapo wanawake ni **1,910** na wanaume ni **1,187**. Udahili huu umekiingizia chuo jumla ya **Shilingi bilioni 3.2**.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na ongezeko la wanafunzi, Chuo kina mpango wa kupanua eneo ili kiweze kuongeza idadi ya wanachuo. Aidha, kwa kushirikiana na sekta binafsi chuo kimeendelea kuendesha tawi la chuo hiki eneo la Kimvi (km 7 kutoka Hombolo). Tawi hili la chuo cha Hombolo lilianzishwa mwaka wa fedha 2009/10 na kwa sasa lina jumla ya wanafunzi 126. Aidha, katika mwaka wa fedha 2015/16, Chuo kimefungua tawi jingine Dodoma mjini ambapo jumla ya wanafunzi 320 walidahiliwa na kukiingizia chuo shilingi **265,000,000.00**. Vile vile Chuo kimeendelea na ujenzi wa kituo cha afya ambapo ujenzi wa vyoo vya nje pamoja na mfumo wa maji taka umefanyika kwa gharama ya shilingi **15,806,100.00**. Chuo kimelipa kodi ya ardhi kwa viwanja viwili (Na: 38 & 40) kwa ajili ya upanuzi wa chuo kampasi Kuu-Hombolo kwa gharama ya shilingi **47,000,000.00**. Katika kuboresha huduma ya usafiri kwa watumishi na wanafunzi, chuo kiliweza kununua basi kubwa aina ya YUTONG lenye uwezo wa kuchukua abiria 56 kwa gharama ya **shilingi 349,872,000.00**.

Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa

Mheshimiwa Spika, jukumu la msingi la Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura ya 290 RE 2002 ni pamoja na kutoa mikopo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya kutekeleza miradi ili kusaidia kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Katika mwaka wa fedha 2015/16, Bodi imeendelea kurekebisha muundo wake ili kuongeza tija na ufanisi na kuwa chombo kinachojitegemea, chenye uwezo wa kiutendaji wa kusimamia na kuendesha shughuli zake na uwezo wa kukidhi mahitaji ya mikopo katika ngazi zote za Mamlaka za Serikali za Mitaa na kwa aina zote za miradi inayokubalika kupata mikopo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/16, uwasilishaji wa mtaji, michango na marejesho ya mikopo umekuwa si wa kuridhisha. Bodi ilikadiria kukopesha halmashauri **shilingi bilioni 2.1**. Hadi Februari, 2016 mikopo yenye thamani ya **shilingi milioni 330** imetolewa kwa halmashauri za wilaya za: Kishapu na Bukombe, na kufanya mikopo yote iliyotolewa tangu mwaka 1986 kufikia jumla ya **shilingi bilioni 9.02** sawa na asilimia 18.5 ya maombi yaliyowasilishwa ya jumla ya **shilingi bilioni 48.8**. Aidha, hadi Februari, 2016 jumla ya marejesho ya mikopo yalifikia **shilingi bilioni 5.01** sawa na **asilimia 55.5** ya **shilingi bilioni 9.02** zinazostahili kurejeshwa. Baadhi ya miradi iliyotekelezwa kwa mikopo toka Bodi hii ni kama inavyoonekana kwenye picha zifuatazo.



**MBINGA BUS TERMINAL – H/WILAYA YA MBINGA
- IMEKAMILIKA**



**JENGO LA UTAWALA– H/WILAYA YA LUSHOTO -
LIMEKAMILIKA**



**BENJAMIN MKAPA HOSTEL - MBEYA JIJI IPO
HATUA ZA KUKAMILIKA**



**SOKO LA KIUSA - MOSHI MANISPAA
LIMEKAMILIKA**

Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa (LAPF)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/15, Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa ulikusanya **shilingi bilioni 338.44** kutoka katika vyanzo mbalimbali kama michango ya wanachama na mapato yatokanayo na vitega uchumi vilivyokomaa. Makusanyo haya ni **asilimia 89** ya lengo la kukusanya jumla ya shilingi bilioni 381.22 yaliyokuwa yamewekwa kwa kipindi hicho. Mfuko uliandikisha wanachama **23,508** kati ya lengo la kuandikisha wanachama **24,471** ambayo ni asilimia 96 ya lengo kwa mwaka 2014/15. Vile vile kwa kipindi hicho Mfuko ulilipa mafao kwa wanachama jumla ya **shilingi bilioni 88.6** kati ya lengo la kulipa **shilingi bilioni 89.69** sawa na **asilimia 99**. Rasilimali za Mfuko ziliongezeka kutoka **shilingi bilioni 775.29** mwaka wa fedha 2013/14 mpaka **shilingi bilioni 961.38** mwaka wa fedha 2014/15 ambayo ni ongezeko la **asilimia 24**.

Mheshimiwa Spika, malengo ya Mfuko wa Pensheni wa LAPF katika mwaka wa fedha wa 2015/16 yalikuwa ni: kuwaandikisha wanachama wapya wapatao **24,471**, kukusanya michango toka kwa waajiri na wanachama kiasi cha shilingi bilioni 287.67; kuwekeza kiasi cha **shilingi bilioni 320.54** katika vitega uchumi mbalimbali; kukusanya mapato yatokanayo na uwekezaji kiasi cha **shilingi bilioni 66.46** na kulipa mafao kiasi cha **shilingi bilioni 110.3**.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Machi 2016, Mfuko umeweza kuandikisha wanachama wapya **14,828** sawa na **asilimia 81** ya lengo. Aidha, Mfuko umekusanya michango kiasi cha **shilingi bilioni 147.45** ambayo ni **asilimia 68** ya lengo kwa kipindi hicho. Vilevile, **shilingi bilioni 3.2** zimekwishalipwa na Serikali kama fidia kutoka mfuko wa akiba kuwa pensheni.

Mheshimiwa Spika, michango inayokusanywa inawekezwa na Mfuko ili kutunza thamani ya fedha na pia kuboresha mafao yanayolipwa. Hadi kufikia Machi 2016, LAPF ilikuwa imewekeza jumla ya **shilingi bilioni 151.62** katika vitegauchumi **sawa na asilimia 47.3** ya lengo. Mapato kutokana na shughuli za uwekezaji yalifikia shilingi **bilioni 48.51** sawa na **asilimia 99** ya lengo katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2015 hadi Machi 2016, Mfuko umelipa mafao yenye thamani ya **shilingi bilioni 84.17** sawa na **asilimia 99** ya lengo. Katika kipindi hichohicho, Mfuko ulianzisha fursa ya mikopo kwa wanachama iitwayo **“Maisha Popote Loans”**. Pamoja na mafanikio katika kuwalipa wanachama mafao bora, pia Mfuko unalipa mafao ndani ya muda wa wastani wa wiki mbili tangu mwanachama alipowasilisha madai yake ya kulipwa.

Tume ya Utumishi wa Walimu – TSC

Mheshimiwa Spika, Tume ya Utumishi wa Walimu ilikuwa Idara ya Utumishi wa Walimu chini ya Tume ya Utumishi wa Umma. Tume ya Utumishi wa Walimu imeanzishwa kwa Sheria Na. 25 ya mwaka 2015. Madhumuni ya kuanzishwa kwake ni kutoa huduma bora za kiutumishi kwa walimu wa shule za Msingi na Sekondari katika Utumishi wa Umma nchini.

Mheshimiwa Spika, chombo hiki, kipo chini ya OR TAMISEMI. Aidha, Tume itakuwa na Ofisi zake katika ngazi za makao makuu na wilaya 139. Ofisi hizo zitatumika kuhudumia walimu walio kwenye halmashauri zote nchini. Kwa sasa idadi ya walimu kwa wilaya ni kati ya 500 na 4,000. Watendaji waliokuwa wakifanya kazi kwenye Ofisi za TSD, wataendelea kutoa huduma kwenye wilaya hizo chini ya Tume hiyo. Aidha, watumishi waliokuwa kwenye ngazi za mikoa watahamishiwa kwenye wilaya zenye upungufu kwa kuwa ngazi ya mikoa hazitakuwepo. Kwa sasa idadi ya watumishi waliopo watakaoanzisha Tume ya Utumishi wa Walimu ni 519.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya kisheria ya Tume ni pamoja na:

- i. Kuendeleza na kusimamia utumishi wa Walimu;
- ii. Kumshauri Waziri mwenye dhamana juu ya kusimamia na kuendeleza utumishi wa walimu;
- iii. Kuajiri, kupandisha vyeo na kuchukua hatua za kinidhamu kwa walimu;
- iv. Kuhakikisha kunakuwa na uwiano sawa katika usambazaji wa walimu ndani ya Serikali za Mitaa na shule;

- v. Kushughulikia masuala ya rufaa zinazotokana na maamuzi ya mamlaka ya kinidhamu;
- vi. Kutunza daftari la kumbukumbu za walimu wote ambao wako katika utumishi wa walimu;
- vii. Kusimamia programu za mafunzo ya walimu kazini;
- viii. Kufanya utafiti na tathmini kuhusu masuala yanayohusu utumishi wa walimu na kumshauri Waziri mwenye dhamana;
- ix. Kutathmini hali ya walimu na kuishauri Wizara yenye dhamana ya masuala ya walimu juu ya mafunzo, idadi na uhitaji wa walimu nchini;
- x. Kuandaa kanuni za maadili ya utendaji kazi ya mwalimu;
- xi. Kuendeleza mfumo wa mawasiliano na Ofisi za Tume katika ngazi ya Wilaya juu ya mambo yote au jambo lolote linalohusiana na maendeleo ya utumishi wa walimu na kuhakikisha kwamba mwajiri na Ofisi ya Tume ngazi ya wilaya, wanatekeleza kazi zao kwa mujibu wa sheria, na
- xii. Kufanya jambo au kitendo chochote ambacho kwa maoni ya Waziri kinafaa au kinategemewa katika utekelezaji bora wa kazi zake.

Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART)

Mheshimiwa Spika, Awamu ya I ya utekelezaji wa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka katika Jiji la Dar es Salaam umegharimu Dola za Kimarekani **milioni 325.37**. Fedha hizi ni mchango wa Benki ya Dunia na Serikali ya Tanzania imetumia **shilingi bilioni 23.5** kwa ajili ya kugharamia ulipaji wa fidia kwa watu ambao mali zao ziliathiriwa kutokana na kupisha mradi. Sekta binafsi inatarajiwa kuchangia Dola za Kimarekani **milioni 100** kwa ajili ya kuwekeza kwenye ununuzi wa mabasi na kuanzisha mfumo wa kisasa wa ukusanyaji nauli.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa miundombinu umefikia kiwango cha **asilimia 95**. Miundombinu hiyo inajumuisha ujenzi wa barabara zenye urefu wa km 20.9 kutoka Kimara mwisho hadi Kivukoni na matawi mawili; barabara ya Kawawa kuanzia Morocco hadi Magomeni Mapipa na barabara ya Msimbazi hadi Kariakoo Gerezani. Aidha, viko vituo vidogo 27 vilivyojengwa katika barabara maalum za mfumo wa DART na vituo vikuu vitano (5) vya mabasi ambavyo ni Kimara, Ubungo, Morocco, Kivukoni na Kariakoo. Vilevile, vituo mlisho vinne (4) (Feeder Bus Stations) ambavyo ni Mwanamboka au Mwinyijuma, Shekilango, Magomeni Mapipa na Magomeni Kanisani; na karakana 2 za mabasi (Depots) eneo la Jangwani na Ubungo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na maandalizi ya kuanza kutoa huduma za mpito. Katika kipindi cha kuanzia Desemba 2015 hadi Machi 2016, Serikali imefanya maboresho ya mkataba ambapo mnamo tarehe 27 Februari 2016, DART na Mtoa Huduma za Mpito (UDA-RT) walitia saina nyongeza ya kwanza ya mkataba (Addendum No. 1 of the Interim Service Provider Contract). Lengo ni kuhakikisha mradi unatekelezwa kwa kuzingatia maslahi mapana ya Taifa. Serikali kupitia Wakala wa Serikali Mtandao (eGA), inafunga mfumo wa kisasa wa ukusanyaji wa nauli "Automated Fare Collection system –AFCs" na mfumo wa kusimamia uendeshaji wa mabasi "Intelligent Transport System –ITS". Vilevile, Wakala unatarajia kutoa elimu kwa Umma kuhusu matumizi ya mfumo wa DART kabla huduma haijaanza kutolewa. Sasa hivi kuna zoezi la kuendesha mabasi hayo kabla ya kuanza kutoa huduma rasmi.

Mheshimiwa Spika, maboresho mengine yaliyofanyika katika mkataba na mtoa huduma ni pamoja na kuongezwa kwa njia nyingine zilizokamilika kujengwa. Barabara hizo ni barabara ya Fire hadi Kariakoo na Magomeni hadi Morocco.

MPANGO NA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17

Mheshimiwa Spika, Mpango na bajeti ya OR- TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, imeandaliwa kwa kuzingatia maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2015, MKUKUTA, Malengo Endelevu ya Maendeleo 2016-2030. Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/2017 – 2020/2021, Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, dhana ya "Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa" na Mwongozo wa Kitaifa wa Mpango na Bajeti. Kutokana na maelekezo hayo, mipango ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, imejikita zaidi katika kukamilisha miradi inayoendelea kabla ya kuanzisha miradi mipya, kuimarisha utawala bora ikiwa ni pamoja na kusimamia ukusanyaji mapato kwa kutumia njia ya kielektroniki, kusimamia matumizi bora ya fedha na rasilimali zingine za umma na kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kazi zitakazofanyika katika mwaka wa fedha wa 2016/17 kwa upande wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa zitazingatia vipaumbele vichache vitakavyochangia ufanisi wa utekelezaji majukumu ya Ofisi kwa mwaka wa fedha 2016/17 ambavyo ni kama ifuatavyo:-

OR TAMISEMI

- i. Kusimamia utendaji kazi wa Serikali katika OR - TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuimarisha uwajibikaji na uadilifu wa watumishi wa umma;
- ii. Kusimamia utekelezaji wa Upelekaji wa Madaraka kwa Umma (D by D);
- iii. Kuimarisha na kusimamia ukusanyaji wa mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- iv. Kusimamia utekelezaji wa shughuli za uendeshaji wa Elimu na Afya pamoja na sekta zingine;
- v. Usimamizi wa Utawala Bora kwa kuandaa Sera, Maelekezo, Miongozo na Nyaraka mbalimbali;
- vi. Kuendeleza rasilimali watu kwa kuwaongezea ujuzi na vitendea kazi; na
- vii. Kusimamia, kuratibu na kuwezesha utekelezaji wa Taasisi, Programu na Miradi iliyo chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mikoa

Mheshimiwa Spika, katika ngazi ya mkoa, vipaumbele vyake vimewekwa katika maeneo machache yafuatayo:-

- i. Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya Mikoa na Wilaya mpya zilizoanzishwa;
- ii. Kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yao kwa kusimamia na kufuatilia shughuli mbalimbali za maendeleo;
- iii. Kuendelea na ukamilishaji wa miradi yote iliyokwishanza hususan ujenzi na ukarabati wa Ofisi na nyumba za Wakuu wa Mikoa, Wilaya na hospitali za Mikoa;
- iv. Kuendesha vikao vya kisheria na vya kazi kama vile Kamati za Ushauri za Mikoa na Wilaya (RCC, DCC na ICF);
- v. Kushughulikia masuala mtambuka kama vile maafa, UKIMWI na usimamizi wa usafi wa miji/majiji na athari za mabadiliko ya tabia nchi;
- vi. Kuzisimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa katika ukusanyaji na kudhibiti wa mapato; na
- vii. Kusimamia ulinzi na usalama ili wananchi waweze kutekeleza majukumu yao kwa amani na utulivu.

Mamlaka za Serikali za Mitaa

Mheshimiwa Spika, Sera, mipango na bajeti ya nchi kwa kiasi kikubwa inatekelezwa katika halmashauri. Vipaumbele vitakavyotekelezwa kwa mwaka wa fedha 2016/17 ni kama ifuatavyo:-

- i. Kuanzisha mifumo ya kielektroniki kwa ajili ya kusimamia na kudhibiti ukusanyaji wa mapato ya MSM, kufuatilia takwimu za utawala, menejimenti na utoaji wa huduma;
- ii. Kuandaa na kutekeleza mipango ya matumizi bora ya ardhi mijini na vijijini na kudhibiti migogoro ya ardhi;
- iii. Kukamilisha miradi ya maendeleo iliyokwishanza, ikiwemo ujenzi na ukarabati wa Ofisi za halmashauri na nyumba, katika Halmashauri mpya zilizoanzishwa;
- iv. Kuboresha na kuongeza mtandao wa barabara za vijijini;
- v. Kukamilisha ujenzi wa shule za sekondari ikiwa ni pamoja na ujenzi wa hosteli na maabara na kupanua baadhi ya shule kwa ajili ya kuongeza kidato cha tano na sita;
- vi. Upangaji, ufuatiliaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo inayohusiana na sekta mbalimbali katika maeneo yao;
- vii. Kusimamia utekelezaji wa Masuala mtambuka ikiwa ni pamoja na usafi wa mazingira mijini na vijijini, hifadhi ya vyanzo vya maji kudhibiti UKIMWI na rushwa; na
- viii. Kuhakikisha amani na utulivu unakuwepo ili majukumu ya kiuchumi na kijamii yaweze kutekelezwa bila bughudha ya aina yeyote.

Malengo ya Taasisi zilizoko chini ya OR-TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2016/17.

Shirika la Elimu Kibaha

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, Shirika linatarajia kutekeleza yafuatayo: -

- Kuendelea kutoa huduma za afya za kinga na tiba katika hospitali Teule ya Rufaa ya Mkoa wa Pwani ya Tumbi;
- Kuendelea kutoa elimu ya afya ya jamii, uuguzi na utabibu kwa wanafunzi 230 katika Chuo cha Sayansi na Tiba Shirikishi Kibaha;
- Kuendelea kutoa elimu na malezi bora kwa wanafunzi 1,712 wa shule ya msingi na 1,001 wa shule ya sekondari na;

- Kutumia ardhi ya Shirika (emptyland), kwa ajili ya uwekezaji ili kupata kipato cha kusaidia uendeshaji wa shirika;
- Kuendelea kutoa huduma za maktaba;
- Kuendelea kutoa huduma za maendeleo ya jamii ili kuwawezesha wananchi kuondokana na umaskini kwa kutoa mafunzo ya ufundi, ujasiriamali, kilimo na mifugo kupitia Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha;
- Kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa watumishi ikiwa ni pamoja na kulipa mishahara na stahiki zao kwa wakati na kuwapatia vitendea kazi;
- Kulipa madeni ya watumishi na wazabuni;
- Kujenga chumba cha kuhifadhia maiti katika ya hospitali ya Tumbi, na
- Kuendeleza ujenzi wa upanuzi wa Hospitali ya Tumbi.

Chuo Cha Serikali Za Mitaa Hombolo

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, Chuo kimepanga kudahili wanafunzi wapya 2,500 hatua hii itakiingizia Chuo shilingi **bilioni 2.7**, kufanya tafiti zisizopungua 2 kuhusu Mamlaka za Serikali za Mitaa, kununua vitabu nakala 500, kompyuta 25 na kuajiri watumishi wapya 107. Aidha, chuo kimepanga kutumia jumla ya **shilingi 4,450,825,000.00** kutokana na vyanzo vyake vya ndani kutekeleza majukumu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Chuo kinaendelea na mpango wa kufungua kampasi visiwani Zanzibar. Tawi hilo litatoa fursa ya mafunzo kuchangia jitihada za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika ugatuaji wa madaraka kwenda Mamlaka za Serikali za Mitaa na pia kuimarisha Muungano. Aidha, chuo kina mipango ya baadaye ya kufungua kampasi kanda ya ziwa-Jijini Mwanza.

Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2016/17, itaendelea na taratibu za kufanya marekebisho ya muundo wa Bodi na kufuatilia michango na marejesho ya mikopo kutoka kwenye halmashauri. Pia, itaendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kutoa mikopo kwenye halmashauri.

Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa (LAPF)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2016/17, Mfuko unalenga kuwaandikisha wanachama wapya **25,200**; kukusanya michango toka kwa waajiri na wanachama kiasi cha shilingi **bilioni 365.82**; kuwekeza kiasi cha **shilingi bilioni 453.53** katika vitega uchumi mbalimbali; kukusanya mapato yatokanayo na uwekezaji yapatayo **shilingi bilioni 100.45**; na kulipa mafao kiasi cha **shilingi bilioni 135.19**.

Mheshimiwa Spika, Mfuko pia, utaendelea kuimarisha ubora wa huduma kwa wanachama kwa kutumia mifumo ya TEHAMA; kusogeza huduma karibu na wanachama kwa kufungua ofisi mpya ya kanda mkoani Geita na kutumia mawakala kwa wilaya na mikoa ambayo haina ofisi za LAPF kwa sasa.

Tume ya Utumishi wa Walimu - TSC

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, Tume itasimamia masuala ya ajira na usajili, kuthibitisha kazini walimu, kupandisha vyeo walimu, na kuwabadilishia walimu kada. Tume pia itafanya kazi ya kukamilisha uundaji wa Tume, kuboresha mazingira ya kazi kwa kununua samani na vitendea kazi. Kazi nyingine zitakazofanyika ni kuboresha mfumo wa kutunza kumbukumbu na kuanzisha kanzidata kwa ajili ya walimu.

Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17 Wakala utatekeleza shughuli zifuatazo:-

- Usimamizi na uendeshaji wa huduma za Mpito (Interim Service Provision – ISP);
- Kukamilisha maandalizi ya kumpata mtoa huduma wa kudumu (Service Provider);
- Ujenzi wa uzio kuzunguka vituo vikuu 4 vya Kimara Mwisho, Ubungo, Kivukoni na Morocco ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya nauli;
- Kwa kushirikiana na SUMATRA, Wakala utaendelea kufuatilia suala la ukamilishaji wa viwango vya nauli katika kipindi cha mpito na kutolewa kwa leseni ya mabasi;
- Kuanza ujenzi wa kituo cha mawasiliano (Control Centre) na jengo la Ofisi ya Wakala katika kituo kikuu cha Mabasi Ubungo ili kusimamia na kudhibiti uendeshaji wa mfumo wa DART;

- Kuendelea kubuni na kuibua njia mbalimbali za kuongeza mapato kupitia maeneo ya uwekezaji ya mfumo wa DART ili kupanua wigo wa mapato;
- Kukamilisha masharti ya msingi ya upatikanaji wa fedha za mkopo wa ujenzi wa mfumo wa DART Awamu ya II barabara ya Kilwa – Mbagala rangi tatu km 19.3 kupitia Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB);
- Kuhakikisha uwepo wa ulinzi katika vituo 27 na vituo vikuu 5 vya mfumo wa DART katika Awamu ya I ili kuepuka uharibifu na wizi wa Miundombinu iliyojengwa kwa gharama kubwa;
- Kuhakikisha uwepo wa matengenezo ya miundombinu ya mfumo wa DART iliyokamilika kujengwa wakati wa uendeshaji wa mfumo, na
- Kuanza maandalizi ya awamu ya IV, V & VI. kwa kuhusisha barabara za Sam Nujoma na Bagamoyo hadi Tegeta km 16.1; Barabara ya Mandela na Barabara mpya km 22.8; na Mwai Kibaki, na barabara mbili mpya km 27.6.

Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka katika Jiji la Dar es salaam, utakuwa na jumla ya km 130 baada ya kukamilisha awamu zote sita.

MALENGO MAHSUSI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17

Ukusanyaji wa Mapato ya Halmashauri

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ya halmashauri kwa kuweka mkazo katika matumizi ya mifumo ya kielektroniki ambayo imeonesha mafanikio katika ukusanyaji wa mapato. Lengo ni kuziwezesha halmashauri kukusanya mapato ya kutosha na kujiendesha. Aidha, marekebishi ya sheria, kanuni na taratibu yataendelea kufanywa ili kuboresha ukusanyaji wa mapato bila kuleta kero kwa wananchi.

Mipango ya matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi yangu itaendelea kuzisimamia halmashauri zote ili ziandae mipango shirikishi ya matumizi ya ardhi vijijini kwenye maeneo yao. Aidha, itaendelea kusimamia uandaaji wa mipango hiyo na kufanya ufuatiliaji sambamba na kutoa ushauri wa kitaalam. Lengo ni kuondoa migogoro ya ardhi ili wananchi waishi kwa amani na kukuza uchumi wao. Vile vile, kwa miji inayochipukia, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaelekezwa kubaini chanzo cha kuibuka miji hiyo, fursa na mahitaji ya uwezo wake katika kutoa huduma kwa wakazi waliopo ili kuweka mipango madhubuti ya uendelezaji wa miji hiyo.

Utawala bora.

Mheshimiwa Spika, Ofisi yangu itaendelea kusimamia uzingatiaji wa misingi ya utawala bora katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa lengo la kuleta tija na nidhamu ya matumizi ya rasilimali na madaraka kwa manufaa ya Umma. Watumishi wote chini ya OR-TAMISEMI, Mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa wanatakiwa kufanya kazi kwa bidii, uaminifu, weledi na kutumia vizuri rasilimali za umma kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu.

Ufuatiliaji wa taarifa za fedha.

Mheshimiwa Spika, mapitio na ufuatiliaji wa taarifa mbalimbali za ukaguzi, ikiwemo taarifa za Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kaguzi maalum yatafanyika kwa lengo la kubainisha maeneo yenye viashiria vya ubadhirifu, wizi na matumizi mabaya ya fedha za umma.

Kurahisisha utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, Ofisi yangu itaendelea kuzihimiza halmashauri kuanzisha na kuimarisha utoaji wa huduma kwenye kituo kimoja (one stop center) mfano vibali vya ujenzi, hati za umiliki wa ardhi, leseni za biashara n.k. ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi kwa wakati pamoja na kuongeza mapato ya Serikali. Halmashauri zote nchini zinatakiwa kufanya marekebisho ya sheria ndogo za kodi, ushuru na ada mbalimbali ili ziendane na wakati na hali ya uchumi wa sasa. Serikali itaendelea kuimarisha mifumo ya utoaji taarifa za mapato na matumizi ya fedha zinazokusanywa kwa wadau na wananchi pamoja na kuimarisha udhhibiti wa matumizi ya fedha za Umma.

Barabara za Halmashauri

Mheshimiwa Spika, Serikali imetenga **shilingi bilioni 249,704,790,000.00** kupitia mfuko wa barabara kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya barabara na madaraja, kujengea uwezo wahandisi, usimamizi na ufuatiliaji kote nchini. Kupitia fedha za ufadhili wa EU, uboreshaji wa barabara utaendelea katika Halmashauri za Iringa, Mufindi, Songea na Mbinga ambapo kiasi cha shilingi **bilioni 39.352** zimetengwa. Aidha, Serikali itaendelea na utekelezaji wa Awamu ya III ya mradi wa uondoaji wa vikwazo vya upitikaji wa barabara za Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia Programu ya Uboreshaji wa Barabara za Vijijini ("Improving Rural Access in Tanzania-IRAT") inayofadhiliwa na "DFID", ambapo kiasi cha **shilingi 22,619,922,449.80** kimetengwa. Vile vile, barabara zenye urefu wa km. 304 katika halmashauri za Kilombero, Kiteto, Kongwa na

Mvomero zitaboreshwa kwa kiwango cha changarawe kwa gharama ya shilingi **bilioni 22.0** kwa ufadhili wa USAID.

Ukarabati wa shule kongwe za sekondari za Serikali

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Serikali imepanga kufanya ukarabati katika shule kongwe 11 za sekondari nchini ambapo kiasi cha **shilingi bilioni 12** zimetengwa. Shule hizo ni Ilboru, Tabora Boys, Tabora Girls, Mzumbe, Kilakala, Pugu, Nganza, Ihungo, Mwenge, Same na Msalato. Lengo la ukarabati ni kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia na hivyo kuinua kiwango cha elimu.

Huduma za Afya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, **shilingi 27,524,268,239.81**, zimetengwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo ya hospitali, vituo vya afya na zahanati, Jumla ya **shilingi 109,714, 225,000** zimetengwa kwa ajili ya kuboresha huduma za afya nchini. Kati ya hizo, **shilingi 3,460,225,000** ni kwa ajili ya Mikoa na **shilingi 106,254,000,000** ni kwa ajili ya halmashauri. Fedha hizi zitatumika kununua dawa, vifaa tiba na vitendanishi. Aidha, jumla ya shilingi **bilioni 3.577** zimetengwa kwa ajili ya tiba za Kifua Kikuu na UKIMWI katika Mikoa na halmashauri.

Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, Serikali imeweka lengo la kuandikisha kaya **1,638,915** kujiunga na CHF ambapo **shilingi 16,389,915,000** zinatarajiwa kuchangwa kama ada ya uanachama. Aidha Serikali kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya itaendelea kutoa fedha za Tele kwa Tele kulingana na michango ya wanachama. Vilevile, Serikali itaendelea kuhamasisha wananchi kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) ili kujihakikishia upatikanaji wa huduma za Afya wakati wote. Natoa wito kwa waheshimiwa wabunge na viongozi wote kuhamasisha wananchi kujiunga na mfuko huu.

Programu ya Maji

Mheshimiwa Spika; katika mwaka wa fedha 2016/17, OR-TAMISEMI itaendelea kuboresha uhifadhi na upatikanaji wa maji kwa kufanya yafuatayo: kutunza vyanzo vya maji kwa kuhifadhi mazingira yanayozunguka vyanzo hivyo; kuendelea kuunda Bodi za Maji katika miji midogo na miji ya Wilaya ili kusimamia usambazaji wa maji; kuendelea kuunda Kamati za Watumiaji Maji (Community Water Users Association-COWSOs) kwenye maeneo yasiyo na

kamati hizo ili kusimamia na kutunza vituo vya kuchotea maji kwenye maeneo yao na kuendeleza miundombinu ya maji na uhifadhi wa mazingira kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Maendeleo ya TEHAMA

Mheshimiwa Spika; katika mwaka wa fedha 2016/17, OR-TAMISEMI itaendelea kuboresha miundombinu na matumizi ya TEHAMA, kujenga uwezo wa watumishi wa Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika matumizi ya miundombinu na mifumo ya TEHAMA, ikiwemo matumizi ya "Video Conferencing Facilities" katika kuratibu na kuendesha vikao kwa haraka pasipo gharama kubwa.

Uendelezaji wa miji ya Kimkakati (Tanzania Strategic Cities Program)

Mheshimiwa Spika, mradi wa TSCP umetengewa jumla ya **shilingi 55,693,858,049.00**. Kati ya fedha hizo **shilingi 52,860,035,200.00** ni kwa ajili ya ukamilishaji wa miundombinu na usimamizi na shilingi **2,833,822,849.00** ni kwa ajili ya kutekeleza shughuli za uratibu, ufuatiliaji na kusaidia masuala ya kiufundi na kitaalam kwenye halmashauri pamoja na CDA. Ukamilishaji wa miundombinu hiyo utapunguza kero ya usafiri katika maeneo ya utekelezaji wa mradi huu na hivyo kupendzesha miji na kurahisisha shughuli za kiuchumi na kijamii.

Programu ya kuimarisha mamlaka za miji 18 (ULGSP).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Programu ya ULGSP imetengewa kiasi cha **shilingi 126, 767,237, 227.90** kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa katika Halmashauri husika. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **shilingi 116,296,382,227.90** ni kwa ajili ya kutekeleza shughuli za ukamilishaji wa miundombinu, ujengaji uwezo, usimamizi na ununuzi wa vifaa na mitambo na **shilingi 10,470,855,000.00** ni kwa ajili ya shughuli za kiufundi na kitaalam kwa halmashauri zinazotekeleza programu. Utekelezaji wa programu hii utaboresha mazingira ya uwekezaji na usafirishaji nchini.

Usimamizi wa Taasisi

OR - TAMISEMI itaendelea kusimamia na kuzipa mwelekeo wa utendaji kazi Taasisi zilizo chini yake ambazo ni, Chuo cha Serikali za Mitaa (Hombolo), Shirika la Elimu Kibaha, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, Tume ya Utumishi wa Walimu, Wakala wa Usafiri wa Haraka Dar es Salaam na Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa (LAPF). Lengo ni kuziwezesha Taasisi hizi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Michezo mashuleni

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/17, mashindano ya FEASSSA yanatarajiwa kufanyika Eldoret nchini Kenya kuanzia tarehe 25/08 hadi 03/09/2016. Mashindano ya UMISSETA na UMITASHUMTA yanatarajiwa kufanyika kuanzia tarehe 13/06/2016 hadi 24/06/2016 katika Chuo cha Ualimu Butimba Jijini Mwanza. Ni matarajio yangu kuwa mashindano haya yataibua vipaji vya vijana ambao Taifa linawahitaji katika kukuza na kuendeleza michezo.

SHUKURANI

Mheshimiwa Spika, natoa shukurani zangu za dhati kwa mashirika ya Kimataifa, taasisi za Kitaifa, Wizara za Kisekta, Mashirika ya Dini na Binafsi, Asasi za Kiraia, Vyuo Vikuu, Vyama vya Kitaaluma na Taasisi za Utafiti kwa mchango mkubwa wanaoutoa katika maendeleo ya nchi yetu. Ushirikiano wenu umetuwezesha kutekeleza majukumu yetu ya kutoa huduma kwa wananchi kwa ufanisi. Ni imani yangu kuwa tutaendelea kushirikiana vizuri katika kuhudumia wananchi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru msaidizi wangu Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo (Mb) Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa ushirikiano anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya Uwaziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI. Aidha, naomba kumshukuru Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mhandisi Alhaj Musa Ibrahim Iyombe, Naibu Makatibu Wakuu Dkt. Deo Michael Mtasiwa **-Afya** na Bernard Mtandi Makali **-Elimu**. Vilevile, nawashukuru Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri, Mameya na Wenyeviti wa Halmashauri kwa ushirikiano wanaonipa na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, vilevile nachukua fursa hii kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika ngazi zote. Wote kwa pamoja nawashukuru kwa ushirikiano wao uliwezesha kutoa huduma kwa wananchi katika ngazi zote. Nawatakia kila la kheri tuendelee kutimiza wajibu wetu pale tulipo.

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru wananchi wa Kibakwe kwa kunichagua tena kuendelea kuwa Mbunge wao ili niendelee kuwaongoza, pia kwa uvumilivu waliouonyesha nilipokuwa mbali nao katika kutekeleza majukumu mengine ya Kitaifa. Kwa imani mlionionesha, nawahidi nitawatumikia kwa nguvu zote. Kwa namna ya pekee kabisa, naishukuru familia yangu, mke wangu Mariana na wanangu, kwa kunipa moyo na uvumilivu wao

wakati wa kutekeleza majukumu yangu ya Kitaifa. Mwenyezi Mungu awabariki sana.

Maombi ya fedha kwa kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka wa fedha 2016/17

Maduhuli na Makusanyo

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/17 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Taasisi zilizo chini yake, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaomba idhini ya kukusanya jumla ya **shilingi 677,519,562,000.00**. Makusanyo haya yatatokana na mauzo ya vifaa chakavu na nyaraka za zabuni, faini mbalimbali, marejesho ya masurufu na marejesho ya mishahara. Kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, makusanyo yatatokana na kodi na ushuru mbalimbali unaotozwa na Mamlaka hizo kutokana na vyanzo vya mapato vilivyokubaliwa. Mchanganuo wa makusanyo hayo ni kama ifuatavyo:-

Ofisi/Taasisi	Makadirio
OR-TAMISEMI	13,503,000
Taasisi	11,761,119,000
Mikoa	330,112,000
Mamlaka za Serikali za Mitaa	665,414,828,000
JUMLA	677,519,562,000

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/17, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaombewa jumla ya **Shilingi 6,023,559,414,000.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 3,775,875,780,000.00** ni Mishahara, ni **shilingi 646,143,492,000** ni Matumizi Mengineyo na **shilingi 1,601,540,142,000.00** ni kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo.

MAOMBI YA FEDHA

Mheshimiwa Spika, sasa naomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha makadirio ya matumizi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2016/17, jumla ya shilingi **Trilioni Sita, Bilioni Ishirini na Tatu, Milioni Mia Tano Hamsini na Tisa na Mia Nne na Kumi na Nne Efu (shilingi 6,023,559,414,000.00)** kwa ajili ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mikoa na Halmashauri kwa mchanganuo ufuatao:-

AINA YA MATUMIZI	2016/17
Matumizi ya Kawaida	
OR – TAMISEMI	
Mishahara Makao Makuu	8,130,978,000
Mishahara ya Taasisi	14,385,939,000
Matumizi Mengineyo Makao Makuu	3,835,054,000
Matumizi Mengineyo Taasisi	2,561,303,000
JUMLA	28,913,274,000
Tume ya Utumishi wa Walimu	
Mishahara	6,442,019,000
Matumizi Mengineyo	3,605,773,000
Jumla	10,047,792,000
Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa	
Mikoa:	
Mishahara	153,036,181,000
Matumizi Mengineyo	37,786,227,000
Jumla	190,822,408,000
Mamlaka za Serikali za Mitaa	
Mishahara	3,593,880,663,000
Matumizi Mengineyo	598,355,135,000
JUMLA	4,192,235,798,000
Mpango wa maendeleo	
OR-TAMISEMI	325,469,218,000
Mikoa	64,701,480,000
Mamlaka za Serikali za Mitaa	1,211,369,444,000
JUMLA	1,601,540,142,000
JUMLA KUU	6,023,559,414,000

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba hii, yapo majedwali ambayo yanafafanua kwa kina makadirio ya matumizi ya fedha ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI na taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii pia inapatikana kwenye tovuti ya OR TAMISEMI ambayo ni www.tamisemi.go.tz

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Hoja imetolewa na imeungwa mkono na Wabunge wengi tu. Tunaendelea, ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Waheshimiwa Wabunge, kama mlivyoona asubuhi tulipoanza, ziliwasilishwa hati mbili; hati ya kwanza ilihusu hoja hii ambayo Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI amewasilisha, ameitoa na imeungwa mkono. Hati ya pili ilihusu Ofisi hiyo hiyo ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Kwa hiyo, anayefuata sasa atakuwa ni Waziri mwenye dhamana hiyo ya Utumishi na Utawala bora.

Hoja hizi zinawasilishwa moja baada ya nyingine kwa sababu zinashabihiana. Shughuli za TAMISEMI zinaguza wananchi wetu, sehemu kubwa ya watumishi wa Serikali wapo TAMISEMI na Serikali za Mitaa lakini pia na Serikali Kuu. Suala la utawala bora ni la nchi nzima katika taasisi zote na Wizara za Serikali, lakini na viongozi wote.

Kwa hiyo, ndiyo maana zinakuja katika sura hiyo. Zitawasilishwa moja baada ya nyingine na itatolewa hoja; na Wenyeviti watatoa taarifa kwa mtiririko huo huo na pia Kambi ya Upinzani Bungeni. Baada ya hapo, mtazijadili hoja hizi kwa pamoja. Tutahitimisha mjadala huo ndani ya siku tatu. Baada ya hapo sasa hoja zitatolewa kwa utaratibu wa kawaida halafu tutaingia kwenye Kamati ya Matumizi.

Tunaendelea na Waziri wa Utumishi na Utawala Bora. *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI NA UTAWALA BORA (MHE. ANGELLAH JASMINE KAIRUKI): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Utawala na Serikali za Mitaa iliyochambua Bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Taasisi zake na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu sasa naomba lipokee na kujadili mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Mpango wa Utekelezaji na Makadirio ya fedha kwa Ofisi ya Rais, Menejiment ya Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa kuniamini na kuiteua kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala bora. Ninaahidi kwamba nitatekeleza wajibu wangu kwa ufanisi na uadilifu mkubwa. Napenda pia kuwashukuru Wajumbe wa UWT Mkoa wa Dar es Salaam, Baraza kuu la UWT Taifa, na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUKTA) kwa ujumla wao kwa kuendelea kuniamini kuwawakilisha wafanyakazi kwa awamu nyingine tena katika Bunge hili Tukufu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kipekee kuishukuru familia yangu kupitia kwa mume wangu, watoto wangu na ndugu zangu wote kwa kuendelea kunipa ushirikano wa dhati na kwa kuwa wavumilivu ninapotekeleza majukumu yangu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Mbunge wa Jimbo la Bukoba Vijijini kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mikoa. Napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe, Mbunge wa Jimbo la Kavuu kwa kuchaguliwa kwake kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo mpya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwapongeza Waheshimiwa Wenyeviti wote na Makamu Wenyeviti na Wajumbe walioteuliwa katika Kamati mbalimbali ili kulitumikia Bunge la Kumi na Moja la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri ambao waliutoa wakati tulipokuwa tukipitia taarifa ya utekelezaji wa

Mipango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016 na mapendekezo ya Mpango wa Utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka wa fedha 2016/2017. Maoni na ushauri wa Kamati umetuwezesha na utaendelea kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, napenda kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Magufuli kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa uongozi wake mahiri wenye kuzingatia uadilifu, uwajibikaji na utendaji unaozingatia matokeo. Hii inathibitisha kiu kubwa aliyonayo ya kuwaletea maendeleo wananchi na kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa ni mwanamke wa kwanza kushika wadhifa huu mzito kwetu katika historia ya nchi hii. Vilevile napenda kumpongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais, kwa namna ambavyo anamsaidia Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa majukumu ili kuleta mabadiliko ya kweli na maendeleo kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa kuwa Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ya Zanzibar kwa kipindi cha pili. Vilevile napenda kumpongeza Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, kwa kuteuliwa kwake kushika wadhifa wa Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na napenda kumpongeza kwa namna ambavyo anatekeleza madaraka yake ya Kikatiba kwa umakini, umahiri na kwa uadilifu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Spika na Naibu Spika, kwa namna ambavyo wanaliongoza Bunge letu Tukufu kwa busara na hekima. Naomba pia kuwapongeza Mheshimiwa Mawaziri wote wa Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kumsaidia katika kuwaletea Watanzania maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Balozi Kijazi, Katibu Mkuu Kiongozi; Bwana Ilomo, Katibu Ofisi ya Rais - Ikulu; Dkt. Ndumbaro - Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Bi Suzane Mlawi, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Makamishina,

Watendaji Wakuu wa Tume na Taasisi, Wakurugenzi na watumishi wote kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kutekeleza majukumu yanayoweza ofisi kufikia malengo ikiwa ni pamoja na kukamilisha hotuba hii kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulithibitisha Bunge lako Tukufu kwamba Ofisi ya Rais, Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaendelea kutekeleza maelekezo yaliyotolewa katika hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wakati alipokuwa akifungua Bunge la Kumi na Moja yaliyohusu kuondoa urasimu katika uendeshaji wa shughuli za Serikali, kubana matumizi na kurejesha nidhamu katika utumishi wa umma na imani ya wananchi kwa Serikali yao kwa kusimamia sheria, kanuni, miongozo na taratibu za uwajibikaji wa viongozi na watumishi wa umma ili wawajibike wa wananchi ambao ndio wateja na waajiri wakuu wa watumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais, katika vita dhidi ya rushwa, ubadhirifu, ufisadi, uzembe, ukiukwaji wa maadili, uvivu, urasimu, pamoja na watumishi hewa. Tunaunga mkono pia vita dhidi ya wanaodhihirika kujihusisha na vitendo hivyo. Hatua ambazo Mheshimiwa Rais anazichukua zinatakiwa kuungwa mkono na Bunge lako Tukufu pamoja na wale wote wanaoitakia mema nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Mheshimiwa Rais ya kuwa na Serikali inayohudumia wananchi wake, itatimia kwa Watumishi wa Umma wote kufanya kazi kwa juhudi, maarifa na uadilifu mkubwa, lakini vile vile kutoa huduma bora kwa haraka na kwa staha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016 ulizingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, 2011 - 2016, Mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umasikini Tanzania pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010/2015. Shughuli zilizotekelezwa na kila taasisi ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Ofisi ya Rais Ikulu na Taasisi zake, katika mwaka wa fedha wa 2015/2016 waliidhinishiwa shilingi 20,575,672,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Machi, 2016 shilingi 13,657,114,667/= zilipokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, katika mwaka wa fedha wa 2015/2016 linalojumuisha Taasisi zilizo chini ya Ikulu, waliidhinishiwa shilingi 445,832,281,000/= na kati ya fedha hizo shilingi 310,329,016,000/=, zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya

kawaida na shilingi 135,503,265,000/= zilikuwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2016, shilingi 400,732,563,366,000/= zilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo, shilingi 292,403,739,579/= zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 109,328,823,817/= ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais - Ikulu imeendelea kuongoza kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali. Katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016, ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma kwa Mheshimiwa Rais na familia yake ziliendelea kutolewa, huduma za ushauri kwa Mheshimiwa Rais zilitolewa, jumla ya mikutano 44 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu na Baraza la Mawaziri ilifanyika ambapo nyaraka 47 zilichambuliwa na kati ya hizo nyaraka 30 zilitolewa ushauri na 17 zilitolewa uamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mikutano ya kazi ya Makatibu Wakuu pia ilifanyika kama ilivyopangwa. Rufaa 71 za watumishi wa umma na Mamlaka za Nidhamu zilichambuliwa na kuwasilishwa kwa uamuzi na vilevile rufaa 51 zilitolewa uamuzi na wahusika walijulishwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAKUKURU inalo jukumu la kuelimisha umma kuhusu athari za rushwa, kuchunguza tuhuma za makosa ya rushwa, kuwafikisha watuhumiwa mbele ya vyombo vya sheria na kuishauri Serikali kuhusu namna bora ya kuziba mianya ya rushwa. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016, jumla ya tuhuma 3,986 zilichunguzwa ambapo uchunguzi wa tuhuma 439 ulikamilika na majalada 277 yaliwasilishwa kwa Mkurugenzi wa Mashitaka kwa ajili ya kuomba kibali.

Vilevile jumla ya kesi 927 ziliendeshwa na kati ya kesi hizo, kesi 320 zilitolewa maamuzi Mahakamani ambapo kesi 142 washitakiwa walifungwa baada ya kupatikana na hatia, kesi 178 washitakiwa waliachiwa huru, kesi 29 ziliondolewa Mahakamani kwa sababu mbalimbali zikiwemo washtakiwa kufariki na kukosekana kwa mashahidi. Vilevile kesi 578 zinaendelea kusikilizwa Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAKUKURU pia iliweza kuokoa shilingi 9,505,000,000/= kutokana na *operation* mbalimbali wanazozifanya. Kwa upande wa MKURABITA, kwa kushirikiana na TAMISEMI, utekelezaji wa uboreshaji wa mbinu za kupanga, kutekeleza, kuratibu na kufuatilia shughuli za urasimishwaji nchini umeanza. Kwa kushirikiana vile vile na Wizara za Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na ile ya Biashara, Viwanda na Masoko za Zanzibar,

urasimishaji wa ardhi vijijini, umefikia hatua ya usajili kwa ajili ya viwanja 5,227 vilivyopimwa katika Shehia ya Kiungoni, Nungwi, Chokocho na Chwaka. Vilevile urasimishaji wa biashara umefanyika kwa kutoa mafunzo kwa wafanyabiashara 2,100 katika Wilaya mbili Unguja na Wilaya mbili Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) unatekeleza mpango wa kunusuru kaya maskini, wenye lengo la kuongeza kipato, fursa na uwezo wa kugharamia mahitaji maalum. Katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016, ilitekeleza shughuli zifuatazo; kwanza, jumla ya kaya maskini milioni 1.3 zilitambuliwa na kati ya kaya hizo kaya maskini milioni 1.1 zenye jumla ya watu milioni tano, ziliandikishwa. Aidha, jumla ya shilingi bilioni 275.9 zilihawilishwa kama ruzuku kwa kaya maskini milioni 1.1 zilizoko Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Mpango wa kutoa ajira za muda, umeandaa miradi 1,880 katika mamlaka za Serikali za Mitaa 40 na Wilaya zote za Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Uongozi ilianzishwa kwa lengo la kuwa kituo cha utaalum, kwa ajili ya kuendeleza viongozi Barani Afrika, kwa kuanzia na Tanzania, Ukanda wa Afrika Mashariki na hatimaye Afrika kwa ujumla. Katika mwaka huu unaomalizika wa fedha ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, iliandaa mikutano mitatu ya majadiliano ya kikanda na Kimataifa, iliandaa Mkutano mmoja wa faragha wa Watendaji Wakuu Serikalini na kuendesha kozi 15 za muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mfuko wa Rais wa kujitegemea, ambapo majukumu yake ni pamoja na kutoa huduma za mikopo kwa wajasiriamali, ushauri na mafunzo ya kibiashara ili kuongeza ufanisi katika biashara zao, ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, PTF iliweza kutoa mikopo, yenye thamani ya shilingi 336,900,000/= ambayo ilitolewa kwa wahitimu wa Vyuvo vya Ufundi Stadi, lakini vilevile shilingi 202,862,688/= zilizokopeshwa zilirejeshwa na walengwa wa mfuko 1,547 walipata mafunzo ya ujasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilitengewa shilingi 6,227,803,160/= na kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 4.7 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, shilingi bilioni 1.4 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2016 shilingi bilioni 3.6 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida zilipokelewa na kutumika. Kwa upande wa miradi ya maendeleo, shilingi milioni 867.1 zilipokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016, Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Maadili Viongozi wa Umma ilipokea malalamiko 114 ya ukiukwaji wa maadili ambayo yalichambuliwa na kushughulikiwa ipasavyo. Vilevile viongozi wa umma 15,624 walitumiwa fomu za tamko la rasilimali na madeni, kwa kipindi kilichoishia tarehe 31/12/2015. Aidha, viongozi wa umma 14,543 walirejesha fomu.

Vilevile mafunzo kwa wenza wa Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Majaji na Wakuu wa Polisi, walipatiwa mafunzo kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, mgongano wa maslahi, uhusiano katika ndoa, pamoja na maadili na umiliki wa mali. Vilevile hati ya ahadi ya uadilifu kwa viongozi wa umma, watumishi wa umma pamoja na sekta binafsi ziliandaliwa. Jumla ya viongozi wa umma 13,189 kati ya viongozi wa umma 15,624 walisaini Hati ya Ahadi ya Uadilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilianzisha mfumo wa kusimamia, kushauri na kutathmini utekelezaji wa miradi ya kipaumbele ya Kitaifa ili kuharakisha kufikiwa kwa Dira ya maendeleo ya Taifa. Katika mwaka wa fedha wa 2015/2016 Bunge liliidhinisha shilingi 17,881,312,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizi shilingi bilioni 3.6 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 14.2 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2016 shilingi bilioni 1.4 za matumizi ya kawaida zilipokelewa na kutumika. Kwa upande wa miradi ya maendeleo, shilingi bilioni tano zilipokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2015 hadi Machi 2016, miradi ya maji ilibuniwa kulingana na vigezo vya mpango wa tekeleza kwa matokeo makubwa sasa, Mikoa 16 ilifanyiwa mapitio, vyanzo vya maji 4,592 vilichaguliwa; kati yake vyanzo 4,294 vilithibitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi Umma pamoja na Wakala zake iliidhinishwa shilingi 43,977,564,000/= kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa mwaka. Kati ya fedha hizo shilingi 37,717,620,000/= zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 6.2 zilikuwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2016 shilingi 25,147,830,333.80 zilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 23.4 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 1.7 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na Wakala zake, imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya

kuhakikisha utumishi wa umma unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora. Maslahi ya watumishi wa umma yaliboreshwa katika mwaka huu wa fedha, ambapo kima cha chini cha mshahara kiliongezwa kwa asilimia 13.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kodi ya mapato katika mishahara ya kima cha chini, ilipunguzwa kutoka asilimia 12 hadi asilimia 11. Mikutano miwili ya Baraza la Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma ilifanyika kwa ajili ya kupitia miundo ya maendeleo ya utumishi. Aidha, miundo na mgawanyo wa majukumu ya Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala wa Serikali sita ilihuishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Tume ya Utumishi wa Walimu ilianzishwa na muundo wake uliidhinishwa mwezi Novemba, 2015. Aidha, Idara ya Mikataba ya Utendaji Kazi Serikalini, kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa mikataba ya utendaji kazi katika taasisi za umma ilianzishwa. Vilevile maandalizi ya ajira za watumishi wapya 71,496 kwa mwaka wa fedha 2015/2016 yanaendelea na kipaumbele kilikuwa ni katika sekta za elimu, afya, kilimo, pamoja na mifugo. Aidha, upandishwaji vyeo nao pia unaendelea kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mafunzo ya maadili ya utendaji kazi katika Utumishi wa Umma yaliendeshwa kwa watumishi 1,396 kutoka katika taasisi 34.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania kilianzishwa ili kutoa mafunzo katika nyanja za Uongozi, Menejimenti na Utawala kwa ngazi za Cheti, Stashahada na Astashahada. Katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016, mafunzo mbalimbali ya muda mfupi na mrefu, pamoja na mitihani ya utumishi wa umma yaliendeshwa, mafunzo ya muda mrefu kwa washiriki 17,192 yalitolewa katika fani mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao Tanzania inalo jukumu la kuwajengea uwezo Watumishi wa Umma kwa kuratibu na kuendesha mafunzo na midahalo kwa kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano ili kuendana na mabadiliko ya utoaji wa huduma kwa wananchi.

Katika mwaka huu wa fedha unaomalizika, iliandaa mikutano tisa ya kazi baina ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Taasisi mbalimbali ngazi ya Taifa pamoja na Sekretarieti za Mikoa yote Tanzania Bara. Vilevile iliweza kufanikisha mikutano 36 ya mafunzo na mijadala ndani na nje ya nchi kwa kutumia mtandao wa Wakala.

Wakala wa Serikali Mtandao inalo jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa jitihada za utoaji wa huduma kwa kutumia TEHAMA katika taasisi za umma ili kuleta ufanisi, kuongeza uwajibikaji na kuboresha utoaji wa huduma. Katika mwaka huu wa fedha, taasisi za umma 72 ziliunganishwa kwenye mfumo wa mawasiliano salama Serikalini. Aidha, taasisi za Serikali 67, ziliunganishwa katika mfumo wa pamoja na salama wa barua pepe wa Serikali na hivyo kupelekea mfumo kufikia taasisi 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, iliidhinishwa shilingi bilioni 3.8 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Machi 2016, shilingi bilioni 1.7 zilipokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha, shughuli zifuatazo zilitekelezwa; kwanza, usaili kwa ajili ya kujaza nafasi za wazi, za kazi 4,310 katika Utumishi wa Umma uliendeshwa, ambapo wasailiwa 3,509 kutoka katika Wizara, Sekretarieti za Mikoa zilikuwa nafasi 281, Mamlaka za Serikali za Mitaa zilikuwa nafasi 1,928 na Taasisi, Idara na Wakala za Serikali nafasi 608, walipangiwa vituo vya kazi. Kati ya wasailiwa 3,509 waliopangiwa vituo vya kazi, utaratibu wa kujaza nafasi 801 upo katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Utumishi wa Umma ni Mamlaka ya Rufaa kwa baadhi ya Watumishi wa Umma, dhidi ya maamuzi yanayotolewa na mamlaka zao za nidhamu na kuhakikisha kwamba masuala ya rasilimali watu yanaendeshwa kwa kuzingatia sheria, kanuni, miongozo na taratibu. Katika mwaka huu wa fedha, Tume iliidhinishwa shilingi bilioni 11.6 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi, 2016 shilingi bilioni 7.1 zilipokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016, shughuli zifuatazo zilitekelezwa na Tume ya Utumishi wa Umma. Rufaa 159 zilifanyiwa uchambuzi na kutolewa uamuzi ambapo rufaa 58 zilikubaliwa. Rufaa 59 zilikataliwa, 38 zilikatwa nje ya muda na nne ziliahirishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malalamiko 95 ya watumishi yalichambuliwa na kutolewa uamuzi na maelekezo. Masuala ya ajira ya walimu yalishughulikiwa ambapo walimu 542 walisajiliwa. Walimu 4,647 walipandishwa vyeo, walimu 947 walibadilishiwa kazi na vibali vya kustaafu kwa walimu 463 vilitolewa. Aidha, mashauri ya nidhamu ya walimu 120 yalitolewa uamuzi, ambapo walimu 89 walifukuzwa kazi, wanne walirudishwa kazini, mashauri mawili yalifutwa na mashauri 25 yalirudishwa kwenye Kamati za Ajira za Walimu za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma, yenye jukumu la kufanya mapitio ya mara kwa mara ya mishahara na kupendekeza viwango vya mishahara, posho na mafao katika utumishi wa umma kwa mamlaka husika. Katika mwaka huu wa fedha Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma, iliidhiniwa shilingi 2,313,146,450/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kukikia Machi, 2016 shilingi 1,443,871,555/= zilipokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 shughuli zifuatazo zilitekelezwa na Bodi ya Mishahara. Tathmini ya kazi na uhuishaji wa madaraja au *job evaluation* na *re-grading* kwa watumishi wa umma, ilianza na tunatarajia itakamilika mwezi Februari, 2017. Aidha, rasimu za vigezo vya kutoa motisha kwa watumishi wa umma, wanaofanya kazi katika maeneo yenye mazingira magumu imeandaliwa. Vilevile rasimu ya mwongozo wa kupendekeza na kupanga mishahara na maslahi, imekamilika katika utumishi wa umma na iko katika hatua za maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa ina jukumu la kusimamia na kuratibu utekelezaji wa sera, sheria, kanuni na taratibu za utunzaji kumbukumbu na nyaraka katika taasisi za umma. Vilevile inakusanya, inatunza na kuhifadhi kumbukumbu na vitu vya Waasisi wa Taifa letu.

Katika mwaka wa fedha wa 2015/2016 Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, iliidhiniwa shilingi bilioni 1.3 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,061,261,000/= zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na shilingi milioni 250 zilikuwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2016 shilingi 459,007,823/= zilipokelewa na kutumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Vilevile katika mwaka huu wa fedha, kumbukumbu tuli kutoka katika taasisi tano za Serikali, makasha 1,400 kutoka Makao Makuu ya Idara yalihamishiwa katika Kituo cha Taifa cha Kumbukumbu kilichoko hapa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kutoa mapendekezo ya mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha wa 2016 na 2017. Katika mwaka wa fedha wa 2016 na 2017 Ofisi ya Rais, Ikulu imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Ofisi ya Rais, Ikulu imepanga kutoa huduma kwa Rais na familia yake;
- (ii) Kutoa huduma za ushauri kwa Rais katika maeneo mbalimbali;

(iii) Imepokea, kupitia na kuchambua rufaa na malalamiko ya Watumishi wa Umma na Wananchi; na

(iv) Vilevile itakamilisha ujenzi wa ukumbi wa mikutano na kuanza ujenzi wa jengo jipya la mapokezi Ikulu na kukarabati nyumba kumi za watumishi Chamwino na majengo ya Ikulu Ndogo ya Mwanza na Lushoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa TAKUKURU katika mwaka ujao wa fedha imepanga kuchunguza tuhuma 3,406 za rushwa zilizopo na mpya zitakazojitokeza. Imepanga vilevile kuendesha kesi 578 zilizopo Mahakamani na ambazo zitaendelea kufunguliwa kutokana na kukamilika kwa uchunguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa MKURABITA imepanga kujenga uwezo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa, kuhusu urasimishaji wa ardhi vijijini katika Halmashauri za Wilaya sita. Vile vile urasimishaji wa ardhi vijijini utafanyika Zanzibar ambapo Hati za Hakimiliki za kimila 17,800 zitaandaliwa na kutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa TASAF itafanya utambuzi na uandikishaji wa kaya maskini katika maeneo ambayo hayakufikiwa katika awamu ya kwanza. Itahaulisha ruzuku kwa kaya maskini zipatazo milioni 1.4 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zote Tanzania Bara na Wilaya zote za Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Taasisi ya Uongozi watatoa mafunzo ya muda mfupi na muda wa kati kwa Viongozi ili kuwajengea uwezo katika maeneo ya uamuzi, usimamizi, maendeleo endelevu na majadiliano ya mikataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mfuko wa Rais wa Kujitegemea itaendelea kutoa mikopo na kukusanya marejesho ya mikopo kutoka kwa walengwa katika Mikoa mitano. Vile vile, itaanzisha Tawi la Kutoa Huduma za Mfuko katika Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza mpango wa fedha wa mwaka 2016/2017, Ofisi ya Rais, Ikulu inaomba sh. 14,962,054,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Aidha, Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri inaomba sh. 793,164,600,000 na kati ya fedha hizi sh. 362,715,571,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na sh. 430,449,029,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, watachapisha, watatuma na kupokea tamko la Viongozi wa Umma kuhusu rasilimali na madeni inayopaswa kutolewa kwa mujibu wa

Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya Mwaka 1995. Vile vile, itafanya uhakiki wa matamko ya rasilimali na madeni kwa Viongozi wa Umma 500 na kuandaa taarifa ya mwaka ya utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu yake ya mwaka wa fedha wa 2016/2017, Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma inaomba kuidhinishiwa sh. 5,913,820,000 na kati ya fedha hizi sh. 4,913,820,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo inaomba kuidhinishiwa sh. 1,000,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Ofisi ya Rais Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi, itaendelea kusimamia utekelezaji wa vituo 53,182 vya maji vitokanavyo na miradi mipya ya vyanzo vya maji. Itafuatilia ujenzi wa skimu 40 za umwagiliaji, ukamilishaji wa maghala 207 ya kuhifadhi mazao na utekelezaji wa mpango wa mashamba makubwa 25 ya kilimo cha biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais Ushauri wa Mafuta na Gesi imeanzishwa ili kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu uchumi wa mafuta na gesi kwa Baraza la Mawaziri. Katika mwaka ujao wa fedha itatoa ushauri wa kitaalam kwa Baraza la Mawaziri kuhusu uchumi wa mafuta na gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza mpango wa mwaka wa fedha 2016/2017, Ofisi ya Rais ya Ushauri wa Mafuta na Gesi inaomba kuidhinishiwa sh. 1,036,239,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2016/2017, Ofisi ya Rais Menejment ya Utumishi wa Umma na Wakala zilizo chini yake, imepanga kujenga uwezo wa ndani wa Serikali katika kuratibu sera na kuanza maandalizi ya kutungwa kwa sheria ya mishahara na maslahi katika utumishi wa umma. Vilev ile, imepanga kuhuisha miundo na mgawanyo wa majukumu ya taasisi za Serikali kulingana na mahitaji ya Serikali ya Awamu ya Tano.

Pia itaboresha michakato ya utoaji huduma na kuimarisha usimamizi wa mifumo na viwango vya utendaji kazi kwa kufupisha utaratibu wa utoaji huduma kwa umma. Vile vile itaanza maandalizi ya kutunga sera ya Serikali Mtandao na mkakati wake wa utekelezaji na kutumia muundo wa kitaasisi wa utekelezaji wa TEHAMA Serikalini. Itaendelea kufanya vikao vya kazi na Sekretarieti za Mikoa yote na mamlaka za Serikali za Mitaa kwa njia ya video. Itasimamia ajira na upandishwaji vyeo kwa Watumishi wa Umma kwa mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tutaendelea kusimamia na kudhibiti mishahara hewa katika Utumishi wa Umma kupitia mfumo wa taarifa za kiutumishi na mishahara, na kuwachukulia hatua wote watakaohusika kuhujumu mfumo huu. Napenda kutoa angalizo kwa wale wote watakaokuwa wameshiriki katika kuwezesha watumishi hewa kupata fedha zisizo haki yao, tutachukua hatua za kijinai. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Wakala ya Serikali ya Mtandao tutamalizia ujenzi wa vituo viwili vya kuhifadhi taarifa na mifumo ya TEHAMA ya Serikali na kujikinga na majanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha niseme kwamba, uchumi imara na endelevu katika nchi yoyote, unahitaji uwepo wa Utumishi wa Umma uliotukuka, unaozingatia utawala bora, maadili na mifumo thabiti ya usimamizi wa utekelezaji. Ofisi ya Rais Ikulu na taasisi zake pamoja na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, zitahakikisha kwamba majukumu hayo muhimu yanatekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango na bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 ya Mafungu niliyoyataja imezingatia dhamana hiyo ambayo imebeba vizuri kabisa dhamira ya Serikali ya kuleta mabadiliko makubwa katika Utumishi wa Umma, kwa kuimarisha uwajibikaji na uadilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa dhamira hiyo utasaidia kuujenga Utumishi wa Umma uliotukuka kwa kuondokana na matumizi mabaya ya madaraka, kuondoa ukiukwaji wa maadili ya uongozi na Utumishi wa Umma, kuondokana na ucheleweshwaji wa maamuzi, kutokusimamia kwa uwazi na kutokuwajibika kwa Viongozi na Watumishi wa Umma katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, imelenga kuwa na utumishi wa umma unaotoa huduma bora kwa staha na kwa haraka kwa kuzingatia sheria, kanuni, miongozo na taratibu. Vile vile kwa kutumia mifumo ya elektroniki katika kuboresha utoaji wa huduma hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, imelenga kujenga Utumishi wa Umma ambao ni mwepesi kusikiliza malalamiko ya wananchi na kuyatafutia ufumbuzi. Utumishi wa Umma unaotoka ofisini na kwenda kuwasikiliza na kuwahudumia wananchi mahali waliko, Utumishi wa Umma unaotumia njia za kielektroniki kuboresha utoaji wa huduma, Utumishi wa Umma wenye maslahi yaliyowianishwa kwa kuzingatia uzito wa kazi na majukumu yanayofanana na

Utumishi wa Umma unaofuatilia kwa makini miradi ya kinkakati katika vipaumbele vya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo ni kuiwezesha nchi yetu kujenga uchumi wa viwanda na maendeleo ya wananchi kwa kuboresha huduma zitolewazo na Utumishi wa Umma, ili kuiwezesha nchi yetu kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza kwa kina utekelezaji wa majukumu kwa mwaka wa fedha 2015/2016, na mipango na bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, naomba kuwasilisha maombi ya fedha kwa muhtasari kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Fungu 20 - Ofisi ya Rais, Ikulu, tunaomba kuidhinishiwa sh. 14,962,054,000 ambapo fedha hizo ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kwa upande wa Fungu 30 - Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri tunaomba waidhinishiwe sh. 793,164,600,000 ambapo kwa Matumizi ya Kawaida sh. 362,715,571,000. Upande wa matumizi ya Miradi ya Maendeleo ni sh. 430,449,029,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Fungu 33 - Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, tunaomba waidhinishiwe sh 5,913,820,000, ambapo kati ya fedha hizo sh. 4,913,820,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo tunaomba kuidhinishiwa katika fedha hizo ni sh. 1,000,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Ofisi ya Rais Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi - Fungu Sita, tunaomba kuidhinishiwa sh 27,616,107,000, ambapo kati ya fedha hizo sh. 397,278,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kwa upande wa Matumizi ya Miradi ya Maendeleo ni sh. 27,218,829,000.

Fungu 11 - Ofisi ya Rais Ushauri wa Mafuta na Gesi, tunaomba waidhinishiwe sh. 1,036,239,000 ambazo ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Fungu 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, tunaomba kuidhinishiwa sh. 30,341,137,000, ambapo kwa Matumizi ya Kawaida ni sh. 22,791,137,000. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo katika fedha hizo ni sh. 7,550,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Fungu 67 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma tunaomba waidhinishiwe sh. 2,205,404,000 ambazo ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Fungu 94 - Ofisi ya Rais Tume ya Utumishi wa Umma, tunaomba waidhinishiwe sh. 3,717,876,000 ambazo ni za Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu la Tisa - Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma, tunaomba waidhinishiwe sh. 1,859,845,000 ambazo ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kwa upande wa Fungu Nne - Ofisi ya Rais Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, tunaomba waidhinishiwe sh. 1,293,851,000 ambazo ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kitabu changu cha hotuba kilichogawiwa kiweze kuingia chote kwenye Hansard. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa ili iamuliwe)
(Hoja ilitolewa na Kuamuliwa)

MWENYEKITI: Ahsante, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunaendelea. Hoja hizi mbili zimewasilishwa rasmi mbele ya Bunge letu.

HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA, MHESHIMIWA ANGELLAH JASMINE KAIRUKI (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA WA 2016/17 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI.

A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa iliyochambua bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu (Fungu 20 na 30), Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Fungu 33), Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi (Fungu 06), Ushauri wa Mafuta na Gesi (Fungu 11), Menejimenti ya Utumishi wa Umma (Fungu 32), Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma (Fungu 67), Tume ya Utumishi wa Umma (Fungu 94), Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma (Fungu 09), na Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa (Fungu 04). Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/16. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha

Mpango wa Utekelezaji na Makadirio ya Fedha kwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17.

2. **Mheshimiwa Spika**, namshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kuniamini na kunitewa katika Wadhifa wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Ninamuahidi kwamba nitatekeleza wajibu wangu kwa ufanisi na uadilifu mkubwa. Nawashukuru pia Wajumbe wa UWT Mkoa wa Dar es Salaam, Baraza Kuu la UWT Taifa na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) na Wafanyakazi kwa ujumla kwa kuendelea kuniamini kuwawakilisha wafanyakazi kwa awamu nyingine tena katika Bunge hili. Vilevile, napenda kuishukuru familia yangu kwa kuendelea kunipa ushirikiano na kuwa wavumilivu ninapotekeleza majukumu yangu.

3. **Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Jimbo la Bukoba Vijijini kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati mpya ya Utawala na Serikali za Mitaa. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mbunge wa Jimbo la Kavuu kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati. Pia, nawapongeza Waheshimiwa Wenyeviti, Makamu Wenyeviti na Wajumbe walioteuliwa katika Kamati mbalimbali ili kulitumikia Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

4. **Mheshimiwa Spika**, napenda pia kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa chini ya Mwenyekiti na Makamu wake kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri walioutoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2015/16 na Mapendekezo ya Mpango wa Utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17. Maoni na ushauri wa Kamati umetuwezesha na utaendelea kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi zaidi.

5. **Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee, naomba kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa uongozi wake mahiri wenye kuzingatia uadilifu, uwajibikaji na utendaji wenye malengo na unaozingatia matokeo katika Utumishi wa Umma. Hii inathibitisha kiu kubwa aliyonayo ya kuwaletea maendeleo kwa wnanchi na kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

6. **Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akiwa ni mwanamke wa kwanza kushika nafasi hiyo katika historia ya

nchi hii. Vilevile nampongeza kwa namna anavyomsaidia Rais katika utekelezaji wa majukumu ya kuleta mabadiliko ya kweli na maendeleo kwa wananchi.

7. **Mheshimiwa Spika**, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa kuwa Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar kwa kipindi cha pili. Vilevile, nampongeza Mheshimiwa Balazi Seif Ali Iddi kwa kuteuliwa kwake kushika wadhifa wa Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kipindi cha pili.

8. **Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa, kwa kupendekezwa na Rais na kuthibitishwa na Bunge kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Serikali ya Awamu ya Tano. Vilevile, nampongeza kwa kutekeleza madaraka yake ya kikatiba ya kumsaidia Mheshimiwa Rais katika udhibiti, usimamiaji, utekelezaji wa siku kwa siku wa kazi na shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwa Kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni.

9. **Mheshimiwa Spika**, naomba nikupongeze wewe binafsi kwa kuchaguliwa kwako katika nafasi ya Spika na kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa busara na hekima. Nampongeza pia Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb) kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika na kwa kuendesha vyema shughuli za Bunge. Nawapongeza pia Wenyeviti wa Bunge kwa umahiri wao wa kuliongoza Bunge lako Tukufu.

10. **Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua fursa hii pia kuwapongeza Mawaziri wote wa Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuaminiwa na kuchaguliwa na Mheshimiwa Rais kumsaidia katika kuwaletea Watanzania maendeleo kwa kasi kubwa zaidi chini ya kauli mbiu ya HAPA KAZI TU!

11. **Mheshimiwa Spika**, namshukuru Mheshimiwa George Boniface Simbachawene (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Mheshimiwa Selemani Said Jafo (Mb), Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa ushirikiano wao mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais.

12. **Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza Wabunge walioteuliwa na Mheshimiwa Rais ambao ni Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Naibu Spika), Mheshimiwa Dkt. Abdallah Saleh Possi (Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu), Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa (Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano), Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango (Waziri wa Fedha na

Mipango), Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako (Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi) na Mheshimiwa Dkt. Augustine Mahiga (Waziri wa Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa) kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

13. **Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Balozi John William Kijazi, Katibu Mkuu Kiongozi; Bwana Peter Alanambula Ilomo, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Ikulu; Dkt. Laurean Josephat Ndumbaro, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Bi. Susan Paul Mlawi, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Makamishna, Watendaji Wakuu wa Tume na Taasisi; Wakurugenzi na Watumishi wote kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kutekeleza majukumu yanayoiwezesha Ofisi kufikia malengo ikiwa ni pamoja na kukamilisha Hotuba hii kwa wakati.

14. **Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kuzishukuru Nchi Wahisani na Washirika wa Maendeleo ambao wameshirikiana na Ofisi ya Rais na wamechangia kwa kiasi kikubwa katika jitihada za kuleta maendeleo kwa wananchi. Hivyo, nachukua fursa hii kushukuru: China, Japan, Uingereza, India, Korea ya Kusini, Ujerumani, Canada, Marekani, Sweden, Australia, Umoja wa Ulaya, Denmark, Norway, Uholanzi, Finland, Uswisi, Indonesia, Brazil, Italia, Malaysia, Misri, Pakistan, Singapore, Thailand, Ubelgiji, Ireland, Israel. Vilevile nashukuru Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa ambayo ni: Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia, OFID-OPEC Fund for International Development, Japan (JICA), Mfuko wa Maendeleo ya Jamii wa Japan (Japanese Social Development Fund), DfID, KOICA, GIZ, DFATD, USAID, SIDA, UNDP, Jumuiya ya Madola, DANIDA, NORAD na Bill and Melinda Gates Foundation.

15. **Mheshimiwa Spika**, naomba kulithibitishia Bunge lako tukufu kwamba Ofisi ya Rais, Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaendelea kutekeleza maelekezo yaliyotolewa katika hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akifungua Bunge la 11 yaliyohusu kuondoa urasimu ili kuongeza kasi ya utekelezaji katika uendeshaji wa shughuli za Serikali, kubana matumizi na kurejesha nidhamu ya Serikali na Utumishi wa Umma kwa kuongeza uwazi na kusimamia sheria, kanuni, miongozo na taratibu za uwajibikaji wa viongozi na watumishi wa umma ili wawajibike kwa wananchi ambao ndio wateja na waajiri wakuu wa watumishi wa umma. Vilevile, tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais katika vita dhidi ya rushwa, ubadhirifu, ufisadi, uzembe, ukiukwaji wa maadili, uvivu, urasimu na utumishi hewa kwa kuwawajibisha wanaodhihirika kujihusisha na vitendo hivyo. Hatua anazochukua Rais zinatakiwa kuungwa mkono na Bunge lako tukufu pamoja na

wale wote wanaoitakia mema nchi yetu. Dhamira ya Rais ya kuwa na Serikali inayowahudumia wananchi wa kawaida itatimia kwa Watumishi wa Umma wote kufanya kazi kwa juhudi, maarifa na uadilifu mkubwa. Pia inasisitizwa utoaji wa huduma bora wa haraka, wenye staha na wenye ufanisi ili kuondokana na kuwasumbua na kuwazungusha wananchi.

16. **Mheshimiwa Spika**, kwa masikitiko makubwa natoa pole kwa Watanzania wenzetu waliopotelewa na ndugu zao kutokana na majanga mbalimbali yaliyotokea katika kipindi hiki yakiwemo ajali na mafuriko yaliyotokea katika sehemu mbalimbali nchini. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema, peponi. Amina.

17. **Mheshimiwa Spika**, hotuba yangu itazungumzia maeneo makuu mawili ambayo ni: Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka wa Fedha wa 2015/16 pamoja na Mpango wa Utekelezaji na Maombi ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17.

B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2015/16

18. **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/16 ulizingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16), Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania (MKUKUTA) na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010-2015. Shughuli zilizotekelezwa na kila Taasisi ni kama ifuatavyo:-

OFISI YA RAIS, IKULU NA TAASISI ZAKE

19. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2015/16, Fungu: 20 Ofisi ya Rais, Ikulu liliidhinishiwa **Shilingi 20,575,672,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2016 **Shilingi 13,657,114,667** zilipokelewa na kutumika.

OFISI YA RAIS NA SEKRETARIETI YA BARAZA LA MAWAZIRI

20. **Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza majukumu yake, katika Mwaka wa Fedha wa 2015/16, Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri (Fungu 30) linalojumuisha Taasisi zilizo chini ya Ikulu, liliidhinishiwa **Shilingi 445,832,281,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 310,329,016,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na

Shilingi 135,503,265,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2016 **Shilingi 400,732,563,396** zilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo **Shilingi 291,403,739,579** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 109,328,823,817** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

(a) Ikulu

21. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais, Ikulu imeendelea kuongoza, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali. Katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016, shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

- (i) Huduma kwa Rais na familia yake ziliendelea kutolewa;
- (ii) Huduma za ushauri kwa Rais katika maeneo ya Uchumi, Siasa, Masuala ya Jamii, Sheria, Mawasiliano na Habari kwa Umma, Uhusiano wa Kimataifa na maeneo mengine zilitolewa kwa ajili ya kumsaidia Rais kufanya maamuzi;
- (iii) Mikutano 28 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ilifanyika ambapo nyaraka 47 zilichambuliwa. Mikutano 12 ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (IMTC) ilifanyika na nyaraka 30 zilichambuliwa na ushauri kutolewa. Aidha, mikutano minne ya Baraza la Mawaziri ilifanyika na nyaraka 17 zilitolewa uamuzi. Aidha, mikutano mitano ya kazi ya Makatibu Wakuu ilifanyika ambapo mada 16 ziliwasilishwa na kujadiliwa;
- (iv) Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu (NACSAP III) utakaotekelezwa kwa miaka mitano (2016/17 hadi 2020/21) umeandaliwa;
- (v) Elimu kwa umma kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Kamati za Uadilifu zilizoanzishwa kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Pili katika maeneo ya kazi ilitolewa;
- (vi) Utekelezaji wa Mpango Kazi wa Pili wa Uendeshaji wa Shughuli za Serikali kwa Uwazi (Open Government Partnership - OGP) kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/15-2015/16 umeendelea kuratibiwa;
- (vii) Uratibu wa Mpango Kazi wa Pili wa OGP wenye vipaumbele vya kutunga Sheria ya Haki ya Kupata Habari; kuweka mfumo huria wa takwimu (open data), kuweka wazi ripoti mbalimbali za fedha, mipango ya matumizi ya ardhi iliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji mkubwa na maeneo yaliyotengwa ya uchimbaji wa madini na mikataba ya madini umeendelea;

(viii) Rufaa 71 za Watumishi wa Umma na Mamlaka za Nidhamu zilichambuliwa na kuwasilishwa kwa uamuzi. Rufaa 51 zilitolewa uamuzi na wahusika kujulishwa. Aidha, malalamiko 300 ya Watumishi wa Umma na wananchi wengine yalichambuliwa na kutolewa maelekezo;

(ix) Taarifa ya Ofisi ya Rais, Ikulu ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Nne kwa mwaka 2005 - 2015 iliandaliwa na kuwasilishwa Ofisi ya Waziri Mkuu. Aidha, Taarifa ya Mafanikio ya siku 100 za Serikali ya Awamu ya Tano iliandaliwa;

(x) Taarifa za utekelezaji za nusu mwaka za Programu za Maboresho za Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP), Maboresho ya Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (BEST), Maboresho katika Serikali za Mitaa (LGRP), Maboresho katika Sekta ya Sheria (LSRP) na Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa (NACSAP II) zimechambuliwa na ushauri kutolewa;

(xi) Ufuatiliaji wa Programu za Maboresho Ngazi ya Wizara zinazojumuisha Programu ya Usimamizi wa Fedha za Umma; Maboresho ya Mazingira ya Biashara na Uwekezaji; Maboresho katika Serikali za Mitaa; Maboresho katika Sekta ya Sheria; na Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Pili ulifanyika;

(xii) Watumishi wanaoishi na VVU na UKIMWI na familia zao wamepata huduma muhimu za dawa, lische na ushauri nasaha kupitia Zahanati ya Ikulu. Aidha, elimu kuhusu magonjwa sugu yasiyoambukizwa pamoja na upimaji wa hiari wa magonjwa hayo umefanyika kwa wafanyakazi wa Ikulu na Ikulu ndogo mikoani. Vilevile, waliobainika na matatizo hayo wanapatiwa huduma zinazopaswa kwa mujibu wa mwongozo;

(xiii) Ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano, Ikulu umekamilika kwa asilimia 98. Kazi iliyosalia ni ufungaji wa vifaa vya mawasiliano;

(xiv) Ukarabati wa majengo ya Makazi ya Rais, Utawala, Mapokezi na nyumba 10 za watumishi katika Ikulu Ndogo ya Chamwino na uchimbaji wa visima 2 vya maji umekamilika. Aidha, ukarabati wa Ikulu Ndogo ya Arusha umekamilika; na

(xv) Ukarabati mdogo wa majengo ya Ikulu na ukuta kuzunguka Ikulu ulifanyika.

(b) Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU)

22. **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na.11 ya mwaka 2007 jukumu kubwa la TAKUKURU ni kuelimisha umma kuhusu athari za rushwa, kuchunguza tuhuma za makosa ya rushwa, kuwafikisha watuhumiwa mbele ya vyombo vya kisheria na kuishauri Serikali kuhusu namna ya kuziba mianya ya rushwa. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Jumla ya tuhuma 3,986 zilichunguzwa ambapo uchunguzi wa tuhuma 439 ulikamilika. Kati ya tuhuma ambazo uchunguzi ulikamilika, majalada 277 yaliwasilishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kwa ajili ya kuomba kibali. Aidha, majalada 190 kati ya yaliyopelekwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka yalipata kibali na kesi kufunguliwa mahakamani;

(ii) Jumla ya kesi 927 ziliendeshwa, na kati ya kesi hizo, kesi 320 zilitolewa maamuzi mahakamani ambapo kesi 142 washtakiwa walifungwa baada ya kupatikana na hatia, kesi 178 washtakiwa waliachiwa huru, kesi 29 ziliondolewa mahakamani kwa sababu mbalimbali zikiwemo washtakiwa kufariki na kukosekana kwa mashahidi. Aidha, kesi 578 zinaendelea kusikilizwa mahakamani;

(iii) Shilingi bilioni 9.505 ziliokolewa kutokana na operesheni zilizofanywa na TAKUKURU ambapo Shilingi bilioni 8.542 fedha taslim zilirejeshwa kwenye Akaunti ya Mamlaka ya Mapato Tanzania. Aidha, Shilingi milioni 867 ziliokolewa kutokana na udhibiti kati ya fedha hizo Shilingi milioni 96 ziliingizwa kwenye Akaunti ya Hazina;

(iv) Utafiti wenye lengo la kuimarisha mifumo ya udhibiti wa mianya ya rushwa katika eneo la biashara umekamilika na mapendekezo yametolewa kwa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Vilevile, utafiti unaendelea kufanyika katika maeneo ya Ardhi, Maji na Bandari. Aidha, mapendekezo ya kuziba mianya ya rushwa katika maeneo ya Mahakama, Polisi na Ardhi yamepelekwa kwenye Mamlaka husika kwa utekelezaji;

(v) Uchambuzi wa mifumo 365 umefanyika katika maeneo ya Fedha, Ardhi, Kilimo, Afya, Elimu, Ujenzi, Maji, Mifugo, Uchukuzi, Madini, Misitu, Nishati, Biashara, Viwanda, Jeshi, Mahakama, TAMISEMI, Siasa, Utalii na Hifadhi ya Jamii kwa lengo la kubaini mianya ya rushwa na kuimarisha mifumo ya utendaji na utoaji huduma. Aidha, Warsha 120 za kujadili matokeo ya utafiti na uchambuzi wa mifumo yenye lengo la kuweka mikakati ya kuziba mianya ya rushwa

ilifanyika sambamba na ufuatiliaji wa utekelezaji wa maazimio yaliyotokana na mapendekezo ya uchambuzi;

(vi) Kupitia ufuatiliaji wa Miradi ya Maendeleo katika Serikali za Mitaa (Public Expenditure Tracking System – PETS), Miradi ya Maendeleo 537 yenye thamani ya Shilingi bilioni 82.55 ilikaguliwa. Miradi 195 yenye thamani ya Shilingi bilioni 29.15 ilibainika kuwa na kasoro zilizoashiria kuwepo kwa rushwa au ubadhirifu ambapo miradi 110 kati ya iliyobainika kuwa na kasoro wahusika walishauriwa namna ya kurekebisha kasoro zilizojitokeza. Aidha, uchunguzi wa kina kwa miradi 85 kati ya miradi yenye kasoro umeanzishwa ili kubaini ukweli wa tuhuma. Vilevile, ufuatiliaji maalum wa miradi ya Afya inayofadhiliwa na Benki ya Dunia unaendelea kufanyika ambapo hatua zimechukuliwa kwenye maeneo yaliyobainika kuwa na kasoro ikiwemo kuanzisha uchunguzi wa awali ambapo majalada 87 yamefunguliwa;

(vii) Elimu kuhusu athari za rushwa ilitolewa kwa makundi mbalimbali ya wananchi kupitia semina 1,976, mikutano ya hadhara 1,303, mijadala ya wazi 96, vipindi vya redio 175, vipindi vya televisheni 4, maonesho 115 na taarifa kwa vyombo vya habari 90 ikiwa ni juhudi za Serikali za kudhibiti rushwa na kuungwa mkono. Aidha, vipindi 84 vya habari vilitolewa, makala 133 ziliandaliwa na nakala za machapisho 123,650 zilitolewa kwa wadau. Katika uelimishaji huo, wananchi 499,671 walifikiwa ana kwa ana;

(viii) Elimu ya athari za rushwa katika uchaguzi ilitolewa nchini kote wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 ikilenga kuhamasisha wananchi na wapiga kura kutumia haki yao ya Kikatiba kupiga kura ili kupata viongozi waadilifu;

(ix) Ushirikishwaji wa vijana uliendelea kuwa ajenda muhimu ambapo vijana walio shuleni, vyuoni na ambao hawapo shuleni walipewa elimu kuhusu athari za rushwa na kusisitizwa kujiunga katika klabu za wapinga rushwa ili kuwajenga kimaadili. Klabu mpya 208 zilizinduliwa zikiwemo mbili za vijana ambao hawapo shuleni na klabu 1,507 ziliimarishwa;

(x) Watumishi 81 walipatiwa mafunzo ya uchunguzi ili kuwapa weledi na kuongeza ufanisi. Kati yao watumishi 13 walipata mafunzo nje ya nchi na watumishi 68 walipata mafunzo ndani ya nchi; na

(xi) Vitengo viwili vya ushauri wa kitaalam vimeanzishwa ambavyo ni Kitengo cha Ubunifu na Usanifu na Kitengo cha Ukadiriaji wa Gharama za Ujenzi. Lengo ni kuimarisha uchunguzi na ushahidi wa mashauri ya rushwa yanayohusiana na maeneo hayo.

(c) Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)

23. Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) unalo jukumu la kuwawezesha wananchi wanaomiliki rasilimali na biashara nje ya mfumo rasmi kuwa na uwezo wa kurasimisha mali na hatimaye kushiriki katika uchumi wa soko unaoendeshwa kwa mujibu wa Sheria. Ili kufikia azma hii MKURABITA inao wajibu wa kuwawezesha Watanzania kutumia mali zao zilizokwisha rasimishwa kama dhamana katika kupata mikopo na fursa nyingine katika uchumi wa soko. Katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Makubaliano na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yamefanyika kwa ajili ya kuboresha mbinu za kupanga, kutekeleza, kuratibu na kufuatilia shughuli za urasimishaji nchini. Utekelezaji wa makubaliano hayo umeanza Januari, 2016. Aidha, kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi mapendekezo ya maboresho katika Sheria za Ardhi yameandaliwa na kupelekwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa hatua zaidi;

(ii) Kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ya Zanzibar, urasimishaji wa ardhi vijijini umefikia hatua ya usajili kwa ajili ya viwanja 5,227 vilivyopimwa katika Shehia za Kiungoni, Nungwi, Chokocho na Chwaka. Aidha, katika maeneo ya Mijini, urasimishaji umefikia hatua ya usajili kwa ajili ya viwanja 4,765 vilivyopimwa katika Shehia za Jang'ombe, Welezo na Limbani;

(iii) Kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, urasimishaji wa biashara umefanyika kwa kutoa mafunzo kwa Wafanyabiashara 2,100 katika Wilaya ya Mjini Magharibi na Kaskazini B (Unguja) pamoja na Chakechake na Wete (Pemba). Aidha, wafanyabiashara 30 wa Unguja wameunda umoja wao uitwao UWEZO KAZI BUSINESS FAMILY kwa ajili ya kuendesha biashara zao katika mfumo rasmi;

(iv) Mafunzo ya kuwajengea uwezo wakulima kutumia Hati za Haki Milki za Kimila yametolewa kwa wakulima 54 kutoka Vijiji vya Mabadaga na Mbuyuni katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali. Aidha, Mpango Kazi wa Jamii ulitekelezwa kwa kuanzisha mashamba darasa katika skimu mbili za umwagiliaji za Senyela na Mbuyuni katika Halmashauri hiyo. Pia, kikundi cha wafugaji wa nyuki kimepewa mizinga ya kisasa minne. Vilevile, utekelezaji wa Mpango Kazi wa Jamii umewezesha wafugaji wa kata ya Sanjaranda katika Halmashauri ya Manyoni kuanza ufugaji wa kisasa baada ya kupata madume 47 ya ng'ombe wa kisasa;

(v) Uratibu wa maandalizi ya awali kwa ajili ya kutekeleza mradi wa majaribio ya matumizi ya mfuko endelevu wa urasimishaji katika Halmashauri za Manispaa za Morogoro na Iringa umekamilika. Utekelezaji wa mradi huu wa majaribio unatarajiwa kuanza Mei, 2016;

(vi) Ufuatiliaji na Tathmini ya shughuli za urasimishaji umefanyika katika Mamlaka 10 za Serikali za Mitaa za Kalambo, Sumbawanga, Mlele, Mpanda, Uvinza, Kigoma, Buhigwe, Kasulu, Nyang'wale na Geita. Mamlaka za Serikali za Mitaa 15 zimeendelea na urasimishaji katika Vijiji 154 ambapo mashamba 12,594 yamepimwa na Hati za Haki Milki za Kimila 9,004 zimetolewa. Aidha, mikopo ya thamani ya Shilingi bilioni 7.1 imetolewa kwa wakulima. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 2.4 zimetolewa kwa wakulima wadogo 107 moja kwa moja kwa kutumia hati zao kama dhamana na Shilingi bilioni 4.7 zimetolewa kwa udhamini wa vyama 9 vya wakulima. Taasisi zilizotoa mikopo hii ni pamoja na CRDB Bank PLC, NMB, Benki ya Posta, Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo, Mfuko wa Pansheni kwa Watumishi wa Umma na SACCOS;

(vii) Uandaaji wa zana za utafiti kwa ajili ya kuingiza dhana ya urasimishaji katika mitaala ya elimu nchini umefanyika kwa kushirikiana na Taasisi ya Elimu Tanzania; na

(viii) Mazungumzo ya awali yamefanyika na Makatibu Wakuu 7 wa Wizara za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ili kupata maoni juu ya uanzishwaji wa Mfuko Endelevu wa Urasimishaji Zanzibar. Wizara zilizoshiriki ni Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Wizara ya Fedha; Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati; Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko; Wizara ya Tawala za Mikoa na Idara Maalum; Wizara ya Uwezesaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto; Wizara ya Katiba na Sheria; na Tume ya Mipango.

(d) Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)

24. Mheshimiwa Spika, Awamu ya Tatu ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) imeandaliwa kufuatia mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Awamu mbili zilizotangulia na pia kama moja ya hatua za kutekeleza MKUKUTA na MKUZA ili kuondoa umaskini. Awamu ya Tatu inatekeleza Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini wenye lengo la kuongeza kipato, fursa na uwezo wa kugharamia mahitaji muhimu. Utekelezaji wa Mpango huu ni wa miaka 10 kuanzia mwaka 2012/13 inayogawanyika katika vipindi viwili vya miaka mitano kwa kila kipindi.

25. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Jumla ya kaya maskini milioni 1.3 zimetambuliwa na kati ya hizo, kaya maskini milioni 1.1 zenye jumla ya watu milioni 5 zimeandikishwa. Kati ya kaya/watu wote waliomo katika Mpango, asilimia 54 ni wanawake. Mpango huu unatekelezwa katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa za Tanzania Bara na Wilaya zote za Zanzibar. Aidha, jumla ya Shilingi bilioni 275.9 zilihawilishwa kama ruzuku kwa kaya maskini milioni 1.1 zilizoko Tanzania Bara na Zanzibar;

(ii) Mpango wa kutoa ajira za muda umeandaa miradi 1,880 kutoka katika Vijiji (1,316), Mitaa (187) na Shehia (70) jumla yake ni 1,573 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 40 na Wilaya zote za Zanzibar. Miradi hiyo ina thamani ya Shilingi milioni 42.6 Miradi hiyo ni ya ujenzi au ukarabati wa majosho, uanzishaji wa vitalu vya miche ya miti, uchimbaji wa visima, uboreshaji wa barabara vijijini, uhifadhi wa vyanzo vya maji na uhifadhi wa mazingira. Miradi hii imepitiwa na Timu ya Wataalam wa Sekta ili kuhakikisha inakidhi vigezo vyote vya kisekta. Aidha, wakati wa utekelezaji wa miradi ya ajira za muda, Wawezeshaji wa Kitaifa 105 kutoka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa walifundishwa jinsi ya kuhifadhi maliasili. Wawezeshaji hawa walitoa mafunzo kwa jumla ya wawezeshaji 1,084 wa ngazi ya jamii;

(iii) Ukusanyaji wa takwimu za hali halisi ya mahitaji ya miundombinu ya afya, elimu na maji kutoka katika maeneo yote ya utekelezaji 161 ulifanyika. Utekelezaji wa miradi ya jamii umeanza kwa kuidhinisha jumla ya miradi 40 ya Sekta za Elimu na Afya yenye thamani ya Shilingi bilioni 2.9;

(iv) Mkakati wa utekelezaji wa shughuli za kuweka akiba na kukuza uchumi wa kaya umeandaliwa na kukamilika. Mafunzo kwa wawezeshaji 120 kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa sita yamefanyika ili wapate stadi, elimu na mbinu za kuunda vikundi endelevu vya kuweka akiba kwa kaya za walengwa. Wawezeshaji kutoka Halmashauri za Wilaya za Bagamoyo, Kibaha, Chamwino, Lindi na Manispaa za Lindi na Mtwara walipata mafunzo ya kuunda vikundi vya kuweka akiba. Pia, jumla ya vikundi 953 viliundwa katika Mamlaka hizo za Serikali za Mitaa vikiwa na wanachama 14,295 wenyue lengo la kuweka akiba na kuwekeza;

(v) Mfumo wa Teknolojia, Habari na Mawasiliano (TEHAMA) wa Utambuzi, Uandikishaji, Malipo na Malalamiko ya Walengwa ulikamilika na unatumika. Mamlaka za Serikali za Mitaa 135 zimeunganishwa na Makao Makuu ya TASAF kupitia Mtandao wa Mawasiliano TAMISEMI na kazi ya kutengeneza mifumo mingine zinaendelea;

(vi) Masjala ya Walengwa iliyoko TASAF Makao Makuu imeimarishwa kwa kuwezesha kutunza taarifa zote za kaya za walengwa milioni 1.1 wa Mpango waliotambuliwa na kuandikishwa;

(vii) Katika kujenga uwezo wa wadau muhimu katika kutekeleza Mpango kwa ufanisi, mafunzo yalitolewa kwa Wawezeshaji 3,150 wa Mamlaka za Serikali za Mitaa; Wajumbe 58,556 wa Kamati za Usimamizi za Jamii; Watendaji 4,675 wa Vijiji, Mitaa na Shehia; Wenyeviti 4,490 wa Vijiji, Mitaa na Shehia, Walimu 5,174 wa Shule za Sekondari na Msingi; Wafanyakazi 2,464 wa Afya, Wajumbe 16,201 wa Halmashauri za Vijiji, Mitaa na Shehia; na Washauri Wafuatilaji, Waratibu na Wahasibu wa Mpango 336;

(viii) Ukaguzi wa ndani ulifanyika ili kuhakikisha kama fedha zilitumika ipasavyo katika utekelezaji wa Mpango wa TASAF Awamu ya Tatu. Ukaguzi ulifanyika TASAF Makao Makuu pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa 27;

(ix) Tathmini ya matokeo ya Mpango kwa Tanzania Bara na Zanzibar imefanyika ili kuwezesha Serikali, Washirika wa Maendeleo na wadau wengine kujua kama utekelezaji wa Mpango unaleta matokeo yaliyokusudiwa; na

(x) Kwa kutumia Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS) Tanzania Bara na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Zanzibar (OCGS) kazi ya ukusanyaji wa taarifa za awali za walengwa wa mpango katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 18 zinazohusika ilikamilishwa. Jumla ya kaya 7,319 zilifanyiwa tathmini.

(e) Taasisi ya Uongozi

26. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya UONGOZI ilianzishwa kwa lengo la kuwa Kituo cha Utaalam wa hali ya juu cha kuendeleza Viongozi Barani Afrika kwa kuanzia na Tanzania, Ukanda wa Afrika Mashariki na hatimaye Afrika kwa ujumla. Walengwa ni Viongozi Waandamizi waliopo na wanaojitokeza wakiwemo Wanasiasa na Watumishi wa Umma.

27. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016, shughuli zifuatazo zimetekelwa:-

(i) Kozi 15 za muda mfupi zilitolewa kwa Viongozi 449 kwa nia ya kuwajengea uwezo wa kiutendaji. Kozi hizi zilikuwa katika maeneo ya Usimamizi wa Mashirika ya Umma, Mawasiliano Fanisi, Ujuzi wa Majadiliano ya Mikataba ya Mafuta na Gesi Asili, Uandaaji na Usimamizi wa Mpango Mkakati Wenye Matokeo, Mitazamo na Dira, Usimamizi wa Vihatarishi na Udhibiti wa Ndani,

Uongozi wa Kimkakati, Mawasiliano na Diplomasia katika Majadiliano ya Mikataba, na Itifaki na Huduma kwa Wateja;

(ii) Vipindi vitano vya mahojiano na viongozi, kimoja kutoka ndani na vipindi vinne nje ya nchi viliandaliwa na kurushwa kwenye runinga na kuwekwa kwenye tovuti ya Taasisi na mitandao ya kijamii kwa nia ya kuimarisha na kujenga uwezo wa viongozi wa sasa na wanaochipukia;

(iii) Kwa kushirikiana na Taasisi za ndani na nje ya nchi, mikutano 3 ya majadiliano ya Kikanda na Kimataifa, kwa nia ya kubadilishana uzoefu na maarifa katika masuala ya maendeleo ya Bara letu la Afrika ilifanyika. Mikutano hiyo ni:

(a) Kongamano la *Viongozi wa Afrika juu ya Namna ya Kuwa na Afrika Jumuishi* lililoandaliwa kwa kushirikiana na Taasisi ya Benjamin Mkapa;

(b) Kongamano la Kimataifa la *Kujadili Changamoto za Rasilimali katika Afrika Mashariki* lililoandaliwa kwa kushirikiana na Taasisi ya BMW ya Ujerumani;

(c) Kongamano la *Wafanyabiashara juu ya Uendelezaji wa Ushirikiano wa Biashara, Kitaifa na Kikanda* lililoandaliwa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Capetown, Afrika ya Kusini.

(iv) Mkutano wa Faragha (Retreat) wa Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu, Makatibu Tawala wa Mikoa na Viongozi Wakuu wa baadhi ya Taasisi za Umma juu ya Wajibu wa Viongozi wa Serikali katika Uchaguzi Mkuu wa 2015 uliandaliwa na kufanyika;

(v) Insha ya Ushindani kwa Vijana wa Afrika kati ya miaka 18-25 ilifanyika kwa madhumuni ya kuwajengea uwezo na utamaduni wa kujenga hoja; uelewa katika eneo la uongozi na kujenga mtandao wa vijana. Vijana 522 kutoka nchi 19 za Afrika walishiriki. Washindi walitoka Zimbabwe, Uganda, Botswana na Kenya;

(vi) Utafiti juu ya Wanawake katika Uongozi ulifanyika ili kubaini fursa na viwezeshi vilivyopo;

(vii) Programu Jumuishi ya Usimamizi wa Rasilimali za Taifa hususan katika Sekta ya Mafuta, Gesi Asili na Madini ilitekelezwa kama ifuatavyo:-

(a) Mikutano miwili ya jopo la Wataalam katika Sekta ya Mafuta, Gesi Asili na Madini ilifanyika;

(b) Utafiti kuhusu uhusiano baina ya wawekezaji katika Sekta za Mafuta, Gesi Asili na Madini na jamii inayowazunguka ulifanyika;

(c) Utafiti kuhusu usimamizi wa mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa yanayotokana na Rasilimali za Gesi Asili na Madini ulifanyika;

(d) Mafunzo kwa ajili ya kujenga uwezo wa majadiliano ya mikataba katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asili yalifanyika kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Columbia Marekani;

(viii) Mchakato wa kuboresha mifumo ya utendaji ndani ya Taasisi (Total Quality Management) ulianzishwa;

(ix) Tathmini ya Muda wa Kati (Mid-Term Review) ya Mpango Mkakati wa Taasisi wa mwaka 2011/12-2015/16 ilifanyika. Mapendekezo yaliyotolewa kwenye Tathmini hiyo yalitumika kuandaa Mpango Mkakati wa Miaka Mitano 2016/17-2021/22; na

(x) Mafunzo ya muda mfupi kuhusu kukasimu na kujenga Utendaji wa Pamoja (Timu) yalitolewa kwa Watumishi 22 wa Taasisi kwa lengo la kuongeza ufanisi.

(f) Mfuko wa Rais wa Kujitegemea

28. Mheshimiwa Spika, majukumu ya Mfuko wa Rais wa Kujitegemea ni pamoja na kutoa huduma za mikopo mbalimbali kwa wajasiriamali na ushauri na mafunzo ya kibiashara ili kuongeza ufanisi katika biashara. Shughuli zilizotekelezwa katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 ni kama ifuatavyo:-

(i) Mikopo 445 yenye thamani ya Shilingi 336,900,000 ilitolewa kwa wahitimu wa Vyuvo vya Ufundi Stadi ambapo Vijana ni 173, Wanawake 231 na kundi maalum linalojumuisha vijana wenye ulemavu 41. Aidha, Shilingi 202,862,688 zilizokopeshwa zimerejeshwa;

(ii) Walengwa wa Mfuko 1,547 walipata mafunzo ya ujasiriamali, namna ya kujitambua na taratibu za mikopo ya Mfuko;

(iii) Walengwa wa Mfuko 314 walipata mafunzo ya kuwawezesha kujiwekea akiba na kubuni miradi endelevu itakayoongeza fursa ya ajira;

(iv) Watendaji 7 wa Mfuko walipata mafunzo kuhusu huduma kwa mteja na tathmini ya miradi; na

(v) Mwongozo wa Ajira na Utawala umeandaliwa na kukamilika.

OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

29. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2015/16 Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilitengewa **Shilingi 6,227,803,160**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 4,741,906,160** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 1,485,897,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2016 **Shilingi 3,619,095,147** za Matumizi ya Kawaida zilipokelewa na kutumika. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, **Shilingi 867,176,507** zilipokelewa na kutumika.

30. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Malalamiko 114 ya ukiukwaji wa maadili dhidi ya Viongozi wa Umma yalipokelewa na kuchambuliwa. Kati ya malalamiko hayo, malalamiko 57 yalihusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na malalamiko 57 hayakuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Uchunguzi wa awali umefanyika kwa malalamiko 9 yanayohusu ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Aidha, malalamiko 57 ambayo hayakuhusu ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma walalamikaji walipewa ushauri na mengine yalielekezwa kwenye mamlaka zinazohusika;

(ii) Viongozi wa Umma 15,624 walitumiwa Fomu za Tamko la Rasilimali na Madeni kwa kipindi kilichoishia tarehe 31 Desemba, 2015. Jumla ya Viongozi wa Umma 14,543 wamerejesha Fomu za Tamko la Rasilimali na Madeni;

(iii) Viongozi wa Umma 3,980 walipatiwa elimu kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Mgongano wa Masilahi na Maadili ya Utumishi wa Umma kupitia semina, midahalo, mafunzo na vikao mbalimbali. Aidha, watumishi wa umma na wananchi wapatao 8,652 walipatiwa elimu ya maadili. Jumla ya vipindi vya redio 30 na vya Televisheni 7 vilirushwa. Vilevile, washiriki 63 kutoka Asasi za Kiraia walipatiwa mafunzo ya maadili;

(iv) Ujenzi wa Mfumo wa Kielektroniki wa Taarifa za Uchunguzi umekamilika, na unafanyiwa majaribio. Mfumo huu utanza rasmi kuingizwa

taarifa za Matamko ya Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma na Malalamiko kuanzia Julai, 2016;

(v) Shughuli za uhamasishaji na kampeni kwa Viongozi wa Umma na wananchi kuhusu kukuza maadili kupitia vipindi vya redio 26 na majadiliano 24 katika redio zimefanyika. Vipindi hivi vilirushwa hewani kupitia redio katika Mikoa saba ya Morogoro, Iringa, Mtwara, Dodoma, Tanga, Pwani na Dar es Salaam;

(vi) Mafunzo kuhusu Maadili kwa Viongozi yalitolewa kwa Mawaziri na Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu na Wakuu wa Mikoa;

(vii) Mafunzo kwa Wenza wa Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Majaji na Wakuu wa Polisi walipatiwa mafunzo kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya mwaka 1995, Mgongano wa Masilahi, Uhusiano katika Ndoa, Maadili na Umiliki wa Mali; na

(viii) Katika kutekeleza Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa, kwa kushirikiana na wadau wengine, Hati ya Ahadi ya Uadilifu kwa Viongozi wa Umma, Watumishi wa Umma pamoja na Sekta Binafsi iliandaliwa. Jumla ya Viongozi wa Umma 13,189 kati ya Viongozi wa Umma 15,624 wamesaini Hati ya Ahadi ya Uadilifu.

OFISI YA RAIS, UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MIRADI

31. **Mheshimiwa Spika**, ili kuongeza ufanisi na udhibiti katika utekelezaji wa miradi na mipango ya maendeleo, Serikali ilianzisha mfumo wa kusimamia, kushauri na kutathmini utekelezaji wa miradi ya kipaumbele ya kitaifa. Mfumo huu wa **Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa** unalenga kuharakisha kufikiwa kwa malengo yaliyoainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025.

32. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2015/16 Bunge liliidhinisha **Shilingi 17,881,312,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 3,604,378,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 14,276,934,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2016 **Shilingi 1,419,841,051** za Matumizi ya Kawaida zilipokelewa na kutumika. Kwa Miradi ya Maendeleo, **Shilingi 5,000,000,000** zilipokelewa na kutumika.

33. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2015 hadi Machi, 2016 shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Miradi ya maji ilipangwa kulingana na vigezo vilivyo kubalika katika maabara ya Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa na kuratibu mafanikio ya upatikanaji wa maji vijijini chini ya Mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa. Uhakiki wa takwimu na utatuzi wa changamoto za vyanzo vya maji katika ngazi za mikoa kwenye miradi ya maji vijijini ulifanyika. Mikoa 16 ilifanyiwa mapitio, vyanzo vya maji 4,592 vilichaguliwa, kati yake vyanzo 4,294 vilithibitishwa. Jumuiya za watumiaji maji 1,812 zilihakikiwa kati ya 5,226 zilizopangwa. Mafunzo sahihi ya kikanda kwa wadau wa maji Vijijini kama vile Maafisa Watendaji wa Kata, Maafisa Watendaji wa Vijiji, Viongozi wa Kamati za Watumiaji Maji katika jamii yalifanyika;

(ii) Ufuatiliaji wa utekelezaji na utatuzi wa changamoto katika skimu za umwagiliaji za Idodi na Mapogolo (Iringa); Makwale, Mbuyuni-Kimani na Igomelo (Mbeya); Mwamkulu na Ugalla (Katavi) ulifanyika. Ufuatiliaji huo uliangalia usambazaji wa ruzuku ya pembejeo za kilimo katika skimu za umwagiliaji, na kuhakikisha kuwa wakulima katika skimu hizo walipata pembejeo kwa wakati;

(iii) Mafunzo kuhusu uendeshaji wa usimamizi wa maghala yalitolewa kwa waendeshaji wa maghala 48. Lengo ni kuwezesha wakulima kutunza mazao ya kilimo cha mahindi na mpunga, wakati wanasubiri kupata masoko ya uhakika;

(iv) Kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania, Benki Kuu na Mamlaka ya Bandari, elimu ya kuhamasisha wadau wa bandari ilitolewa ili kutumia fursa iliyotokana na kuongezeka kwa muda wa mfumo wa malipo kwa njia ya mtandao (Tanzania Interbank Settlement System) kutoka saa 10 jioni hadi saa 2 usiku kwa siku za kazi na kuanzia saa 3 asubuhi hadi saa 8 mchana kwa siku za mapumziko;

(v) Ushauri ulitolewa kwa TANESCO kutumia maji yatokanayo na mgandamizo wa hewa (*condensation*) kwenye Mtambo wa Kinyerezi I na kuyatumia katika mtambo unaojengwa wa Kinyerezi II;

(vi) Kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania, changamoto ambazo zingesababishwa na bomba la gesi kupita karibu na makazi ya wananchi katika baadhi ya maeneo zilifuatiliwa na kutatuliwa;

(vii) Ufuatiliaji wa utekelezaji wa uthamini wa majengo kwa kutumia Uthamini wa Mkupuo kama ilivyoainishwa na maabara ya Matokeo Makubwa Sasa ulifanyika katika Manispaa za Kinondoni, Temeke na Ilala;

(viii) Ushauri na mwongozo wa kitaalam ulitolewa kwa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili katika kukamilisha pendekezo la uendelezaji na uendeshaji wa kitengo cha vipimo kwa njia ya ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi;

(ix) Ufuatiliaji na uratibu wa kufanikisha uanzishaji wa Kituo cha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ya mwaka 2010 ulifanyika;

(x) Mafunzo yalitolewa ya namna ya kuweka vipaumbele katika kutafuta vyanzo mbadala vya mapato kwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na kuweka mfumo wa utekelezaji na utatuzi wa changamoto katika nyanja zote na kuimarisha ushirikiano na wadau;

(xi) Kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Warsha iliyoshirikisha wadau mbalimbali ili kubaini mabadiliko katika Sheria 6 yanayohitajika ili kuboresha biashara na kupambana na rushwa ilifanyika;

(xii) Kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Tanzania, maabara ya Usalama wa Jamii iliandaliwa. Ripoti ya maabara imetayarishwa na kukabidhiwa viongozi wa Jeshi la Polisi na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ili ifanyiwe kazi; na

(xiii) Kuliwezesha Jeshi la Polisi Tanzania kuhamasisha wadau katika kusaidia Mkoa wa Kipolisi wa Kinondoni ambapo Benki ya CRDB imetoa Shilingi milioni 255 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kisasa cha mawasiliano (Call Centre). Aidha, Benki ya NMB imechangia Shilingi Milioni 143 kwa ajili ya kutengeneza vituo viwili vya polisi vinavyohamishika.

OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA WAKALA ZAKE

34. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2015/16, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma (Fungu 32) linalojumuisha pia Wakala zilizo chini yake liliidhinishiwa **Shilingi 43,977,564,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa mwaka. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 37,717,620,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 6,259,944,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2016 **Shilingi 25,147,830,363.80** zimepokelewa na kutumika.

Kati ya fedha hizo **Shilingi 23,437,886,363.80** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 1,709,944,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

35. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na Wakala zake imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuhakikisha Utumishi wa Umma unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora. Aidha, Watumishi wa Umma wanawajibika na kuwa wasikivu kwa wananchi pale wanapotoa huduma kwa ufanisi, staha na uharaka unaotakiwa kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa. Katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

(a) Menejimenti ya Utumishi wa Umma

(i) Masilahi ya Watumishi wa Umma yaliboreshwa kwa kutekeleza Sera ya Malipo ya Mishahara na Motisha katika Utumishi wa Umma ya Mwaka 2010 ambapo kima cha chini cha mishahara kiliongezwa kwa asilimia 13.2. Aidha, kodi ya mapato katika mishahara ya kima cha chini ilipunguzwa kutoka asilimia 12 hadi kufikia asilimia 11 ili kuongeza kipato cha Mtumishi wa Umma;

(ii) Mikutano miwili ya Baraza la Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma ilifanyika. Katika mikutano hiyo, mahusiano ya Vyama vya Wafanyakazi na Serikali yalijadiliwa ikiwa ni pamoja na kupitia Miundo ya Maendeleo ya Utumishi chini ya Wizara ya Fedha, Wakaguzi wa Hesabu za Serikali na Wizara ya Mifugo na Uvuvi;

(iii) Miundo na Mgawanyo wa Majukumu ya Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala wa Serikali 6 ilihuishwa ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi. Taasisi hizo ni Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi; Ofisi ya Msajili wa Hazina; Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; na Tume ya Utumishi wa Umma. Aidha, Ofisi ya Rais, Ushauri wa Mafuta na Gesi iliwezesha kuanzisha muundo na mgawanyo wa majukumu yake. Vilevile, Tume ya Utumishi wa Walimu iliwezesha katika kuanzisha muundo na mgawanyo wa majukumu yake, muundo ambao uliithinishwa tarehe 2 Novemba, 2015;

(iv) Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Mafunzo katika Utumishi wa Umma ya mwaka 2012 unakamilishwa;

(v) Idara ya Mikataba ya Utendaji Kazi Serikalini kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Mikataba ya Utendaji Kazi katika Taasisi za Umma imeanzishwa;

(vi) Huduma kwa Viongozi Wastaafu wa Kitaifa na wajane wa viongozi 16 zilitolewa kwa mujibu wa Sheria. Aidha, Ujenzi wa nyumba ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili umefikia hatua ya uwekaji wa zege kwenye ghorofa ya kwanza. Michoro ya nyumba ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne inakamilishwa;

(vii) Ajira za Watumishi wa Umma zilisimamiwa kwa kufanya maandalizi ya ajira za watumishi wapya 71,496 ambapo kipaumbele ni katika Sekta za Elimu 28,957; Afya 10,870; Kilimo 1,791 na Mifugo 1,130. Aidha, Utekelezaji wa ajira hizi utafanyika kuanzia Mei, 2016, upandishwaji vyeo umefanyika na kuingizwa kwenye Mfumo kwa watumishi 57,898 kati ya 113,520 walioidhinishwa kwa mwaka 2015/16;

(viii) Mkutano wa Wakuu wa Utumishi wa Umma wa Nchi 15 za Afrika wanachama wa Jumuiya ya Madola kwa lengo la kujadili na kubadilishana uzoefu wa kuboresha Utumishi wa Umma ulifanyika tarehe 13-15 Julai, 2015 na kuratibiwa kwa ushirikiano na Sekretarieti ya Jumuiya ya Madola;

(ix) Kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo, upatikanaji wa nafasi za mafunzo kwa watumishi wa umma uliratibiwa ambapo Watumishi wa Umma 395 walijengewa uwezo wa kiutendaji kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika nyanja mbalimbali nje ya nchi. Wadau wa Maendeleo waliotoa ufadhili ni Serikali ya India (140), China (75), Japan (71); Uholanzi (71), Jamhuri ya Korea (28), Australia (6) na Singapore (4);

(x) Watumishi wa Umma wapya 962 walipatiwa Mafunzo Elekezi ya Awali ili kuwapa uelewa wa Utumishi wa Umma na kufahamu misingi yake ambayo ni Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu za utendaji kazi. Mafunzo hayo yalitolewa na Chuo cha Utumishi wa Umma (762), Chuo cha Uongozi wa Mahakama (14) na Chuo cha Serikali za Mitaa (186);

(xi) Usimamizi wa matumizi ya TEHAMA katika Taasisi za Umma ulifanyika ili kurahisisha utendaji kazi, kuboresha utoaji wa huduma na kuokoa gharama zisizo za lazima kwa uendeshaji wa Serikali na upatikanaji wa huduma kwa Wananchi;

(xii) Programu ya Miundombinu ya Mawasiliano ya Kikanda, kwa Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika 'Regional Communication Infrastructure Programme' (RCIP) iliratibiwa. Miradi inayoratibiwa katika Programu iko katika hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na utekelezaji, kuingia mikataba na makandarasi na ununuzi. Miradi hiyo ni Mtandao wa Mawasiliano wa Serikali, Mfumo wa Ununuzi kwa Njia ya Mtandao (e-procurement), Mfumo wa Usajili wa

Vizazi na Vifo, Mfumo wa Matibabu kwa Njia ya Mtandao (telemedicine), Mfumo wa Usajili wa Biashara (business portal) na Mfumo wa Kielektroniki wa Kumbukumbu na Nyaraka (e-records);

(xiii) Viwango na Miongozo kwa ajili ya kutumiwa na Taasisi za Serikali wakati wa kubuni, kujenga na kuendesha mifumo mbalimbali ya TEHAMA imekamilika. Lengo kuu la Viwango na Miongozo hiyo ni kuhakikisha mifumo inayowekwa inakidhi mahitaji. Mahitaji hayo ni pamoja na thamani ya fedha, kubadilishana taarifa, kulinda taarifa za Serikali na kuwa endelevu. Viwango na Miongozo iliyokamilika inapatikana kwenye tovuti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma (www.utumishi.go.tz) na tovuti ya Wakala ya Serikali Mtandao (www.ega.go.tz);

(xiv) Mafunzo kuhusu ubunifu, usanifu, utengenezaji, usimamiaji na uendelezaji wa Mifumo na Mitandao ya TEHAMA yalitolewa kwa Maafisa TEHAMA 210 kutoka kwenye Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(xv) Vikao vya kazi na Sekretarieti za Mikoa yote na Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia huduma ya Mtandao kwa njia ya video viliandaliwa. Aidha, mwongozo wa matumizi ya huduma hiyo katika Taasisi za Serikali ulitolewa;

(xvi) Kikao elekezi kuhusu majukumu na wajibu wa Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu na Sheria, Kanuni na Miongozo inayoongoza utendaji wa kazi zao kilifanyika kwa Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu wa Serikali ya Awamu ya Tano;

(xvii) Mafunzo ya Maadili ya Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma yaliendeshwa kwa watumishi 1,396 kutoka katika Taasisi 34. Aidha, ufuatiliaji wa uzingatiaji wa maadili katika Utumishi wa Umma ulifanyika katika Taasisi 20. Vilevile, miongozo mbalimbali ya uzingatiaji wa maadili iligawiwa katika Taasisi za Umma na wadau wengine;

(xviii) Elimu kwa Umma kuhusu masuala ya kiutumishi ilitolewa kupitia mikutano 18 na kwa kutumia vyombo vya habari. Pia, watumishi walihamasishwa kusaini hati ya Ahadi ya Uadilifu;

(xix) Mafunzo kuhusu udhibiti wa VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa yaliratibiwa kwa Watumishi wa Umma 360 wa Wizara 6 na Wakala 2 za Serikali; na

(xx) Elimu kuhusu Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Sheria Na.9 ya 2010 ilitolewa kwa Makatibu Tawala na Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa za Mikoa 14, ili kutoa huduma hii kwa Watumishi wa Umma wote, wakiwepo wanaume wenye ulemavu 1,263 na wanawake 766.

(b) Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania

36. **Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania kilianzishwa ili kutoa mafunzo katika nyanja za Uongozi, Menejimenti na Utawala kwa ngazi za Cheti, Stashahada na Astashahada. Aidha, Chuo kinafanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalam pamoja na kutoa machapisho mbalimbali ya kitaalam katika Utumishi wa Umma.

37. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 shughuli zifuatazo zimetekelzwa:-

(i) Mafunzo mbalimbali ya muda mfupi na mrefu yaliendeshwa, ambapo mafunzo ya muda mfupi yalijumuisha kujiandaa kufanya Mitihani ya Utumishi wa Umma (Watumishi 510); Uongozi na Maendeleo, Menejimenti na Usimamizi wa Ofisi (Watumishi 1,480) na Mafunzo ya Awali (Watumishi 762);

(ii) Mafunzo ya muda mrefu kwa washiriki 17,192 yalitolewa katika fani za Utunzaji wa Kumbukumbu, Uhazili, Kompyuta, Utunzaji wa Fedha za Umma, Utawala wa Serikali za Mitaa na Menejimenti ya Rasilimali watu, Usimamizi wa Manunuzi ya Umma, Uongozi na Utawala Bora;

(iii) Ushauri wa kitaalam ulitolewa katika maeneo matano ambayo ni Uboreshaji wa Masijala; Mfumo wa Kompyuta; Mfumo wa Usimamizi wa Malipo wa Kompyuta; Maendeleo ya Rasilimali watu; na Tathmini ya Kazi na Uhuishaji Madaraja kwa Taasisi za Umma;

(iv) Mafunzo ya muda mrefu kwa Watumishi wa Chuo 6 ngazi ya Shahada ya Uzamivu; 10 ngazi ya Shahada ya uzamili; 9 Shahada ya kwanza, na wawili ngazi ya Stashahada yaliwezesha. Aidha, watumishi 70 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi; na

(v) Awamu ya Kwanza ya Ujenzi wa jengo la ghorofa tatu kwenye Kampasi ya Tabora unaohusisha hatua za mwanzo hadi upauaji umekamilika.

(c) Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao Tanzania

38. **Mheshimiwa Spika**, Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao Tanzania ina jukumu la kuwajengea uwezo Watumishi wa Umma kwenye

maeneo mbalimbali kwa kuratibu na kuendesha mafunzo na midahalo kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ili kuhimili kasi ya mabadiliko ya utoaji wa huduma kwa wananchi.

39. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Ushirikiano katika taaluma na teknolojia na Taasisi za ndani na nje ya nchi katika kutoa mafunzo umeendelezwa. Taasisi hizo ni pamoja na Chuo Kikuu cha Utawala wa Umma Canada (ENAP), Taasisi ya Stanford (Stanford-SEED), Chuo cha Serikali cha Kenya; Chuo cha Menejimenti cha Uganda; na Vituo vya Maendeleo Duniani (GDLN);

(ii) Mafunzo kwa washiriki 1,295 kutoka Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali na Sekta Binafsi yalitolewa katika maeneo ya Uongozi, Utawala Bora, Maadili, Anuai za Jamii, Tabia Nchi, Kupunguza Umaskini na Afya;

(iii) Mikutano 9 ya kazi baina ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na TAMISEMI, Wizara na Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia Ofisi za Makatibu Tawala wa Sekretarieti za Mikoa yote Tanzania Bara ilifanyika kwa Mtandao wa Video;

(iv) Mikutano 36 ya mafunzo na mijadala ya ndani na nje ya nchi ilifanikishwa kwa kutumia Mtandao wa Wakala;

(v) Kuwa mwenyeji wa mkutano wa Ushirikiano wa Vituo vya Elimu kwa Njia ya Masafa Barani Afrika ambapo nchi 15 ziliwakilishwa;

(vi) Watumishi wawili walipata mafunzo katika kuandaa taarifa za fedha. Mtumishi mmoja aliwezesha kupata mafunzo kuhusu uandaaji wa mafunzo kwa njia ya masafa nchini India. Aidha, watumishi wawili wanapata mafunzo ya muda mrefu ya Uhasibu na TEHAMA hapa nchini; na

(vii) Usimikaji wa lifiti kwenye ofisi ya Makao Makuu ya Wakala unaendelea na unatarajiwa kukamilika ifikapo Juni, 2016.

(d) Wakala ya Serikali Mtandao

40. **Mheshimiwa Spika**, Wakala ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa jitihada za utoaji wa huduma kwa kutumia TEHAMA kwenye Taasisi za Umma ili kuleta ufanisi, kuongeza uwajibikaji na kuboresha utoaji wa huduma (Serikali Mtandao). Aidha, Wakala ina jukumu la kuweka na kusimamia

mifumo ya mawasiliano salama Serikalini itakayoweza utoaji huduma bora kwa urahisi na kwa gharama nafuu.

41. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 shughuli zifuatazo zilitokeleza:-

(i) Taasisi za umma 72, zimeunganishwa kwenye Mfumo wa Mawasiliano Salama Serikalini;

(ii) Usalama wa miundombinu na mifumo ya TEHAMA ya Serikali na Taasisi zake umeimarishwa;

(iii) Ujenzi wa Vituo Vikuu vya Kuhifadhi Taarifa na Mifumo ya Serikali pamoja na kujikinga na majanga unaozingatia viwango vya usalama vya kitaifa na kimataifa unaendelea na utakamilika Juni, 2016;

(iv) Hatua za awali kwa ajili ya kuziunganisha Mamlaka za Serikali za Mitaa 77 kwenye Mfumo wa Mawasiliano Serikalini zimekamilika;

(v) Taasisi za Serikali 67 zimeunganishwa kwenye Mfumo wa Pamoja na Salama wa Barua Pepe wa Serikali. Aidha, Watumishi 130 kutoka Taasisi hizo wamepewa mafunzo ya usimamizi na uendeshaji wa Mfumo huu. Hadi sasa Taasisi za Serikali zinazotumia mfumo huu zimefikia 100;

(vi) Taasisi za Serikali 22 zimeunganishwa kwenye Mfumo wa Simu za Mkononi ili kuziwezesha kutoa taarifa ya huduma zinazotolewa na taasisi zao kwa wananchi;

(vii) Ugawaji na matumizi ya kiasi cha masafa ya intaneti ya Serikali umesimamiwa kwa Taasisi za Serikali 60. Hadi sasa Taasisi 176 zimekwisha unganishwa na zinatumia masafa ya intaneti ya Serikali kwa ajili ya kuwezesha mawasiliano;

(viii) Taasisi za Serikali 42 zimepewa ushauri na utaalamu elekezi kuhusu kubuni, kutengeneza na kusimamia mifumo na miundombinu mbalimbali ya TEHAMA kwenye Taasisi zao;

(ix) Taasisi 135 zimepatiwa ushauri kwenye maeneo mbalimbali ya utekelezaji wa Serikali Mtandao;

(x) Maafisa TEHAMA 88 kutoka Taasisi 72 za Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa walipatiwa mafunzo kuhusu uimarishaji wa usalama wa mifumo na mindombinu ya TEHAMA;

(xi) Mafunzo ya usimamizi wa taarifa za tovuti yalitolewa kwa Taasisi za Umma 69. Kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, mafunzo kuhusu usimamizi wa taarifa na huduma katika Tovuti Kuu ya Serikali yalitolewa kwa Taasisi 86;

(xii) Watumishi 36 wa Wakala wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi ndani ya nchi. Aidha, Mtumishi mmoja anahudhuria mafunzo ya muda mrefu nje ya nchi. Vilevile, viongozi 16 wa Wakala wamepatiwa mafunzo ya uongozi kwa njia ya mtandao kwa awamu tatu; na

(xiii) Mkutano wa kwanza wa mwaka wa Serikali Mtandao kwa ajili ya kuelimisha na kuhamasisha utekelezaji wa Serikali Mtandao uliokuwa na kauli mbiu ya *kuelekea matumizi ya rasilimali TEHAMA zilizoanishwa katika kutoa huduma bora kwa Umma* ulifanyika tarehe 15 Agosti, 2015.

OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

42. **Mheshimiwa Spika**, majukumu ya Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ni: Kutafuta wataalam wenye ujuzi maalum na kuandaa mfumo wa kanzidata za wataalam hao ili kurahisisha utaratibu wa ajira; kuandaa orodha ya wahitimu wa Vyuo Vikuu na wataalam wenye weledi kwa madhumuni ya kurahisisha rejea na ujazaji wa nafasi wazi za ajira katika Utumishi wa Umma; kutangaza nafasi wazi za kazi zinazotokea katika Utumishi wa Umma; kuwatumia wataalam kwa madhumuni ya kuendesha na kufanya usaili; na kuwashauri waajiri kuhusu masuala mbalimbali kuhusu mchakato wa ajira.

43. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2015/16, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma iliidhinishiwa **Shilingi 3,854,488,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi 2016, **Shilingi 1,740,140,213** zimepokelewa na kutumika.

44. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Usaili wa kujaza nafasi wazi za kazi 4,310 katika Utumishi wa Umma (nafasi mpya zikiwa 3,966 na Mbadala 344) uliendeshwa; Wasailiwa 3,509 kutoka Wizara nafasi (692), Sekretarieti za Mikoa nafasi (281), Mamlaka za Serikali za Mitaa nafasi (1,928) na Taasisi, Idara na Wakala wa Serikali nafasi 608

walipangiwa vituo. Kati ya wasailiwa 3,509 waliopangiwa vituo vya kazi, ajira mpya ni 3,284 na mbadala ni 225 na utaratibu wa kujaza nafasi 801 upo kwenye hatua mbalimbali;

(ii) Takwimu za orodha ya wahitimu toka vyuo mbalimbali zilikusanywa. Jumla ya Vyuo Vikuu 12 viliwasilisha orodha ya wahitimu wapatao 10,117;

(iii) Kwa kushirikiana na Wakala ya Serikali Mtandao mfumo wa mchakato wa Ajira wa kielektroniki uliimarishwa kwa kurekebisha mfumo;

(iv) Mikutano minne na waandishi wa habari ili kuelezea utekelezaji wa mchakato wa ajira Serikalini na kuendelea kukuza uelewa juu ya mambo mbalimbali yanayohusu ajira Serikalini ilifanyika; Uelimishwaji wananchi kuhusu mfumo wa upokeaji wa maombi kwa njia ya kielektroniki kupitia vipeperushi, tovuti, mitandao ya kijamii na njia ya ana kwa ana kwa wananchi wanaokuja moja kwa moja ofisini ulifanyika. Aidha, waajiri na wadau mbalimbali walitembelewa ili kupata mrejesho wa huduma;

(v) Watumishi 9 wamepatiwa mafunzo ya kitaaluma ya muda mfupi na wengine 10 wanapatiwa mafunzo ya Shahada ya Uzamili; na

(vi) Kushiriki kama wataalam waalikwa kwenye michakato ya usaili unaoendeshwa na Taasisi mbalimbali ambazo zinatumia sheria zao kuendesha usaili.

OFISI YA RAIS, TUME YA UTUMISHI WA UMMA

45. **Mheshimiwa Spika**, Tume ya Utumishi wa Umma ina wajibu wa kuhakikisha kuwa masuala ya Rasilimali watu katika Utumishi wa Umma yanaendeshwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu mbalimbali kwa lengo la kuimarisha utendaji unaozingatia malengo na matokeo yanayopimika. Aidha, Tume ni Mamlaka ya Rufaa kwa baadhi ya Watumishi wa Umma dhidi ya maamuzi yanayotolewa na mamlaka zao za nidhamu.

46. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2015/16 Tume iliidhinishiwa **Shilingi 11,658,277,015** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2016 **Shilingi 7,186,857,228** zilipokelewa na kutumika.

47. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Rufaa 159 zilifanyiwa uchambuzi na kutolewa uamuzi ambapo rufaa 58 zilikubaliwa, 59 zilikataliwa, 38 zilikatwa nje ya muda na 4 ziliahirishwa;

(ii) Malalamiko 95 ya watumishi yalichambuliwa na kutolewa uamuzi na maelekezo ambapo malalamiko 9 yalitolewa uamuzi na Tume na malalamiko 86 yalihitimishwa kwa kutolewa maelekezo na ufafanuzi na Sekretarieti ya Tume. Kati ya malalamiko yaliyotolewa uamuzi na Tume, 5 yalikubaliwa na 4 yalikataliwa;

(iii) Ukaguzi maalumu kuhusu rasilimali watu ulifanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe na Manispaa ya Kinondoni;

(iv) Watumishi 7 wa Tume walipewa mafunzo ya kuongeza ujuzi;

(v) Masuala ya ajira ya walimu yalishughulikiwa ambapo walimu 542 walisajiliwa, 4,647 walipandishwa vyeo, 947 walibadilishwa kazi na vibali vya kustaafu kwa walimu 463 vilitolewa;

(vi) Mashauri ya nidhamu ya walimu 120 yalitolewa uamuzi ambapo walimu 89 walifukuzwa kazi, wanne walirudishwa kazini, mashauri mawili yalifutwa na 25 yalirudishwa kwenye Kamati za Ajira za Walimu za Wilaya;

(vii) Elimu kuhusu uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu zinazosimamia masuala ya rasilimali watu ilitolewa kwa njia ya mtandao wa video kwa Sekretarieti za Mikoa 18 pamoja na Mamlaka zake za Serikali za Mitaa; na

(viii) Watumishi wanaoishi na VVU na UKIMWI wamepatiwa huduma.

OFISI YA RAIS, BODI YA MISHAHARA NA MASILAHU KATIKA UTUMISHI WA UMMA

48. **Mheshimiwa Spika**, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma ni chombo kilichoanzishwa kwa Tamko la Rais kupitia Tangazo la Serikali Na.162 la tarehe 3 Juni, 2011. Uanzishwaji wa Bodi ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Mishahara na Motisha katika Utumishi wa Umma ya Mwaka 2010. Bodi hii ina jukumu la kufanya mapitio ya mara kwa mara ya mishahara na kupendekeza viwango vya mishahara, posho na mafao katika Utumishi wa Umma kwa mamlaka husika.

49. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2015/16, Bodi kupitia Fungu 09 iliidhinishiwa **Shilingi 2,313,146,450** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2016 **Shilingi 1,443,871,555** zilipokelewa na kutumika.

50. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Tathmini ya Kazi na Uhuishaji wa Madaraja (Job Evaluation and Regrading) kwa Watumishi wa Umma imeanza na itakamilika Februari, 2017;

(ii) Rasimu ya Vigezo vya kuzingatiwa wakati wa kutoa motisha kwa Watumishi wa Umma wanaofanya kazi katika maeneo yenye mazingira magumu vimeandaliwa;

(iii) Rasimu ya Mwongozo wa kupendekeza na kupanga mishahara na masilahi katika Utumishi wa Umma imekamilika na iko katika hatua mbalimbali za maamuzi;

(iv) Maandalizi ya kutungwa kwa Sheria ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma yameanza; na

(v) Watumishi watano wamepatiwa mafunzo ambapo watumishi wanne ni ya muda mrefu na mmoja ya muda mfupi.

OFISI YA RAIS, IDARA YA KUMBUKUMBU NA NYARAKA ZA TAIFA

51. **Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Sheria ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa Na.3 ya mwaka 2002, Idara imepewa jukumu la kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu za utunzaji kumbukumbu na nyaraka katika Taasisi za Umma.

Aidha, Idara ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Kuwaenzi Waasisi wa Taifa, Sheria Na.18 ya Mwaka 2004 katika kukusanya, kutunza na kuhifadhi kumbukumbu na vitu vya Waasisi wa Taifa letu (Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume).

52. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2015/16, Fungu 04: Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, liliidhinishiwa **Shilingi 1,311,291,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,061,291,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 250,000,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2016 **Shilingi 459,007,823** zilipokelewa na kutumika kwa Matumizi ya Kawaida.

53. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Mpango Mkakati wa Idara Inayojitegemea wa kipindi cha mwaka 2016/17 hadi 2021/22 umeandaliwa kwa kufuata muundo mpya;

(ii) Kumbukumbu Tuli kutoka katika Taasisi 5 za Serikali na Makasha 1,400 kutoka Makao Makuu ya Idara yamehamishiwa katika Kituo cha Taifa cha Kumbukumbu Dodoma;

(iii) Jumla ya majalada 153,116 yaliyohifadhiwa katika makasha (*archival boxes*) 5,510 kutoka ofisi za Umma na Vituo vya Kanda vya Idara yamechambuliwa na kuhifadhiwa katika Kituo cha Taifa cha Kumbukumbu Dodoma;

(iv) Andiko la kuboresha utunzaji wa kumbukumbu za Mamlaka za Serikali za Mitaa limeandaliwa na kuwasilishwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa maamuzi;

(v) Uboreshaji wa Mfumo wa utunzaji wa kumbukumbu hai umefanyika katika Wizara ya Fedha, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa pamoja na Ofisi ya Mdhambi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

(vi) Mafunzo ya utunzaji na matumizi sahihi ya kumbukumbu na nyaraka za Serikali yametolewa kwa watumishi wa Wizara ya Maji, Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo na Wakala ya Mkemia Mkuu wa Serikali;

(vii) Mfumo wa utunzaji wa kumbukumbu (Keyword File Classification System) za kiutendaji umewekwa katika Ofisi za Tume ya Vyuo Vikuu, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii, Wakala wa Utafiti wa Majengo, Chuo cha Utalii, Mamlaka ya Usafiri wa Anga na Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha;

(viii) Vitabu vya Wilaya (District Books) vya enzi ya utawala wa Muingereza vimewekwa katika mfumo wa kidijitali;

(ix) Ukaguzi wa uhimilivu wa mfumo wa utunzaji kumbukumbu umefanyika katika Wizara zote;

(x) Mikutano kazi kuhusu Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu za utunzaji taarifa, kumbukumbu na nyaraka za Serikali imefanyika katika Wizara 4

ambazo ni Wizara ya Kilimo na Mifugo; Wizara ya Maji na Umwagiliaji; Wizara ya Ujenzi na Ofisi ya Rais –Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; na

(xi) Baadhi ya Taarifa, kumbukumbu na machapisho mbalimbali ya Waasisi wa Taifa (Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume) zimekusanywa na kuhifadhiwa.

C. MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2016/17 NA MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIWA

54. **Mheshimiwa Spika**, baada ya kutoa maelezo kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/16, sasa naomba kutoa Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17.

55. **Mheshimiwa Spika**, Mipango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17 kwa Mafungu 20; 30; 33; 06; 11; 32; 67, 94, 09 na 04 imeandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015-2020, Mwongozo wa Taifa wa Kuandaa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/17 pamoja na maeneo muhimu ya kuzingatiwa kama yalivyoainishwa na Serikali ya Awamu ya Tano kama ifuatavyo:-

OFISI YA RAIS, IKULU NA TAASISI ZAKE

(a) Ikulu

56. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17, Ofisi ya Rais, Ikulu imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kutoa huduma kwa Rais na familia yake;
- (ii) Kutoa huduma za ushauri kwa Rais katika maeneo ya Uchumi, Siasa, Masuala ya Jamii, Sheria, Mawasiliano na Habari kwa Umma, Mahusiano ya Kikanda, Kimataifa na maeneo mengine;
- (iii) Kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu kwa kushirikisha wadau wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi;
- (iv) Kuelimisha watumishi juu ya Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa na utekelezaji wa Mkakati wa Kupambana na Kujikinga na UKIMWI mahali pa kazi pamoja na kuwezesha watumishi wanaoishi na VVU na UKIMWI kupata huduma muhimu za dawa, lishe na ushauri nasaha;

(v) Kuratibu, kuandaa na kushiriki mikutano 60 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, mikutano 40 ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (IMTC) na mikutano 20 ya Baraza la Mawaziri;

(vi) Kuandaa mkutano wa tathmini wa mwaka kati ya Waratibu wa Shughuli za Baraza la Mawaziri wa Wizara, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na wadau wengine;

(vii) Kutoa mafunzo kuhusu utayarishaji na uwasilishaji wa Nyaraka za Baraza la Mawaziri na uchambuzi wa sera kwa Maofisa wa Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na Waratibu wa Shughuli za Baraza la Mawaziri wa Wizara;

(viii) Kupokea, kupitia na kuchambua rufaa na malalamiko ya watumishi wa umma na wananchi.

(ix) Kuendesha mikutano 2 ya Watendaji na Maafisa wa Serikali 100 kuhusu utaratibu wa kushughulikia malalamiko na rufaa pamoja na kufuatilia utekelezaji wa maagizo mbalimbali ya Katibu Mkuu Kiongozi;

(x) Kuratibu na kuendesha mikutano 8 ya uratibu wa Maboresho kwa Makatibu Wakuu na Waratibu wa Programu za Maboresho kwa lengo la kuimarisha usimamizi, uongozi na umilki wa mchakato wa Maboresho katika sekta ya umma nchini;

(xi) Kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Uendeshaji wa Shughuli za Serikali kwa Uwazi (OGP);

(xii) Kuratibu na kusimamia Miradi ya Maendeleo ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) na Mfuko wa Rais wa Kujitegemea;

(xiii) Kukarabati nyumba 10 za watumishi katika Ikulu Ndogo ya Chamwino na nyumba moja iliyopo Unguja;

(xiv) Kukamilisha ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano, Ikulu kwa kufunga vifaa vya mawasiliano (audio visual equipment);

(xv) Kuanza ujenzi wa jengo jipya la mapokezi upande wa baharini Ikulu; na

(xvi) Kukarabati majengo ya Ikulu Ndogo za Mwanza na Lushoto.

(b) Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU)

57. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

- (i) Kuchunguza tuhuma 3,406 zilizopo na mpya zitakazojitokeza;
- (ii) Kukamilisha uchunguzi wa tuhuma za rushwa kubwa (Grand Corruption) kama ilivyopangwa katika Mpango Mkakati wa Taasisi;
- (iii) Kuendesha kesi 578 zilizopo mahakamani na zitakazoendelea kufunguliwa kutokana na kukamilika kwa uchunguzi;
- (iv) Kubadilisha muundo wa Taasisi ili kuimarisha mfumo wa kuzuia rushwa kwa kuwa na idara kamili ya kuzuia rushwa (corruption prevention) ambapo utafiti na udhibiti utakuwa sehemu ya idara hiyo;
- (v) Kufanya utafiti wa mianya ya rushwa katika Sekta za Umma na Binafsi;
- (vi) Kuweka mikakati kwa kushirikiana na wadau ili kudhibiti mianya ya rushwa na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji;
- (vii) Kufuatilia miradi ya maendeleo katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kudhibiti ubadhirifu wa fedha za umma na kuongeza ufanisi katika utekelezaji;
- (viii) Kuhuisha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007 ili kuongeza ufanisi katika kuzuia na kupambana na makosa ya rushwa nchini;
- (ix) Kujenga uwezo na uelewa kuhusu athari za rushwa kwa makundi mbalimbali katika jamii;
- (x) Kufungua na kuimarisha Klabu za Wapinga Rushwa katika Shule za Msingi, Sekondari na Vyuho pamoja na makundi ya vijana wasio shuleni;
- (xi) Kuwahamasisha vijana wajiunge katika klabu za wapinga rushwa na kushiriki kikamilifu katika vita dhidi ya rushwa. Pia kuwafikia vijana wasiokuwa shuleni kwa njia mbalimbali kama mikutano, semina na kuwashawishi kujiunga katika vikundi;

(xii) Kuimarisha mfumo wa usimamizi na ufuatiliaji wa majalada ya uchunguzi ndani ya Taasisi ili kurahisisha na kuwezesha mtiririko mzuri wa majalada kutoka ngazi za Wilaya, Mkoa na Makao Makuu;

(xiii) Kutoa mafunzo kwenye eneo la mfumo wa takwimu kwa Watumishi wa TAKUKURU kwa ngazi za Wilaya, Mikoa na Makao Makuu; na

(xiv) Kuanza ujenzi wa jengo la ofisi la Makao Makuu ya Bodi ya Ushauri wa Masuala ya Rushwa ya Umoja wa Afrika baada ya kukamilika kwa mchakato wa umiliki wa kiwanja.

(c) Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)

58. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

(i) Kujenga uwezo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa juu ya urasimishaji wa ardhi Vijijini katika Halmashauri za Wilaya 6 za Kilwa, Biharamulo, Bukoba, Lindi, Newala na Songea. Aidha, urasimishaji wa ardhi Vijijini utafanyika katika eneo la Chanjamjawiri katika Wilaya ya Chakechake - Pemba na Mahonda katika Wilaya ya Kaskazini B Unguja. Hati za Haki Milki za Kimila 17,800 zitaandaliwa na kutolewa;

(ii) Kujenga uwezo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili urasimishaji wa ardhi mijini katika Jiji la Mbeya, Manispaa ya Sumbawanga na Mamlaka ya Mji mdogo wa Tandala katika Halmashauri ya Wilaya ya Makete. Aidha, uandaaji wa hati utakamilishwa katika miji ya Tunduma na Babati. Kwa upande wa Zanzibar, urasimishaji wa ardhi mijini utafanyika Wete - Pemba na Mjini Unguja. Jumla ya Hati Milki 10,200 zitaandaliwa na kutolewa;

(iii) Kujenga uwezo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya urasimishaji wa Biashara katika Halmashauri za Jiji la Mwanza, Manispaa za Mtwara Mikindani na Singida. Aidha, urasimishaji wa biashara utafanyika katika Wilaya za Kusini Unguja na Micheweni, Pemba ambapo jumla ya wafanyabiashara 5,000 watapata mafunzo, 4,000 watasajili biashara zao na kati yao 2,000 wataunganishwa na Taasisi za fedha kwa ajili ya kupata mikopo itakayotumika kama mtaji ya kukuza biashara zao;

(iv) Kukamilisha ujenzi wa masijala za Ardhi za Vijiji 10 katika Halmashauri za Wilaya 6 za Mbinga, Mpwapwa, Manyoni, Meru, Chamwino na Mvomero. Aidha, ujenzi wa Ofisi ya Sheha iliyoko Shehia ya Kiungoni Wete, Pemba utakamilishwa;

(v) Kutoa mafunzo kuhusu fursa na matumizi bora ya Hati za Haki Milki za Kimila kwa wakulima 750 waliorasimisha ardhi zao na viongozi 135 wa vyama vya wakulima katika Halmashauri za Wilaya 8 za Mbarali, Mwanga, Meru, Uvinza, Buhigwe, Sumbawanga, Mbinga na Singida. Aidha, Mpango Kazi wa Jamii wa Vijiji vyenye urasimishaji utatekelezwa kwa kuanzisha mashamba darasa na kuunda vikundi vya uzalishaji;

(vi) Ufuatiliaji wa tathmini ya utekelezaji wa miradi ya majaribio ya Mfuko Endelevu wa Urasimishaji wa Wilaya katika Manispaa za Morogoro na Iringa utafanyika;

(vii) Kufanya tathmini ya ukubwa wa sekta isiyo rasmi kwa sasa Tanzania Bara na Zanzibar;

(viii) Kufanya mapitio kwa lengo la kuhuisha Mkakati wa Mawasiliano ya Umma wa mwaka 2009 ili kuhuisha mkakati huo; na

(ix) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya maboresho ya sheria za ardhi na biashara katika Wizara za Kisekta.

(d) Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)

59. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

(i) Kufanya utambuzi na uandikishaji wa kaya maskini katika maeneo ya Vijiji, Mitaa na Shehia zote ambayo hayakufikiwa katika Awamu ya Kwanza. Utambuzi na uandikishaji huu unategemea kufikia jumla ya walengwa 355,000 katika jumla ya Vijiji 4,408; Mitaa 1,189 na Shehia 96;

(ii) Kuhawilisha ruzuku kwa kaya maskini zipatazo 1,400,000 katika vipindi vya mizunguko sita ya malipo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 159 za Tanzania Bara na Wilaya zote za Unguja na Pemba. Uhawilishaji wa fedha utafanywa kwa kufuata Kalenda ya Malipo kila baada ya miezi miwili;

(iii) Kuhakiki kaya zilizoandikishwa katika mpango ili kuziondoa kaya zote ambazo hazina sifa na vigezo vya umaskini uliokithiri;

(iv) Kuandikisha na kutoa ujira wa muda kwa jumla ya kaya za walengwa 348,850 ambazo zitahusika katika utekelezaji wa Mpango wa Ajira za

Muda kwa Kaya Maskini. Walengwa hawa watatoka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 42 na Wilaya zote za Unguja na Pemba;

(v) Kukamilisha Mkakati na Miongozo ya Mpango wa Kuweka Akiba na Kuwekeza kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango huo. Wawezeshaji 200 watapatiwa mafunzo ya kuunda vikundi endelevu vya kuweka akiba kwa kaya za walengwa. Jumla ya vikundi 2,600 vya walengwa wa Mpango vitaundwa na kupewa mafunzo na vitendea kazi;

(vi) Jumla ya miradi 300 itatekelezwa chini ya Mpango wa Kuendeleza Miundombinu katika sekta za afya, elimu na maji. Wafanyakazi 900 wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na kamati 300 za usimamizi za jamii watapewa mafunzo juu ya namna ya kutekeleza miradi hii;

(vii) Kuimarisha mifumo ya TEHAMA ya utunzaji wa kumbukumbu za walengwa pamoja na uendeshaji na utoaji wa taarifa ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli za Mpango hususan kuimarisha mawasiliano kati ya maeneo ya utekelezaji na TASAF Makao Makuu;

(viii) Kufanya utafiti shirikishi katika maeneo mbalimbali ya kijamii na kiuchumi ili kubaini fursa na vikwazo katika kufikia lengo la jamii kujipatia maendeleo. Hii itahusisha kukusanya takwimu katika ngazi mbalimbali za jamii;

(ix) Kujenga uwezo wa ngazi mbalimbali za utekelezaji ikiwa ni pamoja na Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na jamii ili kuweza kusimamia, kufuatilia na kutekeleza shughuli za Mpango kwa ufanisi zaidi; na

(x) Kuimarisha usimamizi, ufuatiliaji na tathmini za shughuli za Mpango pamoja na matumizi ya rasilimali na kuongeza ufanisi na uwajibikaji katika ngazi zote za utekelezaji wa Mpango. Shughuli hii itahusisha kufanya tathmini ya kwanza ya Mpango ili kupima kiwango cha utekelezaji wa malengo.

(e) Taasisi ya UONGOZI

60. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

(i) Kuanzisha Programu ya mafunzo jumuishi ya muda wa kati kwa viongozi ili kuwajengea uwezo katika maeneo ya kufanya maamuzi ya kimkakati, kusimamia rasilimali watu na rasilimali nyingine na sifa binafsi za kiongozi;

(ii) Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa Viongozi ili kuwajengea uwezo katika maeneo ya Uongozi na Maendeleo Endelevu; na Majadiliano ya Mikataba mbalimbali;

(iii) Kuandaa na kutoa mafunzo yatakayokidhi mahitaji mbali mbali ya Wizara, Idara Zinazojitegemea na Taasisi za Umma;

(iv) Kuandaa mikutano 4 ya Kikanda na Kimataifa na Mikutano 4 ya Kitaifa juu ya Uongozi na Maendeleo Endelevu;

(v) Kuandaa vipindi vya televisheni 12 vitakavyoshirikisha Wakuu wa Nchi waliopo madarakani na waliostaafu, ndani na nje ya nchi, na wataalam mbalimbali juu ya Uongozi na Maendeleo Endelevu;

(vi) Kufanya utafiti na kutoa msaada wa kitaalam katika maeneo yanayohusu Uongozi na Maendeleo Endelevu;

(vii) Kuandaa chapisho litakaloelezea maisha na uzoefu wa Kiongozi wa Kitaifa Mstaafu;

(viii) Kutekeleza Programu Jumuishi juu ya Usimamizi wa Rasilimali za Taifa hususan katika Sekta ya Mafuta, Gesi Asili na Madini kwa kufanya mafunzo, utafiti na majadiliano;

(ix) Kuanzisha Programu Jumuishi katika eneo la Maendeleo Endelevu ili kusaidia utekelezaji wa Malengo ya Kimataifa ya Maendeleo Endelevu;

(x) Kusaidia kuanzisha na kuendesha Kituo cha Tathmini kwa lengo la kuboresha mfumo wa uteuzi wa viongozi katika Utumishi wa Umma;

(xi) Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa Watumishi wa Taasisi ili kukuza ufanisi wa kiutendaji; na

(xii) Kuratibu uwekaji wa miundombinu ya barabara, maji na umeme na kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa Taasisi ya Uongozi Kijiji cha Kondo, Bagamoyo.

(f) Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF)

61. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea umepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kutoa mikopo na kukusanya marejesho ya mikopo kutoka kwa walengwa ambao ni Vijana na Wanawake Wajasiriamali waliohitimu Vyuvo vya Ufundi Stadi vinavyotambuliwa na VETA na SIDO katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Njombe na Lindi;

(ii) Kuanzisha tawi la kutoa huduma za Mfuko katika Mkoa wa Lindi;

(iii) Kujenga uwezo wa walengwa katika kukuza mitaji yao na ushirikishaji wa wajasiriamali na jamii inayowazunguka;

(iv) Kuendelea kujenga uwezo wa watendaji ili kutoa huduma bora kwa wateja; na

(v) Kufanya utafiti wa huduma kwa walengwa.

62. **Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha wa 2016/17, Fungu 20 Ofisi ya Rais, Ikulu inaomba **Shilingi 14,962,054,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Aidha, Fungu 30: Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri inaomba **Shilingi 793,164,600,000**. Kati ya fedha hizi **Shilingi 362,715,571,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 430,449,029,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

63. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kama ifuatavyo:

(i) Kuchapisha, kutuma na kupokea Tamko la Viongozi wa Umma kuhusu Rasilimali na Madeni linalopaswa kutolewa kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya mwaka 1995;

(ii) Kufanya uhakiki wa matamko ya Rasilimali na Madeni kwa Viongozi wa Umma 500;

(iii) Kupokea na kushughulikia malalamiko na taarifa kutoka kwa wananchi kuhusu ukiukwaji wa maadili kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma wa Umma;

(iv) Kuchunguza tuhuma dhidi ya Viongozi wa Umma kuhusu ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi;

(v) Kuratibu na kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Baraza la Maadili ya Viongozi wa Umma;

(vi) Kuelimisha Viongozi wa Umma na wananchi kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na hati ya Ahadi ya Uadilifu;

(vii) Kuandaa Taarifa ya mwaka ya Utekelezaji wa shughuli za Sekretarieti na kuiwasilisha kwenye Mamlaka husika;

(viii) Kufanya utafiti kuhusu hali ya uadilifu kwa Viongozi wa Umma;

(ix) Kukamilisha ujenzi wa jengo la Ofisi ya Sekretarieti ya Maadili Kanda ya Kusini Mtwara;

(x) Kuanza ujenzi wa Ofisi ya Sekretarieti Kanda ya Kati Dodoma; na

(xi) Kufanya usanifu wa Jengo la Ofisi ya Sekretarieti Makao Makuu.

64. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17, Fungu 33: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma inaomba kuidhinishiwa **Shilingi 5,913,820,000**. Kati ya fedha hizi **Shilingi 4,913,820,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 1,000,000,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

OFISI YA RAIS, UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MIRADI

65. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17, Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi itatekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kusimamia utekelezaji wa vituo 53,182 vya maji vitokanavyo na miradi mipya ya vyanzo vya maji na kufanya ukarabati wa miradi ya zamani ili kuongeza vyanzo vya maji. Vilevile, kutoa elimu ya uendeshaji kwa Kamati za Maji za Mikoa 26;

(ii) Kufuatilia ukamilishaji wa ujenzi wa skimu 40 za umwagiliaji;

(iii) Kufuatilia ukamilishaji wa maghala 207 kwa ajili ya kuhifadhi mazao;

(iv) Kufuatilia utekelezaji wa mpango wa mashamba makubwa 25 ya kilimo cha biashara;

(v) Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi mikubwa ya njia za umeme za Makambako – Songea, Singida - Arusha, North East Grid, Geita - Nyakanazi na Somanga – Kinyerezi;

(vi) Kufuatilia utekelezaji wa miradi ya umeme ya Wakala ya Umeme Vijijini na Programu nyingine za nishati;

(vii) Kufuatilia utekelezaji wa maamuzi yenye lengo la kuongeza ufanisi wa bandari, reli na barabara za Ukanda wa Kati wa Uchukuzi;

(viii) Kufanya ufuatiliaji kuhusu utendaji wa Shirika la Reli ili kuhakikisha kuwa Vigezo vya Utendaji vilivyowekwa katika maabara vinafikiwa;

(ix) Kufuatilia na kutoa ushauri katika maandalizi ya kutunga Sheria ya Usalama Barabarani;

(x) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo kupitia mfumo wa uthamini wa mkupuo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa yaliyoainishwa katika maabara ya ukusanyaji wa mapato;

(xi) Kutoa mafunzo ya ukusanyaji wa mapato kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuanzia na Mikoa ya Mtwara, Mwanza na Morogoro;

(xii) Kuwezesha ushiriki wa Sekta Binafsi kwenye miradi ya vipaumbele ili kuunga mkono juhudi za Serikali za kuongeza fedha kwenye miradi ya maendeleo;

(xiii) Kufuatilia utekelezaji wa mkakati wa kuhakikisha asilimia 80 ya Vituo vya Afya na Zahanati vinakuwa na hadhi sio chini ya Nyota Tatu ifikapo Juni 2018;

(xiv) Kufuatilia utekelezaji wa mkakati wa kupunguza vifo vya akina mama na watoto kwa asilimia 20, kutoka watoto 54 kati ya 1,000 na kina mama 410 kati ya 100,000 wanaokufa kwa kuanzia na Mikoa ya Mwanza, Geita, Kigoma, Mara na Simiyu ifikapo June 2018; na

(xv) Kutoa mafunzo yanayolenga kupunguza matukio ya uhalifu kwa asilimia 10, kutoka matukio 32 kati ya watu 10,000 hadi matukio 22 na kufuatilia utekelezaji katika Mikoa ya Kipolisi ya Ilala, Temeke, Mwanza na Arusha.

66. **Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha wa 2016/17 Fungu 06: Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi inaomba kuidhinishiwa **Shilingi 27,616,107,000**. Kati ya fedha hizi **Shilingi 397,278,000** kwa

ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 27,218,829,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

OFISI YA RAIS, USHAURI WA MAFUTA NA GESI

67. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Ushauri wa Mafuta na Gesi imeanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 7 cha Sheria ya Petroli ya mwaka 2015. Chombo hiki ni cha Taifa chenye jukumu la kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu uchumi wa mafuta na gesi kwa Baraza la Mawaziri.

68. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

(i) Kutoa ushauri wa kitaalam kwa Baraza la Mawaziri katika masuala yanayohusu uchumi wa mafuta na gesi zikiwemo Sera za Kisekta, Sera ya Uwekezaji, Sheria na Kanuni zinazohusu masuala ya uchumi wa mafuta na gesi na mambo mengine yanayohusiana na uchumi wa mafuta na gesi;

(ii) Kuchambua tafiti mbalimbali za mafuta na gesi na kulishauri Baraza la Mawaziri ili kuchochea maendeleo endelevu kwa faida ya Watanzania wote;

(iii) Kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu aina ya utaalum utakaohusika kwenye majadiliano ya mikataba, ukubwa wa timu, mikakati na mbinu zitakazotumika na kushiriki kama waangalizi katika majadiliano ya uwekezaji wa kimkakati katika sekta ya mafuta na gesi; na

(iv) Kuanzisha shughuli za uendeshaji wa ofisi na kuwajengea uwezo wataalam wa ushauri wa mafuta na gesi kwa kuwapa mafunzo nje na ndani ya nchi.

69. Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha wa 2016/17, Fungu 11: Ofisi ya Rais, Ushauri wa Mafuta na Gesi inaomba kuidhinishiwa **Shilingi 1,036,239,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA WAKALA ZILIZO CHINI YAKE

(a) Menejimenti ya Utumishi wa Umma

70. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuhakikisha kuwa Utumishi wa Umma unaendeshwa kwa kuzingatia

misingi ya utawala bora na kwamba Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu mbalimbali zinazingatiwa.

71. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma itahakikisha kuwa Watumishi wa Umma wanakuwa waadilifu wenye kuwajibika na kuwa na staha na usikivu kwa wananchi wanapotoa huduma kwa haraka. Majukumu haya yatafikiwa kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kuanza maandalizi ya kutungwa kwa Sheria ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma;

(ii) Kujenga uwezo wa Serikali katika kuratibu uchambuzi wa Sera mbalimbali ili zilete maendeleo kutokana na kuwianishwa kwake;

(iii) Kuhuisha Miundo na Mgawanyo wa Majukumu ya Taasisi za Serikali kulingana na mahitaji ya Serikali ya Awamu ya Tano ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa wananchi;

(iv) Kuboresha michakato ya utoaji huduma na kuimarisha usimamizi wa mfumo na viwango vya utendaji kazi kwa kufanya ufuatiliaji wa karibu na kutoa ushauri wa kitaalam katika Taasisi za Serikali;

(v) Kufanya tathmini ya utendaji kazi wa Wakala za Serikali ili kubaini ufanisi na changamoto za uendeshaji wake;

(vi) Kutoa huduma kwa Viongozi Wastaafu wa Kitaifa na Wajane wa Viongozi 16. Aidha, kukamilisha ujenzi wa nyumba ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili na kuanza ujenzi wa nyumba ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne;

(vii) Kuratibu mapendekezo ya kuboresha mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ili kuishauri Serikali kuhusu mfumo madhubuti uliooanishwa ili kurahisisha upatikanaji wa matokeo yatakayosaidia kufanya maamuzi na kuboresha Sera na Mikakati ya Serikali kwa ujumla;

(viii) Kuratibu fursa za mafunzo mbalimbali yanayofadhiliwa na Wadau wa Maendeleo kupitia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kuzingatia tija na vipaumbele vya Taifa;

(ix) Kukamilisha Mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Mafunzo katika Utumishi wa Umma ya mwaka 2012;

(x) Kufuatilia na kuziwezesha Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali kuandaa na kutekeleza Mipango ya Mafunzo, Urithishanaji Madaraka na maendeleo ya Rasilimali watu;

(xi) Kushiriki katika mikutano ya Kikanda na Kimataifa ili kujadili na kubadilishana uzoefu wa kuboresha Utumishi wa Umma wa Nchi wanachama;

(xii) Kuanzisha utaratibu maalum wa tathmini kwa ajili ya kuandaa viongozi katika Utumishi wa Umma ili kuwa na utaratibu bora zaidi wa kuwabaini na kuwafanyia tathmini watumishi waandamizi kabla ya kuteuliwa katika nafasi za uongozi;

(xiii) Kuandaa na kutoa Mwongozo wa kutolea taarifa ya hali halisi na maoteo ya upatikanaji wa rasilimali watu katika Utumishi wa Umma;

(xiv) Kuanza maandalizi ya kutunga Sera ya Serikali Mtandao na Mkakati wake wa utekelezaji;

(xv) Kuanza kutumia muundo wa Kitaasisi wa utekelezaji wa TEHAMA Serikalini;

(xvi) Kufanya vikao vya kazi na Sekretarieti za Mikoa yote na Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia njia ya Video;

(xvii) Kukamilisha uandaaji wa Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao na kusimamia utekelezaji wake;

(xviii) Kuendelea kuratibu Programu ya Miundombinu ya Mawasiliano ya Kikanda, kwa Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika 'Regional Communication Infrastructure Programme' (RCIP) katika eneo la Serikali Mtandao;

(xix) Kugatua usimamizi wa Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara; usanifu wa mfumo utafanyika na kuongeza moduli inayoweza matumizi ya Mfumo katika sekta za Elimu, Afya, Kilimo na Mifugo;

(xx) Kutoa mafunzo ya matumizi ya Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara kwa watumiaji 200 wa Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(xxi) Kusimamia ajira na upandishaji vyeo kwa Watumishi wa Umma kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17;

(xxii) Kusimamia na kudhibiti mishahara hewa katika Utumishi wa Umma kupitia Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara;

(xxiii) Kuchambua na kuhakiki madai ya malimbikizo ya Mishahara ya Watumishi wa Umma;

(xxiv) Kufanya ufuatiliaji wa Uzingatiaji wa Maadili na Ahadi ya Uadilifu katika Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali 20, Sekretarieti ya Mkoa moja na Mamlaka za Serikali za Mitaa saba;

(xxv) Kuhuisha Kanuni za Maadili ya Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma za mwaka 2005;

(xxvi) Kutoa Mafunzo ya Maadili ya Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma;

(xxvii) Kuwezesha uanzishwaji na uimarishaji wa Mfumo wa Kushughulikia Malalamiko kwenye Hospitali za Mikoa ya Lindi na Mtwara;

(xxviii) Kuratibu, kusimamia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mwongozo wa Anuai za Jamii pamoja na Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa kwenye Wakala 20 za Serikali;

(xxix) Kufuatilia utekelezaji wa Mwongozo wa Huduma kwa Watumishi wa Umma Wenye Ulemavu wa mwaka 2008 kwenye Wizara zote na Wakala 37 za Serikali;

(xxx) Kujenga uelewa wa Mfumo wa Mikataba ya Utendaji Kazi kwa Viongozi wa Kiasia na Watendaji Wakuu wa Taasisi za Umma;

(xxxi) Kuweka mazingira wezeshi kwa Majopo ya Kitaalam na Menejimenti za Wizara; Idara Zinazojitegemea; Wakala za Serikali; Sekretarieti za Mikoa; Mamlaka za Serikali za Mitaa; Taasisi za Umma;

(xxxii) Kuzijengea uwezo Wizara; Idara Zinazojitegemea; Wakala za Serikali; Sekretarieti za Mikoa; Mamlaka za Serikali za Mitaa; na Taasisi za Umma juu ya uandaaji na utekelezaji wa Mikataba ya Utendaji Kazi; na

(xxxiii) Kuandaa Mfumo utakaowezesha kuwapatia makazi ya gharama nafuu Watumishi wa Umma.

(b) Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania

72. **Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 kimepanga kutekeleza yafuatayo:

(i) Kutoa mafunzo ya kujiandaa kufanya Mithani ya Utumishi wa Umma kwa Watumishi 1,210;

(ii) Kutoa mafunzo ya Uongozi, Menejimenti na Usimamizi wa ofisi kwa Watumishi wa Umma 3,400;

(iii) Kutoa mafunzo ya awali katika Utumishi wa Umma kwa Watumishi wa Umma 5,000;

(iv) Kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa washiriki 21,586 katika fani za Utunzaji wa Kumbukumbu, Uhazili, Kompyuta, Utunzaji wa Fedha za Umma, na Menejimenti ya Rasilimali watu, Usimamizi wa Manunuzi ya Umma, Uongozi na Utawala Bora;

(v) Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Taasisi za Umma 30;

(vi) Kufanya utafiti katika maeneo manne yanayolenga kuboresha Utumishi wa Umma;

(vii) Kuandaa machapisho mbalimbali kama vile majarida, vitabu, na makala za kitaalamu katika Utumishi wa Umma katika nyanja za Uongozi, Menejimenti na Utawala; na

(viii) Kukamilisha Awamu ya Pili ya ujenzi wa jengo la ghorofa tatu katika kampasi ya Tabora.

(c) Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao

73. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2016/17, Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao inatarajia kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kutoa mafunzo kwa Washiriki 1,800 katika maeneo ya Uongozi, Utawala Bora, Maadili, Anuai za Jamii, Mazingira, Kupunguza Umaskini na Afya;

(ii) Kuongeza ushirikiano na Taasisi za ndani na nje ya nchi ili kutoa mafunzo kwa kutumia teknolojia ya kisasa na kwa gharama nafuu;

(iii) Kukuza mtandao wa Wakala kikanda ili kuwafikia wateja walioko nchini;

(iv) Kujenga uwezo wa watumishi wa Wakala ili kukidhi ongezeko la wateja na mabadiliko ya haraka ya teknolojia sambamba na kuwezesha kuendesha mikutano na mafunzo kwa njia ya video katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala, Taasisi za Umma, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na jamii kwa ujumla;

(v) Kuratibu mikutano ya kazi ya Wizara, Idara Zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa, Wakala za Serikali na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kutumia huduma ya daraja-video (bridging services) na kutoa ushauri wa kitaalamu; na

(vi) Kufanya utafiti na majaribio ya teknolojia rafiki katika nyanja za mawasiliano na mafunzo ili kuziboresha.

(d) Wakala ya Serikali Mtandao

74. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2016/17, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

(i) Kumaliza Ujenzi wa Vituo viwili vya Kuhifadhi Taarifa na Mifumo ya TEHAMA ya Serikali na Kujikinga na Majanga (Government Data Centres) ulioanza kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha wa 2014/15. Vituo hivi vitafanya kazi sambamba na Kituo cha Taifa (National Data Centre);

(ii) Kuunganisha Taasisi za Umma 100 kwenye Mfumo wa Pamoja na Salama wa Barua Pepe wa Serikali (Government Mailing System);

(iii) Kuoanisha mifumo ya TEHAMA ya kimkakati na ya kisekta kwa kutumia Viwango na Miongozo ya TEHAMA na kutengeneza Mfumo wa Kuwezesha Ubadilishanaji Taarifa ili kuondoa urudufu, kupunguza gharama na kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa kwa umma na kuhakikisha usalama wa mawasiliano;

(iv) Kuboresha matumizi ya pamoja ya Miundombinu na Mifumo ya TEHAMA (Rasilimali Shirikishi za TEHAMA) kwa kuongeza matumizi ya Miundombinu ya TEHAMA iliyopo. Rasilimali hizo ni pamoja na Mtandao wa Mawasiliano Serikalini (Government Network), Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (National Information Communication Technology Backbone), Mfumo Unaorahisisha Utoaji wa Huduma kwa Kutumia Simu za Mkononi (Mobile

Platform) na Vituo vya Kuhifadhi Taarifa na Mifumo ya TEHAMA ya Serikali (Data Centres). Lengo ni kuhakikisha Taasisi za Umma 100 zinatumiya rasilimali hizi pamoja na kuongeza huduma za Serikali zinazotolewa kupitia miundo mbinu hii;

(v) Kushiriki kutengeneza na kuboresha Mifumo ya TEHAMA ya Kimkakati kwa lengo la kuboresha utendaji kazi na utoaji huduma ndani ya Serikali katika Sekta za Fedha, Rasilimali watu, Makusanyo ya Mapato ya Serikali, Ardhi, Utambulisho wa Taifa;

(vi) Kutengeneza Mifumo ya TEHAMA itakayowezesha Viongozi Wakuu na Watendaji wa Serikali kufuatilia na kutathmini utendaji kazi Serikalini;

(vii) Kuziwezesha Taasisi za Umma 100 kutoa huduma tatu kwa kutumia TEHAMA kwa kushirikiana na Sekta Binafsi, Taasisi za utafiti na elimu ya juu;

(viii) Kutoa mafunzo ya Serikali Mtandao ili kuongeza uelewa na uwezo wa Taasisi za Umma katika kutumia TEHAMA, kuongeza ufanisi wa kiutendaji na utoaji wa huduma kwa wananchi, Viongozi, Wasimamizi wa TEHAMA na watumiaji wa huduma za Serikali Mtandao kwa Taasisi 100; na

(ix) Kuwajengea uwezo watumishi 80 wa Wakala.

75. **Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha wa 2016/17 kwa ufanisi, Fungu 32: Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma inaomba **Shilingi 30,341,137,000**. Kati ya fedha hizi **Shilingi 22,791,137,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 7,550,000,000** kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo.

OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

76. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kusimamia na kuendesha mchakato wa ajira ili kuwezesha waajiri kupata watumishi wenye sifa zinazotakiwa kwa mujibu wa miundo ya utumishi husika;

(ii) Kuendesha mchakato wa ajira kwa nafasi wazi za kazi katika Utumishi wa Umma;

(iii) Kuimarisha Kanzidata za wahitimu kutoka Vyuo mbalimbali na kutunza takwimu kwa urahisi wa rejea;

(iv) Kufanya utafiti kwa waajiri na wadau mbalimbali ikiwa ni hatua ya kupata mrejesho wa utekelezaji wa shughuli za uendeshaji wa michakato ya ajira pamoja na utendaji wa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;

(v) Kuhuisha mfumo wa kielektroniki wa maombi ya kazi (recruitment portal) ili uwasiliane na mifumo mingine ikiwemo HCMIS chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mfumo wa udahili wa wanachuo chini ya Tume ya Vyuo Vikuu. Aidha, huu utawezesha kuwasiliana na Mfumo wa kuhifadhi matokeo ya Kidato cha Nne na Sita chini ya Baraza la Mitihani Tanzania, Mfumo wa utambuzi chini ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, Mfumo wa Usajili wa Vizazi na Vifo chini ya Wakala wa Udhamini na Ufilisi. Vilevile utaweza kuwasiliana na Mfumo wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa kupitia Mfumo wao wa kufuatilia madeni ya wanafunzi waliofadhiliwa na Serikali, kwa lengo la kuwapata watumishi wenye sifa Serikalini;

(vi) Kufungua Ofisi ya Sekretarieti ya Ajira Zanzibar ili kurahisisha mchakato wa ajira kwa ajira za Muungano na kuimarisha uhusiano wa kiutendaji;

(vii) Kwa kushirikiana na Wakala ya Serikali Mtandao, kuendelea kuboresha na kuimarisha mfumo wa kielektroniki wa kuendesha mchakato wa ajira na utunzaji kumbukumbu za wasailiwa na wataalam mbalimbali;

(viii) Kushiriki kama Wataalam waalikwa kwenye usaili unaoendeshwa na Taasisi zinazotumia Sheria zilizokasimiwa kwao;

(ix) Kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani ya nchi kwa watumishi watano; na

(x) Kuboresha mifumo ya uendeshaji wa usaili kwa kutumia mbinu za kisasa, ikiwemo matumizi ya "psychometric test".

77. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17, Fungu 67: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma inaomba kuidhinishiwa **Shilingi 2,205,404,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

OFISI YA RAIS, TUME YA UTUMISHI WA UMMA

78. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kuratibu mikutano ya kisheria ya kila robo mwaka ya Tume na kutoa uamuzi kwa Ruffaa, Malalamiko na masuala mengine ya kiutumishi kadiri yatakavyopokelewa;

(ii) Kufanya ukaguzi wa kawaida kwa Taasisi 40 (Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu) na ukaguzi maalum kwa taasisi 10 ili kuangalia uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu za Usimamizi wa Rasilimali watu katika Utumishi wa Umma;

(iii) Kuelimisha wadau kupitia Mikutano ya kazi, ziara za viongozi, vyombo vya habari, machapisho na tovuti kuhusu utekelezaji wa Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu zinazosimamia Utumishi wa Umma;

(iv) Kutoa elimu kwa watumishi wa Tume kuhusu maadili ya kazi na kujiepusha na mazingira hatarishi ya maambukizi ya VVU, UKIMWI, Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa na mapambano dhidi ya rushwa; na

(v) Kuwajengea uwezo watumishi 30 wa Tume kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika utunzaji kumbukumbu na ukatibu muhtasi ili kuwaongezea ujuzi na ufanisi katika kutekeleza majukumu ya Tume.

79. **Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha wa 2016/17, Fungu 94: Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma inaomba kuidhinishiwa **Shilingi 3,717,876,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

OFISI YA RAIS, BODI YA MISHAHARA NA MASILAHU KATIKA UTUMISHI WA UMMA

80. **Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2016/17, Bodi ya Mishahara na Masilaha katika Utumishi wa Umma inatarajia kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kukamilisha Tathmini ya Kazi na Uhuishaji Madaraja (Job-evaluation and Regrading) kwa Watumishi wa Umma;

(ii) Kufanya utafiti kwa ajili ya kuandaa Mfumo wa Utoaji Motisha kwa kuzingatia utendaji wenye tija; na

(iii) Kukamilisha Mwongozo wa Kupendekeza na Kupanga Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma.

81. **Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha wa 2016/17, Fungu 09: Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma inaomba kuidhinishiwa **Shilingi 1,859,845,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

OFISI YA RAIS, IDARA YA KUMBUKUMBU NA NYARAKA ZA TAIFA

82. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17, Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa itatekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kuandaa na kuanzisha mfumo wa kielektroniki wa utunzaji, usimamizi na matumizi ya kumbukumbu katika Taasisi za Umma;

(ii) Kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu na vitu vya Waasisi wa Taifa kwa ajili ya kuhifadhi historia ya nchi yetu;

(iii) Kujenga uwezo wa Taasisi za umma katika usimamizi na utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka kwa kuendesha mafunzo na mikutano kazi kwa watumishi wa Umma;

(iv) Kukagua, kuchambua na kuhamisha kumbukumbu tuli kutoka katika Ofisi za Kanda za Idara na Taasisi za umma kwenda Kituo cha Taifa cha Kumbukumbu Dodoma;

(v) Kusaidia Taasisi za Umma kutengeneza Miongozo ya kuhifadhi kumbukumbu hai na kuteketeza kumbukumbu zisizo na umuhimu kwa matumizi ya baadaye;

(vi) Kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya utunzaji wa taarifa, kumbukumbu na nyaraka katika Taasisi za umma;

(vii) Kukusanya taarifa na machapisho mbalimbali yanayohusu historia ya nchi yetu kutoka katika Taasisi za umma na watu binafsi;

(viii) Kuhuisha mifumo ya utunzaji kumbukumbu katika Wizara ili kuendana na mabadiliko ya Miundo ya Wizara katika Serikali ya Awamu ya Tano;

(ix) Kuweka mifumo ya utunzaji kumbukumbu katika Mikoa mipya ya Songwe na Katavi; Wilaya mpya za Kigamboni, Ubungo, Tanganyika, Kibiti na Malinyi; Mamlaka za Serikali za Mitaa za Chalinze, Ifakara pamoja na Mamlaka za Miji Midogo ya Buchosa, Malinyi, Madaba, Manyoni na Mpingwe;

(x) Kukusanya nyaraka za kidiplomasia kutoka Wizara ya Mambo ya Nje, Afrika Mashariki, Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa na katika Balozi zetu nje ya nchi;

(xi) Kukamilisha ujenzi wa jengo la Ofisi, Kanda ya Ziwa Mwanza; na

(xii) Kuendelea kukuza uhusiano wa kitaaluma na nchi rafiki na Taasisi za Kimataifa (ESARBICA, ICA na AAPAM).

83. Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha wa 2016/17, Fungu 04: Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa inaomba kuidhinishiwa **Shilingi 1,293,851,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

MAJUMUISHO

84. Mheshimiwa Spika, uchumi imara na endelevu katika nchi yoyote unahitaji uwepo wa Utumishi wa Umma uliotukuka unaozingatia utawala bora, utawala wa Sheria, maadili na mifumo thabiti ya usimamizi wa utekelezaji. Ofisi ya Rais, Ikulu; Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji wa Utekelezaji Miradi ya Maendeleo; Ofisi ya Rais, Ushauri wa Mafuta na Gesi; Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma; Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma; Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma; na Ofisi ya Rais, Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa; kisheria ndizo zenye dhamana ya kuhakikisha kuwa majukumu hayo muhimu yanatekelezwa.

85. Mheshimiwa Spika, Mipango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2016/17 ya Mafungu haya imezingatia dhamana hiyo ambayo imebeba vizuri dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuleta mabadiliko makubwa katika Utumishi wa Umma kwa kuimarisha uwajibikaji na uadilifu. Utekelezaji wa dhamira hiyo utasaidia kujenga Utumishi wa Umma uliotukuka kwa kuondokana na matumizi mabaya ya madaraka, kuondoa ukiukwaji wa maadili ya uongozi na Utumishi wa Umma, kuondokana na ucheleweshwaji wa maamuzi, kutokusimamia kwa uwazi na kutokuwajibika kwa Viongozi na Watumishi wa Umma katika kutekeleza majukumu yao.

86. **Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma imelenga kuwa na Utumishi wa Umma unaotoa huduma bora kwa staha na haraka kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu; na kwa kutumia mifumo ya elektroniki katika kuboresha utoaji wa huduma hizo. Aidha, imelenga kujenga Utumishi wa Umma ambao ni mwepesi kusikiliza malalamiko ya wananchi na kuyatafutia ufumbuzi. Utumishi wa Umma unaotoka ofisini na kwenda kuwasikiliza na kuwahudumia wananchi mahali waliko. Utumishi wa Umma unaotumia njia za kielektroniki kuboresha utoaji wa huduma. Utumishi wa Umma wenye masilahi yaliyowianishwa kwa kuzingatia uzito wa kazi na majukumu yanayofanana na unaofuatilia kwa makini miradi ya kimkakati katika vipaumbele vya Taifa. Lengo ni kuiwezesha nchi yetu kujenga uchumi wa viwanda na maendeleo ya wananchi kwa kuboresha huduma zitolewazo na Utumishi wa Umma ili kuiwezesha nchi yetu kufikia Uchumi wa Kati ifikapo 2025.

87. **Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza kwa kina utekelezaji wa majukumu kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/16 na mipango na bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha wa 2016/17, naomba kuwasilisha maombi ya fedha kwa muhtasari kama ifuatavyo:-

a. Fungu 20: Ofisi ya Rais, Ikulu

Matumizi ya Kawaida	Sh.	<u>14,962,054,000</u>
Jumla	Sh.	14,962,054,000

b. Fungu 30: Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri

i. Matumizi ya Kawaida	Sh.	362,715,571,000
ii. Matumizi ya Miradi ya Maendeleo	Sh.	<u>430,449,029,000</u>
Jumla	Sh.	793,164,600,000

c. Fungu 33: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma

i. Matumizi ya Kawaida	Sh.	4,913,820,000
------------------------	-----	---------------

ii. Matumizi ya Miradi ya Maendeleo	Sh.	<u>1,000,000,000</u>
Jumla	Sh.	5,913,820,000
d. Fungu 06: Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi		
i. Matumizi ya Kawaida	Sh.	397,278,000
ii. Matumizi ya Miradi ya Maendeleo	Sh.	<u>27,218,829,000</u>
Jumla	Sh.	27,616,107,000
e. Fungu 11: Ofisi ya Rais, Ushauri wa Mafuta na Gesi		
Matumizi ya Kawaida	Sh.	<u>1,036,239,000</u>
Jumla	Sh.	1,036,239,000
f. Fungu 32: Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma		
i. Matumizi ya Kawaida	Sh.	22,791,137,000
ii. Matumizi ya Miradi ya Maendeleo	Sh.	<u>7,550,000,000</u>
Jumla	Sh.	30,341,137,000
g. Fungu 67: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma		
Matumizi ya Kawaida	Sh.	<u>2,205,404,000</u>
Jumla	Sh.	2,205,404,000

h. Fungu 94: Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma

Matumizi ya Kawaida	Sh.	<u>3,717,876,000</u>
Jumla	Sh.	3,717,876,000

i. Fungu 09: Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma

Matumizi ya Kawaida	Sh.	<u>1,859,845,000</u>
Jumla	Sh.	1,859,845,000

j. Fungu 04: Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa

Matumizi ya Kawaida	Sh.	<u>1,293,851,000</u>
Jumla	Sh.	1,293,851,000

a. Fungu 20: Ofisi ya Rais, Ikulu

Matumizi ya Kawaida	Sh.	<u>14,962,054,000</u>	
Jumla	Sh.		4,962,054,000

b. Fungu 30: Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri

i. Matumizi ya Kawaida	Sh.	362,715,571,000	
ii. Matumizi ya Miradi ya Maendeleo	Sh.	<u>430,449,029,000</u>	
Jumla	Sh.		793,164,600,000

c. Fungu 33: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma

i. Matumizi ya Kawaida	Sh.	4,913,820,000	
ii. Matumizi ya Miradi ya Maendeleo	Sh.	<u>1,000,000,000</u>	
Jumla	Sh.		5,913,820,000

d. Fungu 06: Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi

i. Matumizi ya Kawaida	Sh. 397,278,000		
ii. Matumizi ya Miradi ya Maendeleo	Sh. <u>27,218,829,000</u>		
Jumla		Sh.	27,616,107,000

e. Fungu 11: Ofisi ya Rais, Ushauri wa Mafuta na Gesi

Matumizi ya Kawaida	Sh. <u>1,036,239,000</u>		
Jumla		Sh.	1,036,239,000

f. Fungu 32: Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma

i. Matumizi ya Kawaida	Sh. 22,791,137,000		
ii. Matumizi ya Miradi ya Maendeleo	Sh. <u>7,550,000,000</u>		
Jumla		Sh.	30,341,137,000

g. Fungu 67: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma

Matumizi ya Kawaida	Sh. <u>2,205,404,000</u>		
Jumla		Sh.	2,205,404,000

h. Fungu 94: Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma

Matumizi ya Kawaida	Sh. <u>3,717,876,000</u>		
Jumla		Sh.	3,717,876,000

i. Fungu 09: Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma

Matumizi ya Kawaida	Sh. <u>1,859,845,000</u>		
Jumla		Sh.	1,859,845,000

j. Fungu 04: Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa

Matumizi ya Kawaida	Sh. <u>1,293,851,000</u>		
Jumla		Sh.	1,293,851,000

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

MWENYEKITI: Hatua inayofuata sasa, nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa iliyochambua makadirio ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Atafanya hivyo kwa kuwasilisha taarifa ya Kamati kwa TAMISEMI, atamaliza ndani ya muda usiozidi dakika 30, atawasilisha tena Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora kwa muda huo huo usiozidi dakika 30. Mwenyekiti!

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS, UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI

MHE. JASSON S. RWEIKIZA -MWENYEKITI WA KAMATI YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya ofisi hiyo, kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utangulizi; kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2015/2016, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Bunge imeweka sharti kwa Kamati za kisekta ikiwemo hii kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ilifanya ziara za ukaguzi katika miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na kuchambua bajeti ya ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, inahusisha jumla ya mafungu 28. Fungu 56 -Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Fungu 2- Tume ya Utumishi wa Walimu pamoja na mafungu 26 ya Mikoa ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla maelezo ya utangulizi yanatuelekeza katika mambo manne ambayo taarifa hii itajikita katika kutoa ufafanuzi wake. Maeneo hayo ni haya yafuatayo:

- (i) Matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotembelewa na Kamati;
- (ii) Mapitio ya taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti wa mwaka 2015/2016;

(iii) Uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na maoni na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Mweyekiti, matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Ofisi ya Rais, TAMISEMI (Fungu 56) iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 354.5 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Pia mafungu ya Mikoa 25, kila moja lilidhinishiwa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Miongoni mwa miradi hiyo iliyotekelezwa ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI (Fungu 56) ni hii ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi namba 6403 unaojulikana kama Programu ya Uendelezaji Miji ya Mikoa ya Tanzania (*Tanzania Strategic Cities Program*), uliidhinishiwa jumla ya Shilingi bilioni 2.2 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wake. Mradi huu uliopangwa kutekelezwa chini ya kifungu 205 (*Urban Development Division*) cha Fungu 56 unahusika na uratibu na usimamizi wa uendelezaji wa miundombinu katika Miji Mikakati. Fedha iliyotengwa ililenga kuwezesha usimamizi na uratibu wa utekelezaji wa miradi hiyo katika Miji saba, ambayo ni Arusha, Mwanza, Mbeya, Tanga, Dodoma, Mtwara-Mikindani na Kigoma-Ujiji, pamoja na Makao Makuu CDA-Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi namba 6403 uliojulikana kama *Tanzania Strategic Cities Project* uliopangwa kutekelezwa chini ya kifungu 8091, Mamlaka ya Serikali za Mitaa cha Fungu 74, Mkoa wa Kigoma uliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 1.52. Mradi huu ulilenga kuboresha miundombinu ya barabara kwa kujenga barabara kwa kiwango cha lami ngumu, taa za barabarani, kujenga vituo vya mabasi na kituo cha kukusanyia taka ngumu katika Halmashauri ya Manispaa ya Mji wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mradi namba 6403 uliojulikana kama *Tanzania Strategic Cities Project* uliopangwa kutekelezwa chini ya kifungu 8091, Mamlaka ya Serikali za Mitaa cha Fungu 81, Mkoa wa Mwanza uliidhinishiwa shilingi bilioni 1.15 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi yake. Mradi huu ulilenga kuboresha miundombinu ya barabara kwa ujenzi wa kiwango cha lami ngumu, taa za barabarani pamoja na ujenzi wa mifereji ya majitaka katika Jiji la Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mwingine ni namba 3280 ujulikanao kama *Rural Water Supply and Sanitation* uliopangwa kutekelezwa chini ya kifungu 8091 cha fungu 71. Mkoa wa Pwani ulitengewa shilingi milioni 414.3 kwa ajili ya utekelezaji wake. Mradi huu uliopangwa kutekelezwa katika Mji wa Mapinga uliopo katika Wilaya ya Bagamoyo, Mkoani Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi namba 4285 ujulikanao kama Mabasi yaendayo kwa Haraka Dar es Salaam (*DART*) ulipangwa kutekelezwa na Fungu 56 chini ya kifungu 1003. Mradi huu uliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 3.2 na ulilenga kusimamia na kuratibu ujenzi wa miundombinu itakayoweza kutekelezwa kwa mradi wa mabasi yaendayo haraka katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa utekelezaji wa mradi namba 6403 (*Tanzania Strategic Cities Project*) katika Manispaa ya Kigoma Ujiji, Kamati ilibaini kwamba mradi huu umetokelezwa vizuri na umewezeshwa kujengwa kwa barabara za lami zenye urefu wa kilometa tisa ambazo ni *Airport Mwasenga - Gungu*, *Job Lusinde* na *Mji Mwema*. Pia mradi huu umewezeshwa kujengwa kwa vituo vitatu vya mabasi katika maeneo ya *Mwanga*, *Ujiji* na *Kigoma*, ambavyo vimechangia kuboresha mfumo wa usafiri wa mikoani kwa wananchi wanaoingia na kutoka Manispaa ya Kigoma. Mradi pia umewezeshwa kujengwa kwa Dampo la kisasa katika eneo la *Msimba* pamoja na vizimba vya kukusanyia taka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini kuwa licha ya mafanikio yaliyopatikana mradi huu ulikabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na Wakandarasi wa ujenzi wa miundombinu kushindwa kukamilisha kazi kwa wakati kwa mujibu wa makubaliano na gharama kubwa za kuhamisha mifumo ya miundombinu ya maji, umeme na ya simu ya *TTCL* iliyo chini ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mradi namba 6443, *Tanzania Strategic System Project* katika Manispaa ya Jiji la Mwanza, Kamati ilibaini kuwa utekelezaji wake umeenda vizuri. Kupitia mradi huo barabara zenye urefu wa Kilomita 18.3 zimejengwa kwa kiwango cha lami. Baadhi ya barabara hizo ni *Pansiasi- Buzuruga*, *Tunza-Airport*, *Nkuyuni-Butimba* na *Sanga-Kiloleni*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini kuwa licha ya mafanikio mradi huu ulikumbana na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na kuchelewa kuhamisha miundombinu ya huduma za jamii kama vile maji, simu na reli. Pia mradi ulikabiliwa na uhaba wa kuchelewa kwa lami kutoka *Mombasa*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Mabasi yaendayo Haraka Jijini Dar es Salaam (*DART*) ulizinduliwa rasmi Juni, 2008 ili kusimamia uendeshaji wa mfumo wa mabasi yaendayo haraka katika Jiji la Dar es Salaam kwa kuweka mpangilio mzuri wa matumizi ya barabara katika Jiji la Dar es Salaam. Mradi ulilenga kupunguza au kuondoa kabisa athari za msongamano wa magari

katika Jiji la Dar es Salaam, ambazo licha ya kuwa kero kwa wananchi zimekuwa zikichangia upotevu mkubwa wa mapato.

Kwa mfano, kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS) kwa mwaka 2014 pekee, msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam ulisababisha upotevu wa shilingi bilioni 411. Kiasi hicho cha fedha ni kikubwa kuliko shilingi bilioni 322 zilizotumika katika ujenzi wa miundombinu kwenye awamu ya kwanza ya mradi wa mabasi yaendayo haraka, ambayo yanajumuisha ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilometa 20.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na upotevu wa fedha nyingi msongamano katika Jiji la Dar es Salaam umegeuka kuwa kero kubwa sana kwa wakazi wa Dar es Salaam, kwani umekuwa kikwazo na chanzo cha kuwachelewesha kupata huduma za kijamii na zile za uzalishaji mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Dar es Salaam wamesubiri vya kutosha na sasa ni wakati muafaka wa kushuhudia kuanza kwa utekelezaji wa mradi huo wa mabasi yaendayo haraka katika Jiji la Dar es Salaam. Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa ilipotembelea na kukagua utekelezaji wa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka katika Jiji la Dar es Salaam, iliridhishwa na hatua ambayo mradi huo umefikia. Kwa mujibu wa Wakala wa Mabasi yaendayo haraka *DART*, ujenzi wa miundombinu ya awamu ya kwanza umekamilika asilimia 98 na kukabidhiwa na Wakandarasi Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya hatua nzuri iliyofikiwa katika utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi huu, Kamati ilibaini kwamba ukosefu wa fedha umekuwa ukichangia kwa sehemu kubwa kuathiri utekelezaji wa mradi. Ukosefu wa fedha umekuwa unasababishwa na bajeti ndogo inayotengwa na Serikali, pia kuchelewa au kutotolewa kabisa kwa fedha zilizotengwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano katika mwaka wa fedha 2011/2012, *DART* ilitengewa fedha za maendeleo shilingi bilioni 3.2, hadi kufikia robo ya pili ya mwaka wa fedha 2015/2016, hakuna hata shilingi moja iliyotolewa katika mradi huo. Kamati inajiuliza kwa mazingira haya tunatarajia miujiza gani katika utekelezaji wa mradi wa *DART*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, hali hii haiwezi kuwafanya wananchi kuanza kuamini kwamba Serikali haina azma ya dhati katika mradi huu? Hayo na maswali mengine mengi ambayo watajiuliza wananchi yaweza kuwa sababu ya wananchi kutoona kama kuna mikakati ya msingi katika kuondokana na kero ya msongamano katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hali hiyo, napongeza azma ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa ya kutaka kuona utekelezaji wa mradi huu haraka iwezekanavyo kwa mafaniko makubwa hasa kwa kuzingatia kwamba mradi umegharimu fedha nyingi za mkopo, ambao utalipwa kwa fedha za walipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee Kamati inatambua na kupongeza hatua ambazo zimekuwa zikichukuliwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na watendaji wengine katika kuhakikisha kwamba kasoro zote zilizogubika utekelezaji wa mradi huu zinaondolewa, ili kuhakikisha maslahi ya umma yanazingatiwa kikamilifu kabla ya kuanza kwa uzaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua kuwa miongoni mwa mambo yanayosubiriwa sasa ili mradi uanze kutekezwa ni kufungwa kwa mfumo wa *ki-electronic* wa ukusanyaji wa nauli. Kukamilika kwa mfumo huo kutawezesha kuanza kwa huduma za mpito kwa mabasi yaendayo haraka Dar es Salaam. Hivi sasa Serikali imetamka kwamba mradi huu utaanza tarehe 10 mwezi Mei, tunaitaka Serikali kuhakikisha kwamba mradi huo unaanza tarehe hiyo bila visingizio vingine vyovyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Miradi na Uzingatiji wa Maoni ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2015/2016; Uchambuzi wa taarifa kuhusu ukusanyaji maduhuli. Ofisi ya Rais, TAMISEMI Fungu-56 ilitarajiwa kukusanya jumla ya shilingi milioni 13.5 kutoka vyanzo vya ndani, mapato haya yalitarajiwa kutokana na mauzo ya nyaraka za zabuni pamoja na vifaa chakavu. Hadi kufika 16 Machi, ambao ni mwezi wa mwisho wa robo ya tatu ya utekelezaji wa bajeti, jumla ya shilingi milioni 1.65 zilikuwa zimekusanywa na Fungu-56.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo huo wa makusanyo wa maduhuli ni dhaifu sana kwani umeshindwa kufikia hata robo ya lengo la makadirio. Hii ni ishara mbaya katika eneo la makusanyo ya maduhuli na inaleta mashaka iwapo makadirio ya maduhuli kwa mwaka ujao wa fedha yataweza kufikiwa hasa ikizingatiwa kwamba kiwango kinachokadiriwa kukusanywa ni sawa na kilichopita. Ingekuwa vema iwapo makadirio ya ukusanyaji ya maduhuli yangezingatia uhalisia ili kuepuka aibu ya kutokufika kwa malengo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina; uchambuzi unaonesha kuwa hadi kufika mwezi Machi, 2016, Ofisi ya Rais, TAMISEMI pamoja Taasisi zilizo chini yake zilikuwa zimepokea jumla ya shilingi bilioni 20.66 kiasi ambacho ni sawa na asilimia 46 ya fedha zote za matumizi ya kawaida.

Upande wa fedha za maendeleo uchambuzi ulionesha kwamba hadi mwishoni mwa robo ya tatu ya utekelezaji wa bajeti wa mwaka wa fedha 2015/2016, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Taasisi zake zilipokea jumla ya shilingi bilioni 169.74, sawa na asilimia 48 ya fedha yote iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufafanuzi huo, Kamati imebaini kwamba mwenendo wa upatikanaji wa fedha haukuwa mzuri kwa pande zote, yaani Matumizi ya Kawaida na yale ya Maendeleo kwani zilikuwa chini ya asilimia 50. Katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kwamba bajeti ya Maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge ilikuwa ni asilimia 88.7 ya bajeti yote ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina ilikuwa ni asilimia 89.1. Mwonekano huu unatoa taswira kwamba azma ya Serikali ya kuwaletea wananchi maendeleo sasa inaanza kujidhihirisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji na ushauri wa Kamati. Kuanza kuchambua bajeti ya mwaka 2015/2016, Kamati ilishauri kwamba, mambo mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha bajeti hiyo inatekelezwa kwa ufanisi. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati iliainisha maeneo makuu manne ambayo ilihitaji yafanyiwe kazi, kwa sehemu kubwa ushauri na maoni ya Kamati ulizingatiwa. Miongoni mwa maeneo ambayo ushauri wa Kamati ulizingatiwa na Wizara kwa ukamilifu ni ongezeko la fedha za maendeleo kwa ujumla wake kwa asilimia 6.9 kutoka shilingi bilioni 350.9 mwaka wa fedha 2015/2016, hadi shilingi bilioni 358.8 katika mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kuanza kupunguza utegemezi wa fedha za nje kwa ajili ya miradi ya mandeleo. Kwa mfano, utegemezi wa fedha za nje kwa ajili ya maendeleo ulipungua kwa asilimia 1.4. Aidha, Serikali imezingatia na inaendelea kuzingatia ushauri wa Kamati kuhusiana na kutumia mfumo wa *ki-elektroniki* katika ukusanyaji wa mapato ya ndani na mafanikio yameanza kupatikana. Kwa sasa, Halmashauri karibu zote nchini zinatumia mfumo wa *ki-electronic* katika ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Mkoa wa Ruvuma awali makusanyo katika hospitali hiyo yalikuwa sh. 100,000 kwa siku, lakini baada ya kuanza kutumia mfumo huu wa *ki-electronic* mwaka huu mapato yameongezeka hadi shilingi milioni mbili kwa siku. Tofauti ya viwango hivyo ni kuthibitisha kwamba Serikali imekuwa ikipoteza fedha nyingi kutokana na ukosefu wa uaminifu kwa baadhi ya watendaji wake. Pia mfumo huu umewezesha Halmashauri ya Jiji la Arusha, kuongeza mapato ya kiwango cha juu na hivyo kuacha kutoza ushuru mdogomdogo katika masoko ambao umekuwa ukilalamikiwa na wananchi kuwa ni kero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kuzingatia ushauri katika baadhi ya maeneo bado yako maeneo ambayo ushauri wake haujaanza kuzingatiwa, miongoni mwa maeneo hayo ni pamoja na kukosekana kwa mpango wa matumizi bora ya ardhi katika Halmashauri nchini, kwa sehemu kubwa migogoro ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji imekuwa ikichangiwa na changamoto hii ya kutokuwepo kwa mpango wa matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa Kamati kuhusiana na Halmashauri kutenga asilimia 10 ya makusanyo ya ndani kwa ajili ya kuwawezesha wanawake na vijana kiuchumi halikutekelezwa kikamilifu. Hata kwa Halmashauri ambazo zimeanza kutekeleza bado ni kwa kiasi kidogo tu. Kamati inaendelea kusisitiza juu ya ulazima wa kutekeleza jambo hili kwani linatokana na mwongozo wa Serikali hivyo siyo la hiari. Kamati inashauri Serikali kusimamia Halmashauri nchini ili zitekeleze utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kupitia agizo alilolitoa kwa Wakurugenzi wa Halmashauri wote nchini kutekeleza utaratibu huo na kuwa atakayeshindwa, basi ajue amejiondoa kazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maeneo ambayo ushauri haukuzingatiwa kikamilifu, Kamati inakubaliana na maelezo yaliyotolewa. Hata hivyo, inashauri na kuendelea kusisitiza kwamba ni vema Serikali ikawa inazingatia ushauri wa Kamati kwani unalenga kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi pamoja na kuwaletea maendeleo. Pia uzingatiji wa ushauri wa Kamati ni sehemu ya kutimiza wajibu wa Bunge ambao ni kusimamia na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa mpango wa makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, inapanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

(a) Kusimamia utendaji kazi wa Serikali katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kuimarisha uwajibikaji na uadilifu wa Watumishi wa Umma.

(b) Kusimamia utekelezaji na upelekeji wa madaraka kwa umma *(D by D)*.

(c) Kuimarisha na kusimamia ukusanyaji wa mapato katika mamlaka za Serikali za Mitaa.

(d) Kusimamia na kutekeleza shughuli za uendeshaji wa elimu na afya pamoja na Sekta zingine.

(e) Usimamizi wa utawala bora kwa kuandaa Sera, Maelekezo, Miongozo na Nyaraka mbalimbali.

(f) Kuendeleza rasilimali watu na kuwaongezea ujuzi na vitendea kazi.

(g) Kusimamia uratibu na kuwezesha utekelezaji wa taasisi, program ya miradi iliyo chini ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika malengo yaliyoorodheshwa hapo matatu (b), (f) na (g) yanajirudia na yaliyosalia ni mapya. Kupitia uchambuzi Kamati ilibaini kwamba, kulikuwa na haja ya msingi katika kujirudia kwa malengo hayo. Kwa mfano, lengo (b) linahusu kusimamia utekelezaji wa dhana ya Ugatuuji wa madaraka *D by D*. Kamati inaona umuhimu wa kuwepo kwa dhana hii kwa sababu bado Serikali inaendelea na utaratibu wa kupeleka madaraka katika ngazi za chini kwa lengo la kuwafikishia huduma za msingi wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa makadirio ya mapato. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inakadiriwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 677.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa makadirio ya matumizi. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, zinaombewa kuidhinishiwa jumla ya shilingi trilioni 6.062 kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kati ya fedha hizo zinazombwa, shilingi trilioni 4.421 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi trilioni 1.63 ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Pia katika fedha hizo zipo shilingi bilioni 10.047 za mishahara na matumizi mengiyo kwa ajili ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC).

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi umebaini kwamba, kumekuwa na ongezeko kubwa la fedha za miradi ya maendeleo kwa takribani asilimia 75. Kwa ujumla wake Ofisi ya Rais, TAMISEMI ndiyo inayoongoza kwa kuwa na bajeti kubwa dhidi ya Wizara zingine ikilinganishwa katika bajeti ya Taifa. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2016/2017, bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI imefikia asilimia 20.5 ya bajeti ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati. Baada ya kupitia taarifa za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, taarifa za utekelezaji wa bajeti iliyopita na maombi ya makadiro ya mapato na matumizi kwa mwaka wa

fedha ujao, Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo:-

Moja, Serikali ihakikishe Halmashauri zote nchini zinatenga kikamilifu asilimia 10 ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya Wanawake na Vijana. Aidha, kundi la Wajane nao lipewe uzito stahiki kama wanufaika wa fedha hizo.

Mbili, kwa kuwa suala la Watumishi Hewa, narudia; kwa kuwa suala la Watumishi Hewa limekuwa mchwa unaotafuna Taifa kwa muda mrefu kwa kula fedha ambazo zingehudumia na kuwaletea wananchi maendeleo, Kamati inaishauri Serikali kuweka mfumo madhubuti wa ufuatiliaji utakaohusisha uhakiki kwa kuzingatia orodha ya malipo ya mishahara ya kila mwezi na kutoa taarifa katika vikao vya *DCC* na *RCC*.

Tatu, Serikali iendeele kusisitiza matumizi ya mfumo wa *ki-electronic* katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri kwani umeonesha mafanikio makubwa katika kusaidia kuongeza mapato na kudhibiti wizi na ubadhilifu. Mfumo huu ukitumika kikamilifu utawezesha Halmashauri kuachana na Mawakala katika ukusanyaji wa mapato na hivyo kuokoa fedha zilizokuwa zikipotea kutokana na sababu mbalimbali.

Nne, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imekuwa hairejeshi asilimia 30 ya kodi ya ardhi kwa Halmashauri husika kama inavyotakiwa na sheria, Kamati inashauri uandaliwe utaratibu utakaoziruhusu Halmashauri kukata kodi hiyo kabla ya kuziwasilisha Wizara ya Ardhi. (*Makofi*)

Tano, Halmashauri ziandae utaratibu wa kuelimisha na kuhamasisha makundi mbalimbali ya jamii kujiunga na Bima ya Afya na Mfuko wa Afya wa Jamii (*CHF*), kwa lengo la kuwawezesha kupata huduma za afya kwa gharama nafuu. Kamati inashauri kwamba, yawekwe masharti ya lazima kwa makundi yenye kipato kama vile waendesha pikipiki – (*Bodaboda*), Mama na Baba lishe na wafanyabiashara ndogondogo (*Wamachinga*) kujiunga na Bima ya Afya kabla ya kupewa leseni au vibali vingine.

Sita, Halmashauri zibuni vyanzo vya mapato ili kuongeza wigo wa mapato ya ndani na hivyo kuondoa ushuru mdogomdogo ambao ni kero kwa wananchi kama inavyoelezwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Saba, Serikali iangalie namna ya kuwawezesha au kuwalipa Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji na Mitaa ili waweze kusaidia kuhamasisha ulipaji wa kodi, ushuru na tozo mbalimbali katika maeneo yao. (*Makofi*)

Nane, Halmashauri ziandae mpango wa matumizi bora ya ardhi ikiwa ni pamoja na kupima maeneo ili kuondoa migogoro ya wakulima na wafugaji, kudhibiti ukuaji holela wa Miji na kuwezesha utunzaji wa mazingira.

Tisa, kwa kuwa Halmashauri nyingi zinakabiliwa na madeni kutoka kwa Wazabuni na Wakandarasi, Kamati inashauri Serikali kutoa fedha ili madeni hayo yalipwe na kuondoa usumbufu ambao wanakumbana nao Watendaji katika huduma zao.

Kumi, Halmashauri isimamie kikamilifu sheria ndogo za usafi wa mazingira ili kuondoa kabisa uwezekano wa milipuko ya magonjwa hususani kipindupindu.

Kumi na Moja, kwa kuwa kuanza kutekelezwa kwa tamko la kutoa elimu bure, katika ngazi ya shule za msingi na sekondari kumesababisha ongezeko kubwa la wanafunzi wanaojiunga na shule na hivyo kusababisha mahitaji makubwa ya miundombinu ya elimu kama vile madawati, vyumba vya madarasa na kadhalika, Kamati inashauri Serikali ianze mkakati wa kukabiliana na ongezeko hilo la mahitaji ili kutekeleza tamko hilo kwa tija.

Kumi na Mbili, kwa kuwa ukusanyaji wa ushuru wa majengo (*Property Tax*) katika Halmashauri za Manispaa utakuwa chini ya TRA ni vema Serikali ikawa makini na uamuzi huo, hasa ikizingatiwa kwamba mamlaka hii ya TRA haikupata mafanikio makubwa huko nyuma ikilinganishwa na mafanikio yaliyooneshwa na Serikali za Mitaa.

Kumi na Tatu, kwa kuwa ucheleweshwaji au kutotolewa kabisa kwa fedha za maendeleo kumekuwa kunaathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Kamati inashauri Serikali kutoa fedha zote zinazotengwa kwa ajili ya miradi ili kutoathiri utendaji wa maendeleo.

Kumi na Nne, kwa kuwa awamu ya kwanza ya ujenzi wa miundombinu ya mradi wa mabasi yaendayo haraka Dar es Salaam DART imekalilika, Kamati inashauri mamlaka husika ikamilishe mfumo wa ukusanyaji nauli kwa njia ya *electronic* pamoja na kupanga nauli ili huduma ya usafiri huo ianze haraka. Kuanza kwa huduma hiyo kutasaidia kupunguza adha ya msongamano kwa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam ambayo pia imekuwa ina athari nyingine za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati namshukuru Mheshimiwa George Simbachawene, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa akisaidiwa na Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, pamoja na Watendaji wa ofisi hiyo wakiongozwa

na Injiniya Mussa Iyombe, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa jinsi walivyoshiriki kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na kufafanua kwa kina kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuwashukuru Wakuu wa Mikoa yote ya Tanzania Bara, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri zote nchini kwa kuwasilisha vema taarifa za utekelezaji wa bajeti zao iliyopita na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka 2016/2017 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.
(Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante kwa taarifa ya Kamati kwa upande wa Ofisi ya Rais TAMISEMI.

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS, UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 6(4) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 inaipa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, wajibu wa kusimamia shughuli za Ofisi ya Rais, Utawala Bora na Menejementi ya Utumishi wa Umma, pamoja na Tawala za Mikoa na Serikali za

Mitaa. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 jukumu la uchambuzi wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, limewekwa chini ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa.

Vilevile Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Bunge, imeweka sharti kwa Kamati za Kisekta ikiwemo hii ya Utawala na Serikali za Mitaa, kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayokuwa imetengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha. Naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ilifanya ziara za ukaguzi katika miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na kuchambua Bajeti ya ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inahusisha jumla ya Mafungu Ishirini na Nane (28):- Fungu 56 – Ofisi ya Rais TAMISEMI, Fungu 02 – Tume ya Utumishi wa Walimu, pamoja na Mafungu 26 ya Mikoa yote ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla maelezo ya utangulizi yanatuelekeza katika mambo manne ambayo Taarifa hii itajikita katika kutoa ufafanuzi wake. Maeneo hayo ni haya yafuatayo:-

- i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi a Maendeleo iliyotembelewa na Kamati;
- ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016;
- iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017; na
- iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

2.1 Ufafanuzi wa Miradi ya Maendeleo iliyolengwa kukaguliwa

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha 2015/2016, Ofisi ya Rais Tamisemi – Fungu 56 iliidhinishiwa jumla ya shilingi 354,565,626,000/- kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Pia Mafungu ya Mikoa 25, kila moja liliidhinishiwa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo. Miongoni mwa miradi hiyo iliyotekelezwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI - Fungu 56 ni hii ifuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi Namba 6403 uliojulikana kama “Programu ya Uendelezaji Miji Mikakati Tanzania “Tanzania Strategic Cities Programe” uliidhinishiwa jumla ya shilingi 2,200,000,000/= kwa ajili ya utekelezaji wake. Mradi huu uliopangwa kutekelezwa chini ya Kifungu 205 – Urban Development Division, cha Fungu 56 unahusika na uratibu na usimamizi wa uendelezaji wa miundombinu katika miji mikakati.

Fedha iliyotengwa lilenga kuwezesha usimamizi na uratibu wa utekelezaji wa mradi huo katika Miji Saba nchini ambayo ni Arusha, Mwanza, Mbeya, Tanga, Dodoma, Mtwara Mikindani na Kigoma Ujiji, pamoja na Mamlaka ya Usitawishaji Makao Makuu Dodoma (CDA).

Mheshimiwa Spika, Mradi Namba 6403 uliojulikana kama Tanzania Strategic Cities Project, uliopangwa kutekelezwa chini ya Kifungu 8091 - Mamlaka ya Serikali za Mitaa, cha Fungu 74 – Mkoa wa Kigoma uliidhinishiwa jumla ya shilingi 1,520,967,000/- Mradi huu ulilenga kuboresha miundombinu ya barabara kwa kujenga kwa kiwango cha lami ngumu, kuweka taa za barabarani, kujenga vituo vya Mabasi na kituo cha kukusanyia Taka ngumu katika Halmashauri ya Manispaa ya Mji wa Kigoma.

Mheshimiwa Spika, aidha Mradi Na. 6403 uliojulikana kama Tanzania Strategic Cities Project, uliopangwa kutekelezwa chini ya Kifungu 8091 – Mamlaka ya Serikali za Mitaa, cha Fungu 81 – Mkoa wa Mwanza, uliidhinishiwa shilingi 1,151,698,000/= kwa ajili ya utekelezaji wake.

Mradi huu ulilenga kuboresha miundombinu ya barabara kwa ujenzi wa kiwango cha lami ngumu, kuweka taa za barabarani, pamoja na ujenzi wa mifereji ya maji taka katika Jiji la Mwanza.

Mheshimiwa Spika, mradi mwingine ni Namba 3280 ujulikanao kama Rural Water Supply and Sanitation, uliopangwa kutekelezwa chini ya Kifungu 8091 cha Fungu 71 – Mkoa wa Pwani, ulitengewa shilingi 418,342,000 kwa ajili ya utekelezaji wake. Mradi huu uliopangwa kutekelezwa katika mji wa Mapinga uliopo katika Wilaya ya Bagamoyo, mkoani Pwani.

Mheshimiwa Spika, Mradi Namba 4285 ujulikanao kama Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART) uliopangwa kutekelezwa na Fungu 56, chini ya Kifungu 1003. Mradi huo uliidhinishiwa jumla ya shilingi 3,200,000,000/- na ulilenga kusimamia na kuratibu ujenzi wa miundombinu itakayowezesha kutekelezwa kwa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka katika Jiji la Dar esSalaam.

Matokeo ya Ukaguzi

Mheshimiwa Spika, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) na kufanya ziara za ukaguzi wa miradi iliyoanishwa hapo juu ambayo ni baadhi tu ya miradi mingi iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha unaoisha. Kamati kwa kuzingatia Kanuni ya 117 (18) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 inayoruhusu Kamati kuunda Kamati Ndogo kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli zake, ilijigawa katika makundi mawili na kufanya ziara za ukaguzi wa miradi iliyoanishwa.

Mheshimiwa Spika, katika ukaguzi wa Mradi Namba 6403 uliohusu “Programu ya Uendelezaji Miji Mikakati Tanzania “Tanzania Strategic Cities Programme” Kamati ilibaini kuwa, kupitia mradi huo Ofisi ya Rais TAMISEMI imeweza kuratibu na kusimamia uendelezaji wa miundombinu katika miji mikakati Saba iliyotajwa. Mradi huu ambao unatekelezwa kwa fedha za mkopo kutoka Shirika la Maendeleo la Kimataifa (IDA) na Msaada kutoka Shirika la Maendeleo la Denmark (DANIDA), umekuwa na mwenendo mzuri wa upatikanaji fedha na utekelezaji wa miradi hiyo umekuwa mzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utekelezaji wa Mradi Namba 6403 “Tanzania Strategic Cities Project” katika Manispaa ya Kigoma – Ujiji, Kamati ilibaini kuwa mradi huo umetekelezwa vizuri na umewezesha kujengwa kwa barabara za lami zenye urefu wa kilomita 9 ambazo ni Airport – Mwasenga – Gungu (km.4.7), Job Lusinde (km. 2.1 na Mji Mwema (km2.08). Pia mradi huu umewezesha kujengwa kwa vituo vitatu vya mabasi katika maeneo ya Mwanga, Ujiji na Kigoma, ambavyo vimechangia kuboresha mfumo wa usafiri wa mikoani kwa wananchi wanaoingia na kutoka Manispaa ya Kigoma. Mradi pia umewezesha kujengwa kwa Dampo la Kisasa katika eneo la Msimba, pamoja na Vizimba vya kukusanyia taka. Kwa kuzingatia kuwa, ukusanyaji wa mapato imekuwa ni changamoto kubwa inayozikabili Halmashauri nyingi nchini, mradi huu umejengea uwezo watumishi na kununua vifaa vitakavyowezesha uwekaji wa mfumo wa kielektroniki wa kukusanya mapato.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa licha ya mafanikio yaliyopatikana, mradi huu ulikabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na Wakandarasi wa ujenzi wa miundombinu kushindwa kukamilisha kazi kwa wakati kwa mujibu wa makubaliano, na gharama kubwa za kuhamisha mifumo ya miundombinu ya maji, umeme na TTCL iliyo chini ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitaka kujua sababu ya hali hiyo na kuelezwa kwamba, changamoto hizo zilitokana na kutokuwepo kwa kumbukumbu zinazoonesha miundombinu ilipo na hivyo kusababisha ugumu wa utekelezaji

wa miradi hiyo. Jambo linalosisitizwa ni kwamba, Serikali kupitia Halmashauri iwe na utaratibu wa kutunza kumbukumbu kwa kila jambo linalotekelezwa katika Halmashauri ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa siku za baadae. Pia, kuwe na utamaduni wa kufanya upembuzi yakinifu kwa umakini ili kubaini kasoro zinazoweza kujitokeza na hivyo kuepusha gharama zisizo na msingi wakati wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mradi Namba 6443 "Tanzania Strategic Cities Project, katika Manispaa ya Jiji la Mwanza, Kamati ilibaini kuwa utekelezaji wake umeenda vizuri. Kupitia mradi huo barabara zenye urefu wa kilomita 18.316 zimejengwa kwa kiwango cha lami. Baadhi ya Barabara hizo ni, Pasiansi – Buzuruga (km 7.2), Tunza Airport (km 4.7), Mkuyuni – Butimba (2.4) na Sanga – Kiloleli (km 1.9). Mradi huu pia ulihusisha ujenzi wa misingi 30 kwa ajili ya kukalishia pipa za taka ngumu (skip pads).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kujitokeza kwa changamoto ya kutojengwa kwa baadh ya barabara ambazo ziliishafanyiwa upembuzi yakinifu, kutokana na ufinyu wa bajeti. Kamati ilipotaka kujua, namna ambavyo changamoto hiyo imefanyiwa kazi, ilielezwa kwamba, mawasiliano yameishafanyika na Benki ya Dunia na imeweza kuongeza fedha "additional financing" ili kuwezesha barabara hizo zenye urefu wa (km 15.6) zijengwe kwa kiwango cha lami. Pia mradi huu umesaidia kuimarisha uwezo wa Halmashauri za Manispaa za llemela na Nyamagana katika ukusanyaji wa mapato ya ndani (own sources) kutoka katika vyanzo vyake, vikiwemo ushuru wa huduma, kodi na tozo mbalimbali. Ujuzi huu umesaidia kwa kiasi kikubwa utambuzi wa walipa kodi wakubwa, kati na wengineo. Vyanzo vipya vimeibuliwa ikiwa ni pamoja na kubaini changamoto zilizopo katika ukusanyaji wa mapato. Mfano mzuri katika eneo hili ni kuongezeka kwa mapato ya Halmashauri kutoka Shilingi bilioni 4.2 Februari, 2015 hadi shilingi bilioni 7.2 Februari, 2016 kutokana na kutumika kwa mfumo wa kielektroniki katika kukusanya ushuru wa Mabango, vizimba, maduka na maegesho ya magari.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa licha ya mafanikio, mradi huu ulikumbana na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja kuchelewa kuhamisha miundombinu ya huduma za jamii kama vile maji, simu, na reli. Pia mradi ulikabiliwa na uhaba au kuchelewa kwa lami kutoka Mombasa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitaka kujua sababu ya hali hiyo na kueleza kwamba, changamoto hizo zilitokana na kuchelewa kufanyika kwa maamuzi kuhusiana na uhamishaji wa miundombinu ya huduma iliyopo, na pia ununuzi wa lami kutoka Mombasa. Kamati inasisitiza mamlaka husika ziwe na utaratibu wa kutoa maamuzi kwa wakati ili kutoathiri utekelezaji wa miradi iliyopangwa.

Hilo likizingatiwa litawezesha Serikali kuepuka ongezeko la gharama na ucheleweshaji wa kukamilika kwa miradi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatarajia kwamba, mambo hayo yakizingatiwa utekelezaji wa mradi wa Tanzania Strategic Cities Project katika miji mingine iliyosalia utakuwa wa ufanisi zaidi na wa gharama ndogo.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART) ulizinduliwa rasmi Juni, 2008 ili kusimamia uendeshaji wa mfumo wa mabasi yaendayo Haraka katika Jiji la Dar es Salaam kwa kuweka mpangilio mzuri wa matumizi ya barabara katika jiji la Dar es Salaam. Mradi ulilenga kupunguza kama siyo kuondoa kabisa athari za msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam, ambazo licha ya kuwa kero kwa wananchi, zimekuwa zikichangia upotevu mkubwa wa mapato. Kwa mfano; kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS) kwa mwaka 2014 pekee, msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam ulisababisha upotevu wa shilingi bilioni 411. Kiasi hicho cha fedha ni kikubwa zaidi kuliko shilingi bilioni 322 zilizotumika katika ujenzi wa miundombinu kwenye Awamu ya Kwanza ya Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka, ambayo inajumuisha ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 20.9 Mbali na upotevu wa fedha nyingi, msongamano katika jiji la Dar es Salaam umegeuka kuwa kero kwa wakazi wa Dar es Salaam walio wengi kwani umekuwa chanzo cha kuwachelewesha kupata huduma za kijamii, na zile za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, upo msemu wa Wahenga kwamba “kawia ufike”. Kwa maudhui ya msemu huo, Kamati inaamini kwamba, Wananchi wa Dar es Salaam wamesubiri vya kutosha na sasa ni wakati muafaka wa kushuhudia kuanza kwa utekelezaji wa Mradi wa Mabasi yaendayo Haraka katika Jiji la Dar Es Salaam. Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, ilipotembelea na kukagua utekelezaji wa Mradi wa Mabasi yaendayo Haraka katika Jiji la Dar es Salaam, iliridhishwa na hatua ambayo mradi huo umefikia. Kwa mujibu wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), ujenzi wa miundombinu ya Awamu ya Kwanza umekamilika kwa asilimia 98 na kukabidhiwa na Wakandarasi Serikalini.

Ujenzi huo unahusisha barabara zenye urefu wa kilomita 20.9 (Kimara hadi Kivukoni), na matawi mawili ambayo ni barabara ya Kawawa (Morocco - Magomeni Mapipa) na (Msimbazi - Kariakoo Gerezani). Ujenzi wa barabara hizo unahusisha njia maalum za mabasi, njia za magari mchanganyiko na njia za waendesha baiskeli na waenda kwa miguu. Vile vile, ujenzi umehusha vituo vya 27 katika Barabara Maalum za mfumo wa DART, vituo vitano (5) vya Mabasi (Bus Terminals), vituo Mlisho vine (4), Karakana moja eneo la Jangwani na Madaraja ya Watembea kwa miguu katika maeneo ya Kimara, Ubungo na

Morocco. Kamati ilitaka kujua ni kwanini huduma ya usafiri wa mabasi yaendayo haraka haijaanza katika jiji la Dar es Salaam licha ya kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu kwa asilimia 98. Maelezo yaliyotolewa ni kwamba, kuanza kwa mradi huo kunasubiri kukamilika kwa ufungaji wa mfumo wa ukusanyaji wa nauli na uendeshaji wa shughuli za DART. Pia, Wakala kwa kushirikiana na wadau wengine unakamlisha taratibu muhimu kabla ya kuanza kwa huduma ya mpito kwa kuzingatia masharti ya mkataba.

Mheshimiwa Spika, licha ya hatua nzuri iliyofikiwa katika utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi huu, Kamati ilibaini kwamba, ukosefu wa fedha umekuwa ukichangia kwa sehemu kubwa kuathiri utekelezaji wa mradi. Ukosefu wa fedha umekuwa unasababishwa na bajeti ndogo inayotengwa na Serikali, na pia kuchelewa au kutotolewa kabisa kwa fedha zilizotengwa na Serikali. Kwa mfano katika mwaka wa fedha 2015/2016 DART ilitengewa fedha za maendeleo shilingi bilioni 3.2. hadi kufikia robo ya pili ya mwaka wa fedha 2015/2016 hakuna hata shilingi moja iliyokuwa imepokelewa. Kamati inajuliza, kwa mazingira kama hayo tunatarajia miujiza gani katika utekelezaji wa mradi wa DART? Je, hali hii haiwezi kuwafanya Wananchi kuanza kuamini kwamba, Serikali haina azma ya dhati katika utekelezaji wa DART. Hayo na maswali mengine mengi ambayo watajuliza wananchi, vyaweza kuwa sababu ya Wananchi kutoona kama kuna mikakati ya msingi katika kuondokana na kero ya msongamano katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hali hiyo, ninapongeza azma ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, ya kutaka kuona utekelezaji wa mradi huu unaanza haraka iwezekanavyo, kwa mafanikio na tiba kubwa, hasa kwa kuzingatia kwamba, mradi umegharimu fedha nyingi za mkopo ambao utalipwa kwa fedha za walipa kodi. Kwa namna ya pekee, Kamati inatambua na kupongeza hatua ambazo zimekuwa zikichukuliwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI na watendaji wengine katika kuhakikisha kwamba, kasoro zote zilizogubika utekelezaji wa mradi huu zinaondolewa ili kuhakikisha maslahi ya umma yanazingatiwa kikamilifu kabla ya kuanza kwa utekelezaji wa mradi huu. Kamati inatambua kuwa, miongoni mwa mambo yanayosubiriwa sasa ili mradi uanze kutekelezwa ni kufungwa kwa mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji nauli. Kukamilika kwa mfumo huo kutawezesha kuanza kwa huduma za mpito kwa Mabasi yaendayo Haraka Dar es Salaam. Hivi sasa Serikali imetamka kwamba mradi utaanza tarehe 10 mei 2016. Tunaitaka Serikali kuhakikisha mradi unaanza tarehe hiyo na kusiwepo na visingizio vingine.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kwamba, kuanza kwa utekelezaji wa mradi kutakuwa chachu ya kurekebisha kasoro zitakazokuwa zinajitokeza wakati wa utekelezaji wa mradi, na hivyo kuwezesha utekelezaji wa mradi kuimarika siku hadi siku na hatimaye kufikia kiwango cha juu. Kwa mantiki, hiyo, Kamati inashauri mamlaka husika ihakikishe mradi huo unaanza kutekelezwa mapema iwezekanavyo, huku kasoro zilizobainika zikiendelea kufanyiwa kazi.

2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa Fedha 2015/2016

Mheshimiwa Spika, kutokana na ziara kwenye miradi ya Maendeleo, Kamati ina maoni yafuatayo:-

i. Kukosekana kwa kumbukumbu za mtandao wa miundombinu ya huduma za jamii kama maji, simu, katika maeneo ya utekelezaji wa miradi kumechangia kuchelewa kuanza kwa utekelezaji wa miradi ya ya maendeleo na hivyo kuongeza gharama.

ii. Ukosefu wa fedha kwa wakati unachangia kuathiri ufanisi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

iii. Wananchi wakihamasishwa na kuelimishwa vya kutosha kuhusiana na umuhimu wa kutunza miradi iliyokamilika watakuwa walinzi wazuri wa miradi hiyo na hivyo itaweza kudumu.

iv. Maamuzi sahihi na yanayofanyika kwa wakati mwafaka yatawezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa ufanisi na tija.

v. Mfumo wa ukusanyaji mapato kwa njia ya kielektroniki katika taasisi za Serikali umesaidia kuongeza na kudhibiti upotevu wa mapato

vi. Kuanza utekeleUtekelezaji

3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ulijikita katika makusanyo ya maduhuli ikilinganishwa na lengo

pamoja na mwenendo wa upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa. Njia kubwa zilizotumika katika uchambuzi hii ni kuangalia hali halisi, kuzingatia pamoja na kuangalia hali halisi, kuzingatia taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu wakati vikao vya Kamati.

Mheshimiwa Spika, ufafanuzi wa uchambuzi umefanywa kwa kutumia jedwali, asilimia, ulinganishaji na utofautishaji. Ili kurahisisha maelezo, Kamati imetumia chati na grafu kufafanua. Maelezo haya ni kama ifuatavyo:-

3.1.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu ukusanyaji Maduhuli

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI – Fungu 56 ilitarajiwa kukusanya jumla ya Shs. 13,502,000.00 kutoka vyanzo vya ndani. Mapato haya yalitarajiwa kutokana na mauzo ya nyaraka za zabuni pamoja na vifaa chakavu. Hadi kufikia Machi, 2016 ambao ni mwezi wa mwisho wa robo ya Tatu ya utekelezaji wa bajeti, jumla ya **Shs. 1,650,000.00** zilikuwa zimekusanywa na Fungu 56. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 12 ya makusanyo yaliyokadiriwa na pia ni sawa na asilimia 0.004 ya bajeti ya matumizi ya kawaida iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Fungu hilo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016. Sababu iliyotolewa kuhusiana na kiwango hicho kidogo cha ukusanyaji wa maduhuli ni mauzo kidogo ya nyaraka za zabuni na vifaa chakavu vya ofisi. Mwenendo huu wa makusanyo ya maduhuli ni dhaifu sana kwani umeshindwa kufikia hata robo ya lengo la makadirio. Hii ni ishara mbaya katika eneo la makusanyo ya maduhuli, na inaleta mashaka iwapo makadirio ya maduhuli kwa mwaka ujao wa fedha 2016/2017 yataweza kufikiwa, hasa ikizingatiwa kiwango kinachokadiriwa kukusanywa ni sawa ni kilichopita. Ingekuwa vyema iwapo makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli yangezingatia uhalisi, ili kuepuka aibu ya kutofikiwa kwa malengo hayo.

3.1.2 Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina

Mheshimiwa Spika, Wahenga walisema “Mipango si Matumizi”, wakimaanisha kwamba, kupanga ni jambo moja na kutumia ni jambo jingine. Kwa miaka kadhaa tumeshuhudia hilo katika mwenendo wa bajeti ya Serikali, kwani kumekuwa na mipango na fedha zimekuwa zikiidhinishwa ili kuitekeleza, lakini imekuwa ni vigumu kwani upatikanaji wa fedha kutoka Hazina umekuwa ni kitendawili kigumu kisichoteguka. Kwa muktadha huo, Kamati ilijaribu kufanya ulinganisho wa fedha zilizopokelewa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI kutoka Hazina hadi kufikia mwisho wa robo ya Tatu ya mwaka wa fedha na kiasi cha fedha kilichoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Uchambuzi unaonesha kuwa, hadi kufikia mwezi Machi, 2016 Ofisi ya Rais, TAMISEMI pamoja na Taasisi

zilizo chini yake, zilikuwa zimepokea **Shs. 20,667, 177,049** kiacha ambacho ni sawa na asilimia 46 ya fedha zote za matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa fedha za maendeleo uchambuzi unaonesha kwamba, hadi mwishoni mwa robo ya tatu ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016 Ofisi ya Rais, TAMISEMI na taasisi zake, zilikuwa zimepokea jumla ya **Shs. 169,747,018,210** sawa na asilimia 48 ya fedha yote iliyoidhinishwa. Kwa ufafanuzi huo, Kamati imebaini kwamba, mwenendo wa upatikanaji wa fedha haukuwa mzuri kwa pande zote (ie. Matumizi ya Kawaida na Maendeleo) kwani zilikuwa chini ya asilimia 50. Hata hivyo, licha ya upatikanaji kuwa chini ya kiwango hicho, upande wa fedha za Maendeleo ulikuwa na mwenendo mzuri kidogo wa upatikanaji wa fedha ikilinganishwa na Matumizi ya Kawaida kwa kuwa na asilimia 2 zaidi.

Mheshimiwa Spika, ili kulinganisha uwiano wa upatikanaji wa fedha za maendeleo dhidi ya fedha zote zinazopatikana na kubaini uzito unaowekwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Kamati ilitaka kujua ni kiasi gani cha asilimia ya bajeti kilitengwa kwa ajili ya maendeleo katika bajeti nzima iliyoidhinishwa na kulinganisha uwiano wa fedha zilizopatikana kwa ajili ya miradi maendeleo na jumla ya fedha zilizopatikana. Ulinganifu unaokusudiwa umefafanuliwa vizuri kupitia Jedwali Na. 01

Jedwali Na.01: Bajeti iliyoidhinishwa dhidi ya Fedha zilizopatikana


BAJETI ILIYOIDHINISHWA			FEDHA ILIYOPATIKANA		
Mgawanyo	Bajeti	Asilimia ya Jumla	Mgawanyo	Bajeti	Asilimia ya Jumla
OC	23,081,208,000	5.8	OC	6,843,638,656	3.6
Mishahara	21,641,952,000	5.5	Mishahara	13,823,538,393	7.3
Maendeleo	350,588,786,000	88.7	Maendeleo	169,747,018,210	89.1
Jumla	395,588,786,000	100	Jumla	190,414,195,259	100


Chanzo: Randama ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kwamba, bajeti ya mandeleo iliyoidhinishwa na Bunge ilikuwa ni asilimia 88.7 ya Bajeti yote ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina ulikuwa ni asilimia

89.1. Mwonekano huu unatoa taswira kwamba, azma ya Serikali ya kuwaletea Wananchi maendeleo sasa inaanza kujidhihirisha. Sababu kubwa mbili zinaweza kutolewa ili kuipa mashiko dhana hiyo:- Sababu ya ni kwamba, bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya maendeleo ni zaidi ya asilimia 85; na upatikanaji wa fedha umekuwa kwa kiwango kizuri ambacho pia ni zaidi ya asilimia 85.

Tofauti za uwiano wa Bajeti iliyoidhinishwa na uwiano wa Bajeti upatikanaji wa fedha zinaweza kuoneshwa kwa kutumia Chati Mraba Na.01 na Na. 02 kama ifuatavyo:-





Chanzo: Randama ya TAMISEMI

3.1.3 Mapito ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchambua bajeti ya Mwaka 2015/2016, Kamati ilishauri mambo mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha bajeti hiyo inatekelezwa kwa ufanisi. Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba. Kamati ilianisha maeneo makuu manne ambayo ilihitaji yafanyiwe kazi. Kwa sehemu kubwa, ushauri na maoni ya Kamati ulizingatiwa. Miongoni mwa maeneo ambayo ushauri wa Kamati umezingatiwa na Wizara kwa ukamilifu ni ongezeko la fedha ya maendeleo kwa ujumla wake kwa asilimia 9.9 kutoka Shs. Bilioni 350.9 mwaka wa fedha 2015/2016 hadi Shs. Bilioni 385.8 katika mwaka wa fedha 2016/2017.

Eneo lingine ni kuanza kupunguza utegemezi wa fedha za nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kwa mfano, utegemezi wa fedha za nje kwa ajili ya maendeleo ulipungua kwa asilimia 1.4 kutoka asilimia 15.4 katika mwaka wa fedha 2015/2016 hadi asilimia 14.0 katika mwaka wa fedha 2016/2017. Hii ni dalili nzuri kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa fedha za ndani ambazo zimekuwa na uhakika zaidi kuliko za nje.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imezingatia na inaendelea kuzingatia ushauri wa Kamati kuhusiana na kutumia mfumo wa kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato ya ndani na mafanikio yameanza kupatikana. Kwa sasa Halmashauri karibu zote nchini isipokuwa chache ambazo zina changamoto ya

kukosa umeme, zinatumia mfumo wa kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato. Miongoni mwa mifano ya mafanikio katika matumizi ya mfumo huu wa kielektroniki katika ukusanyaji mapato ni katika Hospitali ya Mkoa wa Ruvuma. Awali makusanyo katika hospitali hiyo yalikuwa ni Shs. 100,000 kwa siku, lakini tangu kuanza kutumika kwa mfumo huo mapema mwaka huu, mapato yameongeza hadi zaidi ya Shs. 2,000,000, kwa siku. Tofauti ya viwango hivyo, ni uthibitisho wa kutosha kabisa kwamba, Serikali imekuwa ikipoteza fedha nyingi kutokana na kukosekana uaminifu kwa baadhi ya watendaji wake. Pia mfumo huu umewezesha Halmashauri ya Jiji la Arusha kuongeza mapato kwa kiwango cha juu na hivyo kuacha kutoza ushuru mdogo mdogo katika masoko ambao umekuwa ukilalamikiwa na wananchi kwamba, ni kero.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kuzingatia ushauri katika baadhi ya maeneo, bado yapo maeneo ambayo ushauri wake haujaanza kuzingatiwa. Miongoni mwa maeneo hayo ni pamoja na kukosekana na mpango wa matumizi bora ya ardhi katika Halmashauri nchini. Kwa sehemu kubwa migogoro ya ardhi baina ya Wafugaji na Wakulima imekuwa ikichangiwa na changamoto hii ya kutokuwepo kwa mpango wa matumizi bora ya ardhi. Kamati ilitaka kujua ni kwanini imekuwa vigumu kwa Halmashauri nyingi nchini kuzingatia ushauri huu. Maelezo kutoka katika Halmashauri nyingi yalikuwa ni ufinyu wa bajeti pamoja na ukosefu wa wataalam wa upimaji ardhi.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Kamati kuhusiana na Halmashauri kutenga asilimia kumi (10%) ya makusanyo ya ndani (own source) kwa ajili ya kuwawezesha Wanawake na Vijana kiuchumi haujatekelezwa kikamilifu. Hata kwa Halmashauri ambazo zimeanza kutenga, bado ni kwa kiasi kidogo tu. Kamati inaendelea kuisitiza juu ya ulazima wa kutekeleza jambo hili, kwani linatokana na mwongozo wa Serikali, hivyo si la hiari. Kamati inashauri Serikali kusimamia Halmashauri nchini ili zitekeleze utaratibu huo. Aidha, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu kupitia agizo alilolitoa kwa Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini kutekeleza utaratibu huo na kuwa atakayeshindwa basi ajue amejiondoa kazini.

Mheshimiwa Spika, kwa maeneo ambayo ushauri haukuzingatiwa kikamilifu, Kamati inakubaliana na maelezo yaliyotolewa, hata hivyo inashauri na kuendelea kuisitiza kwamba, ni vyema Serikali ikawa inazingatia ushauri wa Kamati kwani unalenga kuboresha utoaji wa huduma kwa Wananchi pamoja na kuwaletea maendeleo. Pia izingatiaji wa ushauri wa Kamati ni sehemu ya kutimiza Wajibu wa Bunge ambao ni kuisimamia na kuishauri Serikali.

4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

4.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, inapanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kusimamia utendaji kazi wa Serikali katika Ngazi za OR – TAMISEMI, Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kuimarisha uwajibikaji na uadilifu wa Watumishi wa Umma;

b) Kusimamia utekelezaji wa Upelekaji wa Madaraka kwa Umma (D by D) ;

c) Kuimarisha na kusimamia ukusanyaji wa mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

d) Kusimamia utekelezaji wa shughuli za uendeshaji wa Elimu na Afya pamoja na sekta zingine;

e) Usimamizi wa Utawala Bora kwa kuandaa Sera, Maelekezo , miongozo na Nyaraka mbalimbali;

f) Kuendeleza raslimali watu kwa kuwaongezea ujuzi na vitendea kazi;

g) Kusimamia, kuratibu na kuwezesha utekelezaji wa Taasisi, programu na Miradi iliyo chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, katika malengo yaliyoorodheshwa matatu (b,f na g) yanajirudia, na yaliyosalia ni mapya. Kupitia uchambuzi Kamati ilibaini kwamba, kulikuwa na haja ya msingi katika kujirudia kwa malengo hayo. Kwa mfano lengo b linahusu kusimamia utekelezaji wa dhana ya ugatuuji wa madaraka (D by D). Kamati inaona umuhimu wa kuwepo kwa dhana hii kwa sababu, bado Serikali inaendelea na utaratibu wa kupeleka madaraka katika ngazi za chini kwa lengo la kuwafikishia huduma za msingi wananchi.

Pia upo umuhimu wa kutosha wa lengo (f) linalohusu uendelezaji wa rasimali watu kwa lengo la kuwaongezea ujuzi na vitendea kazi. Katika ulimwengu wa sasa ambao unachagizwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia, mambo mengi yanabadilika na rasimali watu pia inapaswa kubadilika ili kuendana na mabadiliko hayo. Njia pekee ya kuwezesha hilo kufanyika ni kutoa mafunzo na vitendea kazi vya kisasa kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati imeridhika na malengo mapya yaliyoingizwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwani baadhi yanalenga kuongeza ukusanyaji wa mapato ambao ni nguzo muhimu ya kuiwezesha Serikali itekeleze majukumu yake kikamilifu, mengine yanalenga kusimamia kikamilifu uendeshaji wa huduma za Elimu na Afya nchini. Aidha, malengo yote yaliyoanishwa hapo juu yanaendana na Mpango wa Taifa wa mwaka 2016/2017, pamoja na majukumu ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

4.2 Uchambuzi wa makadirio ya Mapato

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, inakadiria kukusanya jumla ya **Shs. 677,519,562,143** kwa mgawanyo utakaooneshwa katika Jedwali hapo chini. Mapato hayo yameongezeka kwa Shs. **147,758,981,835** sawa na asimia 27.89 ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, makusanyo hayo yanatarajiwa kutokana na kuuza vifaa chakavu pamoja na nyaraka za zabuni, faini mbalimbali, marejesho ya masurufu na mishahara. Aidha, kwa upande wa Halmashauri, makusanyo yatatokana na ushuru na kodi mbalimbali na vyanzo vingine vya mapato vilivyopo kwa mujibu wa sheria.

Jedwali Na. 02 Mchanganuo wa Maduhuli na Makusanyo ya ndani

Ofisi/Taasisi	Makadirio
OR-TAMISEMI	13,503,000
Taasisi	11,761,119,000
Mikoa	330,112,000
Mamlaka za Serikali za Mitaa	665,414,828,000
JUMLA	677,519,562,000

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa uchambuzi kama unavyoonekana katika Jedwali Na. 02, makusanyo makubwa yanatarajiwa kupatikana kutoka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Sababu kubwa kuhusiana na mafanikio hayo ni kwamba, Mfumo wa Serikali za Mitaa ndiyo wenye watu wengi na unamiliki vyanzo vingi vya mapato. Aidha, Ofisi ya Rais – TAMISEMI ndiyo inaonekana kuwa na kiwango kidogo sana cha ukusanyaji wa maduhuli.

4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, zinaombewa kuidhinishiwa jumla ya **Shs. 6,052,600,953,000** kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Tawala za Mikoa na katika Serikali za Mitaa. Kati ya fedha hizo zinazombwa, **Shs. 4,421,869,501,000** ni za kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shs. 1,630,731,452,000** ni kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo. Pia kati ya Fedha hizo, zipo **Shs. 10,047,792,000** za Mishahara na Matumizi Mengineyo kwa ajili ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC).

Mheshimiwa Spika, kiasi cha Fedha kinachoombwa kimeongezeka kwa **Shs. 635,451,833,031** sawa na asilimia kumi na mbili (12%) ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016 kwa ajili ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Taasisi zake, Mikoa na MSM.

Uchambuzi umebaini kwamba, kumekuwa na ongezeko kubwa la fedha za miradi ya maendeleo, kutoka Shs. **932,741,708,000** katika mwaka wa fedha 2015/2016 hadi **Shs. 1,630,731,452,000** katika mwaka 2016/2017. Hili ni ongezeko la takribani asilimia 74. 83

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla wake Ofisi ya Rais – TAMISEMI ndiyo inayoongoza kwa kuwa na bajeti kubwa dhidi ya Wizara nyingine, zikilinganishwa na bajeti ya Taifa. Kwa mfano katika mwaka wa fedha 2016/2017 bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI imefikia asilimia 20.49 ya Bajeti ya Taifa ambayo ni takribani Shs. Trilioni 29.539. hata hivyo, kiwango hicho ni pungufu ikilinganishwa na uwiano wa namna hiyo katika mwaka wa bajeti uliopita ambapo bajeti ya TAMISEMI ilikuwa ni asilimia 24 ya bajeti yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgawanyo wa makadirio ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ni kama yanavyooneshwa katika jedwali lifuatalo:-

**Jedwali Na 3: Mgawanyo wa makadirio ya Bajeti ya OR- TAMISEMI,
Mikoa na Halmashauri kwa Mwaka wa Fedha 2016/ 2017**

AINA YA MATUMIZI	2015/16	2016/17	Ongezeko	Asilimia
Matumizi ya kawaida				
OR – TAMISEMI				
Mishahara Makao Makuu	6,610,032,000	8,130,978,000	1,520,946,000	29
Mishahara ya Taasisi	15,031,920,000	14,385,939,000	-645,981,000	23
Matumizi Mengineyo Makao Makuu	8,287,248,800	3,835,054,000	-4,452,194,800	-54
Matumizi Mengineyo Taasisi	14,793,959,200	2,561,303,000	-12,232,656,200	-83
JUMLA	44,723,160,000	28,913,274,000	-15,809,886,000	-35
Tume ya Utumishi wa Walimu				
Mishahara	0	6,442,019,000	6,442,019,000	
Matumizi Mengineyo	0	3,605,773,000	3,605,773,000	
Jumla		10,047,792,000	10,047,792,000	

AINA YA MATUMIZI	2015/16	2016/17	Ongezeko	Asilimia
Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa				
Mikoa:				
Mishahara	165,927,484,513	153,036,181,000	-12,891,303,513	22
Matumizi Mengineyo	38,026,727,456	37,786,227,000	-240,500,456	-1
Jumla	203,954,211,969	190,822,408,000	-13,131,803,969	-6
Mamlaka za Serikali za Mitaa				
Mishahara	3,475,326,897,000	3,593,880,663,000	118,553,766,000	18
Matumizi Mengineyo	547,928,284,000	598,205,364,000	50,277,080,000	9
JUMLA	4,023,255,181,000	4,192,086,027,000	168,830,846,000	4
Mpango wa maendeleo				
OR-TAMISEMI	350,865,626,000	325,469,218,000	-25,396,408,000	10
Mikoa	50,905,589,000	64,701,480,000	13,795,891,000	35
Mamlaka za Serikali za Mitaa	743,445,352,000	1,240,560,754,000	497,115,402,000	84
JUMLA	1,145,216,567,000	1,630,731,452,000	485,514,885,000	42
JUMLA KUU	5,417,149,119,969	6,052,600,953,000	635,451,833,031	12

Chanzo: Randama ya TAMISEMI

5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia taarifa za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, taarifa za utekelezaji wa bajeti iliyopita na maombi ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka ujao wa fedha, Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo:-

1. Serikali ihakikishe Halmashauri zote nchini zinatenga kikamilifu asilimia 10 ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya Wanawake na Vijana. Kamati ilibaini kwamba, Halmashauri nyingi zinatenga asilimia 3 - 7 tu kwa lengo hilo na hata fedha hiyo kidogo haitolewi yote kwa makundi hayo. Vile vile, kuwe na utaratibu wa kuanisha vikundi vya Wanawake na Vijana walionufaika na fedha hizo na namna zitakavyorejeshwa ili kutoa fursa kwa wengine kukopeshwa. Aidha, kundi la Wajane nalo lipewe uzito stahili kama wanufaika wa fedha hizo.

2. Kwa kuwa, suala la Watumishi hewa limekuwa mchwa unaotafuna taifa kwa muda mrefu kwa kula fedha ambazo zingehudumia na kuwaletea Wananchi maendeleo, Kamati inashauri Serikali kuweka mfumo madhubuti wa ufuatiliaji utakaohusisha uhakiki kwa kuzingatia orodha ya malipo ya mishahara ya kila mwezi na kutoa taarifa katika vikao vya DCC na RCC.

3. Kwa kuwa, Halmashauri zinashindwa kukusanya ushuru kwa baadhi ya Minara ya Simu kutokana na Kampuni za simu kuwalipa Watu binafsi au Vijiji iliko minara hiyo, Kamati inashauri Serikali iandae utaratibu wa kisheria utakaowezesha Halmashauri nchini kukusanya kikamilifu ushuru wa huduma za Minara ya Simu na Mabango.

4. Serikali iendeele kusisitiza matumizi ya mfumo wa kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri kwani umeonesha mafanikio makubwa katika kusaidia kuongeza mapato na kudhibiti wizi na ubadhilifu. Mfumo huu ukitumika kikamilifu utaziwezesha Halmashauri kuachana na Mawakala katika ukusanyaji wa mapato, na hivyo kuokoa fedha zilizokuwa zikipotea kutokana na sababu mbalimbali.

5. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imekuwa hairejeshi asilimia 30 ya Kodi ya Ardhi kwa Halmashauri husika kama inavyotakiwa na sheria, Kamati inashauri uandaliwe utaratibu utakaoziruhusu Halmashauri kukata kodi hiyo kabla ya kuwasilisha fedha Wizarani.

6. Halmashauri ziandae utaratibu wa kuelimisha na kuhamasisha makundi mbalimbali ya jamii kujiunga na Bima ya Afya na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) kwa lengo la kuwawezesha kupata huduma ya afya kwa gharama

nafuu. Kamati inashauri kwamba, yawekwe masharti ya lazima kwa makundi yenye vipato kama vile Waendesha Pikipiki (Bodaboda), Mama na Baba Lishe, na Wafanyabiashara Ndogo Ndogo (Wamachinga) kujiunga na Bima ya Afya, kabla ya kupatiwa leseni au vibali vingine.

7. Halmashauri zibuni vyanzo vya mapato ili kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani, na hivyo kuondoa ushuru mdogo mdogo ambao ni kero kwa Wananchi, kama inavyoelezwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

8. Serikali iangalie namna ya kuwawezesha au kuwalipa Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa ili waweze kusaidia kuhamasisha ulipaji wa kodi, ushuru na tozo mbalimbali katika maeneo yao.

9. Halmashauri ziandae mpango wa matumizi bora ya ardhi ikiwa ni pamoja na kupima maeneo ili kuondoa migogoro ya Wakulima na Wafugaji, kudhibiti ukuaji holela wa miji, na kuwezesha utunzaji wa mazingira.

10. Kwa kuwa, Halmashauri nyingi zinakabiliwa na madeni kutoka kwa Wazabuni na Wakandarasi, Kamati inashauri Serikali kutoa fedha ili madeni hayo yalipwe na kuondoa usumbufu ambao wanakumbana nao watendaji kutoka kwa wadeni wao.

11. Halmashauri zisimamie kikamilifu Sheria ndogo za usafi wa mazingira, ili kupunguza au kuondoa kabisa uwezekano wa milipuko ya magonjwa hususani kipindupindu.

12. Kwa kuwa shule za kuanza kutekelezwa kwa tamko la kutoa elimu bure katika ngazi ya Msingi na Sekondari kumesababisha ongezeko kubwa la wanafunzi wanaojiunga na shule, na hivyo kuzalisha mahitaji makubwa ya miundombinu ya elimu (madawati, vyumba vya madarasa n.k), Kamati inashauri Serikali ianze mikakati ya kukabiliana na ongezeko hilo la mahitaji ili utekelezaji wa tamko hilo uwe na tija.

13. Kwa kuwa, ukusanyaji wa ushuru wa majengo (Property tax) katika Halmashauri za Manispaa utatekelezwa na TRA, ni vyema Serikali ikawa makini na uamuzi huo hasa ikizingatiwa kuwa mamlaka hiyo haikupata mafanikio huko nyuma, ikilinganishwa na mafanikio yaliyoonyeshwa na Serikali za Mitaa.

14. Kwa kuwa, ucheleweshaji au kutotolewa kabisa kwa fedha za maendeleo kumekuwa kunaathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kamati

inashauri Serikali kutoa fedha zote zinazotengwa kwa ajili ya miradi ili kutoathiri utekelezaji wa miradi hiyo.

15. Kwa kuwa, Awamu ya Kwanza ya Ujenzi wa Miundombinu ya Mradi wa Mabasi yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART) umekamilika, Kamati inashauri mamlaka husika ikamilishe mfumo wa ukusanyaji nauli kwa njia ya kielektroniki pamoja na kupanga nauli, ili huduma ya usafiri huo ianze haraka. Kuanza kwa huduma hiyo, kutasaidia kupunguza adha ya msongamano kwa wakazi wa jiji la Dar es Salaam ambayo pia imekuwa na athari zingine kiuchumi na kijamii.

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa kabisa, naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kwa kuniadini na kunichagua kuwa kiongozi wao. Wameonesha ushirikiano, weledi na utaalumu wa hali ya juu katika kuhoji na kuchambua masuala mbalimbali ya kisera yaliyo chini ya Ofisi ya Rais.

Aidha, niwashukuru kwa mahudhurio mazuri wakati wa vikao na kwa kujitolea kufanya kazi kwa saa nyingi hadi usiku bila kudai malipo ya ziada. Hii ni ishara kwamba Wajumbe wa Kamati wamejitoa kikamilifu kulitumikia Bunge na Taifa kwa ujumla. Kwa umuhimu mkubwa, naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Jasson Samson Rweikiza, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Pudenciana Wifred Kikwembe, Mb –Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Margret Simwanza Sitta, Mb, - Mjumbe
4. Mhe. Angelina Adam Malembeka Mb
5. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb
6. Mhe.Emmanuel Papian John,Mb
7. Mhe.Esther Alexander Mahawe John,Mb
8. Mhe.George Malima Lubeleje,Mb
9. Mhe.Halima Ali Mohamed,Mb
10. Mhe.Hamad Salim Maalim,Mb
11. Mhe.Halima Salim Ibrahim,Mb
12. Mhe.Hassanali Mohamed Raza,Mb
13. Mhe.Innocent Sebba Bilakwate,Mb
14. Mhe.Josephine Tabitha Chagula,Mb
15. Mhe.Khamis Ali Vuai,Mb
16. Mhe.Maida Hamad Abdallah,Mb
17. Mhe.Mariam Ditopile Mzuzuri,Mb

18. Mhe.Mwanne Ismail Mchemba,Mb
19. Mhe.Mwatum Dau Haji,Mb
20. Mhe.Ruth Hiyobi Mollel,Mb
21. Mhe.Saada Mkuya Salum,Mb
22. Mhe.Salum Khamis Salum,Mb
23. Mhe.Sebastian Simon Kapufi,Mb
24. Mhe.Venance Methusela Mwamoto,Mb
25. Mhe.Zacharia Paulo Isaaya,Mb
26. Mhe.Saed Ahmed Kubenea,Mb

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ninamshukuru Mhe. George Boniface Simbachawene, (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa akisaidiwa na Mhe. Seleman Said Jafo (Mb), Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Watendaji wa Ofisi hiyo wakiongozwa na Eng. Musa Iyombe Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa jinsi walivyoshiriki kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge wa Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, na kufafanua kwa kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kuwashukuru Wakuu wa Mikoa yote ya Tanzania Bara, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri zote nchini, kwa kuwasilisha vyema taarifa za utekelezaji wa bajeti iliyopita na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashillilah, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Mambo ya Jumla, Ndg. Angelina Sanga, Makatibu wa Kamati Ndg. Chacha Nyakega, Ndg. Victor Leonard na Ndg. Eunike Shirima, wakisaidiwa na Ndg. Mariam Ally, kwa uratibu wa shughuli zote za Kamati katika kipindi chote hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja hapo awali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Jasson S. Rweikiza (Mb)

MWENYEKITI

Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa

Aprili, 2015

MWENYEKITI: Tunaendelea na Kamati hiyo hiyo kwa upande wa Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mwenyekiti, karibu!

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA
KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS, UTUMISHI NA UTAWALA
BORA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI
KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA
FEDHA 2016/2017 KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI**

MHE. JASSON S. RWEIKIZA- MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ifuatayo ni taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utangulizi; kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2015/2016, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ilifanya ziara za ukaguzi katika miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka 2015/2016, bajeti ya ofisi hii kwa mwaka 2016/2017.

MWENYEKITI: Waheshimiwa, naombeni tushauriane kwa staha!

MHE. JASSON S. RWEIKIZA- MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora inahusisha jumla ya Mafungu kumi kama ifuatavyo:

Fungu 20 - Ofisi ya Rais, Ikulu; Fungu 30 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri; Fungu 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Fungu 33 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; Fungu 67 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma; Fungu 94 - Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma; Fungu 9 - Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Maslahi Katika Utumishi wa Umma; Fungu 6 - Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji na Utekelezaji wa Miradi; Fungu 4 - Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa na Fungu 11 - Ofisi ya Rais, Ushauri wa Mafuta na Gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla maelezo ya utangulizi yanatuelekeza katika mambo manne ambayo taarifa hii itajikita katika kutoa ufafanuzi wake, nayo ni:-

- 1) Matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotembelewa na Kamati.
- 2) Mapitio ya taarifa ya utekelezaji wa mpango kwa bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/16.
- 3) Uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi hii kwa mwaka 2016/17 na;
- 4) Maoni na ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufafanuzi wa miradi ya maendeleo iliyolengwa kukaguliwa. Katika mwaka wa fedha 2015/16, Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora ilitengewa shilingi bilioni 157.7 kwa ajili ya maendeleo ya miradi kupitia Mafungu matano. Miongoni mwa miradi hiyo iliyotekelezwa na ofisi hiyo ni ile ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) na Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara ya Wanyonge - MKURABITA. Ufafanuzi wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

Mradi namba 6220 unaojulikana kama *Support to Tanzania Social Action Fund* ulitengewa jumla ya shilingi bilioni 127.4 na ulipangwa kutekelezwa chini ya Kifungu 1003 cha Fungu 30 cha Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. Kupitia mradi huu kaya maskini nchini zitawezeshwa kuboresha maisha na hatimaye iwe chachu ya kuboresha mahudhurio ya watoto shuleni pamoja na kliniki kwa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano. Mahudhurio ya watoto shuleni na kliniki vinatumika kama vigezo vikuu vya kuzingatwa ili walengwa waendeleo kunufaika na utaratibu wa kupokea fedha kwani watoto kutoka kaya maskini wamekuwa wakiathirika zaidi kwa kukosa huduma za afya na elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Kigoma - Ujiji, Kamati ilitembelea Mitaa ya Mkese na Kibwe iliyopo katika Kata ya Kagera. Mtaa wa Kibwe una jumla ya kaya 370 na walengwa ambao ni wazee, wajane, wagane na watoto. Hadi Machi mwaka huu mtaa ulikwishapokea malipo kwa walengwa kwa awamu kumi yenye thamani ya shilingi milioni 99.8. Kwa upande wa Mtaa wa Mkese, kaya zilionufaika na mpango huu ni 90, hadi mwezi Machi wakati huo mtaa ulikuwa umepokea malipo ya walengwa ya awamu kumi yenye thamani ya shilingi milioni 29.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhawilishaji fedha kwa kaya maskini Mkoani Dar es Salaam. Katika Wilaya ya Kinondoni, Kamati ilitembelea mradi wa uhawilishaji fedha katika Mtaa wa Hananasif katika Kata ya Hananasif na Mtaa wa Kisiwani uliopo Kata ya Makumbusho. Mtaa wa Hananasif una jumla ya kaya 112 zinazonufaika na mpango huu na hadi Machi ulikuwa umepokea malipo ya uhawilishaji kwa awamu nne yenye thamani ya shilingi milioni 23.9. Katika Mtaa wa Kisiwani, jumla ya 155 zilinufaika na hadi Machi uhawilishaji ulikuwa umefanyika kwa awamu nne kwa kiasi cha shilingi milioni 33.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhawilishaji wa fedha kwa kaya maskini katika Mkoa wa Mwanza. Kamati ilitembelea Kata ya Mahina yenye Mitaa ya Wananchi na Isegenge B. Mtaa wa Wananchi wenye kaya 241 una walengwa 964 na hadi Machi malipo yalikuwa yamefanyika kwa awamu tano yakiwa na thamani ya shilingi milioni 47.99. Katika Mtaa wa Isegenge B' jumla ya kaya 163 zenye walengwa 415 zilinufaika na hadi Machi, jumla ya shilingi milioni 36.5 zilitolewa kwa ajili ya malipo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi namba 4921 ujulikanao kama Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania - MKURABITA ullitengewa jumla ya shilingi bilioni tatu na unatekelezwa chini ya Kifungu 1003 cha *Policy and Planning* cha Fungu 30 - Ofisi ya Rais, Sekretariet ya Baraza la Mawaziri. Mradi huu unalenga kuwasaidia wanyonge kurasimisha mali walizonazo ili ziweze kusaidia kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mpango huu katika Vijiji vya Kitongosima na Shinembo Wilayani Magu, ulihusisha urasimishaji wa ardhi ambapo upimaji wa maeneo umefanyika kwa lengo la kubainisha maeneo ya kilimo, makazi, malisho na huduma za jamii. Kupitia MKURABITA, jumla ya mashamba 1,139 yamepimwa na kuandaliwa Hati Stahiki za Kimila zipatazo 1,200, gharama za kuandaa hati moja ni sh. 35,000 na hadi sasa Hati Stahiki za Kimila 331 zimesajiliwa na zinaweza kutumika kama dhamana kupata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya ukaguzi. Katika ukaguzi wa miradi iliyotekelezwa chini ya *Support Tanzania Social Action Fund*, Kamati ilibaini kwamba kuna mwenendo mzuri wa ukusanyaji wa fedha na utekelezaji wa miradi hiyo umekuwa mzuri na hivyo kuleta tija. Kamati ilibaini kwamba mpango wa kuhawilisha fedha katika maeneo yaliyotembelewa na Kamati imeonesha mafanikio makubwa ikiwa ni pamoja na walengwa kuongezewa kipato na hivyo kuweza kumudu mahitaji muhimu kama vile chakula.

Vile vile baadhi ya walengwa wametumia kipato hicho kama mtaji na hivyo kuanzisha miradi ya ujasiriamali kwa lengo la kujiongezea kipato. Miradi wanayojihusisha nayo ni kama vile ufugaji wa kuku na bata, kilimo cha mazao ya chakula na biashara ndogondogo kama za kuuza samaki na dagaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kuongezeka kwa mahudhurio ya watoto shuleni na watoto walio chini ya miaka mitano kliniki kumwezesha kutambulikana kwa lengo la uhawilishaji na kuhakikisha watoto wa kaya maskini wanapata fursa ya kuhudhuria shuleni na katika huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini kuwa licha ya mafaniko yaliyopatikana, utekelezaji wa mradi huu unakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na zifuatazo:-

(1) Serikali kutotoa sehemu ya mchango wake katika fedha za utekelezaji wa mradi huu na kuacha jukumu hilo kwa wahisani peke yake.

(2) Ukosefu wa elimu ya kutosha kwa wananchi kuhusiana na lengo la mradi wa uhawilishaji fedha.

(3) Ukosefu wa taarifa sahihi kutoka kaya maskini, jambo ambalo limesababisha baadhi ya wasio na sifa kunufaika na mradi huku wenye sifa wakiachwa.

(4) Tabia ya baadhi ya walengwa kutuma ndugu na jamaa ili kuwachukulia fedha imekuwa ikisababisha baadhi yao kukosa mafunzo ya afya yatolewayo kabla ya malipo.

(5) Kukosekana kwa vituo vya afya katika baadhi ya mitaa kunakwamisha baadhi ya walengwa kutimiza masharti ya afya kwa maana ya kupeleka kliniki watoto walio chini ya miaka mitano.

(6) Baadhi ya viongozi kuingiza siasa katika zoezi la uhawilishaji fedha na;

(7) Baadhi ya walengwa katika jamii kuwa na mtazamo potofu kwamba fedha hizi ni za kishirikina au zinatokana na kundi la *freemason*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia, baadhi ya walengwa katika jamii kuwa na mtazamo potofu kwamba fedha za *TASAF* ni za kishirikina na zinatolewa na kundi la *freemason*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mradi namba 4621, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania katika Vijiji vya Kitongosima na Shinembo vilivyopo katika Wilaya ya Magu, Kamati ilibaini kwamba utekelezaji wake umeenda vizuri na mashamba 1,133 yamefanikiwa kupimwa na hati 1200 zimeandaliwa. Kamati ilibaini kwamba licha ya mpango huo mzuri na ambao utekelezaji wake umeenda vizuri, bado kuna kasoro kadhaa ikiwemo ya wananchi kutogomboa hati zao ambazo ziko tayari kwa madai kwamba gharama ya kugomboa ni kubwa.

Hadi sasa zaidi ya hati 350 hazijagombolewa kutokana na wananchi kudai kwamba kiasi kinachodaiwa cha sh. 35,000 ni kikubwa, hali hiyo inaathiri kuendelea kwa mradi kwani zilitumika shilingi milioni 44 katika upimaji na uandaaji wa hati hizo za kimila, hivyo zinatakiwa kurudi ili kuwezesha maeneo mengine ya nchi kupata huduma hii. Ni vema Halmashauri kwa kushirikiana na MKURABITA wakaona namna ya hati hizo zitakavyogombolewa ili kuwezesha zoezi hili kuendelea mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ipo changamoto ya kutokuwa na masjala za ardhi za vijiji katika vijiji vyetu ambavyo vitatumika kuhifadhi Hati Stahiki za Kimila. Inashauriwa hili liangaliwe na mamlaka husika kwa kushirikiana na vijiji ili kuwezesha masjala za Hati Stahiki za Kimila kuanzishwa katika vijiji na hivyo kuwapunguzia wananchi usumbufu katika kuhifadhi hati zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2015/16. Kutokana na ziara kwenye miradi ya maendeleo, Kamati ina maoni yafuatayo:-

(1) Mradi wa uhawilishaji fedha kwa kaya maskini unaotekelezwa na *TASAF* uwe na malengo mazuri ya kusaidia familia maskini kujikwamua, lakini elimu zaidi inahitajika ili watu waweze kuelewa malengo hayo.

(2) Elimu zaidi itolewe kuhusuiana na wanaopaswa kunufaika na uhawilishaji wa fedha ili kuepuka watu wasio na sifa kunufaika.

(3) Wananchi wanapaswa kuondokana na dhana potofu kwamba fedha zinazogawiwa katika zoezi la uhawilishaji fedha zina uhusiano na imani za kishirikiana na ni kundi la *freemason*.

(4) Baadhi ya viongozi wamekuwa wakiingiza siasa katika miradi, waache.

(5) Kukosekana kwa vituo vya afya katika baadhi ya mitaa kunakwamisha baadhi ya walengwa kutimiza masharti ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti na uzingatiaji wa maoni ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Kwa miaka kadhaa sasa tumeshuhudia mwenendo wa bajeti wa Serikali usio na ulinganifu kati ya kile kinachoidhinishwa na Bunge lako Tukufu dhidi ya kile kinachotolewa na Serikali au Hazina. Mambo matatu yamekuwa yakijitokeza katika eneo hili kama ifuatavyo:-

- (1) Fedha zilizoidhinishwa kutotolewa kwa wakati.
- (2) Fedha zilizoidhinishwa kutolewa kidogo.
- (3) Fedha zilizoidhinishwa kutotolewa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ya namna hii ni sawa na kitendawili ambacho ama hakina jibu au jibu analijua aliyekitoa. Kwa muktadha huo Kamati ilijaribu kufanya ulinganisho wa fedha zilizopokelewa na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora na Mafungu yake kutoka Hazina hadi kufikia mwisho wa robo ya tatu ya mwaka wa fedha na kiasi cha fedha kilichoidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi unaonesha kwamba hadi kufikia mwezi Machi 2016, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, pamoja na mafungu yaliyo chini yake zilikuwa zimepokea jumla ya shilingi bilioni 458.7 kutoka Hazina kwa ajili ya matumizi ya Kawaida ya Maendeleo, kiasi hicho cha fedha ni sawa na asilimia 82.6 ya fedha yote iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa fedha za maendeleo uchambuzi unaonesha kwamba hadi mwisho mwa robo ya tatu ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2015/2016, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora na mafungu yake ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 116.9 sawa na asilimia 74.2 ya fedha yote iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati. Wakati wa kuchambua bajeti ya mwaka 2015/2016, Kamati ilishauri mambo mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha bajeti hiyo inatekelezwa kwa ufanisi. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora ilizingatia kikamilifu maoni na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2015 ya CCM, mwongozo wa taarifa wa kuandaa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na maeneo muhimu ya kuzingatiwa kama ilivyoainishwa na Serikali ya Awamu ya Tano imepanga kutekeleza mambo yafuatayo:-

- Fungu 20 na 30; Ofisi ya Rais, Ikulu na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri kuendelea kutoa huduma kwa Rais na familia yake, kutoa huduma za ushauri kwa Rais katika maeneo ya uchumi, siasa, masuala ya jamii, sheria, mawasiliano na habari kwa umma, mahusiano ya Kimataifa na maeneo mengine kwa kumshauri Rais.

- TAKUKURU kuandaa Sera ya Taifa ya Kupambana na Rushwa na kufuatilia miradi ya maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kudhibiti uhalifu na kuongeza ufanisi wa miradi hiyo.

- Kuwezesha MKURABITA kukamilisha ujenzi wa masjala za ardhi za vijiji kumi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa sita Tanzania Bara na moja Zanzibar na kufundisha matumizi bora ya Hati za Haki Miliki za Kimila.

- TASAF kuhawilisha ruzuku kwa kaya maskini zipatazo milioni 1.4 katika mizunguko sita ya malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 20 - Ofisi ya Rais, Ikulu inaomba kuidhinishwa shilingi bilioni 15.9 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, Fungu 30 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri inaomba kuidhinishwa shilingi bilioni 785.08; Fungu 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaomba kuidhinishwa kiasi cha shilingi bilioni 38; Fungu 33 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma inaomba kuidhinishwa shilingi bilioni 3.54; Fungu 67 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma inaomba kuidhinishwa shilingi bilioni 2.54; Fungu 94 - Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma inaomba kuidhinishwa shilingi bilioni 4.15; Fungu 09 - Ofisi

ya Rais, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma inaomba kuidhinishiwa shilingi bilioni 1.88.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Fungu 06 - Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji na Utekelezaji wa miradi inaomba kuidhinishiwa shilingi bilioni 3.54; Fungu 04 - Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa inaomba kuidhinishiwa shilingi bilioni 1.67.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 11 - Ofisi ya Rais Ushauri wa Mafuta na Gesi Asilia, hii ni taasisi mpya chini ya Ofisi ya Rais Ikulu ambayo imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Petroli ya mwaka 2015. Hiki ni chombo cha Taifa cha ushauri wa kitaalam kuhusu masuala ya uchumi wa mafuta na gesi asilia, Fungu hili linaomba kuidhinishiwa shilingi milioni 198.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati. Baada ya kupitia taarifa za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, taarifa ya utekelezaji wa bajeti iliyopita na maombi ya makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka ujao, Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo:-

(1) Kwa kuwa, suala la watumishi hewa limekuwa mchwa wanaotafuna Taifa kwa muda mrefu kwa kula fedha ambazo zingewahudumia wananchi katika maendeleo, Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu utakaotambua watumishi wote na pia kufanya ukaguzi wa kushtukiza wa mara kwa mara;

(2) Kwa kuwa, taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora zinakabiliwa na ukosefu wa majengo kwa ajili ya ofisi na pia vitendea kazi vingine; Kamati inaishauri Serikali kuingilia kati jambo hili na kusaidia taasisi hizo ili ziweze kuondokana na adha hiyo ambayo pia inalichafua jina la Ofisi ya Rais;

(3) Wananchi wapewe elimu ya kutosha kuhusiana na utekelezaji wa mpango wa *TASAF III* ili waweze kutoa taarifa zilizo sahihi wakati wa kujaza dodoso;

(4) *TASAF* ifanye tathmini inayolenga kubaini watu wasio na sifa ambao wananufaika na mpango wa uhawilishaji fedha ili iwaondoe katika utaratibu huo na kuwachukulia hatua za kisheria; (*Makofi*)

(5) *TASAF* iangalie namna ya kutumia fedha ya uhawilishaji kuzisaidia kaya maskini ziweze kuanzisha miradi ya kuziingizia kipato ili ziweze kujijengea uwezo wa kiuchumi badala ya kuendelea kuwa tegemezi;

(6) Viongozi na Wanasiasa waelimishwe vya kutosha kuhusiana na TASAF III ili wasaidie kushawishi wananchi kuikubali badala ya kuingiza siasa;

(7) TASAF ijikite katika utekelezaji wa miradi itakayoinufaisha jamii kwa ujumla badala ya kulenga mtu mmoja mmoja. Mfano ni miradi ya maji, shule, zahanati, barabara na kadhalika;

(8) Kuwepo na utaratibu wa kutumia sehemu ya fedha za wanufaika wa uhawilishaji kuwaunganisha na Mifuko ya Afya ya Jamii (CHF) ili kuwawezesha kupata kuduma za afya;

(9) Serikali iwezeshe kifedha Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) ili uweze kuongeza kasi ya kuwafikia wananchi wengi na kuwasaidia kurasimisha mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Kwa heshima na unyenyekevu mkubwa kabisa, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kwa kuniamini na kunichagua kuwa Mwenyekiti wao. Wamedhihirisha ushirikiano, ueledi na utaalum wa hali ya juu katika kuhoji na kuchambua masuala mbalimbali ya kisera yaliyo chini ya ofisi hii. Aidha, nawashukuru kwa mahudhurio mazuri wakati wa vikao na kwa kujitolea kufanya kazi kwa saa nyingi hadi usiku bila kudai malipo ya ziada. Hii ni ishara kwamba Wajumbe wa Kamati wamejitolea kikamilifu kutumikia Bunge na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile nina muda na kwa unyenyekevu mkubwa naomba niwatambue kwa kuwataja majina yao: Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Mwenyekiti.....

MWENYEKITI: Kanuni hazituruhusu sasa hivi kwa hayo.

MHE. JASSON S. RWEIKIZA- MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati, namshukuru Mheshimiwa Angellah Kairuki, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, pamoja na Watendaji wa ofisi hiyo wakiongozwa na Ndugu Peter Ilomo, Katibu Mkuu Ikulu; Ndugu Laurian Ndumbaro, Katibu Mkuu Utumishi; na Bi. Suzan Mlawi; Naibu Katibu Mkuu Utumishi, kwa jinsi walivyoshiriki kujibu hoja za Wajumbe wa Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na kufafanua kwa kina kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/2017. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashilillah, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Mambo ya Jumla; Ndugu Angelina Sanga, Makatibu wa Kamati Ndugu Chacha Nyakega, Ndugu Victor Leonard na Ndugu Eunike Shirima, wakisaidiwa na Ndugu Mariam Ali kwa uratibu wa shughuli zote za Kamati kipindi chote hadi wakati wa kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala bora kwa mwaka wa fedha 2016/2017, kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante, Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa kwa taarifa ya Kamati.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA
KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS, UTUMISHI NA UTAWALA
BORA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI
KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA
2016/2017 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 6(4) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 inaipa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, wajibu wa kusimamia shughuli za Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, pamoja na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kaunui za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 jukumu la uchambuzi wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, limewekwa chini ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa.

Vilevile Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Bunge, imeweka sharti kwa Kamati za Kisekta ikiwemo hii ya Utawala na Serikali za Mitaa, kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayokuwa imetengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha. Naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ilifanya ziara za ukaguzi katika miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na kuchambua Bajeti ya ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora inahusisha jumla ya Mafungu Kumi (10) kama ifuatavyo:-

- i. **Fungu 20:** Ofisi ya Rais, Ikulu;
- ii. **Fungu 30:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri;
- iii. **Fungu 32:** Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma;
- iv. **Fungu 33:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
- v. **Fungu 67:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;
- vi. **Fungu 94:** Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma;
- vii. **Fungu 09:** Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma;
- viii. **Fungu 06:** Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi;
- ix. **Fungu 04:** Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa; na
- x. **Fungu 11:** Ofisi ya Ushauri wa Mafuta na Gesi

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla maelezo ya utangulizi yanatuelekeza katika mambo manne ambayo Taarifa hii itajikita katika kutoa ufafanuzi wake. Mambo hayo ni haya yafuatayo:-

- i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotembelewa na Kamati;
- ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016;
- iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017; na
- iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

2.1 Ufafanuzi wa Miradi ya Maendeleo iliyolengwa kukaguliwa

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha 2015/2016, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora ilitengewa **Tsh.157, 776,040,000/-** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kupitia mafungu matano yafuatayo:

- i. Fungu 30:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri – **Tshs. 135,503,265,000;**
- ii. Fungu 32:** Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma – **Tshs – 6,259,944,000;**
- iii. Fungu 33:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma – **Tshs. 1,485,897,000;**
- iv. Fungu 06:** Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi – **Tshs. 14,276,934,000;**
- v. Fungu 04:** Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa – **Tshs. 250,000,000;** na

Miongoni mwa miradi iliyotekelezwa na ofisi hiyo ni ile ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) na Mpango wa Kurasimisha Rasimali na Biashara za Wanyonge (MKURABITA). Ufafanuzi wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi Na. 6220 unaojulikana kama Support to Tanzania Social Action Fund, ulitengewa jumla ya shilingi 127,416,434,000 na ulipangwa kutekelezwa chini ya kifungu 1003 cha Fungu 30 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri.

Kupitia mradi huu Kaya maskini nchini zitawezeshwa kuboresha maisha na hatimaye iwe chachu ya kuboresha mahudhurio ya Watoto shuleni pamoja na Kliniki kwa Watoto walio chini ya umri wa miaka mitano. Mahudhurio ya Watoto shuleni na Kliniki, vinatumika kama vigezo vikuu vya kuzingatiwa ili walengwa waendeleo kunufaika na utaratibu wa kupokea fedha kwani, watoto kutoka Kaya maskini wamekuwa wakiathirika zaidi kwa kukosa huduma za afya na elimu.

Katika Wilaya ya Kigoma Ujiji, Kamati ilitembelea Mitaa ya Mkese na Kibwe iliyopo katika Kata ya Kagera. Mtaa wa Kibwe una jumla ya Kaya 370 za walengwa ambao ni Wazee, Wajane, Wagane na Watoto. Hadi Machi Mtaa ulikwishapokea malipo ya Walegwa kwa awamu kumi (10) yenye thamani ya **Tshs. 99,818,727-**

Kwa upande wa Mtaa wa Mkese, Kaya zinazonufaika na mpango huu ni 90 na hadi mwezi Machi, wakati huo Mtaa ulikuwa umepokea malipo ya Walengwa kwa awamu ya 10 yenye thamani ya Tshs. **29,925,454.57/=**.

Mheshimiwa Spika, Uhawilishaji Fedha kwa Kaya Maskini – Mkoani Dar es Salaam. Katika Wilaya ya Kinondoni, Kamati ilitembelea Miradi ya Uhawilishaji fedha katika Mtaa wa Hananasifu katika Kata ya Hananasifu na Mtaa wa Kisiwani uliopo Kata ya Makumbusho.

Mtaa wa Hananasifu una jumla ya Kaya 112 zinazonufaika na mpango huu na hadi Machi ulikuwa umepokea malipo ya uhawilishaji kwa awamu nne (4) yenye thamani ya **Tshs. 23,920,909/-**

Katika Mtaa wa Kisiwani jumla ya Kaya 155 zinanufaika na hadi Machi Uhawilishaji ulikuwa umefanyika kwa awamu nne (4) na **Tshs. 33,350,954/-** zilikuwa zimelipwa.

Mheshimiwa Spika, Uhawilishaji fedha kwa Kaya Maskini katika Mkoa kwa Mwanza. Kamati ilitembelea Kata ya Mahina yenye Mitaa ya Wananchi na Isegenge B. Mtaa wa Wananchi wenye kaya 241 una walengwa 964 na hadi Machi, malipo yalikuwa yamefanyika kwa awamu tano (5) yakiwa na thamani ya **Tshs. 47,997,522/=**

Katika Mtaa wa **Isegenge B** jumla ya Kaya 163 zenye Walengwa 815 zinanufaika na hadi mwezi Machi, jumla ya Tsh. **36,518,681** zilikuwa zimetolewa kwa ajili ya malipo.

Mheshimiwa Spika, Mradi Na.4921 ujulikanao kama Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA), ulitengewa jumla ya Tshs. 3,000,000,000/- na unatekelezwa chini ya kifungu 1003 cha Policy and Planning, cha Fungu 30 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. Mradi huu unalenga kuwasaidia Wanyonge kurasimisha maliwalizonazo ili ziweze kuwasaidia kujikwamua kiuchumi.

Utekelezaji wa mpango huu katika Vijiji vya Kitongosima na Shinembo, Wilayani Magu ulihusisha urasimishaji wa Ardhi ambapo upimaji wa maeneo umefanyika kwa lengo la kubainisha maeneo ya kilimo, makazi, malisho na huduma za jamii. Kupitia MKURABITA jumla ya Mashamba 1139 yamepimwa na kuandaliwa Hati Stahiki za Kimila zipatazo 1,200. Gharama ya kuandaa Hati moja ni **shilingi 35,000/=** na hadi sasa Hati Stahiki za Kimila 331 zimesajiliwa na zinaweza kutumika kama dhamana katika mikopo.

Na gharama ya kuandaa Hati moja ya eneo la ekari Tano (5) ni shilingi 35,000/=. Utekelezaji wa Mpango huu katika Kijiji cha Kitongosima umegharimu Tshs. 44,030,000/- na kwa vijiji vya Kitongosima na Shinembo, kwa lengo la kukusanya tshs. 95,000,000/=. Bado halmashauri ya wilaya ipo kwenye utekelezaji wa mpango huu kwa vijiji vingine kuhakikisha malengo yanafikiwa.

2.2 Matokeo ya Ukaguzi

Mheshimiwa Spika, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) na kufanya ziara za ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha unaoisha. Kwa kuzingatia Kanuni ya 117 (18) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 Kamati ilijigawa katika makundi mawili na kufanya ziara za ukaguzi wa miradi iliyoanishwa.

Mheshimiwa Spika, katika ukaguzi wa miradi inayotekelezwa chini Support to Tanzania Social Action Fund, Kamati ilibaini kwamba kuna mwenendo mzuri wa upatikanaji fedha na utekelezaji wa miradi hiyo umekuwa mzuri na hivyo kuleta tija.

Kamati ilibaini kwamba, mpango wa kuhawilisha fedha katika maeneo yaliyotembelewa na Kamati umeonesha mafanikio kadhaa ikiwa ni pamoja na walengwa kuongezewa kipato na hivyo kuweza kumudu mahitaji muhimu kama vile chakula. Vilevile, baadhi ya walengwa wametumia kipato hicho kama mitaji na hivyo kuanzisha miradi ya kiujasiriamali kwa lengo la kujiongeza kipato. Miradi wanayojihusisha nayo ni kama vile, ufugaji wa kuku na bata, kilimo cha mazao ya chakula na biashara ndogo ndogo za kuuza samaki na daga.

Aidha, kuongezeka kwa mahudhurio ya Watoto shuleni na Watoto walio chini ya miaka mitano Kliniki, kumwezesha kutambulikana kwa lengo la uhawilishaji la kuhakikisha Watoto wa Kaya maskini wanapata fursa ya kuhudhuria shuleni na katika huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa licha ya mafanikio yaliyopatikana, utekelezaji wa mradi huu unakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na:-

- Serikali kutotoa sehemu ya mchango wake katika fedha za utekelezaji wa mradi na kuacha jukumu hilo kwa Wahisani tu;
- Ukosefu wa elimu ya kutosha kwa Wananchi kuhusiana na lengo la mradi wa Uhawilishaji fedha;

- Ukosefu wa taarifa sahihi kutoka Kaya maskini, jambo ambalo limesababisha baadhi ya wasio na sifa kunufaika na mradi huku wenye sifa wakiachwa;
- Tabia ya baadhi ya Walengwa kutuma ndugu na jamaa ili wawachukulie fedha, imekuwa ikisababisha baadhi yao kukosa mafunzo ya afya yatolewayo kabla ya malipo
- Kukosekana kwa Vituo vya Afya katika baadhi ya Mitaa kunakwamisha baadhi ya Walengwa kutimiza masharti ya afya, kwa maana ya kupeleka Kliniki watoto walio chini ya miaka mitano;
- Baadhi ya Viongozi kuingiza siasa katika zoezi la uhawilishaji fedha, na
- Baadhi ya walengwa katika jamii kuwa na mtazamo potofu kwamba, fedha zinazotolewa katika uhawilishaji ni za kishirikiana “zinatolewa na kundi la Freemason”

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitaka kujua ni vipi changamoto hizo zinaweza kutatuliwa, na kuelezwa kwamba, upo mpango wa kuelimisha zaidi wananchi kuhusiana na mradi huo, na kuwashawishi kutoa taarifa sahihi pale watakapopelekewa dodoso. Pia watu wanaotoka Kaya zinazoonekana kuwa maskini zaidi, wasione aibu bali watoe taarifa sahihi ili waweze kusaidiwa.

Jambo linalosisitizwa hapa ni kwamba, ili kuondoa baadhi ya kasoro zilizobainika na ambazo zinalalamikiwa na Wananchi, ni vyema kufanya zoezi la uhakiki wa kina kwa lengo la kubaini kasoro zilizopo na kuzitafutia ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mradi Namba 4921 Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania, katika Vijiji vya Kitongosima na Shinembo vilivyopo katika Wilaya ya Magu, Kamati ilibaini kwamba, utekelezaji wake umeenda vizuri na mashamba 1133 yamefanikiwa kupimwa na hati 1200 zimeandaliwa.

Kupitia mradi huu baadhi ya Wananchi wamefanikiwa kupimiwa maeneo yao na kuandaliwa Hati Stahiki za Kimila. Utaratibu huo umewaondoa katika unyonge kwani ardhi waliyokuwanayo kwa miaka mingi sasa ina thamani na wanaweza kuitumia kupata mikopo kutoka taasisi za benki. Ni katika mazingira hayo ndipo inapokuja dhana ya kurasimisha mali za Wanyonge. Kwamba, mtu anayo raslimali lakini haiwezi kumsaidia kwa sababu haijarasimishwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kwamba, licha ya mpango huo mzuri na ambao utekelezaji wake umeenda vizuri, bado kuna kasoro kadhaa ikiwemo ya Wananchi kutogomboa hati zilizo tayari kwa madai ya gharama ya kugombolea kuwa kubwa. Hadi sasa zaidi ya Hati 350 hazijagombolewa

kutokana na Wananchi kudai hawana fedha, huku gharama ya Hati moja ikiwa ni **shilingi 35,000/=** hali hiyo inaathiri kuendelea kwa mradi, kwani zilitumika shilingi milioni 44 katika upimaji na uandaaji wa Hati Stahiki za Kimila, hivyo zinatakiwa kurudi ili kuwezesha maeneo mengine ya nchi kupata mradi huu. Ni vyema Halmashauri kwa kushirikiana na MKURABITA wakaona namna Hati hizo zitakavyogombolewa ili kuwezesha zoezi hilo kuendelea mbele.

Mheshimiwa Spika, aidha, ipo changamoto ya kutokuwa na Masijala za Ardhi za Vijiji, katika vijiji vyetu ambazo zitatumika kuhifadhi Hati Stahiki za Kimila. Inashauriwa hili liangaliwe na mamlaka husika kwa kushirikiana na vijiji, ili kuwezesha Masijala za Hati Stahiki za Kimila kuanzishwa katika vijiji na hivyo kuwapunguzia wananchi usumbufu katika kuhifadhi hati zao.

2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa Fedha 2015/2016

Mheshimiwa Spika, kutokana na ziara kwenye miradi ya Maendeleo, Kamati ina maoni yafuatayo:-

- i. Mradi wa Uhawilishaji fedha kwa Kaya Maskini unaotekelezwa na TASAF una malengo mazuri ya kusaidia familia maskini kujikwamua, lakini elimu zaidi inahitajika ili watu waweze kuelewa malengo hayo.
- ii. Elimu zaidi itolewe kuhusiana na wanaopaswa kunufaika na Uhawilishaji fedha ili kuepuka watu wasio na sifa kunufaika;
- iii. Wananchi wanapaswa kuondokana na dhana potofu kwamba, fedha zinazogaiwa katika zoezi la Uhawilishaji zina uhusiano na imani za kishirikina au kundi la Freemason;
- iv. Baadhi ya Viongozi wamekuwa wakiingiza siasa katika miradi
- v. Kukosekana kwa Vituo vya Afya katika baadhi ya Mitaa kunakwamisha baadhi ya Walengwa kutimiza masharti ya afya.

3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ilijikita katika kuangalia mwenendo na upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa. Njia kubwa zilizotumika katika uchambuzi huu ni kuangalia hali halisi, kuzingatia taarifa mbalimbali

zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu wakati wa vikao vya Kamati.

Mheshimiwa Spika, ufafanuzi wa uchambuzi umefanywa kwa kutumia jedwali, asilimia, ulinganishaji na utofautishaji. Ili kurahisisha maelezo, Kamati imetumia chati na grafu kufafanua. Maelezo haya ni kama ifuatavyo:-

3.1.2 Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina

Mheshimiwa Spika, kwa miaka kadhaa sasa tumeshuhudia mwenendo wa bajeti ya Serikali usio na ulinganifu kati ya kile kinachoidhinishwa na Bunge lako Tukufu, dhidi ya kile kinachotolewa na Hazina. Mambo matatu yamekuwa yakijitokeza katika eneo hili kama ifuatavyo:-

- Fedha zilizoidhinishwa kutotolewa kwa wakati;
- Fedha zilizoidhinishwa kutolewa kidogo;
- Fedha zilizoidhinishwa kutotolewa kabisa.

Mazingira ya namna hii, ni sawa na Kitendawili ambacho ama hakina jibu, au jibu analijua aliyekitoa. Kwa muktadha huo, Kamati ilijaribu kufanya ulinganisho wa fedha zilizopokelewa na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora (na mafungu yake) kutoka Hazina hadi kufikia mwisho wa robo ya Tatu ya mwaka wa fedha na kiasi cha fedha kilichoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Uchambuzi unaonesha kuwa, hadi kufikia mwezi Machi, 2016 Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora pamoja na mafungu yaliyo chini yake, zilikuwa zimepokea **Shs. 458,755,416,118** kutoka Hazina kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kiasi hicho cha fedha ni sawa na asilimia 82.86 ya fedha yote iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa fedha za maendeleo uchambuzi unaonesha kwamba, hadi mwishoni mwa robo ya tatu ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora na Mafungu yake, ilikuwa imepokea jumla ya **Shs. 116,905,944,324** sawa na asilimia 74.21 ya fedha yote iliyoidhinishwa.

Kwa ufafanuzi huo, Kamati imebaini kwamba, mwenendo wa upatikanaji wa fedha (ie. Matumizi ya Kawaida na Maendeleo) kwa ujumla ulikuwa mzuri, kwani fedha zilizopatikana zilikuwa ni takribani asilimia 83 ya fedha zote zilizoidhinishwa. Tafsiri inayoweza kuelezwa hapa ni kwamba, kiwango

kilichokadriwa kwa ajili ya kila robo ya mwaka wa fedha kilipatikana chote pamoja na ziada.

Aidha, katika fedha za maendeleo uwiano unaonesha kwamba, mwenendo wa upatikanaji wa fedha ulikuwa mzuri pia kwani ulikuwa ni takribani asilimia 75. Hata hivyo, bado hapa kuna kasumba kwamba, fedha za matumizi ya kawaida lazima ziwe juu ya fedha za maendeleo.

3.1.3 Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchambua bajeti ya Mwaka 2015/2016, Kamati ilishauri mambo mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha bajeti hiyo inatekelezwa kwa ufanisi. Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora ilizingatia kikamilifu maoni na ushauri wa Kamati

4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

4.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoanishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2015 ya Chama Cha Mapinduzi, Mwongozo wa Taifa wa Kuandaa Mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na maeneo muhimu ya kuzingatiwa kama yalivyoanishwa na Serikali ya Awamu ya Tano, imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

Fungu 20 & 30: Ofisi ya Rais, Ikulu na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri

- Kuendelea kutoa huduma kwa Rais na familia yake
- Kutoa huduma za ushauri kwa Rais katika maeneo ya Uchumi, Siasa, Masuala ya Jamii, Sheria, Mawasiliano na Habari kwa Umma, Mahusiano ya Kimataifa na maeneo mengine kwa kumshauri Rais;
- Kuwezesha TAKUKURU kuandaa Sera ya Taifa ya Kupambana na Rushwa, na kufuatilia miradi ya maendeleo katika mamlaka za Serikali za Mitaa ili kudhibiti uhalifu na kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa miradi hiyo;
- Kuwezesha MKURABITA kukamilisha ujenzi wa masjala za ardhi za Vijiji 10 katika mamlaka za Serikali za Mitaa 6 Tanzania bara na 1 Zanzibar, na kufundisha matumizi bora ya Hati za Haki Miliki za Kimila.

- Kuwezesha TASAF kuhawilisha ruzuku kwa Kaya maskini zipatazo milioni 1.4 katika mizunguko Sita ya malipo.

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kutekeleza Mpango wa mwaka wa fedha 2016/2017, Fungu 20 Ofisi ya Rais, Ikulu inaomba kuidhinishiwa Tshs. 15,995,138,000 kwa ajili ya Matumizi ya kawaida. Aidha, **Fungu 30:** Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, inaomba kuidhinishiwa **Tshs. 785,086,946,000**. Kati ya fedha hizo **Tshs. 354,637,917,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Tshs. 430,449,029,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Fungu 32: Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma.

- Kuandaa mapendekezo ya kutungwa kwa Sheria ya Mishahara katika Utumishi wa Umma;
- Kuandaa Sera ya Serikali Mtandao na Mkakati wa Utekelezaji wake
- Kusimamia ajira za Watumishi wa Umma pamoja na kupandisha vyeo;
- Kutumia Chuo cha Utumishi wa Umma ili kutoa mafunzo kwa Watumishi wa kada mbalimbali;
- Kutumia Wakala wa Serikali Mtandao (eGA) kuunganisha Taasisi za Serikali 100 kwenye mfumo wa pamoja na salama wa barua Pepe wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha 2016/2017, kwa ufanisi, Fungu 32: Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaomba kuidhinishiwa kiasi cha Tshs. 38,003,648,814. Kati ya fedha hizo **Tshs. 30,503,648,814** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Tshs. 7,500,000,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Fungu 33: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

- Kuchapisha ,kutuma na kupokea Tamko la Viongozi wa Umma kuhusu raslimali na madeni linalopaswa kutolewa kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya viongozi wa Umma ya Mwaka 1995; na
- Kufanya uhakiki wa matamko ya raslimali na Madeni kwa Viongozi wa Umma 500.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa Fedha 2016/2017, Fungu 33 Sekretarieti ya maadili ya Viongozi wa Umma linaomba kuidhinishiwa Tshs. 3,542,860,000. Kati ya fedha hizo **Tshs. 2,542,860,000** ni kwa ajili

ya Matumizi ya Kawaida na **Tshs. 1,000,000,000** nikwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Fungu 67: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma

- Kusimamia na kuendesha mchakato wa ajira ili kuwezesha Waajiri kupata Watumishi wenye sifa; na
- Kuimarisha Kanzidata za Wahitimu kutoka Vyuo mbalimbali na kutunza takwimu;

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa Fedha 2016/2017, Fungu 67: Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, linaomba kuidhinishiwa jumla ya Tshs. 2,542,307,000 kwa jili ya Matumizi ya Kawaida.

Fungu 94: Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma

- Kuratibu Mikutano ya Kisheria ya kila robo mwaka kwa ajili ya Tume kutoa uamuzi kwa rufaa, malalamiko na masuala mengine ya kiutumishi; na
- Kufanya Ukaguzi wa Kawaida kwa Taasisi 100 ili kuangalia uzingatiaji wa usimamizi wa rasimali watu katika utumishi wa Umma;

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha 2016/2017, Fungu 94, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma linaomba kuidhinishiwa kiasi cha **Tshs.4,151,577,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Fungu 09: Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma.

- Kukamilisha tathmini ya kazi na uhuishaji Madaraja kwa Watumishi wa Umma
- Kufanya utafiti kwa ajili ya kuandaa mfumo wa Utoaji Motisha kwa kuzingatia tija; na
- Kukamilisha Mwongozo wa kupendekeza na kupanga mishahara na maslahi katika utumishi wa Umma

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza Mpango wa bajeti wa Mwaka wa Fedha 2016/2017, Fungu 09 linaomba kutumia **Tshs. 1,883,005,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Fungu 06: Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi

- Kufuatilia utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati katika Sekta za Nishati na madini, Usafirishaji na Uchukuzi, maabara ya ukusanyaji mapato, utekelezaji wa upatikanaji wa asilimia 100 ya wafanyakazi wa sekta ya afya;
 - Kuwezesha ushiriki wa Sekta binafsi kwenye miradi ya vipaumbele;
- na
- Kufuatilia utekelezaji wa mkakati wa kuhakikisha asilimia 80 ya Vituo vya Afya na Zahanati vinakuwa na hadhi ya nyota tatu na kuendelea ifikapo Juni 2018;

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa Fedha 2016/2017, Fungu 06: Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi linaomba kuidhinishiwa jumla ya **Tshs. 3,542,860,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Fungu 04: Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa

- Kuandaa na kuanzisha mfumo wa kielktroniki wa utunzaji, usimamizi na matumizi ya kumbukumbu katika Taasisi za Umma.
- Kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu na vitu vya Waasisi wa Taifa
- Kukagua, kuchambua na kuhamisha kumbukumbu kutoka Ofisi za Kanda za Idara na taasisi za Umma kwenda Kituo cha taifa cha Kumbukumbu Dodoma na;
- Kuhuisha mifumo ya utunzaji Kumbukumbu katika Wizara ili kuendana na mabadiliko ya miundo ya Wizara katika Serikali ya Awamu ya Tano

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha 2016/2017, Fungu 04: Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa linaomba kuidhinishiwa **Tshs. 1,670,411,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida; na

Fungu 11: Ofisi ya Ushauri ya Mafuta na Gesi

Mheshimiwa Spika, hii ni taasisi mpya chini ya Ofisi ya Rais, Ikulu ambayo imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Petroli ya mwaka 2015. Hiki ni chombo cha Taifa cha ushauri wa kitaalam kuhusu masuala ya uchumi wa mafuta na gesi asilia.

Ili kutekeleza mpango wa Bajeti wa mwaka 2016/2017, Fungu 11 ofisi ya Ushauri wa Mafuta na Gesi Asilia inaomba jumla ya Tshs. **198,939,000**.

Mheshimiwa Spika, malengo mengi yaliyoorodheshwa yanajirudia, na kupitia uchambuzi Kamati ilibaini kwamba, kulikuwa na haja ya msingi katika kujirudia kwa malengo hayo. Kwa mfano malengo ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kuhusiana na Tamko la Mali na Madeni yataendelea kujirudia kwa sababu maadili ni jambo linalotakiwa kukumbushwa kila siku na viongozi ama wanaingia katika madeni au wanapata mali hivyo ni vyema wakaendelea kukumbushwa kutoa taarifa.

5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia taarifa za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, taarifa za utekelezaji wa bajeti iliyopita na maombi ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka ujao wa fedha, Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo:-

1. Kwa kuwa, suala la Watumishi hewa limekuwa mchwa unaotafuna taifa kwa muda mrefu kwa kula fedha ambazo zingewahudumia Wananchi katika maendeleo, Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu utakaotambua Watumishi wote na pia kufanya ukaguzi wa kushitukiza wa mara kwa mara;

2. Kwa kuwa, Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, zinakabiliwa na ukosefu wa majengo kwa ajili ya ofisi na pia vitendea kazi vingine, Kamati inashauri Serikali kuingilia kati jambo hili na kusaidia taasisi hizo ili ziweze kuondokana na adha hiyo ambayo pia inachafua jina la Ofisi ya Rais;

3. Wananchi wapewe elimu ya kutosha kuhusiana na utekelezaji wa Mpango wa TASAF III ili waweze kutoa taarifa zilizo sahihi wakati wa ujazaji wa dodoso;

4. TASAF ifanye tathmini itakayolenga kubaini watu wasio na sifa ambao wananufaika na mpango wa uhawilishajisha fedha, iwaondoe katika utaratibu huo na kuwachukulia hatua za kisheria;

5. TASAF iangalie namna ya kutumia fedha za uhawilishaji kuzisaidia Kaya maskini ziweze kuanzisha miradi ya kuizingizia kipato ili ziweze kujijengea uwezo wa kiuchumi badala ya kuendeleza utegemezi;

6. Viongozi wa siasa waelimishwe vya kutosha kuhusiana na utekelezaji wa miradi ya TASAF ili wasaidie kushawishi Wananchi kuikubali, badala ya kuingiza siasa;

7. TASAF ijikite katika utekelezaji wa miradi itakayonufaisha jamii kwa ujumla badala ya kulenga mtu mmoja mmoja. Mfano ni miradi ya maji, shule, zahanati, barabara na kadhalika;

8. Uwekwe utaratibu wa kutumia sehemu ya fedha za Wanufaika wa Uhawilishaji kuwaunganisha na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) ili kuwawezesha kupata huduma ya afya.

9. Serikali iwezeshe kifedha Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) ili uweze kuongeza kasi ya kuwafikia wananchi wengi na kuwasaidia kurasimisha mali zao.

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa kabisa, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kwa kuniamini na kunichagua kuwa Mwenyekiti wao. Wamedhihirisha ushirikiano, weledi na utaalumu wa hali ya juu katika kuhoji na kuchambua masuala mbalimbali ya kisera yaliyo chini ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

Aidha, niwashukuru kwa mahudhurio mazuri wakati wa vikao na kwa kujitolea kufanya kazi kwa saa nyingi. Hii ni ishara kwamba Wajumbe wa Kamati wamejitoa kikamilifu kulitumikia Bunge na Taifa kwa ujumla. Kwa umuhimu mkubwa, naomba niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Jasson Samson Rweikiza, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mb–Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Margret Simwanza Sitta, Mb, - Mjumbe
4. Mhe. Angelina Adam Malembeka Mb
5. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb
6. Mhe.Emmanuel Papian John,Mb
7. Mhe.Esther Alexander Mahawe,Mb
8. Mhe.George Malima Lubeleje,Mb
9. Mhe.Halima Ali Mohamed,Mb
10. Mhe.Hamad Salim Maalim,Mb
11. Mhe.Halima Salim Ibrahim,Mb
12. Mhe.Hassanali Mohamed Raza,Mb
13. Mhe.Innocent Sebba Bilakwate,Mb
14. Mhe.Josephine Tabitha Chagula,Mb
15. Mhe.Khamis Ali Vuai,Mb
16. Mhe.Maida Hamad Abdallah,Mb

17. Mhe.Mariam Ditopile Mzuzuri,Mb
18. Mhe.Mwanne Ismail Mchemba,Mb
19. Mhe.Mwatum Dau Haji,Mb
20. Mhe.Ruth Hiyobi Mollel,Mb
21. Mhe.Saada M. Salum,Mb
22. Mhe.Salum Khamis Salum,Mb
23. Mhe.Sebastian Simon Kapufi,Mb
24. Mhe.Venance Methusela Mwamoto,Mb
25. Mhe.Zacharia Paulo Isaaya,Mb
26. Mhe.Saed Ahmed Kubenea,Mb

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ninamshukuru Mhe. Angellah Kairuki, (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora pamoja na Watendaji wa Ofisi hiyo wakiongozwa na Ndg. Peter Ilomo, Katibu Mkuu Ikulu Dr. Luran Ndumbalo Katibu Mkuu, Utumishi na Bi. Suzan Mlawi, Naibu Katibu Mkuu, Utumishi, kwa jinsi walivyoshiriki kujibu hoja za Wajumbe wa Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, na kufafanua kwa kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kasilillah, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Husein, Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Mambo ya Jumla, Ndg. Angelina Sanga, Makatibu wa Kamati Ndg. Chacha Nyakega, Ndg. Victor Leonard na Eunike Shirima, wakisaidiwa na Ndg. Mariam Ally, kwa uratibu wa shughuli zote za Kamati katika kipindi chote hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja hapo awali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Jasson S.Rweikiza (Mb)

MWENYEKITI

Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa

Aprili, 2015

MWENYEKITI: Sasa tunahamia upande wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tupate maoni yao. Tunaanza na Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusiana na hoja ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Japhary Michael.

HOTUBA YA MHESHIMIWA JAPHARY MICHAEL, AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KATIKA OFISI YA RAIS – TAMISEMI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17 KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS - TAMISEMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Maoni haya yanatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu ya kuwa ndani ya Bunge hili na kuweza kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Napenda pia kutumia nafasi hii kumshukuru Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe, kwa kuniadini na kunipa nafasi ya kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Naahidi kwake na kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuwashukuru wananchi wa Moshi ambao wamenipa nafasi ya kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, hayo mambo ya kusoma Kifungu cha 154, mambo ya pongezi hayapo tena, tuendeleo.

(Hapa baadhi ya Wabunge walipiga kelele kuashiria kutokubaliana na maneno ya Mwenyekiti wa Bunge)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Raphael hebu keti kidogo. Waheshimiwa Wabunge, mimi sitachoka kuwaeleza mambo ya Kanuni.

(Hapa baadhi ya Wabunge walipiga kelele)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge...

Mheshimiwa Mbunge, tunalinda muda wako.

MBUNGE FULANI: Huyu kampongeza mpaka mume wake, kampongeza mpaka *houseboy*.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Tusiwe na *double standard*.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, niwapeleke kwanza kwenye Kanuni 154.

(Hapa baadhi ya Wabunge walipiga kelele)

MWENYEKITI: Kanuni 154 inazungumzia, endapo litatokea jambo baada ya Spika kutoa pongezi au pole, kwa ajili ya kuokoa muda wa majadiliano, Mbunge yoyote hataruhusiwa kutoa pongezi au pole kwa mahusiano ya mamlaka kwa jambo hilo wakati wowote wa majadiliano Bungeni.

Hii inarudufiwa kwenye eneo ambalo tunalo hivi sasa, kwa hiyo, Mheshimiwa Michael naomba tu uende *straight* kwenye hoja ya maoni yenu.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usiwe na *double standard* Waziri amesoma zaidi ya dakika 10 hapo Mheshimiwa Angellah, kapongeza mpaka wajukuu nyumbani, halafu unakuwa na *double standard*, Kanuni zianze kufuatwa kesho siyo leo.

MBUNGE FULANI: Chama Tawala

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nime mtambua Mheshimiwa Raphael, endelea.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini unatuburuza, tutendee haki Mwenyekiti. Hicho unachokifanya hakilingani na hadhi yako kwa sababu upande wa Serikali umewapongeza kurasa zaidi ya sita.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa nikisimama uketi.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Upande wa Serikali umepongeza zaidi ya dakika sita.

MWENYEKITI: Nakusihi uketi.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Unatulazimisha tufanye hivyo.

MWENYEKITI: Nakusihi uketi.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: *No, you are pushing us too far, unatulazimisha tufanye hivyo kwa sababu unachokifanya ni double standard yaani unatu-push tufanye hivyo, we respect you lakini siyo kwa stahili hiyo.*

MWENYEKITI: Nakusihi uketi mara ya mwisho.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mawaziri wamefanya vyote kama walivyofanya hapa.

MWENYEKITI: Kaa chini basi.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: aaah!

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Raphael!

(Hapa baadhi ya Wabunge walipiga kelele)

MHE. HAJI KHATIB KAI: Mheshimiwa kafanye kama kawaida.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS - TAMISEMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuvunja heshima ya kiti chako nawashukuru sana viongozi...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Haji tujiheshimu.

MHE. HAJI KHATIB KAI: Wewe mwenyewe unatulazimisha

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS - TAMISEMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia muda wangu uliopotea unisaidie kuulinda. Napenda kuwashukuru sana Viongozi wangu wa Kambi ya UKAWA kwa kazi kubwa ambayo wameifanya na mshikamano ambao wamekuwa nao miongoni wetu katika kujenga Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasikitishwa sana kuona Serikali ya CCM ikiwanyima wananchi haki ya kuona shughuli za Bunge moja kwa moja kwa kisingizio cha kubana matumizi, huku Serikali ikisahau

kwamba kupata habari sahihi ni jambo la lazima kama binadamu alivyo na mahitaji ya lazima kama chakula, malazi na mavazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha pia kuona Wabunge wa CCM wakiunga mkono jambo hili na kubeza ushauri wa Upinzani huku wakijua kabisa kuwa taarifa sahihi ni ile inayopatikana moja kwa moja kutoka kwenye chanzo cha habari hiyo na kwamba taarifa inayotolewa na nafasi ya pili na kuendelea huwa inakuwa na upungufu mwingi kiasi kwamba inaweza kupoteza maana yake ya awali na wakati mwingine ikatolewa na watu wasio na nia njema, inaweza kupotoshwa na hatimaye kuleta madhara katika Taifa na kulifanya Taifa kubeba gharama kubwa kuliko ya kuonyesha matangazo hayo moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kuruhusu Vyombo vya Habari vya Umma na vya Binafsi kurusha moja kwa moja mijadala ya Bunge ili wananchi wajue fedha zao zinavyogawanywa katika Halmashauri zao. Wajue ripoti ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inasemaje kuhusu Halmashauri zao, wajue namna ya kuzibana Halmashauri zao zifanye kazi ili zisifanye ubadhirifu na wapate hamasa ya kulipa kodi pale wanaporidhishwa na matumizi ya kodi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inawataka Wabunge wa CCM waache kufanya ushabiki Bungeni kwani tabia yao ya muda mrefu ya kupuuza maoni ya Wapinzani na kuwazomea ndiyo imelifikisha Taifa hapa lilipo, ambapo watu wachache wamepora utajiri wa Watanzania na kujilimbikizia wenyewe huku wakitumia Wabunge wa CCM....

MBUNGE FULANI: Lowassa.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS - TAMISEMI: Kuwatetea na kuwalinda kwenye Muhimili huu muhimu sana wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli ulio dhahiri kwamba tamthilia inayofanyika hivi sasa ya waliokuwa watetezi wakubwa wa ufisadi ya kutumbua majipu ni sawa na mchawi kutaka kurudisha msukule wake ambao yeye mwenyewe ndiye aliye uroga mpaka jamii ikaamini kuwa umekufa, kwa vyovyote vile hata akifanikiwa kuurudisha utakuwa ni zezeta, adhabu anayostahili mchawi huyo ni kuuawa ili asiendelee kuaminisha wengine kwamba kazi ya kuwatetea wengine ni kazi halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo adhabu wanayostahili Wabunge wa CCM walioshabikia ufisadi na ubadhirifu mpaka ukalifikisha Taifa hapa lilipo ya kuwa na majipu kila mahali ni kufutwa kabisa katika Uwakilishi wa wananchi ili Taifa lianze safari mpya ya kutengeneza Viongozi bora wanaomaanisha wanachotamka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uporaji wa madaraka ya Serikali za Mitaa unaofanywa kwa makusudi na Serikali Kuu. Msingi wa dhana ya ugatuzi wa madaraka (*decentralization*) ulikuwa ni kuzipa mamlaka Serikali za Mitaa ili ziweze kuendesha shughuli zake kwa uhuru kwa maslahi ya wananchi wa eneo husika. Aidha, upo mchakato wa kufanya ugatuzi kamilifu, *decentralization by devolution* maarufu kama *program ya D by D* ili kuzipa Serikali za Mitaa mamlaka kamili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifahamike kwamba chimbuko ya dhana ya mamlaka ya umma na uwepo wa Serikali za Mitaa ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 katika Ibara ya 145 na 146 sambamba na Sheria za Serikali za Mitaa ya Mamlaka za Wilaya za mwaka 1982 na Sheria za Serikali za Mitaa ya Mamlaka ya Miji ya mwaka 1982, ambazo kwa pamoja zilianzisha mamlaka hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha Serikali Kuu kuingilia madaraka ya Serikali za Mitaa ni kuvunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuvunja Sheria zilizoanzisha Serikali za Mitaa. Tangu kuundwa kwa Serikali za Mitaa hazijawahi kuwa na madaraka hata nusu tu ya yale yanayotajwa na Sheria zinazoongoza mamlaka hizo. Uongozi wake wote wa juu wa Serikali za Mitaa ukianzia Wakurugenzi wa Halmashauri, Makatibu Tawala wa Wilaya na Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa na hata Waziri mwenye dhamana wa TAMISEMI wote ni wateule wa Serikali Kuu na wanawajibika kwa Serikali Kuu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muundo huo wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa iko Serikali Kuu, Serikali za Mitaa hazina Mamlaka ya kuajiri, kutumia fedha zilizokusanya kwa shughuli zake za maendeleo mpaka zipate kibali kutoka Serikali Kuu. Kimsingi uhusiano uliopo kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ni kama ule wa Mnyapara na Mfungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka Waziri mwenye dhamana na TAMISEMI, ambaye mara kadhaa amesikika akijinasibu kuwa ni mtu anayefuata sheria kikamilifu, aanze kutekeleza sheria kwa kuacha kuingilia utendaji wa Serikali za Mitaa na badala yake kuziacha

zijiendeshe zenyewe ili kukidhi matakwa ya Sura ya Nane ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayohusu Madaraka ya Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kuleta Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Serikali za Mitaa, Mamlaka za Miji na Wilaya pamoja na Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, *Local Government Election Act*. Hii ni pamoja na mambo mengine sheria itamke kuwapa Mameya na Wenyeviti wa Halmashauri wenye nguvu ya kiutendaji (*Executive Power*), tofauti na ilivyo sasa ambapo wanakuwa ni Viongozi wa Kiitifaki (*Ceremonial Recognition*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kwamba, nafasi za kazi za Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji zitangazwe na waombaji wafanyiwe usaili kama ilivyo kwa Watumishi wengine wa umma na siyo kwa uteuzi wa kisiasa kama ilivyo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezo wa kutafuta mapato na uwezo wa kutumia fedha. Serikali kwa kuunda Halmashauri Mjini na Vijijini imetoa uwezo wa Madiwani wa kutafuta na kubuni njia mbalimbali za kupata fedha au mapato zinazolingana na gharama za huduma wanazotakiwa kuzitoa kwa wananchi katika maeneo husika. Halmashauri baada ya kutimiza uwezo wa fedha, zinazopewa uwezo wa kutumia fedha hizo kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1982. Madiwani huzipa Halmashauri uwezo wa kutoza kodi, ushuru, ada na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, urasimu wa Serikali Kuu katika kufanyia kazi maazimio ya Halmashauri mbalimbali nchini, umeziingizia hasara kubwa Halmashauri zetu mfano ni pale ambapo Halmashauri ya Manispaa ya Moshi imeshindwa kupata kibali cha kukopa Benki ya Rasilimali ya Tanzania (*TIB*), kwa miaka mitatu mfululizo kiasi kwamba hata thamani ya fedha ya miradi imebadilika. Jambo la kusikitisha zaidi ni pale unapokosa majibu ya ndiyo au hapana kutoka kwa mamlaka zenye dhamana na Serikali za Mitaa, hata pale majibu yakitokea yanachukua muda mrefu bila sababu za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua ni lini Serikali Kuu itaondoa urasimu huu ili kuzifanya Halmashauri ziweze kutimiza majukumu yake hasa ya miradi mbalimbali ambayo wanakuwa wameianzisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati za Uwekezaji za Halmashauri, Halmashauri zetu zimekuwa na utamaduni wa kuwa na Kamati mbalimbali za Kudumu kwa ajili ya kuendesha shughuli mbalimbali za Halmashauri husika.

Aidha, Halmashauri zinao uwezo wa kuanzisha Kamati mpya za Kudumu baada ya kupata ridhaa ya Waziri mwenye dhamana na TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa Halmashauri zetu kuwezesha kuwa na uwezo wa kungeza mapato yake ya ndani hivyo kuondoa utegemezi kutoka Serikali Kuu katika kujiendesha na kukuza maendeleo ya Taifa letu, ni vema tukaanzisha Kamati mpya ya Kudumu ya Uwekezaji kwenye Halmashauri zote nchini na iwe na jukumu la kuishauri Halmashauri juu ya masuala mbalimbali ya uwekezaji na mitaji.

Hii ni kutokana na ukweli kuwa, kwenye Halmashauri zetu kuna uwekezaji unaofanywa na ambao kutokana na hali halisi Mabaraza ya Madiwani yanakosa watu wenye weledi katika nyanja hii na hivyo kujikuta wakiweza kwenye miradi ambayo mwisho wa siku wanashindwa kuiendeleza au inakuwa haina tija ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasilimali ardhi ndiyo pekee ambayo unaikuta katika kila Halmashauri nchini iwe Jiji, Manispaa au Wilaya. Hivyo basi, ili kuziwezesha Halmashauri zetu kuwa na chanzo cha uhakika cha mapato ya ndani ni vema ule utaratibu wa awali wa Serikali Kuu kuchukua kiasi cha asilimia 70 cha mapato na kuiachia Halmashauri asilimia 30 utazamwe upya. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kuwa mapato yatokanayo na kodi ya tozo mbalimbali za ardhi yagawanywe katika mfumo wa Halmashauri kubakia na asilimia 70 ya mapato yote na Serikali Kuu ibakie na asilimia 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo hili linalenga kuziwezesha Halmashauri zetu kuwa na chanzo cha uhakika cha mapato na pia kuziwezesha Halmashauri zetu kuweza kupanga matumizi bora ya ardhi ikiwemo kupanga, kupima, kumilikisha, kulipa fidia na kutatua migogoro ya ardhi kwenye maeneo yao kwani watakuwa na rasilimali za kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuboresha maslahi ya Madiwani, Madiwani ni watumishi ambao wanafanya wajibu mkubwa sana. Kwa mujibu wa sheria zetu, Madiwani ndiyo wenye wajibu wa kusimamia uendeshaji wa Halmashauri kutafuta na kusimamia mapato yote ya Halmashauri zetu na hata fedha zote ambazo zinatoka Serikali Kuu zinasimamiwa na Madiwani kupitia Baraza la Madiwani. Hii maana yake ni kusema kuwa zaidi ya shilingi triloni sita ambazo zimetengwa na Bunge hili na ambazo Bunge hili litapitisha hapa zitaenda kusimamiwa na Madiwani wetu kwenye Halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Madiwani hawa ambao tumewapa majukumu makubwa ya kusimamia fedha za Halmashauri, malipo yao yamekuwa

hayalingani na ukubwa wa kazi ambazo wanafanya. Hali hiyo imepelekea utendaji kazi wao kuwa siyo wa kiwango cha kuridhisha na imefikia hata mahali pengine wachache wakawa wanachukua rushwa ili kukabiliana na maslahi duni ya Madiwani. Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kuwa maslahi ya Madiwani hasa mshahara na posho viongezwe ili kuweza kuendana na hali halisi ya maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Haki ya Wananchi kufuatilia mwenendo wa mchakato wa Bajeti; Ibara ya 8(1) (a) na (c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inasema kwamba, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi inayofuata misingi ya Demokrasia na haki ya kijamii, na kwa hiyo wananchi ndiyo msingi wa mamlaka yote na Serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba hii. Aidha, Serikali itawajibika kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo wananchi wana haki ya kujua Serikali yao inafanya nini, na Serikali inawajibika kuwapatia wananchi taarifa juu ya utendaji wake wa kazi. Katika hali ambayo haijaeleweka bado, Serikali hii ya Awamu ya Tano imeamua kwa makusudi kutumia mabavu kukataza urushwaji wa moja kwa moja wa vipindi vya majadiliano ya Bunge ili wananchi wasijue kinachondelea Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu Wabunge wakafahamu kwamba, bajeti ya TAMISEMI inayoombwa kuidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ni shilingi zaidi ya trilioni 6.023 ni sawa na asilimia 23 ya bajeti yote ya Serikali. Fedha hizi ni fedha za walipa kodi, ni fedha za umma, kujadili na kupitisha matumizi ya fedha za umma nyingi namna hii, bila ya wananchi kuwa na fursa ya kuona jinsi Bunge lao linavyofanya kazi ya kuwakilishwa katika kazi hiyo, siyo tu kunawakosesha haki yao ya msingi ya kupata habari, bali pia kunazua maswali mengi kwamba, pengine Serikali ina mpango wa siri wa kufuja fedha za umma katika matumizi yasiyo ya lazima, ndiyo maana haitaki wananchi wajue kinachondelea Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kufuta mara moja, katazo la kurusha matangazo ya Bunge moja kwa moja, kupitia televisheni ya Taifa na vyombo vingine vya habari vilivyokuwa vikirusha matangazo hayo awali, ili wananchi ambao ndiyo msingi wa mamlaka ya Serikali wapate haki yao ya msingi ya kufuatilia mwenendo wa mgawanyo wa fedha zao katika bajeti za Serikali kutoka moja kwa moja Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa Serikali itaendelea kuonesha jeuri na ukaidi kuhusu utekelezaji wa jambo hili kama inavyofanya sasa, basi Kambi Rasmi ya

Upinzani Bungeni, italazimika kuishitaki Serikali katika Mahakama ya Wananchi, Serikali hii ya Awamu ya Tano kwa kuwanyima wananchi haki ya kupata habari, tena ni habari zinazohusu fedha za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yafaa ikafahamika hapa kuwa, Bunge ni Mkutano wa hadhara wa wananchi wote, ila kwa kuwa hakuna ukumbi ama eneo ambalo wananchi wote wanaweza wakakusanyika kwa pamoja ndiyo maana utaratibu ukawekwa wa kutuma wawakilishi wachache kwa maana ya Wabunge kwa niaba ya wananchi wote, kwa nini tunawazuia wananchi kufuatilia mkutano wao wa hadhara, tena wa kugawana rasilimali zao kwa maana ya bajeti. Madaraka yasiyo na mwongozo ni sawa na bomu lisilo na mwelekeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa hotuba ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni kuhusu bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu ya tarehe 22 Aprili, 2016 ni kwamba, Serikali hii ya Awamu ya Tano inaendeshwa bila mwongozo na muundo wa kazi za kila Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo utekelezaji wa kazi za Serikali umekuwa ukitegemea zaidi utashi na uwezo binafsi wa kufikiri wa kiongozi wa Serikali ya ngazi husika. Katika kufanya hivyo wapo Viongozi wa Serikali wanafuata mfano wa mamlaka yao ya uteuzi wa kufukuza fukuza bila hata ya kuwasikiliza wale wanaofukuzwa, wakifikiri kwamba hivyo ndivyo mamlaka inavyotaka. Wapo pia wanaopitiliza mipaka ya utendaji wao wa kazi kwa sababu moja tu ya kutojua mipaka yao, kutokana na kutokuwepo kwa mwongozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitazungumzia Mawaziri ingawa somo hili linaweza likawa linawahusu, bali mimi nitawazungumzia Wakuu wa Mkoa, Wakuu wa Wilaya kwa kukosa mwongozo wa kutafsiri mipaka ya madaraka yao, wamekuwa ni sehemu ya migogoro mingi katika Halmashauri nyingi nchini; wamehusika sana kuchochea migogoro mingi katika maeneo yao ya utendaji wa kazi, mathalani migogoro ya wakulima na wafugaji, kwa ajili ya maslahi yao binafsi; wamehusika sana kupora maeneo ya ardhi na mali za Halmashauri kwa manufaa yao na rafiki zao; pia wamehusika sana kuingilia maazimio yanayopitishwa na Baraza la Madiwani katika Halmashauri husika kwa kutoa maagizo yanayokinzana na maazimio ya Baraza la Madiwani katika Halmashauri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilishapendekeza kufutwa kwa nafasi za Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa kutokana na majukumu yao kutojulikana bayana. Aidha, kuendelea kuwepo

kwa nafasi hizi ni kuongeza mzigo wa gharama za uendeshaji wa Serikali kwa kazi ambazo Wakurugenzi wa Halmashauri wakishirikiana na Mabaraza ya Madiwani wa Halmashauri husika wanaweza kufanya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kuangalia upya, tija na faida ya kuwepo kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kiuchumi na kiufanisi. Hii itasaidia kuongeza ufanisi wa Serikali za Mitaa, na pia itapunguza matumizi ya fedha za walipa kodi yasiyo ya lazima kwa ofisi ambazo hazizalishi bali zinatumia tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inawataka Wakuu wa Mikoa na Wilaya waliopo waache mara moja kutokuingilia utendaji wa Halmashauri na badala yake waheshimu maamuzi ya Mabaraza ya Madiwani kwa kuwa ndiyo vyombo halali vya maamuzi, kikatiba na kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muundo tata wa kiutawala katika Serikali za Mitaa. Licha ya Serikali za Mitaa kupewa mamlaka ya kikatiba na kisheria kujiendesha, lakini zimeshindwa kufanya hivyo kutokana na muundo tata wa kiutawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara zote zikifika ngazi ya TAMISEMI zinakuta utawala na uongozi mwingine, hivyo watendaji kulazimika kuwajibika sehemu mbili na mwisho wa hilo ni kurushiana mpira pale mambo yanapoharibika. Mfano mzuri pale unapokuwa na Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI anayehusika na elimu au afya, huyo anawajibika kwa Katibu Mkuu TAMISEMI au Katibu Mkuu Wizara husika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukirudi ngazi ya Halmashauri unamkuta Mkurugenzi ndiye Msimamizi Mkuu wa masuala yote ya maendeleo ya rasilimali za watu, lakini katika rasilimali hizo kuna baadhi ya kada ambazo zinawajibika moja kwa moja kwa Wizara husika. Halmashauri zina uwezo wa kuajiri kisheria lakini haziwezi kufanya hivyo mpaka zipate kibali kutoka Serikali Kuu. Uwajibikaji wa wote walioajiriwa bado uko katika hali ya utata. Mfano, Mkaguzi wa Ndani anawajibika kwa nani? Afisa Kilimo na Mifugo wa Wilaya na Mganga Mkuu wa Wilaya, Afisa Ardhi, Afisa Elimu wa Wilaya, wanawajibika kwa nani? Hali hii inasababisha *dual accountability* jambo ambalo linasababisha nidhamu ya uwajibikaji kuwa duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali za Mitaa haziwezi kujiendesha na kuleta tija kama muundo wake wa kiutawala na kiuwajibikaji hautafanyiwa marekebisho makubwa. Ili kuondoa tabia ya mfumo wa kikoloni wa Serikali Kuu

kuendelea kuzitawala na kuzinyonya Serikali za Mitaa. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kuandaa Muswada binafsi wa Sheria ya Serikali za Mitaa kwa kuwa Serikali inaonekana haina nia ya kufanya hivyo ili muundo na mfumo wa utawala na utendaji katika Serikali za Mitaa ufanyiwe *overwhelm* ili Serikali za Mitaa ziweze kujiendesha kwa tija na kufikia lengo la ugatuzi kamili wa madaraka, *decentralization by devolution* dhana ya (*D by D*). (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufisadi katika Serikali unaofanywa na Watendaji wa Serikali Kuu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haipingi kwamba kuna ufujaji wa hali ya juu wa fedha za umma katika Halmashauri zetu. Hata hivyo, Viongozi wa Serikali Kuu ambao ndiyo Watendaji, kwa maana ya *Accounting Officers* katika Serikali za Mitaa, wamekuwa vinara katika ubadhirifu unaoendelea, huku wakijificha kwenye kivuli cha jumla cha ubadhirifu wa Halmashauri na kuwaaminisha wananchi kwamba Madiwani wao ndiyo wabadhirifu wakati wao ndiyo wasukaji wa mtandao wa wizi na wanufaikaji wakubwa wa fedha za walipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli Serikali hii ina nia madhubuti ya kusimamia matumizi sahihi ya fedha za umma basi ianze kwanza kusafisha mtandao uliowekwa na Wakurugenzi na Wahasibu wa Halmashauri bila kufuata kanuni za ushindani na badala yake unafuata kujuana na urafiki binafsi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, programu ya uboreshwaji wa Serikali za Mitaa (*Local Government Reformed Program*). Programu za maboresho ya Serikali za Mitaa iliyoanzishwa mwaka 1998 ililenga kupeleka madaraka kwa wananchi kutokana na ukaribu uliopo kati ya Serikali za Mitaa na jamii. Wananchi wana matumaini makubwa na Serikali za Mitaa hivyo ngazi za chini katika Serikali za Mitaa zinahitaji kuwezesha sana kwa kuwa wao ndiyo wenye taarifa halisi za hali ya wananchi katika ngazi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, litakuwa ni jambo la ajabu kuzungumza Serikali za Mitaa bila kuwahusisha Wenyeviti wa Vijiji, Mitaa na Vitongoji pamoja na Wajumbe wao kama wanavyochaguliwa na wananchi katika maeneo husika, wao ndiyo kiunganisha kati ya wananchi na ngazi za juu zinazofuata kuhusu suala lolote linalohusu maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina mtazamo kwamba kada hii ya uongozi katika jamii ndiyo inayotakiwa kuwezesha ikiwa ni pamoja na kupatiwa mafunzo ya mara kwa mara, kuhusiana na mabadiliko yoyote yanayotokea na ambayo yanahusiana moja kwa moja na jamii.

Mipango yote ya huduma za kijamii inatakiwa ianzie na kuendelezwa kutoka katika ngazi hii ya uongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika muktadha huo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikisisitiza hoja ya kuwalipa posho ya majukumu Wenyeviti wa Mitaa, Vijiji na Vitongoji pamoja na Wajumbe wao, ili waweze kufanyakazi zao kwa ufanisi. Wananchi watakumbuka kwamba hoja ya kuwalipa posho Wenyeviti wa Mitaa, Vijiji na Vitongoji ni mojawapo ya sera za UKAWA kwenye Ilani ya Uchaguzi Mkuu uliopita. Tulipendekeza hivi kutokana na ukweli kwamba Wenyeviti na Wajumbe wao ndiyo wanafanya kazi za kuhamasisha wananchi katika ngazi za chini, na wamekuwa wakifanya hivyo kwa kujitolea miaka yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza asilimia 40 ya fedha hizo zitumike kuwalipa posho ya majukumu Wenyeviti wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji pamoja na Wajumbe wao, ili kuongeza ufanisi wa kada hizo katika maeneo yao ya kazi. Aidha, asilimia 60 inayobaki kwa maana ya fedha iliyotengwa shilingi bilioni 59 ndiyo iende kwenye mchakato wa mambo ya kiuchumi yatakayosaidia shughuli ya ujasiriamali katika maeneo ya Vijiji na Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; yapo mambo mengi sana ya kuzungumza katika Wizara ya TAMISEMI kwa kuwa huko ndiko kwenye wananchi, lakini inasaidia nini kujadili hayo yote gizani, ni kwa nini Serikali haitaki wananchi wafahamu kinachoendelea Bungeni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaendelea kuweka msisitizo wa hotuba ya Kiongozi wa Upinzani Bungeni wa kuitaka Serikali iheshimu Katiba ya nchi yetu na Sheria za nchi yetu katika kutekeleza majukumu yake. Katika hotuba hiyo ya Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, imebainika vilevile kwamba Serikali imevunja kifungu cha 41(1) cha Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015, na Kifungu cha 18 (3)na (4) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2011; ambapo kwa pamoja vinaitaka Serikali kuleta Bungeni nyongeza ya bajeti ili kupata idhini ya Bunge ikiwa fedha hizo zilizoidhinishwa awali hazikutosha kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa; lakini Serikali mara kadhaa imefanya matumizi ya fedha za umma nje ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge bila kuomba Bunge liidhinishhe bajeti ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni dharau kubwa sana kwa Bunge na uvunjwaji mkubwa sana wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.
(Makofi)

MWENYEKITI: Tunakushukuru kwa wasilisho lako.

**HOTUBA YA MHESHIMIWA JAPHARY MICHAEL (MB), AKIWASILISHA BUNGENI
MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU MAKADIRIO
YA MAPATO NA MATUMIZI KATIKA OFISI YA RAIS – TAMISEMI KWA
MWAKA WA FEDHA 2016/17 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*Inatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge,
Toleo la Januari, 2016*

1. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu na uwezo wa kusimama mbele ya Bunge lako tukufu ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya fedha katika Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2016/17.

Mheshimiwa Spika, Napenda pia kutumia nafasi hii kumshukuru Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman Mbowe (Mb), kwa imani kubwa aliyonayo kwangu ambayo ilimfanya aniteue kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Ninamwahidi utumishi uliotuka katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa kulihutubia Taifa kupitia Bunge, napenda kuchukua nafasi hii vilevile kutoa shukrani zangu za dhati kwa Chama changu cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) pamoja na wananchi wote wa Moshi Mjini kwa kunipa ridhaa yao ya kuwa mtumishi wao katika ngazi ya Ubunge, sambamba na kukipa chama chetu ridhaa ya kuongoza Halmashauri ya Manispaa Moshi.

Mheshimiwa Spika, Kwa namna ya pekee natoa pongezi kwa viongozi wetu wakuu wa vyama vinavyounda UKAWA kwa kazi kubwa waliyofanya ya kujenga umoja na mshikamano miongoni mwa vyama hivyo jambo ambalo limetupatia ushindi mkubwa katika Uchaguzi Mkuu uliopita.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasikitishwa sana kuona Serikali ya CCM ikiwanyima wananchi haki ya kuona shughuli za bunge moja kwa moja kwa kisingizio cha kubana matumizi huku serikali ikisahau kwamba kupata habari sahihi ni ni jambo la lazima kama binadamu alivyo na mahitaji ya lazima kama chakula, mavazi na malazi.

Mheshimiwa Spika, Inasikitisha pia kuona wabunge wa CCM wakiunga mkono jambo hili na kubeza ushauri wa upinzani huku wakijua kabisa kuwa taarifa sahihi ni ile inayopatikana moja kwa moja kutoka kwenye chanzo cha habari hiyo; na kwamba taarifa inayotolewa nafasi ya pili na kuendelea huwa inakuwa na mapungufu mengi kiasi kwamba inaweza kupoteza maana yake ya awali na wakati mwingine ikitolewa na watu wasio na nia njema inaweza kupotoshwa na hatimaye kuleta madhara katika taifa na kulifanya taifa kubeba gharama kubwa kuliko ya kuonyesha matangazo hayo moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuruhusu vyombo vya habari vya umma na vya binafsi kurusha moja kwa moja mijadala ya bunge ili wananchi wajue fedha zao zinavyogawanywa katika halmashauri zao, wajue ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali inasemaje kuhusu halmashauri zao, wajue namna ya kuzibana halmashauri zao ili zisifanye ubadhirifu na wapate hamasa ya kulipa kodi pale wanaporidhishwa na matumizi ya kodi zao. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inawataka Wabunge wa CCM, waache kufanya ushabiki bungeni kwani tabia yao ya muda mrefu ya kupuuza maoni ya wapinzani na kuwazomea ndio imelifikisha taifa hapa lilipo, ambapo watu wachache wamepora utajiri wa watanzania na kujilimbikizia wenyewe huku wakitumia wabunge wa CCM kuwatetea na kuwalinda kwenye mhimili huu muhimu sana wa bunge.

Mheshimiwa Spika, Ni ukweli ulio dhahiri kwamba tamthilia inayofanyika hivi sasa ya waliokuwa watetezi wakubwa wa ufisadi ya kutumbua majipu ni sawa na mchawi kutaka kurudisha msukule wake ambao yeye mwenyewe ndiye aliyeuroga mpaka jamii ikaamini kuwa umekufa . Kwa vyovyote vile hata akifanikiwa kuurudisha utakuwa ni zezeta. Adhabu anayostahili mchawi huyo ni kuuwawa ili asiendeleo kuwaaminisha wengine kwamba kazi ya kuwatesa wengine ni kazi halali.

Mheshimiwa Spika, Kwa muktadha huo, adhabu wanayostahili wabunge wa CCM walioshabikia ufisadi na ubadhirifu mpaka ukalifikisha taifa hapa lilipo ya kuwa na majipu kila mahali ni kufutwa kabisa katika uwakilishi wa wananchi ili taifa lianze safari mpya ya kutengeneza viongozi bora wanaomaanisha wanachotamka.

2. UPORAJI WA MADARAKA YA SERIKALI ZA MITAA UNAOFANYWA KWA MAKUSUDI NA SERIKALI KUU.

Mheshimiwa Spika, Msingi wa dhana ya ugatuzi wa madaraka (decentralization) ulikuwa ni kuzipa mamlaka Serikali za Mitaa ili ziweze

kuendesha shughuli zake kwa uhuru kwa maslahi ya wananchi wa eneo husika. Aidha, upo mchakato wa kufanya ugatuzi kamilifu (Decentralization by Devolution) almaarufu kama programu ya D by D ili kuzipa Serikali za Mitaa Mamlaka kamili.

Mheshimiwa Spika, Ifahamike kwamba chimbuko la dhana ya mamlaka ya umma na uwepo wa Serikali za Mitaa ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 (katika ibara ya 145 na 146, sambamba na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ya mwaka 1982 na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) ya mwaka 1982 ambazo kwa pamoja zilianzisha mamlaka hizo.

Mheshimiwa Spika, Kitendo cha Serikali Kuu kuingilia madaraka ya Serikali za Mitaa ni kuvunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ni kuvunja Sheria zilizoanzisha Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Tangu kuundwa kwake, Serikali za Mitaa haizijawahi kuwa na madaraka hata nusu tu ya yale yanayotajwa na Katiba na Sheria zinazoongoza Mamlaka hizo. Uongozi wote wa juu wa Serikali za Mitaa ukianza Wakurugenzi wa Halmashauri, Makatibu Tawala wa Wilaya na Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Mikoa na Waziri mwenye dhamana ya TAMISEMI – wote ni wateule wa Serikali Kuu na wanawajibika kwa Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, Kwa muundo huo, mamlaka ya Serikali za Mitaa iko Serikali Kuu. Serikali za Mitaa hazina mamlaka ya kuajiri, hazina mamlaka ya kutumia fedha zilizokusanya kwa shughuli zake za maendeleo mpaka zipate kibali kutoka Serikali Kuu. Kimsingi uhusiano uliopo kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ni kama ule wa Mnyapara na Mfungwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka waziri mwenye dhamana na TAMISEMI, ambaye mara kadhaa amesikika akijinasibu kwa ni mtu anayefuata sheria kikamilifu, aanze kutekeleza sheria, kwa kuacha kuingilia utendaji wa Serikali za Mitaa na badala yake kuziacha zijiendeshe zenyewe ili kukidhi matakwa ya sura ya nane ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayohusu “Madaraka ya Umma”.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali vilevile kuleta muswada wa Marekebisho ya Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji na Wilaya) pamoja na Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Local Government Elections Act) ili pamoja na mambo mengine sheria itamke kuwapa Mameya na Wenyeviti wa Halmashauri nguvu ya kiutendaji (executive power) tofauti na ilivyo sasa ambapo wanatambulika ki-itifaki tu (ceremonial

recognition). Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kwamba, nafasi za kazi za Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji zitangazwe, na waombaji wafanyiwe usaili kama ilivyo kwa watumishi wengine wa umma, na si kwa uteuzi wa kisiasa kama ilivyo sasa.

2.2 Uwezo wa kutafuta Mapato na Uwezo wa kutumia Fedha.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kuunda Halmashauri mijini na vijijini imetoa uwezo kwa madiwani wa kutafuta na kubuni njia mbalimbali za kupata fedha/mapato zinazolingana na gharama za huduma wanazotakiwa kuzitoa kwa wananchi katika maeneo husika. Halmashauri baada ya kutimiza uwezo wa fedha zinapewa uwezo wa kutumia fedha hizo kwa mujibu wa sheria ya fedha ya Serikali za mitaa ya mwaka 1982. Madiwani huzipa Halmashauri uwezo wa kutoza kodi, ushuru, ada n.k.

Mheshimiwa Spika, Urasimu wa serikali kuu katika kufanyia kazi maazimio ya Halimashauri mbalimbali nchini umeziingizia hasara kubwa sana Halimashauri zetu. Mfano ni pale ambapo halimashauri ya Manispaa ya Moshi imeshindwa kupata kibali cha Kukopa benki ya Rasilimali ya Tanzania (TIB) kwa miaka mitatu mfululizo kiasi kwamba hata thamani ya miradi imebadilika. Jambo la kusikitisha zaidi ni pale unapokosa majibu ya ndiyo au hapana kutoka kwa mamlaka zenye dhamana na serikali za Mitaa na hata pale majibu yakitokea yanachukua muda mrefu bila sababu za msingi.

Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua ni lini serikali kuu itaondoa urasimu huu ili kuzifanya Halimashauri ziweze kutimiza majukumu yake na hasa miradi mbalimbali ambayo wanakua wameianzisha.

2.3 Kamati za Uwekezaji za Halimashauri.

Mheshimiwa Spika, Halimashauri zetu zimekuwa na utamaduni wa kuwa na Kamati mbalimbali za kudumu kwa ajili ya kuendesha shughuli mbalimbali za Halimashauri husika. Aidha, Halimashauri zinao uwezo wa kuanzisha kamati mpya za kudumu baada ya kupata ridhaa ya waziri mwenye dhamana na TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na umuhimu wa Halimashauri zetu kuwezesha kuwa na uwezo wa kuongeza mapato yake ya ndani na hivyo kuondoa utegemezi kutoka serikali kuu katika kujiendesha na kukuza maendeleo ya Taifa letu ni vyema tukaanzisha kamati mpya ya kudumu ya **'Uwekezaji'** kwenye Halimashauri zote nchini na iwe na jukumu la kuishauri Halimashauri juu ya masuala mbalimbali ya uwekezaji na mitaji. Hii ni kutokana

na ukweli kuwa kwenye Halimashauri zetu kuna uwekezaji unafanywa na ambao kutokana na hali halisi Mabaraza ya madiwani yanakosa watu wenye weledi katika Nyanja hii na hivyo kujikuta wakiwekeza kwenye miradi ambayo mwisho wa siku wanashindwa kuiendeleza au inakuwa ni ile ile ya siku zote ya kujenga soko ama stendi.

Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni , inashauri kuwa kamati hii iundwe na wajumbe kutokana na utaalumu wao kwenye Nyanja hiyo na sio lazima wawe Madiwani ila wawe watu miongoni mwa jamii kwenye Halimashauri husika ambao wako tayari kujitolea kwa kutumia utaalumu wao kuishauri Halimashauri katika uwekezaji na kutafuta mitaji.

2.4 Ardhi kama chanzo kikuu cha Mapato ya Halimashauri.

Mheshimiwa Spika, Rasilimali Ardhi ndio kitu pekee ambacho unakikuta kwenye kila Halimashauri nchini iwe Jiji, Manispaa au Wilaya . Hivyo basi ili kuziwezesha Halimashauri zetu kuwa na chanzo cha uhakika cha mapato ya ndani (own source) ni vyema ule utaratibu wa awali wa serikali kuu kuchukua kiasi cha asilimia 70 ya mapato na kuiachia Halimashauri asilimia 30 ukatazamwa upya. **Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni**, inapendekeza kuwa mapato yatokanayo na kodi na tozo mbalimbali za ardhi yagawanywe katika mfumo wa Halimashauri kubakia na asilimia 70 ya mapato yote na Serikali kuu ibakie na asilimia 30 , pendekezo hili linalenga kuziwezesha Halimashauri zote kuwa na chanzo cha uhakika cha mapato na pia kuziwezesha Halimashauri kuweza kupanga matumizi bora ya ardhi ikiwemo kupanga,kupima,kumilikisha,kulipa fidia na kutatua migogoro ya ardhi kwenye maeneo yao kwani watakuwa na rasilimali za kufanya kazi hiyo.

1.5 Kuboresha Maslahi ya Madiwani

Mheshimiwa Spika, Madiwani ni watumishi ambao wanafanya wajibu mkubwa sana kwa mujibu wa sheria zetu ndio wenye wajibu wakusimamia uendeshaji wa Halimashauri, kutafuta na kusimamia mapato yote ya Halimashauri zetu na hata fedha zote ambazo zinatoka serikali kuu zinasimamiwa na Madiwani kupita baraza la madiwani. Hii maana yake ni kusema kuwa zaidi ya shilingi Trilioni 6 ambazo Bunge hili litapitisha hapa zitaenda kusimamiwa na Madiwani wetu kwenye Halimashauri zote nchini.

Mheshimiwa Spika, Madiwani hawa ambao tumewapa majukumu makubwa ya kusimamia fedha za Halimashauri malipo yao yamekuwa hayalingani na ukubwa wa kazi ambazo wanafanya na hali hiyo imepelekea utendaji kazi wao kuwa sio wa kiwango cha kuridhisha na imefikia hata mahali

pengine wachache wakawa wanachukua rushwa. Ili kukabiliana na maslahi duni ya Madiwani **Kambi rasmi ya upinzani Bungeni**, inapendekeza kuwa maslahi ya madiwani hasa mishahara na posho vikaongezwa ili kuweza kuendana na hali halisi ya maisha.

2. HAKI YA WANANCHI KUFUATILIA MWENENDO WA MCHAKATO WA BAJETI YA SERIKALI

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 8(1) (a) na (c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 inasema kwamba: **“Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi inayofuata misingi ya demokrasia na haki ya kijamii, na kwa hiyo: - wananchi ndio msingi wa mamlaka yote, na Serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba hii”** Aidha, **“Serikali itawajibika kwa Wananchi”**

Mheshimiwa Spika, Kwa muktadha huo, wananchi wana haki ya kujua Serikali yao inafanya nini na Serikali inawajibika kuwapatia wananchi taarifa juu ya utendaji wake wa kazi. Katika hali ambayo haijaeleweka bado, Serikali hii ya awamu ya tano imeamua kwa makusudi kutumia mabavu kukataza urushwaji wa moja kwa moja wa vipindi vya majadiliano ya Bunge ili wananchi wasijue kinachoendelea Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Ni muhimu wabunge wakafahamu kwamba, bajeti ya TAMISEMI inayoombwa kuidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2016/17 ni shilingi trilioni 6.8 sawa na asilimia 23 ya bajeti yote ya Serikali. Fedha hizi ni fedha za Walipa kodi – ni fedha za umma. Kujadili na kupitisha matumizi ya fedha za umma nyingi namna hii bila wananchi kuwa na fursa ya kuona jinsi bunge lao linavyofanya kazi ya kuwawakilisha katika kazi hiyo, sio tu kunawakosesha haki yao ya msingi ya kupata habari, bali pia kunazua maswali mengi kwamba; pengine Serikali ina mpango wa siri wa kufuja fedha za umma katika matumizi yasiyo ya lazima ndio maana haitaki wananchi wajue kinachoendelea bungeni.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kufuta mara moja katazo la kurusha matangazo ya Bunge moja kwa moja kupitia television ya Taifa na vyombo vingine vya habari vilivyokuwa vikirusha matangazo hayo awali ili wananchi ambao ndio msingi wa mamlaka ya Serikali wapate haki yao ya msingi ya kufuatilia mwenendo wa mgawanyo wa fedha zao katika Bajeti ya Serikali kutoka moja kwa moja Bungeni.

Mheshimiwa Spika, ikiwa Serikali itaendelea kuonyesha jeuri na ukaidi kuhusu utekelezaji wa jambo hili kama inavyofanya sasa, Basi Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni italazimika kuishtaki Serikali katika Mahakama ya Wananchi

Serikali hii ya awamu ya tano kwa kuwanyima wananchi haki ya kupata habari, tena habari zinazohusu fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, Yafaa ikafahamika hapa kuwa Bunge ni mkutano wa hadhara wa wananchi wote, ila kwa kuwa hakuna ukumbi ama eneo ambalo wananchi wote wanaweza kukusanyika kwa pamoja ndio maana utaratibu ukawekwa wa kutuma wawakilishi wachache (Wabunge) kwa niaba ya wananchi wote ,kwanini tunawazuia wananchi kuhudhuria/kufuatilia mkutano wao wa hadhara?tena wa kugawana rasilimali (bajeti)zao ?

4. MADARAKA YASIYO NA MWONGOZO NI SAWA NA BOMU LISILO NA MWELEKEO (UNGUIDED MISSILE)

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa hotuba ya Kiongozi wa Upinzani Bungeni kuhusu bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu ya tarehe 22 Aprili, 2016 ni kwamba; Serikali hii ya awamu ya tano inaendeshwa bila mwongozo wa muundo na kazi za kila wizara. Kwa msingi huo, utekelezaji wa kazi za Serikali umekuwa ukitegemea zaidi utashi na uwezo binafsi wa kufikiri wa kiongozi wa Serikali wa ngazi husika.

Mheshimiwa Spika, Katika kufanya hivyo, wako viongozi wa Serikali wanafuata mfano wa mamlaka yao ya uteuzi wa **fukuza-fukuza** bila hata kuwasikiliza wale wanaofukuzwa wakifikiri kwamba hivyo ndiyo mamlaka inataka, lakini wapo pia wanaopitiliza mipaka ya utendaji wao wa kazi kwa sababu moja tu ya kutojua mipaka yao kutokana na kutokuwepo kwa mwongozo.

Mheshimiwa Spika, sitazungumzia mawaziri ingawa somo hili linawahusu lakini nitazungumzia habari ya Wakuu wa Mikoa na Wilaya ambao wapo chini ya Wizara ninayoshughulikia.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Wakuu wa Mikoa na Wilaya kwa kukosa mwongozo wa kutafisiri mipaka ya madaraka yao Wamekuwa ni sehemu ya migogoro mingi katika Halmashauri nyingi nchini. Wamehusika sana kuchochea migogoro mingi katika maeneo yao ya utendaji kazi mathalani migogoro ya Wakulima na Wafugaji kwa ajili ya maslahi binafsi, wamehusika sana kupora maeneo ya Ardhi na Mali za Halimashauri kwa manufaa yao na rafiki zao na pia wamehusika sana kuingilia maazimio yanayopitishwa na Baraza la Madiwani katika Halmashauri husika kwa kutoa maagizo yanayokinzana na maazimio ya Baraza la Madiwani la Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilishapendekeza kufutwa kwa nafasi za Wakuu wa Wilaya na Mikoa kutokana na majukumu yao kutojulikana bayana. Aidha, kuendelea kuwepo kwa nafasi hizo ni kuongeza mzigo wa gharama za uendeshaji wa Serikali kwa kazi ambazo Wakurugenzi wa Halmashauri wakishirikiana na mabaraza ya madiwani wa Halmashauri husika wanaweza kufanya.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuangalia upya tija na faida ya kuwepo kwa wakuu wa Mikoa na Wilaya kiuchumi na kiufanisi. Hii itasaidia kuongeza ufanisi wa serikali za Mitaa na Pia itapunguza Matumizi ya fedha za walipa kodi yasiyo ya lazima kwa ofisi ambazo hazizalishi bali zinatumia tu.

Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inawataka Wakuu wa Mikoa na Wilaya waliopo waache mara moja kuingilia utendaji wa Halmashauri na badala yake waheshimu maamuzi ya mabaraza ya madiwani kwa kuwa ndivyo vyombo halali vya maamuzi kikatiba na kisheria.

5. MUUNDO TATA WA KI-UTAWALA KATIKA SERIKALI ZA MITAA

Mheshimiwa Spika, Licha ya Serikali za mitaa kupewa mamlaka kikatiba na kisheria kujijendesha, lakini zimeshindwa kufanya hivyo kutokana na muundo tata wa ki-utawala.

Mheshimiwa Spika, Wizara zote zikifika ngazi ya TAMISEMI zinakuta utawala au Uongozi mwingine na hivyo watendaji kulazimika kuwajibika sehemu mbili mbili na mwisho wa hilo ni kurushiana mpira pale mambo yanapoharibika. Mfano mzuri ni pale unapokuwa na Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI anayehusika na Elimu au Afya. Huyu anawajibika kwa Katibu Mkuu TAMISEMI au Katibu Mkuu wa Wizara Husika?

Mheshimiwa Spika, Ukirudi ngazi ya Halmashauri unamkuta Mkurugenzi ndiye msimamizi mkuu wa maswala yote ya Maendeleo na Rasilimali watu, lakini katika rasilimali hizo kuna baadhi ya kada ambazo zinawajibika moja kwa moja kwa wizara husika. Halmashauri zinaweza wa kuajiri kisheria lakini haziwezi kufanya hivyo mpaka ziombe kibali toka Serikali kuu na pia uwajibikaji wa wale wanaoajiriwa bado uko katika hali ya utata. Mfano, Mkaguzi wa Ndani anawajibika kwa nani, Afisa Kilimo na Mifugo wa Wilaya (DALDO), Mganga Mkuu wa Wilaya, Afisa Ardhi, Afisa Elimu wa Wilaya, Afisa ardhi wa Wilaya n.k wanawajibika kwa nani? Hali hii inasababisha **'dual accountability'** jambo ambalo linasababisha nidhamu ya uwajibikaji kuwa duni.

Mheshimiwa Spika, Serikali za mitaa haziwezi kujiendesha na kuleta tija kama muundo wake wa ki-utawala na ki-uwajibikaji hautafanyiwa marekebisha makubwa ili kuondoa tabia ya mfumo wa kikoloni ya Serikali Kuu ya kuendelea kuzitawala na kuzinyonya Serikali za Mitaa. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuandaa Muswada Binafsi wa Sheria ya Serikali za Mitaa kwa kuwa Serikali inaonekana haina nia ya kufanya hivyo, ili muundo na mfumo wa utawala na utendaji katika Serikali za Mitaa ufanyiwe “Overhaul” ili Serikali za Mitaa ziweze kujiendesha kwa tija na kufikia lengo la ugatuzi kamili wa madaraka – Decentralization by Devolution (D by D).

6. UFISADI KATIKA SERIKALI ZA MITAA UNAOFANYWA NA WATENDAJI WA SERIKALI KUU

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haipingi kwamba kuna ufujaji wa hali ya juu wa fedha za umma katika Halmashauri zetu. Hata hivyo, viongozi wa Serikali Kuu ambao ndio watendaji (accounting officers) katika Serikali za Mitaa wamekuwa vinara katika ubadhirifu unaondelea huko huku wakijificha kwenye kivuli cha jumla cha ubadhirifu wa Halmashauri na kwaaminisha wananchi kwamba madiwani wao ndio wabadhirifu wakati wao ndio wasukaji wa mtandao wa wizi na wanufaikaji wakubwa wa fedha za walipa kodi.

Mheshimiwa Spika, Kama kweli Serikali hii ina nia madhubuti ya kusimamia matumizi sahihi ya fedha za umma basi ianze kwanza kusafisha mtandao uliowekwa wa wakurugenzi na wahasibu wa Halmashauri bila ya kufuata kanuni za ushindani (meritocratic principle) na badala yake unafuata kujuana na urafiki binafsi

7. PROGRAMU YA UBORESHAJI WA SERIKALI ZA MITAA. (LOCAL GOVERNMENT REFORM PROGRAM)

Mheshimiwa Spika, Programu ya maboresho ya Serikali za Mitaa iliyoanzishwa mwaka 1998 ililenga kupeleka madaraka kwa wananchi. Kutokana na ukaribu uliopo kati ya Serikali za Mitaa na jamii, Wananchi wana matumaini makubwa na Serikali za Mitaa hivyo ngazi za chini katika Serikali za Mitaa zinahitaji kuwezesha sana kwa kuwa wao ndio wenye taarifa halisi za hali ya wananchi katika ngazi hizo.

Mheshimiwa Spika, Litakuwa ni jambo la ajabu kuzungumzia Serikali za Mitaa bila ya kuwahusisha Wenyevidi wa Vijiji, Mitaa na Vitongoji pamoja na wajumbe wao kama wanavyochaguliwa na wananchi katika maeneo husika.

Wao ndio kiunganishi kati ya wananchi na ngazi za juu zinazofuata kuhusu suala lolote linalohusu maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina mtazamo kwamba Kada hii ya Uongozi katika jamii ndiyo inayotakiwa kuwezesha ikiwa ni pamoja na kupatiwa mafunzo ya mara kwa mara kuhusiana na mabadiliko yoyote yanayotokea na ambayo yana uhusiano wa moja kwa moja na jamii. Mipango yote ya huduma za kijamii inatakiwa ianzie na kuendelezwa kutoka katika ngazi hii ya uongozi.

Mheshimiwa Spika, Ni katika muktadha huo ambapo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikisitiza hoja ya kuwalipa posho ya majukumu Wenyeviti wa Mitaa, Vijiji, Vitongoji pamoja na wajumbe wao ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi. Wananchi watakumbuka kwamba hoja ya kuwalipa posho wenyeviti wa Mitaa, Vijiji na Vitongoji ilikuwa ni mojawapo ya Sera za UKAWA kwenye ilani ya Uchaguzi Mkuu uliopita. Tulipendekeza hivi kutokana na ukweli kwamba wenyeviti na wajumbe wao ndio wanafanya kazi za kuhamasisha wananchi katika ngazi za chini na wamekuwa wakifanya hivyo kwa kujitolea miaka yote.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili ina mpango gani wa kuwalipa posho ya majukumu wenyeviti wa Serikali za Mitaa, Vijiji, Vitongoji pamoja na wajumbe wao kwa kazi wanazofanya?

Mheshimiwa Spika, Katika bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Serikali inaomba kuidhinishiwa shilingi bilioni 59 na milioni mia tano (59,500,000,000/=) kwa ajili ya uwezesaji wa vijiji. Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji, ni kwa nini uwezesaji huo umeenda vijijini pekee usiende pia mijini ambapo Serikali za Mitaa huko zina changamoto lukuki zinazohitaji fedha? Aidha, Serikali imejipanga vipi kuweka mfumo wa usimamizi wa fedha hizo zisije zikaishia mikononi mwa watu binafsi na kushindwa kufikia lengo lililokusudiwa?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rami ya Upinzani Bungeni inapendekeza asilimia 40 ya fedha hizo zitumike kuwalipa posho ya majukumu wenyeviti wa Serikali za mitaa, vijiji na vitongoji pamoja na wajumbe wao ili kuongeza ufanisi wa Serikali hizo katika maeneo yao ya kazi. Aidha, asilimia 60 inayobaki iende kwenye shughuli za kuchechemua uchumi ili kupambana na umasikini wa wananchi.

7. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, Yapo mambo mengi sana ya kuzungumzia katika Wizara ya TAMISEMI kwa kuwa huko ndiko kwenye wananchi. Lakini inasaidia nini kujadili hayo yote gizani? Ni kwa nini Serikali haitaki wananchi wafahamu kinachoendelea bungeni?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaendelea kuweka msisitizo wa Hotuba ya Kiongozi wa Upinzani Bungeni wa kuitaka Serikali iheshimu Katiba ya nchi na Sheria za nchi katika kutekeleza majukumu yake. Katika hotuba hiyo ya KUB imeabinika vilevile kwamba Serikali imevunja kifungu cha 41(1) cha sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 na kifungu cha 18(3) na (4) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 ambavyo kwa pamoja vinaitaka Serikali kuleta Bungeni nyongeza ya bajeti ili kupata idhini ya Bunge ikiwa fedha zilizoidhinishwa awali hazikutosha kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa, lakini Serikali mara kadhaa imefanya matumizi ya fedha za umma nje ya fedha zilizoidhinishwa na bunge bila kuomba bunge liidhinishhe bajeti ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Hiyo ni dharau kubwa kwa bunge na uvunjaji wa ibara ya 63(2) na 63 (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayolipa Bunge mamlaka ya kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha.

Japhary Michael (Mb)

**WAZIRI KIVULI NA MSEMAJI KAMBI RASMI YA UPINZANI
BUNGENI KATIKA OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

27 Aprili, 2016

MWENYEKITI: Tunaendelea na Kambi hiyo ya Upinzani, maoni kuhusiana na hoja ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, kwa kadri mlivyojipanga. Karibuni Mheshimiwa Ruth Mollel. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI OFISI YA
RAIS, UTUMISHI NA UTAWALA BORA, MHE. RUTH HIYOB MOLLEL (MB), KUHUSU
UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI MWAKA 2015/2016 NA MAKADIRIO
YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA
FEDHA 2016/2017 KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI**

**MHE. RUTH H. MOLLEL - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI
RAIS, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa

maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa mwaka 2015/16 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora, kwa mwaka 2016/2017 kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9), Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru kwanza Mungu kunipa afya njema ya kusimama hapa. Nichukue nafasi hii pia kukishukuru Chama changu cha Demokrasia na Maendeleo kwa kuniadini na kunipa fursa hii adimu na nimshukuru Kiongozi wa Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman Mbowe, kwa imani yake kwangu ya kuwa Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na Nje ya Bunge kwa masuala yote yanayohusu Utumishi na Utawala Bora. Kipekee niwashukuru Wabunge wenzangu wote ambao wamechangia hotuba hii na niishukuru familia yangu kwa uvumilivu wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia sasa suala la Utawala Bora katika Utumishi wa Umma. Sekta ya Utumishi wa Umma ni sekta inayotoa huduma katika jamii na ndiyo sekta ambayo kwa maana rahisi inayouza bidhaa inayotengenezwa na kuuzwa na Serikali. Hivyo basi, wale wanaotoa huduma hiyo wanaposhindwa kutoa huduma hiyo kwa viwango stahiki maana yake ni kwamba Serikali imeshindwa kukidhi matakwa na matarajio ya wananchi ambao ndiyo wateja wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kitabu cha mwongozo kilichotolewa na mwavuli wa Asasi za Kiraia zinazojihusisha na Utawala Bora pamoja na uwajibikaji kimtoa tafsiri ya neno Utawala kuwa ni matumizi ya Mamlaka ya Kisiasa, Kiuchumi na Kijamii, katika kusimamia masuala ya nchi kwenye ngazi zote. *(Makofi)*

Aidha, Utawala Bora ni matumizi ya mamlaka ambayo yanakuwa na uwazi, uwajibikaji, ushirikishaji wa watu, ufanisi, tija, uadilifu, usawa na unaofuata utawala wa sheria. Ili kutekeleza dhana ya Utawala Bora mambo yafuatayo lazima yazingatiwe:-

- (i) Matumizi sahihi ya dola na vyombo vyake;
- (ii) Matumizi mazuri ya rasilimali kwa faida ya wananchi;
- (iii) Matumizi mazuri ya madaraka na muda;
- (iv) Kujua na kutambua madaraka na mipaka yake kwa mujibu wa Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali hii ya Awamu ya Tano, kujitazama na kujihoji kama inafuata misingi ya Utawala Bora, katika utendaji kazi wake wa kila siku, tangu ilipoingia madarakani ama lah! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya rasilimali watu. Tangu Awamu ya Tano iingie madarakani tumeshuhudia majipu mengi yakitumbuliwa ikiwa ni jitihada za kupiga vita rushwa na ufisadi, ajenda ambayo imekuwa ikipigiwa kelele na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na wananchi kwa ujumla kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Rais wa Tanzania ametengua teuzi za Makatibu Wakuu 23 sasa kuanzia tarehe 6 Aprili, 2016. Imechukua takribani miezi mitano kabla ya viongozi hao kuelezwa kuhusu hatma yao, baadhi wamestaafishwa kwa lazima na baadhi kwa kufutwa kwa nafasi za kazi japokuwa baadhi zimejazwa na wateule wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais anayo mamlaka ya kufukuza, kusimamisha na kutengua uteuzi wa wateule wake. Pamoja na mamlaka hayo ana wajibu, kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zilizoko, kuwapa haki zao baada ya kuwastaafisha kwa lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wengi wao hawajatimiza miaka 60 na baadhi hawajafika hata miaka 50, kwa kuwa, hawakutenda kosa lolote na kwa kuwa wamepongezwa katika barua zao kwa kuitumikia Serikali hii vizuri, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri ifuatavyo:-

(i) Serikali iwalipe kifuta jasho, kwa mujibu wa taratibu na uzoefu wa miaka iliyopita iliyotumika kuwalipa Watumishi waliostaafishwa kwa lazima na Serikali;

(ii) Serikali ijenge Utumishi wa Umma imara, endelevu na wenye kujiamini kwa kuwa ndiyo *engine* ya maendeleo katika kutekeleza sera za Serikali iliyoko madarakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Mheshimiwa Rais, kuanza kutumbua majipu, Mawaziri, Naibu Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya nao wameanza kusimamisha watumishi tena wa ngazi za chini bila kutafakari mamlaka waliyonayo. Haiwezekani katika dhana ya utawala bora ukamsimamisha kazi Mkurugenzi ukamwacha Mtendaji Mkuu wa Shirika au Wizara husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiongozi anayewajibishwa kwanza ni Mtendaji Mkuu kwa sababu ameshindwa kusimamia watumishi walio nchini yake, huu siyo utawala bora na inasikitisha, hatua hiyo inaleta hisia ya uonevu na matumizi mabaya ya mamlaka. Tofauti na wanyama ambao wao hujeruhi kwa kujilinda, binadamu ana hulka ya chuki, visasi na upendeleo. Ndiyo maana zimewekwa sheria, kanuni na taratibu kudhibiti hisia hizo, ili haki itendeke. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasilimali watu ndiyo nyenzo kubwa ya kuleta maendeleo katika nchi yoyote duniani. Wanahitaji kuwezesha kwa kupatiwa mazingira mazuri ya kazi, vitendea kazi, bajeti, mafunzo na kuthaminiwa ili waweze kutekeleza majukumu yao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuzingatia Sheria na Kanuni zilizopitishwa na Bunge lako Tukufu ili haki itendeke kwa wote na kuepuka kesi za madai zinazoweza kuisababishia Serikali hasara kubwa. Vile vile wale wote watakaokutwa na hatia za ufiisadi na rushwa wachukuliwe hatua za kinidhamu pamoja na kufilisiwa mali zao kwa mujibu wa sheria ili iwe fundisho kwa wengine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Viongozi wa Kisiasa wanaoteuliwa nao wapate mafunzo ya Utawala Bora, Uongozi na Maadili na wapitishwe katika mchakato wa uchunguzi ili kupata viongozi wa kisiasa wenye maadili na weledi katika nafasi zao, kwa sababu Viongozi wa Kisiasa ni kioo cha jamii, hivyo uadilifu wao ni muhimu ili kujenga imani ya wananchi kwa Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maslahi bora kwa watumishi ni nyenzo muhimu inayomotisha watumishi kufanya kazi kwa bidii. Bila bajeti ya kutosha kwa mwaka husika malengo hayatafikiwa, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kuchagua vipaumbele vichache na bajeti kubwa ikaelekezwa kwenye maeneo hayo, kuliko utamaduni uliozoeleka wa kutenga bajeti kidogo kidogo kwa kila eneo mwishowe miradi na shughuli zingine hutekelezwa nusu nusu bila kukamilika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kwamba Bunge hili Tukufu, liliridhia mkataba wa misingi ya Kanuni za Utumishi wa Umma na Utawala Barani Afrika wa mwaka 2011, tarehe 25 Machi, 2015 (*The African Charter and Values and Principles of Public Service and Administration, 2011*). Ibara ya 3(1) kifungu kidogo cha mkataba huu inatambua usawa wa watumiaji wote wa Utumishi wa Umma na Utawala. Ibara ya 3(2) inakataza aina zote za ubaguzi kwa misingi yoyote ikiwa ni pamoja na asili ya kutoka, rangi, jinsia, ulemavu, dini, ukabila, msimamo wa kisiasa, uanachama wa chama cha wafanyakazi au vyama

vingine halali. Ibara ya 3(7) inahusu uhamasishaji na hifadhi za haki za binadamu za watumiaji na mawakala wa utumishi wa umma.

Neno watumiaji limetafsiriwa kwenye Ibara ya Kwanza ya mkataba likiwa na maana kwamba mtu yoyote wa asili au wa kisheria anayehitaji huduma ya utumishi wa umma. Kwa upande wake maneno, Mawakala wa Watumishi wa Umma yametafsiriwa kwenye Ibara hiyo hiyo kuwa ni mfanyakazi au ni mwajiriwa yeyote wa dola au taasisi zake ikiwa ni pamoja na wale walioteuliwa au kuchagulia kuendesha shughuli kwa jina la au kwa niaba ya dola katika ngazi zake zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misingi iliyotajwa katika Ibara ya 3 ya Mkataba huu imefafanuliwa kwa ufasaha mkubwa katika Sura ya Nne ya Mkataba inayohusu haki za Mawakala za Utumishi wa Umma. Hivyo kwa mfano, Ibara ya 14(1) inazikataza Mamlaka za Utumishi wa Umma na Utawala kuendeleza usawa miongoni mwa wakala wake ili kufikia lengo hilo. Ibara ya 14(2) inaelekeza kwamba Utumishi wa Umma na Utawala hautahamasisha au kuendeleza ubaguzi kwa misingi ya asili, rangi, jinsia, ulemavu, dini, ukabila, msimamo wa kisiasa au sababu nyingine yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa mujibu ya Ibara ya 15(1), Mawakala wa Utumishi wa Umma watakuwa na uhuru wa maoni kwa kuzingatia hadhi yao kama Watumishi wa Umma. Vile vile kufuatana na maslahi ya Ibara ya 15(2), Mawakala wa Utumishi wa Umma watakuwa na haki ya kuunda au kujiunga na mashirika, Vyama vya Wafanyakazi au makundi mengine ili kuendeleza kulinda haki zao kwa mujibu wa sheria za nchi. Muhimu zaidi Ibara ya 15(3) inatamka wazi bila kujali sheria za nchi, uanachama au ukosefu wa uanachama katika chama cha siasa hautaathiri kwa namna yoyote ile utumishi wa Mtumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwa mujibu wa masharti haya ya mkataba huu tunaotakiwa kuupatia nguvu za kisheria katika nchi yetu kwa kuridhia Azimio hili, kwamba Watumishi wote wa Umma wa ngazi zote wana haki ya kujiunga na vyama vya wafanyakazi pamoja na vyama vya siasa vyenye usajili halali kwa mujibu wa sheria za Tanzania. Kwa mujibu wa Ibara ya 34 ya Mkataba huu, Tanzania ilikuwa na haki ya kuweka masharti yaani *reservations* kwa lugha ya sheria ya Kimataifa wakati wa kusaini mkataba huu badala yake haikufanya hivyo na iliusaini na kuridhiwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili ni kwa nini imewafukuza kazi baadhi ya Watumishi wa Umma ambao waligombea nafasi mbalimbali za kisiasa kama vile Ubunge wa

Majimbo na Viti Maalum, ilhali ikijua wazi kuwa wanavunja Mkataba wa Kimataifa ambao waliusaini na kuridhiwa na Bunge hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Watumishi Hewa, kuanzia tarehe kumi na tano Machi mwaka huu, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, aliwaagiza Wakuu wa Mikoa yote Tanzania Bara kusimamia zoezi la kuhakiki Watumishi wa Umma katika Mikoa yao kwa lengo la kubaini wanaoitwa watumishi hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii siyo mara ya kwanza kwa Serikali ya Tanzania kufanya uhakiki wa Watumishi wa Umma ili kuondoa watumishi hewa. Itakumbukwa mwaka wa 1993 Serikali ilisimamisha kwa muda utaratibu wa kulipa mishahara ya watumishi benki na kulipa kupitia katika dirisha, badala yake Serikali ilihakiki Watumishi wa Umma kwa kuwalipa mishahara yao kupitia dirishani, yaani malipo moja kwa moja. Watumishi ambao hawakujitokeza kuchukua mishahara yao dirishani walihesabika kuwa ni watumishi hewa na majina yao yaliondolewa katika *payroll*. Hata hivyo, uhakiki huo ulishindwa kuondoa tatizo la watumishi hewa ambalo liliendela kuwa sugu katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhakiki mwingine wa Watumishi wa Umma ulifanyika mwaka 2006 na 2011. Jitihada za Serikali za Awamu ya Nne nazo hazikufua dafu, Serikali iliendelea kupoteza mabilioni ya fedha kutokana na malipo ya mishahara na marupurupu ya watumishi hewa. Aidha, kama sehemu ya jitihada za kuondoa tatizo hili tangu miaka ya katikati ya tisini, Serikali ilianzisha mfumo wa *Lawson*, chini ya mfumo huu taarifa za watumishi wa umma ambao utumishi wao umekoma kwa sababu yoyote ile zinapoingizwa katika kumbukumbu za mahali pao pa kazi hupelekwa moja kwa moja Hazina kwa ajili ya hatua zaidi kama vile kuwaondoa katika *payroll* na kuandaa malipo yao ya pensheni, kiinua mgongo na kadhalika. Kwa sasa mfumo wa *Lawson* umepelekwa katika Mikoa na Halmashauri zote za Wilaya katika Tanzania Bara. Mfumo huu pia umeshindwa kuondoa tatizo la watumishi hewa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu kubwa ya kushindikana kutatuliwa kwa tatizo la watumishi hewa ni kukosekana kwa uadilifu katika mfumo mzima wa Utumishi wa Umma. Watumishi hewa ni tatizo linalotengenezwa kwa makusudi, mabilioni yanapotea kila mwaka kutokana na malipo ya watumishi hewa yanakwenda kwenye mifuko binafsi ya Viongozi na Watendaji wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa ndiyo wamehakikisha kuwa jitihada zote za nyuma za kupambana na tatizo hili hazifanikiwi na hawa ndiyo watahakikisha kuwa jitihada sasa za Mheshimiwa Rais Magufuli zinakwama.

Viongozi na Watendaji hawa wa Serikali hawapo katika ngazi za chini za utumishi wa umma tu Wilayani na Mikoani peke yake, wapo katika ngazi zote katika mfumo mzima wa utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana licha ya kelele za jitihada zote, licha ya taarifa rasmi za kila mwaka za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuonyesha ukubwa na upana wa tatizo hili, hakuna Kiongozi wala Mtendaji wa Idara ya Serikali au Taasisi zake yeyote ambaye amewajibishwa kutokana na Idara au Taasisi yake kukutwa imelipa mishahara ya watumishi hewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kadri tunavyofahamu hakuna Kiongozi au Mtendaji wa Serikali au Taasisi, kwa ngazi yoyote ambaye amewajibishwa kwa sababu ya kuwa na watumishi hewa. Aidha, zoezi la uhakiki limefanywa na wahusika wa tatizo lenyewe. Kwa mujibu wa Sheria ya Tawala za Mikoa, Wakuu wa Mikoa ndiyo wakuu wa Watumishi wote wa Umma katika mikoa yao. Aidha, Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Serikali za Mitaa, ndiyo waajiri wa watumishi katika Halmashauri zao, kwa sababu hiyo Wakuu wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri wanahusika moja kwa moja na uwepo wa watumishi hewa katika Mikoa na katika Halmashauri za Serikali za Mitaa. Hawa ndiyo ambao wamepeva jukumu na Mheshimiwa Rais Magufuli kuwabaini watumishi hewa katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutoa taarifa, zinaonesha uwepo wa maelfu ya watumishi hewa katika Mikoa na Halmashauri zao, Viongozi na Watendaji hawa sasa wamejitia hatiani kwa kuonesha kuhusika kwao na tatizo hili. Tunasubiri kuona hatua zitakazochukuliwa na Mheshimiwa Rais dhidi ya Wakuu wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri ambao kwa maksudi au kwa uzembe wao wamesababisha kuwepo kwa watumishi hewa katika Mikoa na Halmashauri zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo la pili ambalo limechangia kuwepo kwa tatizo la watumishi hewa katika utumishi wa umma. Tatizo hili ni udhaifu mkubwa wa Tume ya Utumishi wa Umma ambayo ndiyo Tume rekebu yenye jukumu la kuhakiki rasilimali watu katika utumishi wote wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa rasmi zilizotolewa na Tume hiyo kwa Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa hivi karibuni, Tume hiyo inakabiliwa na matatizo makuwa yanayokwamisha utendaji wake. Kwa mfano, Tume hiyo haina watumishi wa kada mbalimbali, vitendea kazi vya aina mbalimbali, magari, kompyuta, vifaa vingine vya ofisi na katika mwaka wa fedha uliopita, walipata bajeti kidogo sana ambayo haikuweza kukidhi mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira haya Tume hiyo imeshindwa kabisa kutekeleza majukumu yake ya kuhakiki Watumishi wa Umma katika maeneo mbalimbali ya Nchi yetu. Kama kweli tuna maana ya kupambana na tatizo la watumishi hewa Serikalini, tunataka kuona fedha za kutosha zinatengwa kwa ajili ya Tume hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la tatu ambalo limechangia kuwepo, kuongezeka kwa watumishi hewa ni kutokuwepo kwa mfumo mmoja wa rasilimali watu unaojumuisha na kuunganisha mifumo mingine yote. Kwa mfano, kwa utaratibu wa sasa mfumo wa kusajili uzazi na vifo uliopo chini ya RITA haujaunganishwa na mifumo mingine ya utumishi wa umma wala mfumo ya Hifadhi ya Jamii kama vile NSSF na LAPF. Kwa sababu ya mifumo hiyo kuwa inajitegemea (*stand alone*), taarifa inazoingizwa katika mfumo mmoja hazipelekwi katika mfumo mwingine. Kwa mfano, taarifa za vifo zinavyotolewa na RITA haziingizwi katika mfumo ya Utumishi wa Umma wala Hifadhi ya Jamii ili majina ya wahusika yaweze kuondolewa katika payroll na orodha za malipo ya pensheni au kiinua mgongo, matokeo yake ni kuwepo kwa watumishi hewa, yaani watumishi ambao wameshafariki dunia lakini taarifa zao hazijapelekwa kunakohusika na wanaendelea kulipwa mishahara ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kupambana na tatizo hili la watumishi hewa ichukue hatua zifuatazo ili kumaliza tatizo hili kama ifuatavyo:-

(1) Wakurugenzi Watendaji na Makatibu Tawala wa Mikoa waliosababisha watumishi hewa wakati mfumo wa kuwaondoa upo, wachukuliwe hatua za kisheria na kinidhamu kwa mujibu wa taratibu zilizopo. (Makofi)

(2) Tume ya Utumishi wa Umma wapewe watumishi wa kutosha, magari na vitendea kazi ili watekeleze jukumu lao la kuhakiki Watumishi wa Umma na kutoa taarifa kwa mamlaka husika.

(3) Serikali iunganishe mifumo ya rasilimali watu inayojitegemea hizi tunazoita (*standalone systems*), namba za vitambulisho vya Taifa ziunganishwe na mifumo ya vizazi na vifo, mfumo wa malipo Serikalini, mfumo wa malipo ya pensheni, mfumo wa mlipa kodi na kadhalika. Hivyo, mtumishi anapofariki, kustaafu, kuacha kazi, mfumo wa Lawson nilioutaja hapo juu unamwondoa mara moja katika orodha ya watumishi wa Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha Taasisi za Utawala Bora; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuwa ili mapambano dhidi ya rushwa na ufiadini nchini yaweze kuendelea kwa kasi ni lazima TAKUKURU iimarishwe kwa kupatiwa rasilimali watu na bajeti ya kutosha ili kutekeleza majukumu yake. Aidha, ni rai yetu kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi hii muhimu, nyeti apewa uhuru wa mamlaka kamili awe na mamlaka ya kutekeleza majukumu yake kwa uhuru bila kuingiliwa na mamlaka yoyote.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuwa ni wakati muafaka sasa ukaletwa Muswada wa Sheria Bungeni ili kumpa mamlaka Mkurugenzi Mkuu TAKUKURU kufungua kesi mahakamani mara baada ya uchunguzi wake kukamilika, badala ya hali ya sasa ambapo ni mpaka aombe kibali kutoka kwa DPP na tumeshuhudia kuwa DPP amekuwa mzito kutoa vibali hivyo na badala yake TAKUKURU inaonekana imeshindwa kupambana na rushwa na ufiadini nchini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha ni kwamba, watumishi wa TAKUKURU wamezuiwa kwenda kwenye mafunzo, najua ni pamoja na watumishi wengine pia, lakini TAKUKURU kwa suala la rushwa wangepata nafasi ya masomo hata kama wataletwa walimu kutoka nje waje wawafundishe, kwa sababu mbinu za wala rushwa zinabadilika kila mwaka. Kwa hiyo na wenyewe wanatakiwa wawe *updated*, waweze kusimamia kazi zao na kusaidia kupigana vita na hili suala la rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Maadili ya Viongozi; Tume hii ipo kwa mujibu wa Katiba na Sheria zetu na ni wajibu wa Viongozi wote kutangaza mali zao kwa wakati kwa mujibu wa sheria. Hata hivyo baadhi ya viongozi huhelewa kutangaza mali zao na wakati mwingine baada ya kukumbushwa mara kwa mara. Vile vile wanapotoka madarakani wachache sana wanaotangaza mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume hii ina Watendaji wachache sana na imepewa jukumu la kufuatilia taarifa za mali na madeni ya Watumishi wa Umma na Viongozi wa Kiasia kuanzia ngazi ya juu hadi Madiwani, majukumu haya ni makubwa sana kwa Tume ambayo haina ofisi, nchi nzima na hivyo kupelekea kushindwa kuyamudu majukumu yake vema kutokana na ukubwa wa kazi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kuwa, ili Tume hii iweze kumudu vema majukumu yake ni bora sasa ikawezeshwa kufungua ofisi kila mkoa na kuajiri watumishi ambao watakuwa na wajibu wa kushughulikia fomu za Madiwani na watumishi wengine wa

Halmashauri, ili Tume ikabakia na majukumu ya kushughulikia Watumishi wa Umma ngazi ya Kitaifa pamoja na Wabunge.

Mheshimiwa Mweyekiti, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri kuwa mali na madeni ya viongozi itangazwe kwa uwazi wakati viongozi wanapoingia madarakani na wakati viongozi wanapotoka madarakani watangaze kwa uwazi tena mali na madeni yao, ili kuwapa wananchi fursa ya kupima kama kiongozi husika ametumia madaraka yake kujilimbikizia mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 2(2), imeweka bayana mamlaka ya Rais wa Jamhuri ya Mkuungano kuigawa nchi katika maeneo ya kiutawala; inasomeka nanukuu:

“Kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Rais anaweza kuigawa Jamhuri ya Muungano katika Mikoa, Wilaya na maeneo mengineyo kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria au kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni tumekuwa na utaratibu ambao umeshamiri kwa kasi wa kugawa maeneo mbalimbali ya kiutawala nchini ikiwa ni pamoja na Vijiji, Kata, Wilaya na Mikoa. Aidha, ugawaji huu unajenga utamaduni kwa wananchi kutaka maeneo yao yaendeleo kugawanywa mara kwa mara na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nchi yetu inajipatia uhuru kulikuwa na Majimbo kumi ambayo yalirithiwa toka kwa mkoloni, kutokana na mamlaka aliyokuwa nayo Baba wa Taifa, Rais Mwalimu Julius Kambarage Nyerere mwaka 1966 alianzisha Mikoa 15 ambapo kwa sasa idadi ya Mikoa ni zaidi ya nusu ya Mikoa iliyoanzishwa na Rais wa kwanza wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hapa siyo tu kuanzisha Mikoa na maeneo mengine ya utawala, bali ni namna Serikali inavyoongeza matumizi ya masuala ya kiutawala badala ya mapato hayo kuelekezwa kwenye miradi ya maendeleo. Hii inathibitishwa na Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji vipya vingi vilivyoanzishwa bado havijapata huduma muhimu kwa ajili ya kuanza kazi ikiwemo ukosefu wa ofisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huu kwa baadhi ya maeneo umeanza kuleta viashiria vya ukabila pamoja na migogoro ya mipaka na mgawanyo wa rasilimali. Hili siyo jambo la kupuuzwa hata kidogo. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kusitisha zoezi la kugawa maeneo ya utawala, badala yake pawepo na utaratibu mwingine ambao utahakikisha maeneo hayo

yakigawanywa kiutawala kuwe na mpango wa namna ya kupata mapato ya kujiendesha kuliko hali ilivyo sasa ya kutegemea Serikali Kuu na fedha nyingi kutumika kulipa mishahara ya watumishi na kujenga miundombinu mipya, badala ya kutumika katika miradi ya maendeleo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaishauri Serikali ya Awamu ya Tano katika kutekeleza kwa vitendo mpango wa kudhibiti matumizi makubwa ya uendeshaji wa Serikali, iamue kusitisha utaratibu huu kwa kuigawa nchi katika vipande vidogovidogo vya utawala, kwani hii ni kuongeza zaidi gharama za uendeshaji wa Serikali na mapato kidogo yanayokusanywa yaelekezwe katika kuendeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Maendeleo wa TASAF. Kwa mujibu wa randama ya Wizara ukurasa wa 19, kifungu cha 2.4.3(ii) kinasomeka kama ifuatavyo:

"Kiasi cha shilingi bilioni 275.9 kimehaulishwa kwa kaya maskini milioni 1.1 kama ruzuku kufikia mwezi Machi 2016, ruzuku hii ilihaulishwa kwa kaya zote maskini zilizoandikishwa Tanzania Bara pamoja na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi ni nyingi sana kama zingetumika vizuri kwa ufanisi, kitendo cha kuzigawa kwenye kaya maskini, tena kwa mfumo wa fedha taslimu kamwe haziwezi kuondoa kiwango cha umaskini kwenye kaya hizo, kwani mfumo huo siyo endelevu hata kidogo. Ukitazama mgawanyo wa ruzuku hiyo utaona wazi kuwa, kila Kaya ilipata kiasi cha sh. 250,000 au kila mwanakaya alipata labda elfu hamsini na tano hivi. Kwa kweli, kiasi cha shilingi elfu hamsini na tano kwa mwaka kinaweza kumwondolea kweli mwananchi umaskini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kufanya ukaguzi maalum wa ufanisi katika Mfuko na kuangalia kama kuendelea kugawa fedha badala ya kuanzisha miradi kunaweza kuwaondolea wananchi umaskini wa kutupwa, maana zipo tuhuma kuwa wapo baadhi wa watumishi wa Halmashauri ambao huwaweka ndugu na jamaa zao kama watu maskini ilihali siyo maskini halisi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ruth, bado dakika tano.

MHE. RUTH H. MOLLEL - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI KWA OFISI YA RAIS UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; kama nilivyoainisha hapo juu, kusimamisha, kufukuza watumishi sio muarubaini wa kujenga Watumishi wa Umma uliotukuka, mifumo na miundo ya utawala bora

iimarishwe na kusimamiwa. Hatua zilizoanza kuchukuliwa kudhibiti matumizi holela ya kodi za wananchi uendeleo na wanaokiuka wachukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria, ikibidi mali zao zitaifishwe kwa mujibu wa sheria, mipaka ya madaraka izingatiwe ili haki itendeke, viongozi wa kisiasa wawe mstari wa mbele katika uadilifu, uwajibikiaji na uzalendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaendelea kuweka msisitizo wa Hotuba ya Kiongozi wa Upinzani Bungeni wa kuitaka Serikali iheshimu Katiba ya nchi na sheria za nchi katika kutekeleza majukumu yake. Katika Hotuba ya Kiongozi wa Upinzani Bungeni imebainika kwamba Serikali inaongozwa kiholela bila kufuata *instrument* inayoweka mwongozo wa muundo wa Wizara na kazi zake, jambo linalopelekea Waziri kutekeleza majukumu yake kwa kutumia utashi na uwezo binafsi wa kufikiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imebainika kuwa Serikali imevunja Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuwanyima wananchi haki ya kupata habari kwa kukataa vyombo vya habari vya umma na vile vya binafsi kurusha moja kwa moja mjadala wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imebainika vile vile kwamba Serikali imevunja Kifungu namba 41(1) cha Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 na Kifungu 18(3)(4) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 ambavyo kwa pamoja vinaitaka Serikali kuleta Bungeni nyongeza ya bajeti ili kupata idhini ya Bunge ikiwa fedha zilizoidhinishwa awali hazikutosha kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa. Hata hivyo, Serikali mara kadhaa imefanya matumizi ya fedha za umma nje ya fedha zilizoidhinisha na Bunge bila kuomba Bunge liidhinishhe bajeti ya nyongeza hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuwa hii ni dharau kubwa kwa Bunge na uvunjaji wa Ibara ya 62(3) na 63(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayolipa Bunge mamlaka ya kusimamia na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ruth Mollel kwa taarifa yako.

HOTUBA YA MSEMaji MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI OFISI YA RAIS, UTUMISHI NA UTAWALA BORA, MHE. RUTH HIYOB MOLLEL (MB), KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI MWAKA 2015/2016 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

(Yanatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016)

1. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Kwa heshima kubwa napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwakunipa afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais- Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuwa humu Bungeni, kukishukuru chama changu cha DEMOKRASIA NA MAENDELEO kwa kuniamini na kunipa fursa hii adhimu niliyopatiwa, pia nimshukuru Kiongozi wa Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman Mbowe kwa imani yake kwangu ya kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na Nje ya Bunge kwa masuala yote yanayohusu Utumishi na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, Kwa upekee niwashukuru wabunge wenzangu wote kwa ushirikiano walionipa kila nilipohitaji na hatimae kufanikisha maandalizi ya Maoni haya ya Kambi Rasmi ya Upinzani. Pia niishukuru familia yangu kwa uvumilivu na msaada wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, Na mwisho lakini si kwa umuhimu ni kwa wadau wote ambao wameshiriki kwa njia moja au nyingine katika kutoa ushauri au maoni yao binafsi au kupitia maandiko yao kwenye machapisho au mawasilishao mbalimbali.

2.0 UTAWALA BORA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

2.1 Malalamiko kuhusu utendaji usiozingatia Utawala Bora katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, sekta ya utumishi wa umma ni sekta inayotoa huduma katika jamii na ndio sekta ambayo kwa maana rahisi inayouza bidhaa

inayotengenezwa na kuuzwa na Serikali. Hivyo basi wale wanaotoa huduma hiyo wanaposhindwa kutoa huduma hiyo kwa viwango stahiki maana yake ni kwamba Serikali imeshindwa kukidhi matakwa na matarajio ya wananchi ambao ndio wateja wake.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kitabu cha mwongozo kilichotolewa na mwamvuli wa asasi za kiraia, zinazojihusisha na Utawala Bora pamoja na uwajibikaji, kimetoa tafsiri ya neno **Utawala** kuwa ni matumizi ya mamlaka ya kisiasa, kiuchumi na kijamii katika kusimamia masuala ya nchi kwenye ngazi zote. **Aidha Utawala Bora** ni matumizi ya mamlaka ambayo yanakuwa na uwazi, uwajibikaji, ushirikishaji wa watu, ufanisi, tija, uadilifu, usawa na unaofuata utawala wa sheria. Ili kutekeleza dhana ya utawala bora mambo yafuatayo lazima yazingatiwe:

- Matumizi sahihi ya Dola na vyombo vyake
- Matumizi mazuri ya rasilimali kwa faida ya wananchi
- Matumizi mazuri ya madaraka na muda
- Kujua na kutambua madaraka na mipaka yake kwa mujibu wa katiba na sheria

Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka serikali hii ya awamu ya tano kujitazama na kujihoji kama inafuata misingi ya utawala bora katika utendaji kazi wake wa kila siku tangu ilipoingia madarakani ama la!

2.2 MATUMIZI MAZURI YA RASILIMALI.

2.2.1. Rasilimali watu

Mheshimiwa Spika Tangu awamu ya tano iingie madarakani, tumeshuhudia "*Majipu Mengi yakitumbuliwa*" ikiwa ni jitihada za kupiga vita rushwa na ufisadi, ajenda ambayo imekuwa ikipigiwa kelele na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni (**KRUB**) na wananchi kwa ujumla kwa muda mrefu. Sambamba na hilo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ametengua teuzi za makatibu Wakuu na Manaibu 24 kuaanzia tarehe 6 Aprili 2016, imechukua takriban miezi mitano (5) kabla ya viongozi hao kuelezwa kuhusu hatma yao. Baadhi wamestaafishwa kwa lazima na baadhi kwa kufutwa kwa nafasi za kazi, ijapokuwa nafasi hizo zimejazwa na wateule wengine.

Mheshimiwa Spika kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzani, Rais anayo mamlaka ya kufukuza, kusimamisha na kutengua uteuzi wa wateule wake, pamoja na mamlaka hayo ana wajibu kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zilizopo kuwapa haki zao baada ya kuwastaafisha kwa lazima. Kwa

kuwa wengi wao hawajatimiza miaka sitini (60) na baadhi hawajafika hata miaka hamsini (50), kwa kuwa hawakutenda kosa lolote na kwa kuwa wamepongezwa katika barua zao kwa kuitumikia Serikali vizuri, Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri ifuatavyo;

1. Serikali iwalipe kifuta jasho au" golden handshake" kwa mujibu wa taratibu na uzoefu wa miaka iliyopita uliotumika kuwalipa watumishi waliostaafishwa kwa lazima na Serkali.

2. Serikali ijenge utumishi wa umma imara, endelevu na wenye kujiamini kwa kuwa ndio ingini ya maendeleo katika kutekeleza sera za Serkali iliyoko madarakani

Mheshimiwa Spika baada ya Mhe Rais, kuanza kutumbua majipu, mawaziri, naibu Mawaziri, wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya nao wameanza kusimamisha watumishi tena wa ngazi za chini, bila kutafakari mamlaka waliyo nayo. Haiwezekani, katika dhana ya utawala Bora ukamsimamisha kazi mkurugenzi, ukamuacha Mtendaji Mkuu wa shirika au Wizara husika. Kiongozi anayewajibishwa kwanza ni Mtendaji Mkuu kwa sababu ameshindwa kusimamia watumishi walio chini yake. Huu si utawala bora na inasikitisha, hatua hiyo inaleta hisia za uonevu na matumizi mabaya ya mamlaka.

Mheshimiwa Spika, tofauti na wanyama ambao wao hujeruhi kwa kujilinda, Binadamu ana hulka ya chuki, visasi na upendeleo na ndio maana zimewekwa sheria, kanuni na taratibu za kudhibiti hisia hizo ili haki itendeke. Rasilimali watu ndio nyenzo kubwa ya kuleta maendeleo katika nchi yoyote duniani. Wanahitaji kuwezesha kwa kupatiwa mazingira mazuri ya kazi, vitendea kazi, bajeti, mafunzo na kuthaminiwa ili waweze kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, Aidha **KRUB** inaitaka Serikali kuzingatia Sheria na Kanuni zilizopitishwa na Bunge lako tukufu ili haki itendeke kwa wote na kuepuka kesi za madaizi zinazoweza kuisababishia serikali hasara kubwa. Vile vile, wale wote watakaokutwa na hatia za ufiadini na rushwa wachukuliwe hatua za kinidhamu pamoja na kufilisiwa mali zao kwa mujibu wa sheria ili iwe fundisho kwa wengine.

Mheshimiwa Spika, viongozi wa kisiasa nao, wanaoteuliwa wapate mafunzo ya utawala bora, uongozi na maadili, na wapitishwe katika mchakato wa uchunguzi ili kupata Viongozi wa Kisiasa wenye maadili na weledi katika

nafasi zao kwa sababu viongozi wakisiasa ni kioo cha jamii, hivyo uadilifu wao ni muhimu ili kujenga imani ya wananchi kwa Serkali.

Mheshimiwa Spika, maslahi bora kwa watumishi, ni nyenzo muhimu inayomotisha watumishi kufanya kazi kwa bidii, bila bajeti ya kutosha kwa mwaka husika, malengo hayatafikiwa. KRUB inaishauri serikali kuchagua vipaumbele vichache na bajeti kubwa ikaelekezwa kwenye maeneo hayo, kuliko utamaduni uliozoeleka wa kutenga bajeti kidogo kidogo kwa kila eneo mwishowe miradi na utekelezaji wa shughuli zingine hutekelezwa nusu nusu bila kukamilika.

2.2.2 MKATABA WA MISINGI NA KANUNI ZA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BARANI AFRIKA WA MWAKA 2011 (THE AFRICAN CHARTER ON VALUES AND PRINCIPLES OF PUBLIC SERVICE AND ADMINISTRATION, 2011)

Mheshimiwa Spika ,itakumbukwa kuwa Bunge hili liliridhia mkataba wa *missingi na kanuni za utumishi wa umma na utawala barani afrika wa mwaka 2011* tarehe 25 Machi, 2015

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 3(1) ya Mkataba huu inatambua “usawa wa watumiaji wote wa *Utumishi wa Umma na Utawala*.” Ibara ya 3(2) inakataza “... aina zote za ubaguzi kwa msingi wowote, ikiwa ni pamoja na asili ya kutoka, rangi, jinsia, ulemavu, dini, ukabila, msimamo wa kisiasa, uanachama wa chama cha wafanyakazi au vyama vingine halali.” Ibara ya 3(7) inahusu uhamasishaji na hifadhi ya haki za binadamu za ‘watumiaji’ na ‘Mawakala wa Utumishi wa Umma.’ Neno ‘watumiaji’ limetafsiriwa kwenye ibara ya 1 ya Mkataba kumaanisha “*mtu yeyote wa asili au wa kisheria anayehitaji huduma ya utumishi wa umma.*”

Kwa upande wake, maneno ‘Mawakala wa Utumishi wa Umma’ yametafsiriwa kwenye ibara hiyo hiyo kuwa ni “*mfanyakazi au mwajiriwa yeyote wa dola au wa taasisi zake, ikiwa ni pamoja na wale walioteuliwa au kuchaguliwa kuendesha shughuli kwa jina la, au kwa niaba ya, Dola, katika ngazi zake zote.*”

Mheshimiwa Spika, Misingi iliyotajwa katika ibara ya 3 ya Mkataba huu imefafanuliwa kwa ufasaha mkubwa katika Sura ya IV ya Mkataba inayohusu ‘Haki za Mawakala wa Utumishi wa Umma.’ Hivyo, kwa mfano, ibara ya 14(1) inazitaka mamlaka za Utumishi wa Umma na Utawala kuendeleza usawa miongoni mwa mawakala wake. Ili kufikia lengo hilo, ibara ya 14(2) inaelekeza kwamba “*Utumishi wa Umma na Utawala hautahamasisha au kuendeleza ubaguzi kwa missingi ya asili, rangi, jinsia, ulemavu, dini, ukabila, msimamo wa*

kisiasa au sababu nyingine yoyote.” Aidha, kwa mujibu wa ibara ya 15(1), “Mawakala wa Utumishi wa Umma watakuwa na uhuru wa maoni kwa kuzingatia hadhi yao kama watumishi wa umma.” Vile vile, kufuatana na masharti ya ibara ya 15(2), “Mawakala wa Utumishi wa Umma watakuwa na haki ya kuunda au kujiunga na mashirika, vyama vya wafanyakazi au makundi mengine ili kuendeleza na kulinda haki zao kwa mujibu wa sheria za nchi.” Muhimu zaidi, ibara ya 15(3) inatamka wazi: “Bila kujali sheria za nchi, uanachama au ukosefu wa uanachama katika chama cha siasa hautaathiri, kwa namna yoyote ile, utumishi (‘career’) wa mtumishi wa umma.”

Mheshimiwa Spika, Ni wazi, kwa mujibu wa masharti haya ya Mkataba huu tunaotakiwa kuupatia nguvu za kisheria katika nchi yetu kwa kuridhia Azimio hili, kwamba watumishi wote wa umma wa ngazi zote wana haki ya kujiunga na vyama vya wafanyakazi pamoja na, *inter alia*, vyama vya siasa vyenye usajili halali kwa mujibu wa sheria za Tanzania. Kwa mujibu wa ibara ya 34 ya Mkataba huu, Tanzania ilikuwa na haki ya kuweka masharti, yaani *reservations* - kwa lugha ya sheria za kimataifa – wakati wa kusaini Mkataba huu, badala yake haikufanya hivyo na iliusaini na kuridhiwa na Bunge .1

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni , inaitaka serikali kulieleza Bunge hili ni kwanini imewafukuza kazi baadhi ya watumishi wa umma ambao waligombea nafasi mbalimbali za kisiasa kama vile ubunge wa Majimbo na Viti maalum ile hali ikijua wazi kuwa wanavunja mkataba wa kimataifa ambao waliusaini na kuridhiwa na Bunge hili?

3.0 WATUMISHI HEWA SERIKALINI

Mheshimiwa Spika, kuanzia tarehe 15 Machi, 2016, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Dkt. John Pombe Magufuli, aliwaagiza Wakuu wa Mikoa yote ya Tanzania Bara kusimamia zoezi la kuhakiki watumishi wa umma katika Mikoa yao kwa lengo la kubaini wanaoitwa ‘watumishi hewa.

Mheshimiwa Spika, Hii sio mara ya kwanza kwa Serikali ya Tanzania kufanya uhakiki wa watumishi wa umma ili kuondoa watumishi hewa. Itakumbukwa kwamba, mwaka 1993 Serikali ilisimamisha kwa muda utaratibu wa kulipa mishahara ya watumishi wa umma kwa kuipitishia kwenye akaunti zao benki. Badala yake, Serikali ilihakiki watumishi wa umma kwa kuwalipa mishahara yao kupitia dirishani, yaani malipo ya moja kwa moja kwa watumishi husika. Watumishi ambao hawakujitokeza kuchukua mishahara yao dirishani walihesabika kuwa ni ‘watumishi hewa’ na majina yao yaliondolewa katika ‘payroll.’ Hata hivyo uhakiki huo ulishindwa kuondoa tatizo la ‘watumishi hewa’ ambalo liliendelea kuwa sugu katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, Uhakiki mwingine wa watumishi wa umma ulifanyika mwaka 2006 na mwaka 2011. Jitihada za Serikali ya awamu ya nne nazo hazikufua dafu. Serikali iliendelea kupoteza mabilioni ya fedha kutokana na malipo ya mishahara na marupurupu ya watumishi hewa.

Aidha, kama sehemu ya jitihada za kuondoa tatizo hili, tangu miaka ya katikati ya tisini, Serikali ilianzisha mfumo wa taarifa za utumishi na malipo ya watumishi wa umma uitwao Lawson. Chini ya mfumo huu, taarifa za watumishi wa umma ambao utumishi wao umekoma kwa sababu yoyote ile zinapoingizwa katika kumbukumbu za mahala pao pa kazi, hupelekwa moja kwa moja Hazina kwa ajili ya hatua zaidi kama vile kuwaondoa katika 'payroll' na kuandaa malipo yao ya pensheni, kiinua mgongo, n.k. Kwa sasa mfumo wa Lawson umepelekwa katika mikoa na halmashauri zote za wilaya katika Tanzania Bara, mfumo huu pia umeshindwa kuondoa tatizo la watumishi hewa.

Mheshimiwa Spika, Sababu kubwa ya kushindikana kutatuliwa kwa tatizo la watumishi hewa ni kukosekana kwa **uadilifu** katika mfumo mzima wa utumishi wa umma. Watumishi hewa ni tatizo la kutengenezwa kwa makusudi. Mabilioni yanayopotea kila mwaka kutokana na malipo ya watumishi hewa yanakwenda kwenye mifuko binafsi ya viongozi na watendaji hao.

Mheshimiwa Spika, Hawa ndio ambao wamehakikisha kuwa jitihada zote za nyuma za kupambana na tatizo hili hazifanikiwi. Na hawa ndio watakaohakikisha kuwa jitihada za sasa za Mhe Rais Magufuli zinakwama. Viongozi na watendaji hawa wa Serikali hawapo katika ngazi za chini za utumishi wa umma wilayani na mikoani peke yake. Wako katika ngazi zote katika mfumo mzima wa utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, Ndio maana licha ya kelele na jitihada zote, licha ya taarifa rasmi za kila mwaka za Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuonyesha ukubwa na upana wa tatizo hili, hakuna kiongozi wala mtendaji wa idara ya Serikali au taasisi zake yeyote ambaye amewajibishwa kutokana na idara au taasisi yake kukutwa imelipa mishahara ya watumishi hewa.

Mheshimiwa Spika, Kwa kadri tunavyofahamu, hakuna kiongozi au mtendaji wa Serikali au taasisi wa ngazi yoyote ambaye amewajibishwa kwa sababu ya kuwa na watumishi hewa. Aidha, zoezi la uhakiki limefanywa na wahusika wa tatizo lenyewe. Kwa mujibu wa Sheria ya Tawala za Mikoa, Wakuu wa Mikoa ndio wakuu wa utumishi wote wa umma katika mikoa yao.

Aidha, Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Serikali za Mitaa ndio waajiri wa watumishi katika halmashauri zao. Kwa sababu hiyo, Wakuu wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri wanahusika moja kwa moja na uwepo wa watumishi hewa katika mikoa na katika halmashauri za Serikali za mitaa. Na hawa ndio ambao wamepeva jukumu na Mhe. Rais Magufuli la kuwabaini watumishi hewa katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, Kwa kutoa taarifa zinazoonyesha uwepo wamaelfu ya watumishi hewa katika mikoa na halmashauri zao, viongozi na watendaji hawa sasa wamejitia hatiani kwa kuonyesha kuhusika kwao na tatizo hili. Tunasubiri kuona hatua zitakazochukuliwa na Mhe Rais Magufuli dhidi ya Wakuu wa Mikoa na Wakurugenzi wa halmashauri ambao, kwa makusudi au kwa uzembe wao, wamesababisha kuwepo kwa watumishi hewa katika mikoa na halmashauri zao.

Mheshimiwa Spika, Lipo tatizo la pili ambalo limechangia kuwepo au kukua kwa tatizo la watumishi hewa katika utumishi wa umma. Tatizo hilo ni udhaifu mkubwa wa Tume ya Utumishi wa Umma ambayo ndio Tume Rekebu yenye jukumu la kuhakiki rasilmali watu katika utumishi wote wa umma. Kwa mujibu wa taarifa rasmi zilizotolewa na Tume hiyo kwa Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa hivi karibuni, Tume hiyo inakabiliwa na matatizo makubwa yanayokwamisha utendaji kazi wake. Kwa mfano, Tume hiyo haina watumishi wa kada mbali mbali, vitendea kazi vya aina mbali mbali kama vile magari, kompyuta na vifaa vingine vya ofisi. Na katika mwaka huu wa fedha, Tume ya Utumishi wa Umma imepatiwa 9.3% ya fedha iliyotengwa kwenye bajeti kwa ajili yake. Katika mazingira haya, Tume hiyo imeshindwa kabisa kutekeleza majukumu ya kuhakiki watumishi wa umma katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu. Kama kweli tunamaanisha kupambana na tatizo la watumishi hewa serikalini tunataka kuona fedha za kutosha zinatengwa kwa ajili ya tume hii.

Mheshimiwa Spika, Tatizo la tatu ambalo limechangia kuwepo au kuongezeka kwa watumishi hewa ni kutokuwepo kwa mfumo mmoja wa rasilimali watu unaojumisha na kuunganisha mifumo mingine yote. Kwa mfano, kwa utaratibu wa sasa, mfumo wa kusajili uzazi na vifo uliopo chini ya RITA haujaunganishwa na mfumo wa utumishi wa umma wala na mifumo ya hifadhi ya jamii kama vile NSSF, LAPF, PSPF, n.k. Kwa sababu ya mifumo hiyo kuwa inajitegemea, yaani 'stand-alone systems', taarifa zinazoingizwa katika mfumo mmoja hazipelekwi katika mifumo mingine. Kwa mfano, taarifa za vifo zinazotolewa na RITA haziingizwi katika mifumo ya utumishi wa umma wala ya hifadhi ya jamii ili majina ya wahusika yaweze kuondolewa katika 'payroll' na orodha za malipo ya pensheni au kiinua mgongo. Matokeo yake ni kuwepo

kwa watumishi hewa, yaani watumishi ambao wameshafariki dunia lakini taarifa zao hazijapelekwa kunakohusika na wanaendelea kulipwa mishahara na Serikali.

Kambi rasmi ya upinzani Bungeni inaitaka serikali kama kweli iko 'serious' katika kupambana na tatizo hili la watumishi hewa ichukue hatua zifuatazo ili kulimaliza tatizo hili kama ifuatavyo;

1. Wakurugenzi Watendaji na Makatibu Tawala wa mikoa waliosababisha watumishi hewa wakati mfumo wa kuwaondoa upo, wachukuliwe hatua za kisheria na kinidhamu kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

2. Tume ya Utumishi wa Umma wapewa watumishi wa kutosha, magari na vitendea kazi ili watekeleze jukumu lao la kuhakiki watumishi wa Umma na kutoa taarifa kwa mamlaka husika.

3. Serikali iunganishe mifumo ya rasilimali watu inayojitegemea "Stand alone systems". Namba ya kitambulisho cha taifa iunganishwe na mfumo wa vizazi na vifo, mfumo wa malipo serikalini, mfumo wa malipo ya pensheni, mfumo wa mlipa kodi nk. Hivyo mtumishi anapofariki, kustaafu au kuacha kazi mfumo wa Lawson nilioutaja hapo juu unamwondoa mara moja katika orodha ya watumishi wa Serikali.

4.0 KUIMARISHA TAASISI ZA UTAWALA BORA

4.1 Taasisi ya Kudhibiti na kupambana na Rushwa (TAKUKURU)

Mheshimiwa Spika, Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuwa ili mapambano dhidi ya Rushwa na Ufisadi nchini yaweze kuendelea kwa kasi ni lazima TAKUKURU iimarishwe kwa kupatiwa rasilimali watu na bajeti ya kutosha ili kutekeleza majukumu yake. Aidha, ni rai yetu kuwa Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hii muhimu na nyeti apewe uhuru na mamlaka kamili ili awe na Mamlaka ya kutekeleza majukumu yake kwa Uhuru bila ya kuingiliwa na mamlaka yoyote ile.

Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni, inaona kuwa ni wakati muafaka sasa ukaletwa mswada wa sheria hapa Bungeni ili kumpa Mamlaka Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU kufungua kesi mahakamani mara baada ya uchunguzi wake kukamilika badala ya hali ya sasa ambapo ni mpaka aombe kibali kutoka kwa DPP na tumeshuhudia kuwa DPP amekuwa mzito kutoa vibali hivyo na badala yake TAKUKURU inaonekana imeshindwa kupambana na Rushwa na Ufisadi Nchini.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la ajabu sana kusikia kuwa eti Serikali imewazuia watumishi wa TAKUKURU kwenda masomoni nje ya nchi kwa kigezo kuwa inabana matumizi. Serikali inapaswa kuelewa kuwa wala rushwa na watoa rushwa kila mwaka wanabadili mbinu zao na hivyo ili uweze kukabiliana nao huna budi kuwa na watumishi wenye weledi wa kutosha katika Nyanja hiyo na njia pekee ya kuwa na watumishi wa aina hiyo ni kuwaongezea ujuzi watumishi kwa kuwapeleka masomoni ndani na nje ya nchi.

4.2 Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma

Mheshimiwa Spika, tume hii ipo kwa mujibu wa Katiba na sheria zetu na ni wajibu kwa Viongozi wote kutangaza mali zao kwa wakati, kwa mujibu wa sherai, hata hivyo baadhi ya viongozi huchelewa kutangaza mali zao na wakati mwingine baada ya kukumbushwa mara mara, vile vile wanapotoka madarakani ni wachache sana wanaotangaza mali zao .

Mheshimiwa Spika, Tume hii ina watendaji wachache sana na imepewa jukumu la kufuatilia taarifa za mali na madeni ya watumishi wa umma na viongozi wa kisiasa kuanzia ngazi ya juu hadi kwa Madiwani , majukumu haya ni makubwa sana kwa Tume ambayo haina ofisi nchi nzima na hivyo kupelekea kushindwa kuyamudu majukumu yake vyema kutokana na ukubwa wa kazi husika.

Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni, inashauri kuwa ili tume hii iweze kuyamudu vyema majukumu yake ni bora sasa ikawezeshwa kufungua ofisi kila mkoa na kuajiri watumishi ambao watakuwa na wajibu wa kushughulikia fomu za Madiwani na watumishi wengine wa Halimashauri ili Tume ikabakia na majukumu ya kushughulikia watumishi wa umma ngazi ya Kitaifa pamoja na Wabunge.

Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaishauri kuwa Mali na Madeni ya Viongozi itangazwe kwa uwazi wakati viongozi wanapoingia madarakani na wakati Viongozi wanapotoka madarakani watangaze kwa uwazi tena mali na madeni yao ili kuwapa wananchi fursa ya kupima kama kiongozi husika ametumia madaraka yake kujilimbikizia mali.

5.0 MGAWANYO WA MAENEO YA KIUTAWALA

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 2(2) imeweka bayana mamlaka ya Rais wa Jamhuri ya Muungano kuigawa nchi katika maeneo ya kiutawala, inasomeka **'Kwa ajili ya**

utekelezaji bora wa shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar .Rais aweza kuigawa Jamhuri ya Muungano katika Mikoa, Wilaya na maeneo mengineyo kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria au kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge'

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kumekuwa na utaratibu ambao umeshamiri kwa kasi wa kugawa maeneo mbalimbali ya kiutawala nchini ikiwa ni pamoja na Vijiji, Kata, Wilaya na Mikoa. Aidha ugawaji huo unajenga utamaduni kwa wananchi kutaka maeneo yao yaendeleo kugawanywa mara kwa mara na serikali.

Mheshimiwa Spika, wakati nchi yetu inajipatia uhuru kulikuwa na Majimbo 10 ambayo yalirithiwa toka kwa Mkoloni. Kutokana na mamlaka aliyokuwa nayo Rais Nyerere mwaka 1966 alianzisha Mikoa 152, ambapo kwa sasa idadi ya Mikoa ni zaidi ya nusu ya Mikoa aliyozanza Rais wa kwanza wa taifa letu.

Mheshimiwa Spika, hoja hapa sio tu kuanzisha Mikoa na maeneo mengine ya utawala bali ni namna serikali inavyongeza matumizi ya masuala ya kiutawala badala ya mapato hayo kuelekezwa kwenye miradi ya maendeleo. Hii inathibitishwa na Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji vipya vingi vilivyoanzishwa bado havijapata huduma muhimu kwa ajili ya kuanza kazi ikiwemo ukosefu wa ofisi.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu kwa baadhi ya maeneo umeanza kuleta viashiria vya ukabila pamoja na migogoro ya mipaka na mgawanyo wa rasilimali, hili si jambo la kupuuzwa hata kidogo. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kusitisha zoezi la kugawa maeneo ya utawala na badala yake pawepo na utaratibu mwingine ambao utahakikisha maeneo hayo yakigawanywa kiutawala kuwe na mpango wa namna ya kupata mapato ya kujiendesha kuliko hali ilivyo sasa ya kutegemea serikali kuu na fedha nyingi kutumika kulipa mishahara ya watumishi na kujenga miundombinu mipya badala ya kutumika katika miradi ya Maendeleo.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni , inaishauri serikali ya awamu ya tano katika kutekeleza kwa vitendo mpango wa kuthibiti matumizi makubwa ya uendeshaji wa serikali iamue kusitisha utaratibu huu wa kuigawa nchi katika vipande vidogovidogo vya utawala kwani hii ni kuongeza zaidi gharama za uendeshaji wa serikali na mapato kidogo yanayokusanywa yaelekezwe katika kuendeleza miradi ya Maendeleo .

6.0 MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (TASAF)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa randama ya wizara uk 19 kifungu cha 2.4.3 (ii) kinasomeka kama ifuatavyo, nanukuu **“kiasi cha shilingi bilioni 275.9 zimehawilishwa kwa kaya maskini milioni 1.1 kama ruzuku kufikia mwezi Machi 2016 .Ruzuku hii ilihawilishwa kwa kaya zote masikini zilizoandikishwa Tanzania Bara pamoja na Zanzibar”**

Mheshimiwa Spika, fedha hizi ni nyingi sana kama zingetumika vizuri na kwa ufanisi. Kwa kitendo cha kuzigawa kwenye kaya masikini tena kwa mfumo wa fedha taslimu kamwe haziwezi kuondoa kiwango cha umaskini kwenye kaya hizo kwani mfumo huo sio endelevu hata kidogo.Ukitazama mgawanyo wa ruzuku hiyo utaona wazi ya kuwa kila kaya ilipata kiasi cha shilingi 250,818 au kila mwanakaya alipata kiasi cha shilingi 55,180.Hivi kweli kiasi cha shilingi 55,818 kwa mwaka kinaweza kumuondolewa mwananchi umasikini?

Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni, inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kufanya ukaguzi maalum wa ufanisi katika mfuko huu na kuangalia kama kuendelea kugawa fedha badala ya kuanzisha miradi kunaweza kuwaondolea wananchi umaskini wa kutupwa. Maana zipo tuhuma kuwa wapo baadhi ya watumishi wa Halimashauri ambao huwaweka ndugu na jamaa zao kama watu masikini ile hali sio na masikini halisi wakiachwa.

7.0 MAPITIO YA BAJETI NA MATUMIZI YA 2015/16 NA BAJETI YA 2016/17

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais Menejimenti Utumishi na Utawala bora, iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu **37,717,620,000** mwaka 2015/16 kwa matumizi ya kawaida na kwa mwaka wa fedha 2016/17 wameomba kuidhinishiwa **30,503,648,814** ikiwa ni punguzo la **7,213,971,186**. Kwa upande wa bajeti ya maendeleo 2015/16 waliidhinishiwa 6,259,944,000 na mwaka huu 2016/17 wameomba jumla ya 7,500,000,000. Kutokana na unyeti wa Ofisi hii ambayo ndio inasimamia uendeshaji wa Serikali, bajeti iliyotengwa ni finyu sana, hivyo **Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni** inalishauri Bunge kuongeza Bajeti hii ili zipatikane fedha za kutosha na ziweze kuelekezwa Zaidi kwenye kuimarisha mifumo ya utendaji serikalini ili taifa liweze kupiga hatua ya kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha unaoisha, Ofisi ya Rais fungu 30, ziliidhinishwa jumla ya shilingi **310,329,016,000/-** kati ya hizo shilingi **3,833,959,000** zilikuwa ni mishahara na shilingi **306,495,057,000/-** zilikuwa ni matumizi mengineyo kwa ajili ya idara ya utawala (usalama wa taifa, baraza la usalama la taifa, Taasisi ya kuzuia na kupambana na rushwa, mkurabita, taasisi ya uongozi n.k)Kwa mwaka huu wa bajeti 2016/17 fedha zinazombwa ni jumla

ya shilingi **354,637,917,000/-**. Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa vitengo na idara na watumishi bado ni wale wale, hivyo mfano wa kubana matumizi ulitakiwa uonekane kutoka kwa Kiongozi. Lakini Bajeti ya matumizi ya kawaida baddala ya kupungua imeongezeka kwa kulinganisha na ile ya mwaka jana. Ni bora viongozi tutembeee katika yale tunayoyaongea.

7.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha, kama nilivyoainisha hapo juu, kusimamisha/kufukuza watumishi sio mwarobaini wa kujenga utumishi wa umma uliotukuka. Mifumo na miundo ya utawala bora iimarishwe na kusimamiwa, hatua zilizoanza kuchukuliwa kudhibiti matumizi holela ya kodi za wananchi uendelee na wanokiuka wachukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria, ikibidi mali zao zitaifishwe kwa mujibu wa sheria. Mipaka ya madaraka izingatiwe ili haki itendeke. Viongozi wa kisiasa wawe mstari wa mbele katika uadilifu, uwajibikaji, uwazi na uzalendo, na watumishi wengine wataiga.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaendelea kuweka msisitizo wa Hotuba ya Kiongozi wa Upinzani Bungeni wa kuitaka Serikali iheshimu Katiba ya nchi na Sheria za nchi katika kutekeleza majukumu yake. Katika hotuba ya Kiongozi wa Upinzani Bungeni imebainika kwamba Serikali hii inaongozwa kiholela bila kufuata **instrument** inayoweka mwongozo wa muundo wa wizara na kazi zake jambo linalopelekea kila waziri kutekeleza majukumu yake kwa kutumia utashi na uwezo binafsi wa kufikiri;

Imebainika kuwa Serikali imevunja ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuwanyima wananchi haki ya kupata habari kwa kukataza vyombo vya habari vya umma na vile vya binafsi kurusha moja kwa moja mjadala wa Bajeti Bungeni;

Imeabinika vilevile kwamba Serikali imevunja kifungu cha 41(1) cha sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 na kifungu cha 18(3) na (4) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 ambavyo kwa pamoja vinaitaka Serikali kuleta Bungeni nyongeza ya bajeti ili kupata idhini ya Bunge ikiwa fedha zilizoidhinishwa awali hazikutosha kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa, lakini Serikali mara kadhaa imefanya matumizi ya fedha za umma nje ya fedha zilizoidhinishwa na bunge bila kuomba bunge liidhinishhe bajeti ya nyongeza.

Hivyo basi, **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuwa hii ni dharau kubwa kwa bunge na uvunjaji wa ibara ya 63(2) na 63 (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayolipa Bunge mamlaka ya kuisimamia na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni naomba kuwasilisha.

RUTH HIYOB MOLLEL (MB)

MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI-OFISI YA RAIS
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA

27.04.2016

MWENYEKITI: Tuendeleo, Waheshimiwa Wabunge hapo sasa ndiyo tumetekeleza matakwu ya Kanuni ya 99(9), tumepokea taarifa za Kamati zilizopelekewa kazi ya kuchambua maombi ya makadirio ya matumizi kwa hoja hizo mbili na sasa tumepata maoni kutoka Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hoja hizi mbili nazitoa kwenu, sasa ninyi kama Wabunge mziame tunaanza na mjadala ambao utahimishwa baadaye kwa hoja kutolewa kabla hatujaingia kwenye Kamati ya Matumizi. Haitawezekana kwa leo kuna wasemaji wengi hapa, kazi yangu ni kusimamia Kanuni tu.

Waheshimiwa Wabunge, katika hatua hii Fasili ya 10 inasema hivi:

“Wakati wa kujadili Makadirio ya Matumizi ya Wizara, hizi hoja mbili Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora ni Wizara katika Ofisi ya Rais inayoongozwa na Waziri wa Nchi mwenye dhamana ni Rais mwenyewe inasema hivi, muda wa Wabunge kuchangia utatolewa kulingana na uwiano wa idadi ya Wabunge kutoka katika kila chama”.

Waheshimiwa Wabunge, tunajua uwiano wetu humu ndani, nategemea orodha mmbayo naletewa na uongozi wa vyama vinavyowakilishwa humu Bungeni. *I cannot move myself*, siwezi kusema fulani achange ni lazima niletewe hapa rasmi. Kwa uwiano huo lazima itakuwa wanaanza walio wengi watatu *then* wanafuatilwa na wapinzani wawili, tunaenda hivyo, lakini nitaona jinsi ninavyocheza mwenyewe lazima *sometimes* unaleta uhai ndani ya Bunge kwa kuangalia wachezaji wako.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijafanya hivyo nina maagizo ya Spika, nazingatia muda lakini nina maelekezo ya Spika, lazima niyafikishe kwenu.

Waheshimiwa Wabunge, nina waraka wa Mheshimiwa Spika ambaye ameagiza niusome mbele yenu na nitausoma kama ulivyo na baadaye naamini utagawiwa kwenu.

Waheshimiwa Wabunge, Waraka wa Spika Na. 4 wa mwaka 2016 wa Mabadiliko ya Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Bunge. Ibara ya 96 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, imelipa uhalali Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuunda Kamati za Bunge za namna mbalimbali kadri itakavyoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora wa madaraka yake.

Waheshimiwa Wabunge, Ibara hiyo imeweka wazi kwamba, Kanuni za Kudumu za Bunge zitafafanua muundo wa shughuli za Kamati za Bunge. Kwa msingi wa maelezo haya na kwa mamlaka niliyopewa chini ya Kanuni ya 116 ya Fasili ya (3) na ya (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2016, nimelazimika kufanya mabadiliko ya Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Bunge. Sababu kubwa ya mabadiliko hayo ni kuhakikisha kuwa kila Mbunge ikiwa pamoja na Wabunge wengine wanne wapya walioapishwa tarehe 19 mwezi huu, anakuwa Mjumbe kwenye Kamati mojawapo ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, Wabunge hao wapya ni Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, Mheshimiwa Ritta E. Kabati, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya na Mheshimiwa Oliver Daniel Senguruka. Aidha, mabadiliko haya ni kwa ajili ya kuhakikisha pia kuwa kwa kadri itakavyowezekana muundo wa Kamati za Kudumu za Bunge unazingatia aina za Wabunge yaani jinsia, pande mbili za Muungano na vyama vya siasa vyenye uwakilishi Bungeni, ujuzi maalum, idadi ya wajumbe kwa kila Kamati na matakwa ya Wabunge wenyewe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, orodha ya majina ya Wabunge na namna walivyobadilishwa katika Kamati mbalimbali imeambatishwa kwenye waraka huu mtakaogawiwa. Aidha baada ya mabadiliko haya, naelekeza sasa Ofisi ya Katibu wa Bunge iratibu uchaguzi wa Kamati zifuatazo:-

(I) Kamati ya Nishati na Madini, kwa nafasi ya Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti.

(II) Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii, nafasi ya Mwenyekiti na Makamu wa Mwenyekiti.

(III) Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), nafasi ya Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti.

- (IV) Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) nafasi ya Mwenyekiti.
- (V) Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma PIC nafasi ya Mwenyekiti.
- (VI) Kamati ya Kudumu na Maendeleo ya Jamii nafasi ya Makamu Mwenyekiti.

Waheshimiwa Wabunge, taarifa imesainiwa na Job Agustino Ndugai, Spika wa Bunge tarehe 20 Aprili, 2016. Hii ndiyo taarifa ya Spika kwetu kama Wabunge, kwa hiyo itagawiwa sasa hivi ili tufahamu tumepelekwa baadhi yetu kwenye Kamati zipi na tumebaki kwenye Kamati zipi.

Baada ya kusema hayo, tuna dakika 35 ingawa tunahitaji hizo 30, dakika kumi kumi tuone tunazitumia vipi, hivyo mnivumilie tutumie muda wetu vizuri kwa kuchangia.

MWONGOZO WA SPIKA

MWENYEKITI: Mwongozo nitachukua tu, haya Mheshimiwa.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7). Wakati tunaahirisha kipindi cha asubuhi, Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati anahitimisha hoja yake, alikiri kwamba kuna upungufu wa sukari hapa nchini na akakiri kwamba Serikali inaagiza au imeshaagiza sukari kutoka nje ya nchi, lakini siku za nyuma zilizopita ni Serikali hii hii ilisema kwamba, haitakubali kupokea sukari zozote kutoka nje na hata mojawapo ya Kamati za Bunge ikiwemo Kamati ya Kilimo ilipoitahadharisha Serikali kwamba kutokuagiza sukari nje kunaweza kusababisha uhaba wa sukari nchini, Mwenyekiti wa Kamati alitwa na kuhojiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako, hii Serikali kwa nini inakuwa na kigeugeu mara leo inatoa kauli hii, mara kesho kauli hii ambazo haziwezi kutekelezeka. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mimi nikujibu kwa Kanuni hizi. Mwongozo ni sahihi kabisa matamko hayo yametamkwa mapema leo, sawa. Unachoomba kutoka kwenye kiti hiki, ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa kanuni na taratibu za Bunge, inaruhusiwa au hairuhusiwi. Maelezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni shughuli za utendaji wa Serikali mimi naangalia, nalea Kanuni hizi inaruhusiwa au hairuhusiwi, ningelikujibu! *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, mchangiaji wetu wa kwanza kwa jioni ya leo atakuwa ni Mheshimiwa Esther Lukago Midimu atafuatiwa na Mheshimiwa Felista Bura. *(Makofi)*

MHE. ESTHER L. MIDIMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anazozifanya. Vile vile nampongeza Waziri Mkuu kwa kazi nzuri anazozifanya, wananchi wote wanaziaminia. Pili, nawapongeza akinamama wa Mkoa wa Simiyu kwa kunipa kura ili niweze kuwawakilisha katika Bunge lako Tukufu na nawaahidi utumishi uliotukuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawapongeza sana Mawaziri wote wawili kwa hotuba yao nzuri. Naanza na uboreshaji wa maslahi ya Madiwani. Madiwani wanafanya kazi katika mazingira magumu sana hawana hata usafiri. Naiomba Serikali yangu sikivu iweze kuwapatia hata pikipiki ili waweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la afya Wilaya ya Maswa; hospitali ya Wilaya ya Maswa ina tatizo la umeme, umeme siyo wa uhakika unasukasua, miundombinu imekuwa ya kizamani. Naiomba Serikali yangu iweze kuboresha miundombinu ya hospitali ya Wilaya ya Maswa. Vile vile hospitali ya Wilaya ya Maswa ina majengo ambayo yameshakamilika, jengo la *OPD*, *theater* na wodi ya wazazi, lakini hayajaanza kutumika. Naiomba Serikali yangu sikivu ya Chama cha Mapinduzi hayo majengo yaanze kutumika yaweze kuhudumia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika Wilaya hospitali ya Maswa ina tatizo la maji. Jambo la kusikitisha Maswa Mjini kuna maji na hospitali ya Maswa na Maswa Mjini ni pua na mdomo, lakini hospitalini hakuna maji. Naiomba Serikali yangu ifanye haraka ivute maji kutoka pale Maswa Mjini ipeleke hospitali ya Maswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu afya katika Wilaya ya Itilima, Wilaya ya Itilima tunayo zahanati kubwa sana Kata ya Luguru. Hiyo zahanati ina majengo mengi sana. Tunaomba kibali kwa zahanati hiyo ili iweze kupandishwa hadhi iwe kituo cha afya. Tuna jengo kubwa la upasuaji limejengwa na Mfuko wa Mkapa *Foundation* na vifaa tiba tayari vipo, tatizo hatuna wataalam wa upasuaji. Naiomba Serikali yangu itupelekee Madaktari Bingwa wa upasuaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kituo cha afya Zagayu. Kituo cha afya cha Zagayu kina wafanyakazi watano ambapo mahitaji ni wafanyakazi 32. Tunaomba mtupelekee watumishi 32 ili waweze kuhudumia vizuri. Tunacho kituo cha afya Kata ya Nkoma, tunaiomba Serikali itupatie kibali kama kuna uwezekano tukipandishe hadhi kwa Wilaya ya Itilima tuwe na Hospitali ya Wilaya, kwa sababu wananchi wa Itilima wanahangaika sana, wakipata matatizo wanaenda kutibiwa Bariadi, Somanda. Tukikipandisha hadhi kile kituo cha afya cha Itilima, nina imani hata msongamano wa wagonjwa Somanda utapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya maji; naipongeza sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kuahidi kuvuta maji kutoka Ziwa Victoria kuleta Mkoani Simiyu kupitia Wilaya zake za Busega, Bariadi, Maswa, Itilima na Meatu. Naiomba Serikali yangu ihakikishe hayo maji itakapovuta, maji yapitie kwenye shule zote za Mkoa wa Simiyu za Sekondari, vituo vya afya vyote na zahanati ili yaweze kusaidia kwa sababu maji ni muhimu kwenye vituo vya afya na hospitali, ukizingatia na sera yetu ya sasa hivi ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kila Kijiji kutakuwa na zahanati na kila Kata kutakuwa na kituo cha afya. Naomba na maji yafike huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna vijiji katika Wilaya ya Maswa havina maji kabisa ambavyo ni Gudekwa, Masanwa, Mwabalatulu na Isegenge, akinamama wa vijiji vile wanahangaika sana. Naiomba Serikali yangu iweze kuchimba visima virefu kwa hivyo vijiji nilivyovitaja ili mradi akinamama waweze kupata maji. Wameshindwa kufanya kazi zao za ujasiriamali na mambo mengine ya maendeleo wamebaki kutafuta maji, wanasafiri kilometa nane mpaka kilometa 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ya elimu; naishukuru sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kujenga shule nyingi za Kata, naipongeza sana. Naiomba Serikali yangu kama kuna uwezekano kwa Mkoa wetu wa Simiyu iweze kutenga kila Wilaya shule ya bweni kwa watoto wa kike, kwa sababu watoto wa kike wanahangaika sana, watoto wa kike tukijenga shule za bweni tutawaepusha na vishawishi vya chipsi na bodaboda wakiwa wanarudi makwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Bariadi tuna Chuo cha Ufundi, Bunamhala, chuo kile naomba kiborreshwe, vijana wengi wapate ujuzi ili waweze kujajiri wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mkoa wetu una changamoto, una upungufu wa nyumba za Walimu 1,471, madarasa 563 na matundu ya vyoo 2,107. Tunaomba Serikali iweze kutuletea pesa kupitia TAMISEMI ili tuweze kukamilisha ujenzi huu. Vile vile naomba Serikali iweze kuweka Chuo cha VETA Mkoani Simiyu na iweze kutuletea pesa haraka sana tuweze kujenga hospitali ya Mkoa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi, naunga mkono hotuba ya Waziri Mkuu kwa asilimia mia moja. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Midimu ahsante sana kwa mchango wako mzuri. Tunaendelea na anayefuata Mheshimiwa Felista Bura.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia, pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya njema aliyotujalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza hotuba za Mawaziri, Mwenyekiti wa Kamati, Kambi ya Upinzani na kuna hotuba nzuri ambazo zinaleta msisimko kwamba, Watanzania hakika Rais hakukosea kuwateua hawa Mawaziri kuwa Mawaziri katika Wizara wanazozihudumia. Niwahakikishie tu wale ambao wana wasiwasi kwamba, watumishi hewa wataendelea katika Serikali yetu, haipo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale waliokuwa wanakwamisha tatizo hili la watumishi hewa kuondoka katika Serikali yetu wameondoka na wengine tunao humu humu ndani. Naomba pia Serikali iangalie namna sasa ya kuhakikisha kwamba hizi milioni 50 ambazo zitakwenda kila Kijiji ziwe na utaratibu maalum wa kuzifuatilia. Vijana au wanawake na makundi mbalimbali ambayo yamekwishaunda SACCOS yao na SACCOS yao ina uongozi unaoaminika, wao wapewe hizi milioni 50 kwa utaratibu maalum ambao pia utaruhusu kufuatiliwa kwa karibu kwa sababu hizi hela najua ni *revolving fund*, wengine watahitaji hizi fedha kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi kabla hazijatolewa makundi yapate elimu nzuri na zaidi ya yote yawe na uongozi, pia zifuatiliwe kwa karibu kuhakikisha kwamba, hazitumiki ovyo kama fedha ambazo zimewahi kutolewa na Serikali na hatukujua zimetumikaje. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Manispaa yangu ya Dodoma Mjini, tuna upungufu wa watumishi 590 wa kada mbalimbali. Kukosekana kwa Watumishi hawa kunafanya maendeleo yasifuatiliwe kwa ukaribu zaidi. Mheshimiwa Waziri

unayehusika na utumishi wa umma nakuamini kwa kazi zako nzuri na ofisi yako kwa sasa naiamini, kwamba tutakapoleta barua kwani tuliandika barua mwezi wa Machi mwaka huu hatutajibiwa, naomba sasa nitakapokuletea hiyo copy ya barua uhakikishe kwamba wale watumishi wa kada mbalimbali katika Halmashauri yetu ya Manispaa ya Dodoma tunawapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna ukosefu wa Walimu 105 wa Sayansi na Walimu wa sayansi wamesomeshwa hapa *UDOM (University of Dodoma)*, siyo vizuri Manispaa ya Dodoma tukakosa Walimu 105 wa Sayansi ambao wangewasaidia wanafunzi wetu. Sasa hivi tunajenga maabara na maeneo mengine katika Manispaa yetu tumekwishakamilisha maabara, lakini Walimu 105 hawapo. Nakuomba Waziri unayehusika na Wizara hii tusaidie kupata Walimu hao 105 na wale watumishi 590 hasa wa kada za chini ambao ni watendaji katika vijiji vyetu, watendaji katika mitaa yetu, watusaidie katika kusimamia maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Manispaa ya Dodoma haina ofisi. Tunafanya kazi katika shule iliyokuwa Sekondari ya Aghakan na wameshatuandikia barua wakitaka majengo yao. Iko siku tutakuta vifaa na samani na kila kitu vikiwa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kupewa barua na aliyekuwa Waziri wa Ujenzi Dkt. Kawambwa kwamba tunapewa ofisi ambayo inatumika na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma kwa sasa, lakini kwa sababu Mkuu wa Mkoa wa Dodoma hana ofisi na jengo lake linalojengwa kila mwaka tunaomba fedha, lakini fedha zinazoletwa ni kidogo mno hazisaidii kitu chochote, naiomba Serikali yetu sikivu, tumeomba pesa kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ya Halmashauri ya Manispaa, tumeomba pesa kwa ajili ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, tunaomba hata kama ni *floor* moja ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, hata kama ni *ground floor*, basi ijengwe imalizike ili Mkuu wa Mkoa aweze kuhamia kwenye Ofisi yake na Halmashauri ya Manispaa wapate ofisi yao. Pale tunapofanya kazi kama Manispaa huwezi kuongeza hata kibanda cha mlinzi kwa sababu majengo yale siyo ya kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, hata hospitali ya Wilaya hatuna. Tumeomba bilioni 25 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya Wilaya, Dodoma imekua, watu wako wengi, Wabunge wenyewe mmeongezeka, kwa hiyo hatuna hospitali ya Wilaya. Naomba sana kwamba zile bilioni 25 tulizoziomba, basi tufikiriwe kupewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wilaya ya Bahi hawana Hospitali, asilimia 80 ya wagonjwa wanaokuja Hospitali ya Mkoa wa Dodoma wanatoka Wilaya ya Bahi, kwa sababu hawana hospitali ya Wilaya. Naiomba Serikali yetu sikivu

waone namna ya kujenga Hospitali ya Wilaya Bahi na hospitali ya Mkoa ibaki kama hospitali ya rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maslahi ya Watumishi wa kada za chini sasa kwa sababu Mheshimiwa Rais ameagiza kwamba kusiwepo madeni kwa watumishi kama Walimu, Manesi, Maafisa Ugani, Polisi na kadhalika, Serikali ione kwamba madeni yale ya nyuma ambayo wanadaiwa na watumishi yahakikiwe na kama yamekwisha hakikiwa basi Watumishi walipwe haki zao maana naiamini Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwamba inafanya kazi kwa uhakika na kwa juhudi nyingi, kuhakikisha kwamba watumishi wanapata maslahi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya yangu ya Chamwino tuna jengo la Halmashauri pale. Lile Jengo Mkandarasi anadai bilioni tatu ili kukamilisha ujenzi wa Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino. Naomba sana Serikali ikamlipe Mkandarasi anayejenga Ofisi ya Halmashauri ya Chamwino ili watumishi wale wawe katika jengo moja, kwa sababu Watumishi wa Wilaya ya Chamwino wamesambaa, wengine wako Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, wengine wanafanya kazi kwenye nyumba za watu binafsi, wengine wapo kwenye nyumba zisizoeleweka, lakini Mkandarasi akipata bilioni tatu alizoziomba jengo lile litakuwa limekamilika.(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya yetu ya Chemba pia hatuna Hospitali, hatuna nyumba za Watumishi, hatuna maji, hatuna kitu chochote. Naiomba Serikali yetu sikivu sasa ione namna kwa sababu Wilaya ya Chemba ni Wilaya mpya. Pia tuna mradi wa umwagiliaji wa maji wa GAWAE tuliomba milioni 533. Naiomba Serikali ione namna ya kupata hizi fedha ili kazi ya umwagiliaji kwa wananchi maana Dodoma ni Mkoa kame sasa iweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatamani kuwashusha wanawake wa Wilaya ya Bahi ndoo vichwani. Tuliomba shilingi milioni 400 kuvuta maji kutoka katika Kijiji cha Mkakatika. lakini tulipewa milioni 100 tu. Naiomba Serikali katika bajeti hii itukumbuke tunatamani wanawake wa Wilaya ya Bahi katika eneo la Makao Makuu ya Wilaya wapumzike kubeba ndoo vichwani. Tukipata milioni 400 tutapata maji Bahi katika Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia hotuba za upande wa pili katika Bunge hili wakijinasibu kwa mambo mengi, kwamba Serikali inagawa maeneo na kulipa watumishi pesa nyingi na kuweka miundombinu badala ya kusimamia miradi michache ya maendeleo, hatuwezi kuacha kuwalipa watumishi, miundombinu ndiyo maendeleo...

(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Tunakushukuru sana Mheshimiwa Bura kwa mchango wako mzuri. Mchangiaji wetu anayefuata nadhani ndiye atakuwa lala salama yetu kwa leo, Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kufika siku ya leo. Kwa vile ni siku ya kwanza leo kuchangia humu Bungeni, nawashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Mufindi Kusini kwa kunichagua na kunirudisha tena Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nawashukuru Watanzania wote kwa ujumla wake kwa kumchagua Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kuwa Rais wa nchi hii. Tena narudia mara mbili, Watanzania walisema wenyewe tunataka Kiongozi anayefanya maamuzi ya haraka. Nadhani Watanzania hawajakosea, Rais wetu anajitahidi sana kufanya kazi pamoja na Waziri Mkuu na Viongozi wote waliochaguliwa wa ngazi za juu. Nawapongeza sana kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wameanza kulalamika masuala ya kutumbua majipu, kuna majipu ya aina tatu, kuna jipu ambalo linakuwa limeiva, sasa kazi ya Wabunge ni kutoa ushauri, ukiona jipu limeiva ni nafuu ujitumbue mwenyewe kwa sababu ukingoja kutumbuliwa inakuwa ni hatari. Serikali hii ya sasa hivi imejipanga vizuri kutekeleza mahitaji wa wananchi ambao wametuchagua. Wafanyakazi hewa ambao sasa hivi zoezi linaendelea, kama uliibia Serikali miaka ya nyuma jiandae hilo ni jipu tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite sana TAMISEMI, sasa hivi tumesema kwamba asilimia 40 ya fedha ya Bajeti ya Serikali inakwenda kwenye maendeleo. Bahati nzuri sana hata Rais wetu anasisitiza sana hilo, TAMISEMI imechukua asilimia kubwa sana ya maendeleo vijijini. Tatizo kubwa la Watanzania vijijini na Wabunge walio wengi wakija hapa wanalalamika sana masuala ya maji, maji ni tatizo sugu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali kwa bajeti hii tujitahidi sana vijiji ambavyo havijapata maji viweze kupata maji. Haya maswali tunayouliza kila siku yanajirudia rudia, kwa mwaka huu tukifuata bajeti vizuri na kusiwe na ufisadi, wananchi watatatuliwa tatizo lao la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano katika Jimbo langu la Mufindi Kusini kuna matenki mengi sana ya maji yalijengwa mwaka 1970 mpaka leo hii, sasa hivi miundombinu imeharibika sana. Naiomba sana Serikali, ile miundombinu ambayo imeharibika sana, kwa bajeti hii TAMISEMI, Mawaziri wote waliochaguliwa TAMISEMI ni vijana halafu wapo makini sana na wanakwenda kwa speed.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tenki moja lipo pale Igowole, kuna tenki moja lipo pale Nyololo, tenki moja lipo Itandula, kuna tenki moja lipo Idunda na tenki moja liko Luhunga. Vile vijiji vyote ambavyo matenki ya maji yapo, miundombinu imechakaa, naomba Serikali ijitahidi kwa Bajeti hii waweze kutengeneza miundombinu ya maji ili watu waweze kupata maji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la elimu. Kwanza namshukuru sana Rais kwa kuamua ile bilioni sita kupeleka kwenye madawati, ile amepiga bao tayari! Bahati nzuri sana amesema kila Mbunge atapewa madawati 500, lakini yale madawati yale nadhani mwezi wa Julai tunapoondoka madawati yangu nitayachukua mwenyewe. Kule kuna shule katika Jimbo langu la Mufindi Kusini hazina madawati, wananchi wameshasikia tayari na mimi yale madawati bahati nzuri mmesema tutapewa Wabunge nitasimamia vizuri, mtu akianza kuzungusha yale madawati sijui itabidi nitumbue jipu! Hili suala la kutumbua majipu tutatumbua mpaka kwenye vijiji kule. Sasa tatizo la madawati nadhani kwa nchi hii tutakuwa tumepunguza kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la elimu, nataka nimshukuru Waziri wa Elimu kwa kuwa na vision nzuri sana. Wabunge ni washauri tunaishauri Serikali, naomba nimshauri Waziri, hii kubadilisha badilisha madaraja siyo tija sana, kwa ku-improve elimu. Tatizo kubwa ambalo lipo, hatuna Walimu wa sayansi katika sekondari zetu, ni tatizo kubwa sana Mheshimiwa Waziri. Unaweza ukaona mtoto anasoma, amechagua masomo ya sayansi kuanzia form three mpaka form four anaingia kwenye mtihani hana Mwalimu wa sayansi, tusitegemee kwamba atafaulu mtihani hata siku moja! Hilo ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri Serikali imetoa msukumo mzuri sana wa kujenga maabara, Wakurugenzi pamoja na Wakuu wa Wilaya walijitahidi sana kusimamia maabara na tunaendelea kujenga maabara kule, shule nyingine vifaa vipo tayari, lakini hatuna Walimu wa sayansi, tusije tukategemea kwamba watapata division nzuri, watafeli tu, kwa sababu hakuna Walimu na wao wanaingia kwenye mitihani hawajafundishwa masomo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matatizo makubwa ya Walimu wa sayansi pamoja na Walimu wa hesabu. Kama kweli tunalenga ku-*improve* elimu, tatizo siyo kubadilisha madaraja, sijui GPA haisadii! Tuhakikishe kwamba Serikali inasomesha Walimu wa sayansi, tena itoe motisha kwa mfano, Vyuu Vikuu wale wanao-*opt* masomo ya sayansi, basi walipiwe ada, wakilipiwa ada tutakuwa na Walimu wengi sana wa sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni katika Shule za Msingi. Shule za msingi bado kuna matatizo. Kwa mfano, wale tunaowaita Maafisa wa Tarafa Elimu, Afisa Tarafa Elimu anatembelea baiskeli, kwa mfano kwangu kule vijiji ni vikubwa, anatembea karibu kilometa 30 mpaka 40 kwa baiskeli, unategemea kweli ataweza kukagua shule zote za msingi? Ni ngumu sana, hebu mtafute hata pikipiki tu tumpe. Maafisa Elimu wa Kata tuwatafutie usafiri ili waweze kuzifikia zile shule, imekuwa ni tatizo kweli hata ofisi hawana wanashindwa kufanya kazi vizuri. Kwa sababu tunataka tu-*improve* elimu, naiomba Serikali ifanye mchakato kuhakikisha wanapata vyombo vya usafiri ili waweze kusimamia elimu.(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika shule za msingi, kuna suala moja huwa linaleta matatizo sana, sijui sasa turudishe *system* ya zamani, hebu mliangalie na mlipime vizuri. Kuna Walimu wengine wanafanya biashara, badala ya kufundisha wanaanza kufanya biashara kwa sababu ya ugumu wa maisha. Serikali iangalie hilo tunafanyeje, sijui mrudishe *teaching allowance*, sasa ninyi mtaliangalia, zamani kulikuwa kuna *teaching allowance*, mtapima wenyewe lakini lazima muweke mazingira mazuri ya Walimu wa shule za msingi kwani wana mazingira magumu.(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ni Wenyeviti wa Vijiji, TAMISEMI. Wenyeviti wa Vijiji kuanzia Mbunge kama anataka kufanya mkutano kwenye Kata yake, kwenye kijiji chake, ni lazima amwambie Mwenyekiti wa Kijiji. Mkuu wa Wilaya kama anafanya mkutano kwenye kijiji lazima amwambie Mwenyekiti wa Kijiji. Naiomba Serikali, Wenyeviti wa Vijiji angalau wapewe posho. Bahati nzuri sasa hivi tumesema kwamba kila mtu ni lazima afanye kazi, yule Mwenyekiti wa Kijiji anafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtendaji analipwa na Serikali lakini Mwenyekiti wa Kijiji halipwi mshahara, tutafute hata posho, tunapata shida kweli. Diwani kama anaitisha mkutano ni lazima amwambie Mwenyekiti wa Kijiji pale, Serikali lazima iangalie kwa makini suala hilo. Mwenyekiti wa Kijiji ana kazi kubwa kweli, kama Mtendaji analipwa hela, yeye halipwi na yeye ndiye mkuu, ndiye anayefungua hata vikao vya kijiji, ndiye anayeendesha maendeleo ya kijiji pale,

halafu hapewi chochote, hii inaleta shida. Naiomba Serikali ifikirie vizuri juu ya hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Diwani anafanya kazi kama Mbunge, tukiwa hapa Bungeni sasa hivi Madiwani wako kule wanafanya kazi, wanasimamia miradi yote; miradi ya ujenzi wa Zahanati, miradi ya barabara, miradi ya maji anasimamia Diwani, tatizo kubwa la Madiwani wetu hawana vyombo vya usafiri. Kuna Kata kubwa sana anashindwa kuzifikia. Katika Kata moja unaweza kuona ina vijiji sita, karibu kilometa 12. Kwa mfano, kuna Kata moja kutoka Idepu.....

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema huyo ndiye mchangiaji wetu wa mwisho kwa leo, lakini niwatendee haki Waheshimiwa Wabunge ambao vyama vilileta, msije mkasema labda Kiti na Meza wanachakachua, hapana, wakayapange vizuri kwa kesho haya majina machache yaliyokuwa yameletwa, vyama vina hiari ya kupangua kwa kadri wanavyoona wao.

Mimi nayasema tu yaliyoletwa mbele yangu. Hivyo, watatu hao ndiyo walikuwa Chama Tawala. Vyama vya Upinzani kwa mpangilio wa uwiano huo, Mheshimiwa Mariam Msabaha CHADEMA na Mheshimiwa Abdallah Mtolea wa CUF, then unarudi tena upande wa CCM walikuwa Mheshimiwa Jitu Soni mpaka hapo ndiyo waliokuwa wameletwa, kwa hiyo kuna majina mawili ambayo itabidi asubuhi yawekwe hapo. Kwa upande wa CHADEMA na CUF ambayo yapo hapa ni Mheshimiwa Godbless Lema na Mheshimiwa Riziki Shahari Mngwali. Nataka tutende haki *bin* haki, hilo la kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, kwa taarifa zote mbili za Kambi ya Upinzani, hili suala la ukiukwaji wa Katiba linaendelea kurudiwa, ni haki yao kutoa maoni, lakini waende zaidi ya hapo! Itapendeza sana na tutakuwa tunajenga demokrasia na *legal jurisprudence* ya nchi yetu kama wataweza kwenda Mahakamani na kuomba *declaration* kama kweli kwa vitendo vinavyofanywa na Serikali tumekiuka Katiba, tusiishie hapo! Nawasihi sana, hoja ya uvunjaji wa Katiba *is a very serious allegation*, nawaombeni sana tusiliache juu juu tu hivi!

Pili, Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati anachangia katika hoja ya Waziri Mkuu, alielezea kilichotokea na nadhani ili tusiendeleo kupotosha yale yaliyosemwa na Serikali yapo kwenye *Hansard*. Naagiza Serikali *statement* ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha igawanywe kwa Wabunge wote ili anayejielekeza kushambulia, ajielekeze kwa vifungu vya sheria ambavyo Waziri wa Fedha amevitumia.

Kambi ya Upinzani haijielekezi huko inasema yale ya jumla tu *for public consumption*, hapana! Tuyajibu hayo na kwa vile *we have very enlighten mind* humu, tutajibishana, mtiririko huu ningependa hata mimi mtu aniambie kwamba Serikali hapa imekiuka sheria zilizotajwa. Nadhani tukienda hivyo tutakuwa tunakwenda vizuri kuliko hii ya kunyoosheana vidole, haitusaidii. Tuko hapa kusaidia wananchi, Taifa hili liende mbele kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, sina cha kuongezea, nawashukuru sana kwa kazi nzuri mliyoifanya kwa leo, kama nimewakwaza baadhi yenu, mimi ndivyo nilivyo, samahani sana, tusonge mbele!

Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.00 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,
Tarehe 28 Aprili, 2016, Saa Tatu Asubuhi)*